Al-Islam.org
Ahlul Bayt Digital Islamic Library Project
Published on *Books on Islam and Muslims* | *Al-Islam.org* (https://www.al-islam.org)

Ujumbe – Sehemu Ya Tatu

Author(s):

Sheikh Jafar Subhani [3]

Publisher(s):

Al Itrah Foundation [4]

Kitabu kilichoko mikononi mwako ni tarjuma ya kitabu cha Kiingereza kiitwacho, The Message, kilichoandikwa na Sheikh Ja'far Subhani. Sisi tumekiita, Ujumbe. Kwa vile kitabu hiki ni kikubwa, tumekigawa katika juzuu nne ili kuwarahisishia wasomaji wetu kukisoma kwa makini katika kila sehemu. Hii uliyonayo mkononi ni Juzuu ya Tatu.

Kitabu hiki kilichoandikwa na mwanachuoni mkubwa Sheikh Ja'far Subhani kimekuwa ni miongoni mwa vitabu bora vilivyofanya utafiti wa kina kuhusu historia ya Uislamu na Waislamu.

Translator(s):

Maalim Dhikiri U.M. Kiondo [5]

Category:

General [6]

Topic Tags:

Historia [7]
Wayahudi [8]
Vita [9]

Waqurayshi [10]
Jeshi [11]

Person Tags:

Mtume Muhammad (s.a.w) [12]
Bibi Zainab (as) [13]
Imam Ali (as) [14]

Kuhusiana Nasi

(Inawahusu watoaji wa toleo la Kiingereza ambalo kitabu hiki ni tafsiri yake)

Leo hii, akili iliyo macho huyaona mabadiliko kwenye maisha ya kiakili ya mwanaadamu. Sayansi na teknolojia, vikiwa kwenye ustawi wake wa juu zaidi, vyaelekea kukifikia kipeo chake cha mwisho. Mahitaji ya kimwili pamoja na tamaa ya mamlaka na tawala vimemwongoza mwanaadamu kwenye ufisadi wa dhahiri wa maadili yake.

Katika hali hii ya kukatisha tamaa, mtu alazimika kutulia na kuitathmini hatari iliyojificha na inayowatishia wanaadamu wote kwa ujumla. Mwanaadamu, tayari kaisha mkodolea macho tena Allah, Mwingi wa rehema, Rahimu, kwa kuwa, sasa kaishatambua ya kwamba ufumbuzi wa matatizo yake na wokovu wake umo kwenye kuzifuata Amri za Allah.

Mgeuko huu, wa kutoka kwenye fikara za kimwili na kuja kwenye fikara za kiroho unaafikiana kabisa na malengo na shabaha za hii Seminari ya kiislamu. Mafundisho ya dini yanakwenda sambamba na maendeleo ya huu wakati wetu, yakitoa kimbilio lihitajiwalo mno na akili yenye kusum- buka na mashaka.

Haya ni matokeo ya mtanabahisho, ya kwamba sasa inatambulikana ya kwamba siri ya kuishi maisha ya kiuchamungu kwenye ulimwengu huu huongoza kwenye baraka ya milele ya maisha ya Ahera. Huu ndio ujumbe wa UISLAMU kwa ulimwengu mzima.

Hii Seminari ya kiislamu inadhamiria kuinua juu kurunzi ya mwongozo wa kiroho na kusaidia kwa juhudi zote katika kuukuza urithi wa mwanaadamu. Inaionyesha njia ya maisha ifundishwayo na Qur'ani kati- ka utukufu wake wa asili. Inayaonyesha yale yenye nguvu na yaliyo ya kweli tu. Vitabu vyake vimekusudiwa kufaa katika kuyafikia mahitaji ya kiroho ya zama zetu hizi. Vitatumika kama kijito kitiririkacho maji daima, kwa wale walio na kiu ya elimu.

Hii Seminari ya kiislamu ni taasisi ya ulimwengu mzima yenye kujitahidi katika kudumisha udugu wa kiislamu. Inafurahia mchango wa akili zilizo bora zaidi, zaidi ya kuwa na msaada wa kimataifa kwa ajili

ya kuyafikia malengo yake makuu. Inavyo vituo Canada, na Mashariki ya Mbali.

Orodha ya anwani iko kwenye kurasa za mwisho za kitabu hiki. Msomaji (wa Kiingereza) anaweza kukiandikia barua chochote miongoni mwa vituo hivi ili kuvipata vitabu vyetu.

Islamic Seminary Publications

Kwa Ndugu Msomaji,

Asalaam Alaykum

Kitabu hiki kinatolewa na Seminari ya kiislamu (S.L.B. 5425, Karachi, Pakistan). Vitabu vyake vimelengwa kuyatimiza mahitaji ya kiroho ya zama zetu hizi, na msisitizo maalum juu ya kuzisafisha akili na fikara. Juhudi nyingi zimefanywa na Seminari hii kuweka kwenye vitabu vyake yale yaliyo na nguvu na yaliyo ukweli halisi kwenye Uislamu.

Unaombwa kukisoma kitabu hiki katika hali iliyodhamiriwa. Vilevile unaombwa kuwasiliana nasi, kuhusu maoni yaliyo huru kuhusu vitabu vyetu, jambo tutakalolipenda mno.

Kuubalighisha ujumbe wa Uislamu ni jukumu lihitajilo ushirikiano wa watu wote. Seminari hii inakukaribisha ushiriki kwenye jukumu hili

قُلْ إِنَّمَا أَعِظُكُمْ بِوَاحِدَةٍ ۖ أَنْ تَقُومُوا لِلَّهِ مَثْنَىٰ وَفُرَادَىٰ ثُمَّ تَتَفَكَّرُوا ۚ{46}

"...Sema: Mimi ninakuahidini jambo moja tu, ya kwamba msimame kwa ajili ya Allah, wawili-wawili na mmoja-mmoja..." **(*As-Saba, 34:46*).**

Allah na Akubariki.
Nduguyo katika Uislamu,
Katibu wa Uchapishaji.

Utangulizi

Kwa Jina La Allah, Mwingi Wa Rehema, Rahimu.

Tangu zamani za kale, mwanadamu amekuwa akiitafuta elimu kupitia milango yake ya fahamu. Hivyo basi, kwa kuvitambua vitu, hujaribu kulitatua tatizo lake. Katika mchakato huu, amekuwa akifanya majaribio, na hatimaye kwa kubahatisha alifikie kwenye ufumbuzi uwezekanao wa matatizo yake. Ikiwa imetegemea juu ya dhana na utendaji huu, sayansi ilistawi kwa ukubwa mno kwenye maeneo na nyanja mbali mbali za matumizi yake.

Kwenye zama hizi mpya za sayansi, mamia na maelfu ya maabara ya utafiti yanavutia nadharia ya wanasayansi ambao hufanya ugunduzi na ubuni– fu mkubwa mno wa kiwango cha kutoaminika cha usahihi wa ala na zana. Vivyo, kitu pekee ambacho hadi sasa sayansi imeshindwa kukikamata ni tatizo la kijamii. Ni dhahiri kwamba matatizo ya kijamii ni matatizo ya wanadamu. Na matatizo ya wanadamu ni ya hali ambayo haiwezi kuin– gizwa kwenye neli ya majaribio /testityubu (test–tube). Ili kuisadiki habari hii, mtu yuatambua vizuri mno kwa mfano, ya kwamba bado sayansi hai– jatoa jibu la kutoafikiana na chuki iliyomo miongoni mwa watu au tofauti za kimatabaka zinazokithiri kwenye matabaka ya jamii za wanaadamu.

Historia inatuambia kuhusu ustaarabu mkubwa uliopita hapo kale na mwishowe ukapotea. Hivi sasa tumebakiwa na masalio na magofu bubu yanayotukumbusha zama za kale za wanaadamu, zilizochakaa. Hakuna shaka kwamba sayansi inagundua habari za maisha kwa njia ya ufukuaji wa mashimo yanayodhaniwa kuwa na vitu vya kale kwa ajili ya uchunguzi, na kwa kujifunza masalio ya vitu visivyo na uhai (relics) na (vikisukuku) vile vyenye uhai vilivyogeuka kuwa mawe (fossilis), vilivyogandamana na miamba ya ardhi. Lakini tukiyaachilia mbali yote hayo, hakuna matokeo ya dhahiri yaliyopatikana kuhusiana na matatizo mengi ya wanaadamu.

Imam Ali (a.s.) alimpa dokezo la fikara zake mwanawe ambalo ni lenye kuhusika na jambo hili. Alisema: “Mwanangu mpenzi! Ingawa muda wa maisha yangu si mkubwa kama ule wa watu wengine waliofariki dunia kabla yangu, lakini nilijichukulia hadhari kubwa kujifunza maisha yao, kwa juhudu nyingi niliyapitia matendo yao, nilizifikiria fikara na matendo yao.

Niliyachunguza masalio ya vitu vyao visivyo na uhai na magofu; na nikayafikiria maisha yao kwa makini mno kiasi kwamba nilijihisi kana kwamba niliishi na kufanya kazi pamoja nao tangu kwenye zama za awali za historia hadi kwenye hizi nyakati zetu, na ninayajua yaliyowatendea mema na yaliyowadhuru.”

Hakika, historia imeandika habari zote, zile zenye kupendeza na zenye kuchukiza, lakini lile lisikitishalo ni kwamba hakuna yeyote aliyejali kuzama ndani ya kina cha sababu za habari hizo. Ama kuhusu ufumbuzi halisi wa tatizo, liwe kubwa au dogo, hakuna juhudi katika upande wa mwanaadamu

uonekanao kwenye historia. Ni yale mambo yasiyo muhimu ndiyo yaliyoshughulikiwa kwa maelezo marefu yaogofyayo.

Kwa kuwa historia ni masimulizi ya matukio ya kale yaliyoandikwa, yanapata kuwepo kwake kutoka kwa mwandishi wake. Watu walioiandika historia hawakuwa huru kutokana na kiburi cha ubinafsi, rangi au sehemu atokayo mtu, na hivyo basi, lengo lake hasa laonekana kushindwa. Mbele ya tafsiri mbaya na uzushi wa habari za kihistoria, msomaji wa kawaida wa historia yumo kwenye hasara ya kuuelewa ukweli wa jambo hilo. Ni kama daktari ambaye, kama hana taarifa sahihi kuhusu maradhi ya mgonjwa wake anayemwuguza, hataweza kuchunguza maradhi halisi ya mgonjwa wake huyo.

Hakika sifa moja ya historia iangazayo mno ni kwamba, inazichukua taar– ifa za maisha ya watu wakuu wa kale. Hakika watu hawa waliiunda historia kwa kuwa walileta mapinduzi na mabadiliko kwenye mtindo wa maisha ya wanaadamu.

Miongoni mwa hawa watu wakuu hakuna hata mmoja aliyeishi maisha yenye mambo mengi, ya kimapinduzi na yenye maana kama aliyoishi Mtukufu Mtume Muhammad (s.a.w.w.). Hakuna yeyote miongoni mwao aliyeziacha athari za kudumu kwenye jamii aliyojitokeza kama alivyofanya Mtume wa Uislamu (s.a.w.w.). Huu ni ukweli uliokubaliwa na karibuni wanahistoria wote, wawe ni wa Mashariki au wa Magharibi.

Kujifunza maisha ya Mtukufu Mtume Muhammad (s.a.w.), mkuu zaidi miongoni mwa wanaadamu wote, kunachukuliwa kuwa ni kwenye kuleta hofu na kujierevusha. Nyororo ya matukio ya kabla na ya baada ya kuzaliwa kwa huyu mtu mkuu kunatoa mawazo kwa ajili ya kila mtu aliye na japo punje ndogo tu ya akili na hisia za ulinganifu.

Kuzaliwa kwa Mtukufu Mtume (s.a.w.) akiwa yu mtoto aliyezaliwa baada ya baba yake kufariki dunia, na kifo cha mama yake, Bibi Amina (a.s.), alipokuwa na umri wa miaka sita tu, na kulelewa kwake, kwanza na babu yake na kisha na ami yake ni mambo yasiyo kifani.

Baada ya kuyapitisha maisha yenye mambo mengi, kujitenga kwake kwenye Pango la Mlima Hira na Ufunuo wa Allah uliofuatia, kuwaitia watu kwenye dini ya Allah, upinzani wa makafiri na wenye kuabudu masanamu, maonevu na mateso yao, umadhubuti wake uliodumu katika kuimarisha ujumbe wa Allah kwenye kipindi cha miaka kumi na mitatu ya mwanzo ya Utume wake mjini Makkahh hadi kwenye muda wa kuhamia kwake Madinah, ni matukio yasiyo kifani kwenye historia.

Miaka kumi ya mwisho ya maisha yake mjini Madina, kuimarisha kwake juhudi za ujumbe wake kwa ajili ya uenezaji wa Uislamu, kushiriki kwake kwenye vita nyingi dhidi ya makafiri na hatimaye kutekwa kwa Makkahh bado ni matukio makuu yenye kuonekana kuwa si ya kuaminika, lakini yameandikwa kwenye historia kuwa ni mafanikio ya kimiujiza.

Mamia ya vitabu yameandika kuhusiana na maisha na ujumbe wa Mtukufu Mtume (s.a.w.) lakini vitabu hivi haviwezi kuchukuliwa kuwa ni wasifu kamili juu ya sifa na mafanikio yake. Hasa yale maandishi ya

mustashrik yameingiliwa na chuki, makosa na tafsiri potofu.

Kitabu hiki sio tu kwamba kinatoa mambo yenye kuongoza, bali vile vile kimezitegemeza taarifa zake kwenye maandiko ya kihistoria yaliyo ukweli. Moja ya sifa zake zijidhihirishazo mno ni kwamba mwandishi amechukua hadhari kubwa katika kuyasimulia matukio ya kihistoria, na wakati huohuo amejitahidi, akiwa yu mwanachuoni mtafiti, kuyaendea matukio hayo kwa fikara zenye kuchanganua mambo pia.

Sifa nyingine, ya kitabu hiki yenye kuvutia ni kuwa kiko huru kabisa kutokana na uzushi na hadithi zilizobuniwa zilizozushwa na faida zilizofichwa. Kwa maneno mengine ni kwamba, kiko kabisa kwenye hali ya kusalia kwenye kiwango kihitajikacho cha ukweli wa kihistoria. Kwa kifupi ni kwamba, kinapelekwa kwa Waislamu kwa ujumla, bila ya upendeleo na kiburi.

Tunategemea ya kwamba kitabu hiki kitalifikia lengo lake la kukiongoza kizazi kichanga chenye shauku kuu ya kujipatia taarifa za kweli na zenye kutegemewa juu ya huyu Mtume Mkuu wa Uislamu (s.a.w.), na tunaamini ya kwamba vijana wetu wa kiislamu watajipatia mwongozo kutokana na kitabu hiki katika kuyatengeneza maisha yao kwa mujibu wa maamrisho ya Allah pamoja na sifa tukufu za Mtukufu Mtume (s.a.w.) na Dhuria wake Wateule (a.s.).

Neno La Mchapishaji

Kitabu kilichoko mikononi mwako ni tarjuma ya kitabu cha Kiingereza kiitwacho, The *Message,* kilichoandikwa na Sheikh Ja'far Subhani. Sisi tumekiita, *Ujumbe.* Kwa vile kitabu hiki ni kikubwa, tumekigawa katika juzuu nne ili kuwarahisishia wasomaji wetu kukisoma kwa makini katika kila sehemu. Hii uliyonayo mkononi ni Juzuu ya Tatu.

Kitabu hiki kilichoandikwa na mwanachuoni mkubwa Sheikh Ja'far Subhani kimekuwa ni miongoni mwa vitabu bora vilivyofanya utafiti wa kina kuhusu historia ya Uislamu na Waislamu.

Haya ni matokea ya utafiti wa kielimu pamoja na hoja zenye nguvu na utumiaji sahihi wa akili uliofanywa na mwanachuoni mwandishi wa kitabu hiki juu ya maudhui haya yaliyotaja hapo juu.

Kitabu hiki ni chenye manufaa sana, hususan wakati huu wa maendeleo makubwa ya elimu katika nyanja zote, ambapo uwongo, ngano za kale na upotoshaji wa historia ni mambo ambayo hayana nafasi tena katika akili za watu. Kutokana na ukweli huu, Taasisi yetu ya Al-Itrah Foundation imeamua kuchapisha kitabu hiki kwa lugha ya Kiswahili kwa madhumuni yake yaleyale ya kuwahudumia Waislamu, hususan wazungumzaji wa Kiswahili, ili kuongeza ujuzi wao katika masuala ya dini na ya kijamii.

Tunamshukuru ndugu yetu, Maalim Dhikiri Kiondo (Allah *'Azza wa Jalla* amkubalie amali zake na amweke karibu na Maasumina 14 [a.s.] – Amin) kwa kukubali jukumu hili la kukitarjumi kitabu hiki. Vilevile tunawashukuru wale wote walioshiriki kwa njia moja au nyingine hadi kufanikisha kuchapishwa kwa kitabu hiki.

Mchapishaji:
Al–Itrah Foundation
S. L. P. 19701
Dar–es–Salaam, Tanzania.

Sura Ya 33: Matukio Ya Mwaka Wa Tatu Na Wa Nne Hijiriya

Athari za kisiasa za kushindwa walizozipata Waislamu kwenye vita ya Uhud zilidhihirika kabisa mwishoni mwa vita vile. Ingawa walionyesha uthabiti mbele ya yule adui mwovu, na wakayazuia marejeo yake (mjini Madina), lakini baada ya tukio la Uhud fitina za ndani na za nje na kujaribu kupindua Uislamu viliongezeka.

Wanafiki na Wayahudi wa Madina na washirikina waishio nje ya mji pamoja na makabila yanayoabudu masanamu waishio mbali nao walipata shauku isiyo ya kawaida, nao hawakuacha kupanga makri na kukusanya askari na silaha dhidi ya Uislamu.

Mtume (s.a.w.w.) alizinyamazisha fitina za ndani kwa ustadi mkuu, na akakomesha kwa kuyapelekea vikosi yale makabila yaishio nje, yaliyotaka kuushambulia mji wa Madina. Wakati huo huo ilipokewa taarifa ya kwam– ba kabila la Bani Asad lilijaribu kuuteka mji wa Madina na kuwaua Waislamu na kuziteka nyara mali zao.

Upesi sana Mtume (s.a.w.w.) alipeleka kikosi cha askari 150 chini ya uongozi wa Abu Salman kwenye makao makuu ya wahaini. Alimwamrisha yule kamanda wa kikosi hiki alifiche lengo lake, asafiri kwa njia iliyopindapinda na kupumzika wakati wa mchana na kusafiri wakati wa usiku. Alifanya kama alivyoagizwa na Mtume (s.a.w.w.) na wakalizingira kabila la Bani Asad wakati wa usiku, wakaikomesha makri ile tangu mwanzoni kabisa, na wakarejea Madina wakiwa ni washindi wakiwa na ngawira za vita. Tukio hili lilitokea katika mwezi wa 35 wa Hijiriya.

Mpango Wa Kistadi Wa Kuwauwa Wahubiri

Mtume (s.a.w.w.) aliivuruga mipango ya wahaini kwa kupeleka vikosi, na akayavutia makabila adilifu kwenye Uislamu kwa kuvipeleka vikundi vya wahubiri kwenye makabila mbalimbali na vituo vya maeneo yenye watu wengi.

Wahubiri waliofunzwa na walioihifadhi Qur'ani Tukufu pamoja na amri na Hadith za Mtume (s.a.w.w.) walitayarishwa kwa moyo na nafsi kwenda kuwabalighishia mafunzo ya Uislamu wakazi wa yale maeneo ya mbali, kwa ufafanuzi na adabu njema, kwa gharama ya maisha yao wenyewe.

Kwa kuvipeleka vikosi vya kijeshi na vikundi vya wahubiri Mtume (s.a.w.w.) aliyatekeleza majukumu mawili makuu yahusianayo na cheo kikuu cha Utume. Kwa hakika lengo la kuvipeleka vikosi vya kijeshi lilikuwa ni kudumisha amani na kufutilia mbali hali ya hatari na vurugu ili kwamba lile kundi la wahubiri liweze kulitekeleza jukumu lake la kuzitawala nyoyo na kuziongoza fikara za watu kwenye hali ya hewa ya amani na uhuru.

Hata hivyo, baadhi ya makabila ya kishenzi na duni yalifanya udanganyifu dhidi ya lile kundi la wahubiri, lililokuwa la jeshi la kiroho la Uislamu na ambao hawakuwa na lengo lolote jingine ila maendeleo ya haki na uhuru na kuondoa ukafiri na ibada ya masanamu. Waliwauwa katika hali ya kuhuzunisha mno. Hapo chini tunatoa maelezo ya kile kilichotokea kwa baadhi ya hawa wahubiri wa Kiislamu waliofunzwa, ambao idadi yao kwa mujibu wa Ibn Hisham walikuwa sita, na kwa mujibu wa Ibn Sa'ad walikwua kumi.

Mauwaji Ya Kikatili Ya Wahubiri Wa Uislamu

Kikundi cha wawakilishi wa makabila yaliyokuwa yakiishi kwenye mae– neo ya jirani yalifanya udanganyifu ili kuidhoofisha nguvu ya Uislamu na kulipiza kisasi. Walimjia Mtume (s.a.w.w.) na kusema: "Ewe Mtume wa Allah! Nyoyo zetu zinauelekea Uislamu na mazingira yetu yako tayari kwa kuupokea. Ni muhimu kwamba uwatoe baadhi ya masahaba zako twende nao ili wakauhubiri Uislamu miongoni mwa kabila letu na kutufundisha Qur'ani Tukufu na kutueleza mambo yaliyohalalishwa na yaliyoharimishwa na Allah."1

Ulikuwa ni wajibu wa Mtume (s.a.w.w.) kulikubalia kundi hili la wawak– ilishi wa makabila makuu, na Waislamu wanao wajibu wa kuitumia fursa ya aina hiyo kwa vyovyote vile.
Hivyo Mtume (s.a.w.w.) aliamrisha kikundi cha wahubiri waende kwenye maeneo hayo chini ya uongozi wa Marsab, pamoja na wale wawakilishi wa yale makabila.

Kikundi hiki kilifuatana na wale wawakilishi wa yale makabila, waliutoka mji wa Madina na wakaenda hadi wakalitoka eneo lililoko chini ya mamlaka ya Waislamu hata wakafika mahali paitwapo Raji. Hapo wale wawakilishi wa yale makabila walionyesha nia yao mbaya na kwa msaada wa kabila moja lililoitwa Huzayl, waliamua kuwafunga na kuwaua wale watu waliotumwa na Mtume (s.a.w.w.). Wakati ule Waislamu wakiwa wamezungukwa pande zote na kikundi chenye silaha hawakuwa na njia yoyote ya

kujihami. Hawakuwa na chochote cha kufanya bila ya kufuta panga zao.

Hivyo basi, wakazifuta panga zao na wakawa tayari kujitetea. Hata hivyo, maadui zao waliapa kwamba hawakuwa na lengo lolote ila kwamba wawafunge ili kwamba wawapeleke kwa wakuu wa Waquraishi wakiwa hai na waweze kupata pesa, ikiwa ni zawadi yao.

Waislamu walitazamana na wakaamua kupigana. Hivyo, walijibu kwamba hawazitegemei ahadi za washirikina na waabudu masanamu, na kisha wakaamua kushika silaha na wakayatoa maisha yao kishujaa katika njia ya mahubiri na ulinzi wa Uislamu. Hata hivyo watu watatu, Zayd bin Dasinah, Khubayb Adiy na Taarah, walizichomeka silaha zao alani na wakajisalimisha. Walipokuwa njiani Taarah alijuta na akaona aibu kwa kujisalimisha kwake. Hivyo alifaulu kuutoa mkono wake kwenye nyororo, akaushika upanga mkononi mwake na kuanza kuwashambulia wale maadui. Wale maadui walianza kurudi nyuma na wakamfanya ashindwe kwa kumvurumishia mawe. Walimpiga mno mawe kiasi kwamba alianguka chini na akafariki dunia kutokana na majeraha. Alizikwa kwenye sehe– mu hiyo hiyo.

Hata hivyo, wale wafungwa wengine wawili walifikishwa kwa maafisa wa Kiquraishi wenye mamlaka nao kama fidia, wafungwa wawili wa kabila lile lililokuwa limewafunga wale waislamu waliachiwa huru.

Safwan bin Umayyah, ambaye baba yake aliuawa kwenye Vita vya Badr alimnunua Zayd ili alipize kisasi cha baba yake. Iliamuliwa kwamba Zayd anyongwe mbele ya mkutano mkuu wa watu. Miti ya kunyongea ikawek– wa mahali paitwapo Tan'im2

Waquraish na marafiki zao walikusanyika mahali hapo katika siku maalumu. Yule mtu aliyehukumiwa kunyongwa alisimama kandoni mwa ile miti ya kunyongea na dakika chache tu za uhai wake zilimbakia, wakati Abu Sufyan, aliyekuwa Firauni wa Makka na ambaye mkono wake ulikuwa ukifanya kazi nyuma ya pazia kwenye matukio yote haya alimgeukia Zayd na akasema: "Ninakutaka uniapie kwa jina la yule Mola unayemwamini kama unapenda kwamba Muhammad angaliuawa badala yako nawe ukaachiliwa huru na ukarudi nyumbani." Zayd alijibu kwa ushujaa akisema: "Sitaki japo kwamba mwiba uchome mguu wa Mtume, ingawa ningaliweza kuachiliwa kwa hilo." Jibu la Zayd lilikuwa na athari kubwa kwa Abu Sufyan. Alishangazwa na kujitolea kusiko kifani kwa masahaba wa Mtume (s.a.w.w.) na akasema: "Maishani mwangu mwote sijapata kuwaona marafiki wa mtu yeyote walio waaminifu na wenye kujitoa mhanga kama wale wa Muhammad!'

Mara tu baada ya hapo Zayd alinyongwa kwenye ile miti ya kunyongea na roho yake ikatoka kuuendea ulimwengu wa Akhera. Aliyatoa mhanga maisha yake kwa ajili ya Uislamu.

Yule mtu wa pili Khubayb aliwekwa kifungoni kwa muda fulani. Baadaye Halmashauri ya Makka iliamua kwamba yeye naye anyongwe pale Tan'im.3 Matayarisho yalifanywa kuiweka tayari ile miti ya kunyongea. Akiwa amesimama karibu na miti ile, Khubayl aliomba ruhusa kutoka kwa wale maafisa wenye mamlaka ili asali rakaa mbili. Baada ya kuruhusiwa alisali ile sala ya rakaa mbili kwa ushujaa mkubwa na kamilifu.

Kisha akarejea kwa wale machifu wa Waquraishi na kusema: “Kama isingalikuwa kwamba mnanifikiria kwamba nilikuwa nikukiogopa kifo, ningalisali zaidi[4] na ningalizirefusha rukuu na sujuud (kurukuu na kusujudu) za sala hizo.” Kisha aliuinua mbinguni uso wake na akasema: “Ee Allah! Tumefanya wajibu tuliyopewa na Mtume.” Ilitolewa amri na Khubay akanyongwa hadi akafa. Alipokuwa kwenye ile miti ya kunyongea alisema: “Ee Allah! Unaweza kuona kwamba hayupo hata rafiki mmoja karibu yangu awezaye kuzifikisha salamu zangu kwa Mtume. Ee Mola wangu! Nifikishie salam zangu kwake.” Itaweza kuonekana kwamba hisia za kidi– ni za mtu huyu mchamungu, zilimuudhi Abu Uqbah. Aliamka na kumwua kwa kumpiga pigo mwilini mwake.

Ibn Hishamu[5] amenakili ya kwamba Khubayb alizisoma beti fulani za shairi kabla ya kufa kwake pale kwenye ile miti ya kunyongea: “Ninaapa kwa jina la Allah. Kama nikifa hali ya kuwa ni Mwislamu, sitakuwa na wasiwasi wowote juu ya sehemu nitakayozikiwa. Kifo changu hiki chenye kuhuzunisha kimo kwenye njia ya Allah, na kama Akipenda anaweza kukifanya kifo hiki cha kishahidi kuwa heri kwa ajili ya kuvunjwa vunjwa kwa viungo vyangu.”

Tukio hili lenye kuupasua moyo lilimghadhibisha mno Mtume (s.a.w.w.) na kuliwafanya Waislamu wote washikwe na huzuni.

Hassan bin Thabit, mshairi mkuu wa Waislamu alizisoma beti za huzuni zilizonakiliwa na Ibn Hisham kwenye *Siirah* yake. Mtume (s.a.w.w.) alichelea kwamba tukio hili litarudiwa tena na kikundi cha wahubiri kilichofunzwa kwa taabu kubwa, kwa njia hii kinaweza kupata pigo lisilotengenezeka. Vile vile alichelea kwamba kikundi hiki kitakatifu kilichokuwa bora kilichokuwa kikipigana kwenye mstari wa mbele kinaweza kikakumbwa na makri za maadui wa Uislamu.

Maiti ya Khubayb ilibakia kwenye miti ile ya kunyongea kwa kipindi kirefu na kikundi cha watu kilikuwa kikiilinda. Hata hivyo, hatimaye kutokana na amri ya Mtume (s.a.w.w.) watu wawili mashujaa walikwenda usiku na wakaizika.[6]

Masaibu Ya Bi’r Ma’unah

Mwaka wa tatu Hijiriya, pamoja na matukio yake yote machungu na yenye mafunzo ulimalizika, na mwaka wa nne ukaanza kwa kuandama kwa mwezi wa Muharram. Kwenye mwezi wa Safar wa mwaka ule ule, Abu Baraa’a alikuja Madina na Mtume (s.a.w.w.) alimkaribisha asilimu. Hakulikubali hilo lakini vile vile hakutaka kujitenga.

Alimwambia Mtume (s.a.w.w.) kama ukiwapelekea watu wa Najd kikundi chenye nguvu cha wahubiri inaweza kutegemewa kwamba watasilimu kwa vile wao wanaelekea mno kwenye Uislamu.” Mtume (s.a.w.w.) akamjibu akasema: “Mimi nachelea udanganyifu na uadui wa watu wa Najd. Ninatambua kwamba mhanga wa Raji’, uliozaa kuuawa kwa idadi fulani ya watu waso– mi na wahubiri, unaweza kurudiwa.” Abu Baraa’a akasema:

“Hicho kikundi utakachokipeleka kitakuwa chini ya ulinzi wangu nami ninakuthibitishia kwamba mimi nitawahami kutokana na kila dhara.”

Waislamu arobaini walio wasomi waliohifadhi Qur’ani na mafunzo mbalimbali ya Uislamu walitoka kwenda Najd chini ya uongozi wa Munzir na wakaenda wakapiga kambi karibu na Bi’r Ma’unah. Mtume (s.a.w.w.) aliandika barua yenye kuwaita watu kwenye dini ya Uislamu kwa chifu mmoja wa Najd aliyeitwa Aamr. Sio tu kwamba Aamr hakuisoma barua ile bali vilevile aliwauwa wale watu waliokuja na barua ile. Vile vile aliomba msaada wa makabila jirani na lile eneo kilipopigia kambi kile kikundi cha wahubiri lilizungukwa na watu wake.
Wale watu waliounda kile kikundi cha wahubiri hawakuwa wahubiri wakuu na hodari tu, bali vile vile walikuwa wakifikiriwa kuwa mashujaa na watu wafaao kwa vita. Hivyo, walifikiria kwamba ni aibu kwao kujisalimisha. Hivyo walichukua silaha na wote, isipokuwa mmoja tu, walikufa kishahidi baada ya kupigana mapigano makali. Yule aliyebakia hai alikuwa Ka’ab bin Zayd ambaye alifika Madina akiwa na mwili uliojeruhiwa na akatoa taarifa za kile kilichotokea.7

Haya matukio mawili ya kimsiba yalikuwa matokeo maovu ya kule kushindwa kwa Waislamu pale Uhud, kulikoyashawishi makabila jirani kukimbilia kuwauwa Waislamu.

Tabia Ya Upendeleo Ya Mustashirik

Mustashirik wapendao kulikuza donda lililoko usoni mwa waabudu masanamu na kuutupia Uislamu na Waislamu masingizio ili kuthibitisha kwamba Uislamu ulienea kwa nguvu ya upanga, wameifunga midomo yao kuhusiana na hii misiba miwili na hawatamki japo neno moja juu ya misiba hii. Ni wapi ulimwenguni ambako wanachuoni na watu watakatifu wamekatwa panga? Kama Uislamu umestawi chini ya kivuli cha upanga, basi ni kwa nini wahubiri hawa wayatoe mhanga maisha yao?

Haya matukio mawili yana mambo makuu ya mafunzo fulani fulani. Nguvu ya imani, kujitolea mhanga, ushujaa na ujasiri wa roho hizi mashuhuri ndio msingi yalimosimamia mafanikio ya Waislamu. Inastahili wao kuvutiwa nayo na haina budi kuwa mfano kwa ajili yao.

Muumini Wa Kweli Kamwe Hang’atwi Kutokea Kwenye Tundu Lilelile

Matukio ya masaibu ya Raji’ na Bi’r Ma’unah yaliyoishilizia kwenye mauaji ya wahubiri wa Uislamu yaliwasikitisha mno Waislamu. Kufikia hapa bila shaka wengi wa wasomaji watapatwa na mwelekeo wa kuuliza ni kwa nini Mtume (s.a.w.w.) alikifanya kitendo hiki? Alipokuwa tayari kaishapatwa na tukio chungu la (Raji) ni kwa nini aliwapeleka wale watu arobaini kule Bi’r Ma’unah? Je, yeye Mtume (s.a.w.w.) mwenyewe hakusema: “Katu Muumini wa kweli hang’atwi mara mbili kutokea kwenye tundu lile lile?”

Jibu la swali hili hudhihirika tunapoyarejea maelezo ya kihistoria, kwa sababu usalama wa hiki kikundi cha pili ulihakikishwa na Abu Bara'a Aamr bin Malik bin Ja'afar, aliyekuwa chifu wa kabila la Bani Aamr, na kamwe kabila (la Kiarabu la zama zile) halikwenda kinyume na shabaha za chifu wake. Zaidi ya hapo, ili kutoa uhakikisho zaidi, yeye mwenyewe aliamua kubakia mjini Madina hadi kile kikundi cha wahubiri kirejee.

Mpango uliopangwa na Mtume (s.a.w.w.) ulikuwa sahihi na ulikuwa na uwezo wa kutoa matokeo. Ukweli uliopo ni kwamba wale watu wa kile kikundi hawakuuawa na watu wa kabila la Abu Bara'a. Hakuna shaka kwamba mwana wa nduguye, yaani Aamr bin Tufayl alilichochea kabila la Abu Bara'a dhidi ya kile kikundi cha wahubiuri lakini hakuna yeyote aliyemsikiliza na wote wakasema: "Ami yako amewathibitishia usalama wao." Hatimaye Aamr bin Tufayl alipata msaada kutoka kwenye makabila mengine kama vile Salim na Zakwaan na wakawauwa wale watu wa kikundi cha wahubiri wa Kiislamu.

Kile kikundi cha wahubiri wa Kiislamu kilipokuwa kikienda kwenye jimbo lile la Abu Bara'a, kiliwateuwa watu wawili kutoka miongoni mwao ambao ni 'Amr bin Umayyah na Hirith bin Simmah8 ili waweze kuwapeleka ngamia wao malishoni na kuwachunga. Watu hawa wawili walitekeleza jukumu lao walilolibeba, nao hawakuitambua hali ya baadae ya wale wenzao.
Mara kwa ghafla, Aamir bin Tufayl aliwaotea. Matokeo yake ni kwamba Harith bin Simah aliuwawa, na Amr bin Umayyah aliponyoka.

Alipokuwa njiani akirejea Madina Amr Bin Umayyah alikutana na watu wawili na alikuwa na uhakika kwamba walikuwa watu wa yale makabila ambayo watu wao walikiuwa kile kikundi cha wahubiri wa Kiislamu. hivyo basi, aliwauwa wote wawili walipokuwa wamelala na kisha akarejea Madina.

Amr alifanya uamuzi wenye makosa. Watu wale walikuwa wa kabila la Abu Bara'a (kabila la Bani Aamir) lililoiheshimu damu ya wahubiri wa Kiisilamu kutokana na ile heshima waliyo nayo kwa ajili ya chifu wao. Tukio hili nalo liliongeza ile huzuni ya Mtume (s.a.w.w.) na akaanza kuli– pa dia kwa ajili ya wale watu wawili.

---

1. Maghaazil Waaqidi, Juz. 1, uk. 354.
2. Tan'im ni mahali panapochukuliwa kuwa ndio mwanzo wa Haraam na mwishilizio wa 'Hil' na 'Ihraam' inavaliwa hapo kwa ajili ya 'Uimratul– Mufradah'
3. Waaqid anasema kwamba mateka wote wawili walinyongwa kwenye siku ile moja. (Mughaazi, Juz. 1, uk. 358).
4. Maghaazil Waaqidi, Juz. 1, uk. 359.
5. Siiratu Ibn Hisham, Juz. 2, uk. 170.
6. Safinatul Bihaar, Juz. 1, uk. 382.
7. Maghaazil Waaqidi, Juz. 1, uk. 349–364.
8. Kutegemeana na ilivyonukuliwa na Ibn Hisham kwenye Siira yake, Juz. 2, uk. 186, Mtu yule alikuwa ni Munzir bin Muhammad

Sura Ya 34: Wayahudi Wautoka Ukanda Wa Waislamu

Wanafiki na Wayahudi wa Madina walifurahi kutokana na kushindwa kwa kikundi hicho cha wahubiri. Walikuwa wakiisubiri fursa ya kujengea ghasia mle mjini Madina na kuyafanya makabila yaishiyo nje ya Madina kutambua kwamba haukuwapo umoja mle ili kwamba ile Dola changa ya Uislamu iweze kupinduliwa kwa njia ya mashambulizi ya maadui wa nje.

Ili kupata taarifa juu ya dhamira na fikira za Wayahudi wa kabila la Bani Nuzayr, Mtume (s.a.w.w.) alizitembelea ngome zao pamoja na masahaba zake, hata hivyo lengo hasa la Mtume (s.a.w.w.) kukutana na Bani Nuzayr lilikuwa ni kupata msaada wao katika kulipa dia ya wale watu wawili waliouwawa na 'Amr bin Umayyah, kwa kuwa kabila la Bani Nuzayr walikuwa wakiishi chini ya ulinzi wa Dola ya Kiislamu na ilikuwa sahihi tu kwamba kwenye tukio la aina hiyo, walilazimika kuichangia ile fidia iliyolazimika kulipwa.

Zaidi ya hapo, vile vile Wayahudi hawa walikuwa wamefanya mapatano baina yao kuwa daima watasaidiana kwenye matukio ya aina hiyo.

Mtume (s.a.w.w.) alishuka kutoka kwenye mnyama wake upande wa pili wa lango la kuwatembelea wale machifu wa kabila lile. Walimpokea kwa mikono miwili na wakaahidi kuchangia kwa ajili ya ile dia. Kisha walipokuwa wakizungumza na Mtume (s.a.w.w.) wakimtaja kwa jina la Abul Qaasim (babie Qassim) walimuomba aingie mle ngomeni na aitumie siku ile pamoja nao.

Hata hivyo, Mtume (s.a.w.w.) hakuliridhia ombi lao, na kulingana na ilivyonakiliwa na baadhi ya wanahistoria ni kuwa alishu- ka tu upande wa pili wa ngome na baada ya kukaa kwenye kivuli cha ukuta wa ngome ile pamoja na masahaba zake alianza kuzungumza na wale machifu wa Bani Nuzayr.1

Mtume (s.a.w.w.) alihisi ya kwamba mazungumzo yake mengi yaliandamana na matendo ya siri. Ulikuwepo mzunguko mkubwa wa watu kandokando mwa sehemu ile aliyokaa Mtume (s.a.w.w.). Walikuwa wakinong'onezana jambo lililojenga dhana kubwa ya kwamba mambo yalikuwa mabaya pale. Kwa kweli wale machifu wa Bani Nuzayr waliamua kumweka Mtume (s.a.w.w.) katika hali ya kutotambua. Wakimteuwa mmoja wa mtu wao aliyeitwa Amr Hajash kushuka kutoka kwenye paa na kumuuwa Mtume (s.a.w.w.) kwa kumtupia jiwe kubwa kichwani mwake.

Kwa bahati, mpango wao ule ulishindwa. Njama na mipango yao miovu vilifichuka kutokana na matendo yao, na kutegemeana na alivyonukuu Waaqidi, Mtume (s.a.w.w.) alitambua makri ile ya Wayahudi kupitia ufun- uo utokao kwa Allah. Aliitoka sehemu ile katika hali ambayo Wayahudi walifikiria kwamba alikuwa akienda kwa ajili ya kazi fulani na kwamba atarejea. Kwa kweli Mtume aliamua kwenda Madina moja kwa moja na hakuwaeleza hata wale masahaba zake juu ya uamuzi wake ule. Nao pia walibakia

wakimsubiri pale, lakini yote yakawa hewa, patupu.

Wayahudi wa kabila la Bani Nuzayr waliingiwa na wasiwasi sana. Walidhania ya kwamba huenda Mtume (s.a.w.w.) aliitambua ile makri yao, na hivyo basi atawaadhibu vikali, vile vile walidhania nafsini mwao kuwa: “Sasa kwa vile Mtume yuko mbali hatuwezi kumfikia, tunaweza kulipiza kisasi juu ya masahaba zake.” Lakini wazo likawapitia akili mwao upesi sana kwamba katika hali ile jambo lile litakuwa kubwa mno na bila shaka Mtume (s.a.w.w.) atalipiza kisasi dhidi yao.

Kufikia hapa, wale masahaba wa Mtume (s.a.w.w.) waliamua kumfuata na kupata kujua mahali alipo. Walikuwa bado hawajafika mbali sana kutoka kwenye ile ngome, walipokutana na mtu mmoja aliyewaambia kwamba Mtume (s.a.w.w.) alikuwa tayari kaishawasili Madina. Walimtembelea na wakaigundua ile makri ya Wayahudi ambayo vile vile ilithibitishwa na wahyi.2

Jinsi Ya Kulishughulikia Jinai Hili

Sasa wajibu wa Mtume (s.a.w.w.) ungalikuwa upi kuhusiana na kundi hili? Hawa walikuwa ni wale watu waliozifaidi fursa zilizoletwa na Dola ya Kiislamu na ambao mali zao na heshima zao vilikuwa vikilindwa na askari wa Kiislamu! Wao walikuwa ni jamii iliyozishuhudia dalili za dhahiri za Utume kwa Mtume (s.a.w.w.) na waliosoma vitabuni mwao juu ya uthibitisho wa Utume wake na ushahidi wa ukweli wake.

Ni ipi njia sahihi ya kulishughulikia hili kundi la watu ambao licha ya kunufaika kutokana na aina zote za faida, lakini walipanga makri dhidi yake (Mtume s.a.w.w) na wakaamua kumwua badala ya kuonyesha ukarimu? Haki ilitakaje kuhusiana na jambo hili? Na ilitakikana kutendekaje ili kwamba matukio ya aina hii yasirudiwe tena hapo baadae?

Njia ya kulitatulia tatizo hili ilikuwa ni ileile aliyoitumia Mtume (s.a.w.w.). Aliwaamrisha askari wote kukaa tayari tayari. Kisha alimwita Muhammad bin Maslamah, mtu wa kabila la Aws, na akamwamrisha kuwapelekea machifu wa Bani Nuzayr ujumbe wake upesi iwezekanavyo. Muhammad bin Maslamah aliwasiliana na wale machifu wa Bani Nuzayr na akawaambia:

“Yule kiongozi mtukufu wa Uislamu amekuleteeni ujumbe kupitia kwangu ya kwamba mtoke mahali hapa upesi iwezekanavyo, tena ndani ya siku kumi, kwa kuwa mmetenda udanganyifu, na kama hamtaondoka kwenye ukanda huu ndani ya siku kumi, damu yenu itamwagwa!”

Bani Nuzayr walisikitika walipoupata ujumbe ule na kila mtu alimchukulia mwenzie kuwa ndiye mwenye kuhusika na hali ile ya mambo. Mmoja wa viongozi wao alishauri ya kwamba wote wasilimu. Hata hivyo ushauri huu haukukubaliwa na wengi wa watu hawa walio wakaidi. Walijihisi kuwa kwenye hali ya kutokuwa na msaada. Hatimaye walimgeukia Muhammad bin Maslamah na kumwambia: “Ewe Muhammad! Wewe ni wa kabila la Aws na kabla ya kuwasili kwa huyu Mtume wa Uislamu, sisi tulikuwa na mapatano ya ulinzi na kabila lako. Sasa vipi wewe unakuwa kwenye hali ya kivita dhidi yetu?” Akilijibu swali hili alisema kwa ujasiri kamili uliompasa kila Mwislamu. “Wakati ule ulishapita. Siku hizi

nyoyo zimeshabadilika.”

Msingi wa lengo la Mtume (s.a.w.w.) ulikuwa ni yaleyale mapatano ambayo Waislamu waliyafanya baina yao na yale makabila ya Wayahudi kwenye siku za awali na yaliyosainiwa na Hay bin Akhtab kwa niaba ya Bani Nuzayr. Tayari tumeshatoa maelezo ya mapatano haya kwenye kurasa zilizotangulia na hapa tunanukuu sehemu ya maelezo hayo: “Mtume anafanya mapatano na kila moja ya yale makundi matatu (Bani Nuzayr, Bani Qaynaqaa na Bani Quraydha) kwamba hawatachukua hatua yoyote ile dhidi ya Mtume wa Allah na masahaba zake nao hawatamdhuru kwa mikono yao au ndimi zao. Na endapo lolote kati ya makabila haya litakwenda kinyume na mapatano haya, Mtume atakuwa huru kuimwaga damu yao, kuzinyakua mali zao na kuwateka wanawake na watoto wao.”

Machozi Ya Mamba

Kufikia hapa, vilevile mustashirik wameyatiririsha machozi ya mamba kwa kuwahurumia Wayahudi wadanganyifu, walioyageuka mapatano na wakasema kwamba kitendo cha Mtume (s.a.w.w.) hakikuafikiana na usawa na uadilifu. Huo ni udanganyifu na ulalamishi hafifu uliofanywa na hawa mustashirik ulikuwa ni kwa ajili ya kuuficha ukweli, kwa sababu rejea za maelezo ya mapatano zaonyesha kwamba ile adhabu aliyoitoa Mtume (s.a.w.w.) ilikuwa nyepesi mno kuliko ile iliyoelezwa kwenye ule mkataba wao.

Siku hizi mamia ya majinai na mateso hutokea kwenye nchi za Mashariki na za Magharibi mikononi mwa mabwana hawa mustashirik na hakuna yeyote miongoni mwao awakanushaye, japo kidogo tu. Hata hivyo, Mtume wa Uislamu (s.a.w.w.) anapoliadhibu kundi la wapanga makri japo kwa adhabu iliyo ndogo kuliko ile iliyokubaliwa hapo awali, baadhi ya waan- dishi wanaolichanganua tukio lile kwa nia zao mbalimbali za kibinfsi, hupiga makelele dhidi ya tukio lile.

Nafasi Ya Wanafiki

Maadui na hatari zaidi wa Uislamu walikuwa ni kikundi cha wanafiki waliokuwa wakivalia kinyago cha urafiki nyusoni mwao na Abdullah bin Ubayy na Malik bin Ubayy Nawfal n.k. walikuwa ndio viongozi wao.

Upesi upesi waliwapelekea machifu wa Bani Nuzayr ujumbe usemao kwamba wao (wanafiki) watawasaidia askari mashujaa elfu mbili na marafiki zao, yaani makabila ya Bani Quraydha na Ghatfan vile vile nayo hayatawaacha peke yao. Hii ahadi ya uwongo iliwashawishi Wayahudi, na ingawa hapo awali waliamua kujisalimisha na kutoka mahali pale, sasa wakaubadili uamuzi wao.

Waliyafunga malango ya ngome zao, na baada ya kujikusanyia silaha wakaona kuwa wataweza kujihami kwa gharama zozote zile kutoka kwenye minara ya ngome zile nao hawataliruhusu jeshi la Uislamu kuchukua utawala wa bustani na mashamba yao.

Mmoja wa viongozi wa Bani Nuzayr (Salaam bin Mushkam) aliifikiria ahadi ya Abdullah kuwa isiyo kuwa na maana, na akasema: “Ni bora kwetu kutoka mjini humu.” Hata hivyo, Hay bin Akhtab aliwashauri wabakie kuwa thabiti na madhubuti.

Mtume (s.a.w.w.) aliutambua ule ujumbe uliopelekwa na Abdullah akiwapelekea wale Wayahudi. Alimteua Ibn Ummi Makhtum kuwa naibu wake mle mjini Madina na kwa *Takbir* (Allah Yu Mkubwa) kinywani mwake alikwenda kuizingira ngome ya Bani Nuzayr. Alilifanya eneo la baina ya Bani Quraydha na Bani Nuzayr kuwa kambi yake na kwa kufanya hivyo aliyakata mawasiliano baina ya yale makabila mawili.

Kufuatana na kauli ya Ibn Hisham3 ngome ile ilizingirwa kwa mchana mmoja na usiku mmoja, na kwa mujibu wa baadhi ya waandishi, ilizingirwa kwa muda wa siku kumi na tano. Hata hivyo, wale Wayahudi wakawa madhubuti zaidi na thabiti. Mtume (s.a.w.w.) aliamrisha ya kwamba mitende iliyoizunguka ngome ile ikatwe ili kwamba ile sababu iwafanyayo wale Wayahudi waitamani sana nchi ile iondoke kabisa. Katika hali hii, vilio vya Wayahudi vilikuwa vikubwa mno kutoka mle ngomeni na wote wakasema: “Ewe Abul Qaasim! Daima umekuwa ukiwakataza askari wako kuikata miti! Basi, kwa nini sasa unalitenda jambo hili?” Hata hivyo sababu ya kufanya hivi ni kama tulivyoeleza hapo juu.

Hatimaye Wayahudi walisalimu amri na wakasema: “Tuko tayari kuwa wakimbizi, ili mradi tu turuhusiwe kuvichukua vitu vyetu.” Mtume (s.a.w.w.) alikubali kwamba wangaliweza kuvichukua vitu vyao ila silaha ambazo ni lazima wazisalimishe kwa Waislamu.

Wayahudi hawa waliojawa na choyo walijitahidi kwa kadiri ya uwezo wao wote kuzichukua mali zao, kiasi kwamba waliing’oa milango ya nyumba zao, ili waichukue na kisha wabomoe majengo. Baadhi yao walikwenda Khaybar na wengine wakaenda Shamu. Wawili miongoni mwao walisil– imu.

Ili kuficha kufunika kushindwa kwao wale Wayahudi walioshindwa na wasio na msaada wowote ule sasa, waliutoka mji wa Madina wakiwa wanapiga ngoma na kuimba nyimbo. Hivyo basi, walitaka kutoa dhana ya kwamba hawakuwa wenye huzuni hata kidogo kuitoka sehemu ile.

Mashamba Ya Bani Nuzayr Ya Gawanywa Miongoni Mwa Muhajiriin.

Kwa mujibu wa Qur’ani Tukufu (*Surat Al–Hashr*, 59:6) ngawira waipatayo Waislamu bila ya kupigana ni mali ya Mtume (s.a.w.w.) na anaweza kuitumia kwa ajili ya ustawi wa Uislamu na Waislamu kufuatana na aonavyo kuwa inafaa. Mtume (s.a.w.w.) aliona kuwa inafaa kuyagawa mashamba hayo, marambo ya maji na bustani (vitu vilivyoachwa na Bani Nuzayr) miongoni mwa Muhajiriin, kwa sababu tangu kuhamia kwao kutoka Makka walikuwa masikini, na kwa kweli walikuwa wakiwategemea Ansar wa Madina nao walikuwa wageni wao.

Sa’ad bin Mu’aaz na Saad bin Ubadah nao waliyaunga mkono maoni haya. Hivyo basi, mali yote

iligawanywa miongoni mwa Muhajiriin na hakuna yeyote miongoni mwa Ansar aliyepata fungu lolote lile, ila Sahl bin Hunayf na Abu Dujanah, waliokuwa masikini zaidi. Kwa njia hii hali ya kiuchumi ya Waislamu ilitengenezeka kwa ujumla. Upanga wa bei ya juu ambao hapo awali ulikuwa mali ya mmoja wa machifu wa Bani Nuzayr, alipewa Sa'ad bin Mu'aaz.

Tukio hili lilitokea kwenye mwezi wa Rabi'ul Awwal (Mfunguo sita) wa mwaka wa nne hijiriya wakati *Surat Al–Hashr* nayo ilipofunuliwa ili kuzitaja sababu za tukio hili na kuiibua tahadhari ya Waislamu. Wengi wa wanahistoria wa Kiislamu wanaamini ya kwamba hakuna umwagaji damu uliotokea kwenye tukio hili. Hata hivyo, marehemu Shaykh Mufid4 anasema kwamba katika usiku wa kutekwa kwa ngome hii mapigano madogo yalitokea na Wayahudi kumi waliuawa na vifo vyao vilitoa msingi wa kusalimu amri kwa majeshi ya Wayahudi.

---

1. Maghaazil anasema kwamba Mtume (s.a.w.w.) alifika kwenye mkutano wao (Juz. 1, uk. 364).
2. Maghaazil– Waaqidi, juz. 1, uk. 305.
3. Siiratu Ibn Hisham, juz. 2, uk. 191.
4. Al –Irshaad, uk. 47–48.

Sura Ya 35: Matukio Ya Mwaka Wa Nne Hijiriya Kuharimishwa Kwa Pombe

Mvinyo na vinywaji vyenye kulevya kwa ujumla vimekuwa, na bado ni moja ya misiba yenye kuharibu jamii ya mwanadamu, na inatosha kusema kuwa, kwa ajili ya kuikemea hii sumu yenye kuua, kwamba inapigana vita dhidi ya neema ya mwanaadamu iliyo kuu zaidi inayomuainisha yeye na viumbe vingine vyenye uhai yaani akili na busara. Ustawi wa mwanaadamu unategemea hekima zake, na tafauti iliyopo baina yake na viumbe vingine vyenye uhai ni kutokana na uwezo wake wa kiakili, na pombe inatambulikana kuwa ni adui mkuu wa hekima na akili. Ni kutokana na sababu hii kwamba Mitume wote wa Allah wameharamisha matumizi ya pombe. Kusema kweli vitu hivi vimetangazwa kuwa ni hara– mu kwenye dini zote zilizofunuliwa.

Kwenye Rasi ya Uarabuni, ulevi ulikuwako kama ilivyokuwa misiba ya ujumla, ambayo kampeni thabiti dhidi yao ilihitaji muda mrefu mno, na hali ya mambo iliyokuwapo kwenye jamii ile na hali ya Waarabu kwa ujumla, nayo haikuruhusu kwamba Mtume (s.a.w.w.) aitangaze kuwa ni haramu kabla ya kuchukua hatua za awali. Vile vile alilazimika kuuta– yarisha mwenendo wa jamii ili ufae katika kukipiga vita kitendo hiki.

Hivyo basi, zile Aya nne zilizofunuliwa kuonyesha kuchukiza kwa pombe hazifanani. Mtume (s.a.w.w.)

alianza kwa ushauri hadi alipofaulu kuy- atangaza matumizi yake kuwa ni haramu. Kuchunguza Aya hizi kwa makini hutufahamisha njia aliyoitumia Mtume (s.a.w.w.) kuhusu uhubiri wa sheria za Uislamu, na inafaa kwamba waandishi na wazungumzaji stadi hawana budi kuifuata njia hii ya ufundishaji na wafanye kampeni dhidi ya maovu ya kijamii kwa njia hii hii.

Sharti muhimu kwa kufanya kampeni dhidi ya kitendo kiovu katika hatua ya kwanza ni kuziamsha fikira za jamii na kuuibua usikivu wa nyoyo zao kuhusu hasara zake na athari zake zilizo mbaya. Haiwezekani kufanya kampeni dhidi ya kitendo kiovu mpaka kwanza upate kuwapo tayari kwa kiroho na uamsho wa nafsi kwenye jamii, na watu wenyewe wawe na wajibu juu ya jambo lile, vinginevyo itakuwa haiwezikani kufanya kampeini dhidi ya kitendo kiovu.

Hivyo basi, mara ya kwanza kabisa Qur'ani Tukufu iliiambia jamii, sehemu ambayo maisha yao yalikuwa ni ya ulevi, kwamba kutengeneza pombe kutokana na tende na zabibu kulikuwa kinyume na lishe nzuri, na aina hii ya mazungumzo kwa hakika ilikuwa onyo la kuziamsha fikira za watu. Inasema: **"Na katika matunda ya mitende na mizabibu mnatengeneza ulevi na riziki nzuri. Hakika katika hayo mna mazingatio kwa watu wanaotumia akili."** (***Surah al-Nahl,*** **16:67**).

Kwa mara ya kwanza hiki Kitabu kitakatifu kilitamka kwamba kuten- geneza pombe kwa vitu hivi sio 'lishe nzuri' hasa. 'Lishe nzuri' ina maana ya kwamba inapasa kuliwa ikiwa kwenye hali yake ya asilia.

Aya hii iliwatia watu mshituko akilini mwao na kuufanya mwenendo wao kuwa tayari ili Mtume (s.a.w.w.) aweze kuifanya kauli yake kuwa na nguvu zaidi na kwa kupitia Aya nyingine aweze kutangaza kwamba 'baadhi ya matumizi ya vitu' yatokanavyo na (mapato ya) pombe na kamari ni vitu visivyo na maana, vinapolinganishwa na athari zake mbaya. Ukweli huu umetajwa kwenye Aya hii:
"Wanakuuliza kuhusu ulevi na kamari. Waambie: Katika hayo mna uovu mkubwa na manufaa (kidogo) kwa watu; na uovu wake ni mkubwa zaidi kuliko manufaa yake..." (*Surat al-Baqarah*; 2:219).

Hakuna shaka kwamba ulinganisho huu baina ya faida na hasara, uonye- shao kwamba kitu fulani kina madhara zaidi kuliko manufaa, unatosha kuwafanya watu wenye kuitumia akili kuonyesha kuchukizwa kwao na pombe. Hata hivyo, watu wote kwa ujumla hawaliepuki tendo baya isipokuwa kama likipigwa marufuku kabisa.

Ingawa ni kweli kwamba aya tuliyoinukuu hapo juu ilikuwa tayari ime- shafunuliwa, Abdur Rahman bin Awf alitayarisha karamu na kisha akagawa pombe kwenye kitambaa chake cha chakula. Wale waliokuwapo pale karamuni wakaanza kusali baada ya kunywa pombe. Mmoja wao aliisoma Aya fulani kwa makosa na kuibadili maana yake, yaani badala ya kusema: "Enyi waabudu masanamu! Mimi sikiabudu kile mkiabuducho" aliitamka sentensi yenye maana iliyo kinyume na hivyo, kwa kuliacha neno 'laa' (si) kutoka kwenye Aya ile.

Matukio haya yaliufanya mwenendo wa watu kuwa tayari, kwani hali iliruhusu ulevi kukatazwe, kwa uchechefu kwenye hali fulani fulani maalumu.

Kutokana na masharti haya, ilitangazwa dhahiri kwamba hakuna Mwislamu aliyekuwa na haki ya kusali awapo kwenye hali ya ulevi na amri hii ya Allah ilitangazwa kwa maneno haya: **“Enyi mlioamini! Msikaribie swala hali ya kuwa mmelewa mpaka myajue mnayoyasema…”**
(*Surah al-Nisa*, 4:43)[1]

Athari ya Aya hii ilikuwa kwamba kikundi cha watu fulani kiliacha kabisa kulewa, na hoja yao katika kufanya hivyo ilikuwa kwamba kitu chenye madhara katika sala chapasika kuachwa kabisa. Hata hivyo, wengine hawakuiacha tabia hii hata kidogo kiasi kwamba mtu mmoja kutoka mion- goni mwa Ansar alitayarisha karamu na ukiachilia mbali ukweli uliopo kwamba mtu yule alikuwa akiitambua Aya ile, aliandaa pombe pia kwenye kitambaa cha chakula.
Wale wageni baada ya kunywa pombe, walianza kugombana wakajeruhiana. Baada ya hapo walilalamika mbele ya Mtume (s.a.w.w.). Khalifa wa Pili, aliyekuwa na desturi ya kulewa pombe hadi wakati ule, akiwa na dhana ya kwamba Aya zilizotajwa hapo juu hazikuharimisha kabisa ulevi wa pombe, aliinua mikono yake alipokuwa kwenye sala na akasema: “Ewe Allah! Tufunulie amri iliyodhahiri na yenye kusadikisha.”

Ni dhahiri kwamba matukio haya yasiyopendeza yaliitayarisha hali ya hewa kuwa tayari kwa jambo hili kwamba kama matumizi ya pombe yakipigwa marufuku kabisa, Waislamu wote wangeliikubali marufuku hii kwa moyo mmoja. Hivyo basi, katika hatua ya mwisho, Aya hii ilifunuliwa: **“Enyi mlioamini! Hakika pombe na kamari na kupiga ramli ni uchafu wa kazi ya shetani, basi jiepusheni nayo ili mpate kufaulu.” (*Suratul-Ma'idah*, 5:90).**

Matokeo ya amri hii fasaha na yenye kusisitiza ni kwamba wale watu waliokuwa wakinywa pombe hadi wakati ule kwa udhuru wa kwamba amri ihusianayo na kuiacha pombe haikukamilika, sasa nao walijiepusha nayo, Khalifa wa pili alipoisikia Aya hii alisema: “Ninaikana (pombe) tangu sasa na kuendelea.”[2]

Vita (Ghazwah) Vya Dha Atur Riqaa

Katika lugha ya Kiarabu, neno ‘Riqaa’ lina maana ya ‘kiraka’. Hii jihadi takatifu inaitwa ‘Dhaatur Riqaa’ kwa sababu kwenye uwanja huu wa mapambano Waislamu walifika kwenye mlolongo wa sehemu zilizoinuka na za chini ambao ulionekana na viraka. Kufuatana na masimulizi mengine, iliitwa ‘Dhaatur Riqaa’ kwa sababu askari walifunga matambara miguuni mwao ili kupunguza taabu za kutembea.

Kwa vyovyote vile iwavyo, vita hivi havikuwa kampeni ya lazima hasa kwamba jeshi la Uislamu liangukie kwenye jamii kwa sababu ya kuwa kwao washirikina. Bali kusema kweli lengo lao lilikuwa ni kuizima cheche iliyokuwa karibuni kuwaka, yaani kuikomesha shauku iliyoonyeshwa na watu wa familia mbili za Ghatfan (Bani Mah?rib na Bani Sa’lahab) dhidi ya Uislamu.

Ilikuwa ni desturi ya Mtume (s.a.w.w.) kuwapeleka watu wenye busara na hekima kwenye sehemu mbalimbali ili waweze kumwarifu kuhusu hali ya ujumla ya sehemu zile. Kwa ghafla ilipokewa taarifa ya

kwamba familia mbili tulizozitaja hapo juu zilikuwa zikikusanya silaha na watu ili kuja kuiteka Madina. Mtume (s.a.w.w.) alikwenda Najd akifuatana na kikosi maalumu na akapiga kambi karibu na nchi ya maadui wale. Kumbukumbu nzuri ya siku za awali za jeshi la Uislamu na kujitolea kwao mhanga na ujasiri, vitu vilivyoishangaza Rasi ya Uarabuni viliwafanya maadui kurudi nyuma na kukimbilia milimani na sehemu za juu bila ya kupigana.

Hata hivyo, kwa kuwa Mtume (s.a.w.w.) alikuwa akisali sala za wajibu kwenye vita vile pamoja na askari wa jeshi la Uislamu kama *Salat–i Khawf* (sala ya hofu) na aliwafundisha Waislamu jinsi ya kuisali kwa njia ya Aya ya 103 ya *Suratun–Nisa*, basi inaweza kudhaniwa kwamba majeshi ya maadui yalikuwa na silaha za kutosha na kwamba mapigano yaliichukua hali iliyo nyeti mno, lakini hatimaye Waislamu walishinda.

Walinzi Wavumilivu

Ingawa kwenye vita hivi jeshi la Waislamu lilirejea kutoka kwenye makao makuu ya adui na kuja Madina bila ya mapigano, walijipatia ngawira ndogo. Wakiwa njiani wakati wa kurejea, wakati wa usiku walikaa kwenye bonde pana ili wapumzike. Wakiwa hapo Mtume (s.a.w.w.) aliwateuwa askari wawili mashujaa ili wailinde njia iingiayo kwenye bonde lile.

Askari hawa wawili walioitwa ‘Abbad na ‘Ammar waliyagawa masaa ya usiku ule baina yao na walikubaliana kwamba ‘Abbad ailinde njia ile katika nusu ya kwanza ya usiku ule.

Mtu mmoja wa kabila la Ghatfan alikuwa akiwafuatilia Waislamu ili awadhuru na kisha arejee kwao upesi sana. Mtu huyu alijinufaisha kutokana na giza la usiku na akampiga mshale yule mtu aliyekuwa akilinda lile bonde wakati mlinzi yule akiwa anasali. Yule mlinzi alijishughulisha mno na du’a kiasi kwamba hakuyahisi mno maumivu yaliyosababishwa na ule mshale. Aliung’oa ule mshale kutoka mguuni mwake na akaendelea na du’a zake.

Hata hivyo, mashambulizi yale yalirudiwa kwa mara ya pili na ya tatu. Mshale wa mwisho wa adui yule uliufunua mguu wake vikali mno kiasi kwamba hakuweza kuendelea na du’a zake kama alivyotaka. Hivyo akazikomesha du’a zake upesi sana na kisha akamwamsha ‘Ammaar.

Hali ya kuhuzunisha ya Abbad ilimsikitisha mno Ammaar na akasema kwa njia ya malalamiko: “Kwa nini hukuniamsha tangu mwanzoni?” Yule mlinzi aliyejeruhiwa akajibu akasema: “Nilikuwa nikisali na nilikuwa nikisoma Sura ya Qur’ani Tukufu wakati mshale wa kwanza uliponichoma kwa ghafla. Ule utamu wa du’a na utamu wa utambuzi wa Allah Mwenye nguvu zote ulinizuia kuivunja sala yangu. Kama Mtume (s.a.w.w.) asingaliniwajibisha kuilinda sehemu hii katu nisingaliivunja sala yangu na ile Sura niliyokuwa nikiisoma. Na ningeliyatoa maisha yangu kwa Allah kabla ya kudhamiria kuivunja sala yangu.”3

Badri Ya Pili

Mwishoni mwa vita vya Uhud Abu Sufyan alitangaza akisema: “Mwaka ujao tutakutana nanyi kwenye jangwa la Badr kwenye wakati huu huu nasi tutalipiza kisasi vikali mno juu yenu.

Kwa amri ya Mtume (s.a.w.w.) Waislamu wakatangaza kuwako kwao tayari kupigana. Muda wa mwaka uliowekwa ulipita naye Abu Sufyan ambaye wakati ule alikuwa mtawala wa Waquraishi, alihusika na matatizo mbalimbali. Na’im bin Mas’ud aliyekuwa na uhusiano wa kirafiki na pande zote mbili (Waislamu na Waquraishi) aliwasili mjini Makka. Abu Sufyan alimwomba arejee Madina upesi na amshawishi Muhammad asia– mue kutoka mjini Madina.

Aliongeza kusema hivi: “Haiwezekani kwetu sisi kutoka mjini Makka mwaka huu, na maonyesho na mbinu za kivita alizozionyesha Muhammad pale Badr, ambapo ni eneo la soko la Waarabu, yatasababisha kushindwa kwetu.”

Dhamira yoyote ile aliyoweza kuwa nayo, Na’im alirejea Madina. Hata hivyo, maneno yake hayakuwa na athahri yoyote katika malengo ya Mtume (s.a.w.w.). Alipiga kambi pale Badr mwanzoni mwa mwezi wa *Dhil Qaadul Haraam* akiwa na askari wapiganaji 1500, na kiasi cha farasi na kiasi cha bidhaa, na akakaa hapo kwa kiasi cha siku nane zilizokwenda sawa na siku ya soko la mwaka la Waarabu, Waislamu waliziuza bidhaa zao hapo na kupata faida kubwa. Baada ya hapo watu waliokuja kutoka sehemu mbalimbali walitawanyika, lakini lile jeshi la Waislamu liliendelea kusubiri kuwasili kwa jeshi la Waquraishi.

Taarifa zilifika Makka kwamba Muhammad amefika Badr. Machifu wa Waquraishi hawakuwa na lolote jingine la kufanya kwa kujiokoa kutokana na fedheha ile isipokuwa watoke Makka na kwenda Badr. Abu Sufyan aliyekuwa na silaha za kutosha, alikuja hadi Maruz Zahraan, lakini alirejea baada ya kufika katikati ya njia akitoa udhuru wa njaa na vifo. Kurejea kwa jeshi la waabudu masanamu kulishtusha mno kiasi kwamba Safwan alimlalamikia Abu Sufyan na kusema: “Kwa kurudi nyuma huku, tumeshaipoteza heshima yote tuliyoipata, na kama isingalikuwa umeahidi pale mwaka jana kupigana vita basi tusingalikabiliwa na huku kushindwa kwa kisaikolojia.”4

---

1. Rejea kwenye Sunan Abi Daudi, Juzuu 2, uk. 128.
2. Mustadrak, juz. 4, uk. 143. na Ruhul Ma’aani, juz. 7, uk. 15.
3. Siiratu Ibn Hisham, juz. 2, uk. 208–209.
4. Kufuatana na ilivyoandikwa kwenye Mughaazi–i Waqidi, Juz. 1, uk. 484, tukio hili lilitokea kwenye mwezi wa 45 wa Hijiriya.

Sura Ya 36: Matukio Ya Mwaka Wa Tano Hijiriya

Matukio ya kihistoria ya mwaka wa tano hijiriya yaliyo muhimu zaidi ni Vita vya Ahzaab, hadith ya Bani Quraydha na ndoa ya Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) na Bibi Zaynab bint Jahasha. Kufuatana na kauli ya wanahistoria, tukio la kwamza kutokea lilikuwa ni ile ndoa ya Mtume (s.a.w.w.) na Bibi Zaynab.

Qur'ani Tukufu imeihadithia hadith tuliyoitaja hapo juu kwenye Aya ya 4, 5, 36, 37 na 40 ya Sura al-Ahzaab (Sura ya 33) na haikuacha nafasi yoyote kwa uzushi wa uwongo wa mustashirik na waandishi wa hadithi za kubuni. Tutajifunza tukio hili kutoka kwenye maandishi yakubalikayo (yaani Qur'ani Tukufu) na vilevile tuta chunguza maelezo ya mustashirik kwa makini kabisa.

Zayd Bin Harith Alikuwa Ni Nani?

Zayd alikuwa ni mtu aliyetekwa wakati wa utotoni mwake kutoka kwenye msafara. Alitekwa na wanyang'anyi wa kibedui na akauzwa utumwani kwenye soko la Ukaz. Alinunuliwa na Hakim bin Hizaam kwa ajili ya shangazi yake Bibi Khadija, na Bibi huyu akampa Mtume (s.a.w.w.) kijana huyu akiwa ni zawadi, baada ya ndoa yao.

Zayd alikuwa na mapenzi makubwa mno na ule mtazamo halisi wa kiroho, hisia tukufu na tabia njema za Mtume (s.a.w.w.) kiasi kwamba, baada ya kupita kiasi fulani cha muda baba yake alikuja mjini Makka na kumwom- ba Mtume (s.a.w.w.) kumpa ungwana, ili amrejeshe kwa mama yake na watu wengine wa familia yake. Zayd alikataa kwenda na akapendelea kukaa na Mtume (s.a.w.w.). Baba yake Zayd alimpa Mtume (s.a.w.w.) mamlaka kamili ya ima Zayd abakie naye au amrejeshe makwao.

Hiki kiungo cha kiroho na hizi hisia zake za ndani zaidi kilikuwamo kwenye pande zote mbili. Kama Zayd alizipenda mno tabia za Mtume (s.a.w.w.), Mtume naye vile vile alimpenda mno Zayd kiasi kwamba alim- chagua kuwa mwanawe na watu wakaanza kumwita Zayd bin Muhammad badala ya Zayd bin Harith. Kulifanya jambo hili kuwa rasmi kama ilivyokuwa desturi ya Waarabu wa zama zile, siku moja Mtume (s.a.w.w.) aliushika mkono wa Zayd na akawaambia Waquraishi: "Huyu ni mwanangu, nasi tunarithiana." Uhusiano huu wa wema uliendelea kuwapo hadi Zayd alipofariki dunia kwenye Vita vya Mu'ta na Mtume (s.a.w.w.) alisiki- tishwa mno na jambo hili kana kwamba alimpoteza mwanawe wa kumzaa.1

Zayd Amwoa Binamu (Binti Wa Shangazi) Yake Mtume (S.A.W.W)

Moja ya malengo matakatifu ya Mtume (s.a.w.w.) lilikuwa ni kupunguza ubaguzi wa matabaka ndani ya jamii na kuwaleta pamoja wanadamu wote chini ya bendera ya ubinadamu na uchamungu, na kuweka ubora wa tabia na sifa bora za kihulka kuwa ndio kipimo cha ubora na heshima. Hivyo basi, ilikuwa ni

jambo muhimu kwamba azing'oe upesi iwezekanavyo zile desturi mbaya za Waarabu wa kale za kwamba mabinti wa watu watukufu wasiolewe na watu maskini.

Hivyo hakuna lililoweza kuwa bora zaidi ya mpango huu kuliko kuanzia kwenye familia yake mwenyewe na amwoze binamu yake Zainab mjukuu wa Abdul Muttalib kwa mtumwa wake wa zamani, ambaye tangu muda mrefu uliopita alikuwa keshapewa ungwana, ili watu watambue kwamba hivi vizuizi vya kufikiriwa tu havina budi kuondolewa upesi iwezekanavyo. Na vile vile watambue ya kwamba Mtume (s.a.w.w.) anaposema: "Kipimo cha ubora wa mtu ni uchamungu na mwanamke wa Kiislamu yu sawa na mwanaume wa Kiislamu" yeye mwenyewe alikuwa mtu wa kwanza kabisa kuitekeleza sheria hii na wa kwanza kuifanyia kazi. Ili kuing'oa desturi hii isiyo sahihi alikwenda nyumbani kwa Bibi Zaynab, yeye mwenyewe na kumwomba aolewe na Zayd.

Hapo awali yeye na kaka yake hawakuelekea kuikubali posa ile, kwa sababu fikara za siku za ujinga zilikuwa bado hazijafutika kutoka akilini mwao.

Hivyo, ingawa hili lilikuwa ni jukumu lisilopendeza, kwao wao kukataa kuitii amri ya Mtume (s.a.w.w.) walitoa udhuru wa Zayd kuwa mtumwa hapo kale.

Mara tu baadae ufunuo wa Allah ulikilaumu kitendo cha Zaynab na kaka yake kwa maneno haya: "Haiwi kwa mwanaume aliyeamini wala mwanamke aliyeamini Mwenyezi Mungu na Mtume Wake wanapokata shauri, wawe na hiari katika shauri lao. Na Mwenye kumwasi Mwenyezi Mungu na Mtume Wake, hakika amepotea upotovu ulio wazi." (*Surat al Ahzaab*, 33:36).

Haraka sana Mtume (s.a.w.w.) aliwasomea Aya hii. Itikadi safi na kamili ya Bibi Zaynab na kaka yake Abdullah juu ya Mtume (s.a.w.w.) na tabia zake tukufu ilikuwa zana katika kukubali kwa yule binti Jahash tena bila ya kukawia, na matokeo yake ni kwamba yule mwanamke wa kizazi kitukufu aliolewa na mtumwa wa Mtume Muhammad (s.a.w.w.) aliyepewa uungwana. Hivyo basi, kwa njia hii, sehemu ya mpango wa Uislamu wenye kuimarisha jamii ulitimizwa na ile desturi isiyo sahihi iliondolewa kivitendo.

Zayd Atengana Na Mkewe

Hatimaye, kwa sababu fulani fulani ndoa hii iliishia kwenye talaka. Baadhi ya watu wanasema kwamba sababu ya mtengano huu ilikuwa ni fikira za mkewe Zayd, kwa kuwa alikuwa akiutaja uduni wa nasaba ya mumewe mbele yake na kujifaharisha mwenyewe kutokana na umaarufu wa familia yake na kwa kufanya hivyo akayafanya maisha ya Zayd kuwa machungu.

Hata hivyo, inawezekana kwamba Zayd mwenyewe alihusika na talaka ile, kwa sababu kumbukumbu za maisha yake zaonyesha kwamba alikuwa akiishi maisha ya kujitenga, kwa kuwa alioa wake wengi na kisha akawataliki wote (ila yule wa mwisho aliyekuwa bado yu hai wakati alipouawa kwenye vita), na talaka hizi za mfuatano zaonyesha kwamba Zayd alikuwa na moyo usiopenda kuishi na jamii.

Ushahidi wa pili juu ya maoni ya kwamba Zayd alikuwa na fungu kwenye tukio hili ni ile tabia ya ukali

ambayo Mtume (s.a.w.w.) alimkanya nayo. Kwa sababu Mtume (s.a.w.w.) alipotambua ya kwamba Zayd ameamua kumwacha mkewe, aliudhika na akasema: 'Kaa na mkeo na ichelee ghadhabu ya Allah." Endapo kama kosa lilikuwa la mkewe hasa, kutengana kwa Zayd na yeye, hakukuwa kinyume na uchamungu na uadilifu. Hatimaye Zayd alitengana na Zaynab.

Ndoa Kwa Ajili Ya Kukomesha Desturi Nyingine Mbaya

Kabla hatujaitazama sababu ya msingi ya ndoa hii, ni muhimu kuzingatia wajibu wa nasaba ambayo ni kipengele muhimu mno kwa jamii iliyoimarika. Ikubalike kwamba uhusiano kama ule wa baba kwa mwana una msingi endelevu na kwa kweli baba yu chanzo cha kimaada cha uzazi wa mtoto na mtoto yu mrithi wa sifa za kimwili na kiakili za wazazi. Kutokana na umoja huu na damu moja, baba na mwana wanarithiana mali, na sheria makhususi zinazohusu ndoa na talaka zinakuwa ni zenye kutekelezeka kwa ajili yao.

Hivyo basi, uhusiano ambao una misingi ya kinasaba, hauwezi kuanzish– wa kwa maneno, (tazama aya 4 na ya 5 ya *Surah Al–Ahzaab*) na mtoto wa kulea wa mtu hawezi kuwa mtoto halisi wa mtu huyo mleaji (kama alivyo mtoto wa kuzaa). Hivyo basi, amri mbalimbali zihusianazo na mirathi, ndoa, talaka n.k. kama zitumikavyo kwa mtoto wa kuzaa, haziwezi kutumika kwa mtoto wa kulea. Kwa mfano, ingawa mtoto wa kuzaa anamrithi baba yake, na baba anamrithi mwanawe wa kuzaa, na ingawa ni haramu kwa mtu kumwoa mke aliyetalikiwa na mwanawe wa kuzaa, hata kidogo haiwezi kusemwa kwamba mtoto wa kulea vilevile anayo haki hiyo kwenye mambo haya kama alivyo huyu mtoto wa kuzaa. Bila shaka nyoro– ro ya haki hizi, zaidi ya kukosa msingi sahihi vile vile huwa aina fulani ya kichekesho kuhusiana na kisababisho kilicho muhimu (nasaba) kwenye jamii madhubuti.
Katika hali hiyo, kama ulezi wa watoto ukifanyika kwa lengo la kuzidhihirisha hisia tu hiyo inakubalika sana na ni sahihi, lakini kama itapendekezwa ili kumshirikisha mtoto wa kulea na sheria mbalimbali za kijamii ambazo zote huanzia kwenye mambo ya husikanayo na damu, basi kitendo hiki kitakuwa mbali kutoka kwenye mipaka ya kijamii.

Jamii ya kiarabu ilimchukulia mtoto wa kulea kuwa ni bora kama alivyo mtoto wa kuzaa. Kwa hiyo, Mtume (s.a.w.w.) alijulishwa ili kuifutilia mbali desturi hii isiyo sahihi kwa kumwoa Bibi Zaynab, ambaye hapo awali alikuwa mke wa mwanawe wa kulea (Zayd), na hivyo kuweza kuing'oa kivitendo tabia hii isiyofaa kutoka miongoni mwa Waarabu, kwa sababu njia hii ni yenye kufaa zaidi kuliko kuitangaza tu sheria.

Ndoa hii haikuwa na sababu yoyote nyingine zaidi ya hii, kwa sababu kwenye siku hizo hakuna aliyeweza kuwa na moyo wa kuichukua hatua hii, kwa sababu ya ukweli uliopo kwamba ilidhaniwa kuwa ni kitendo cha aibu kwa mtu kumwoa mwanamke ambaye hapo awali alikuwa mke wa mwanawe wa kulea. Hivyo basi, Allah Mwenye nguvu zote hapo awali alimjulisha Mtume (s.a.w.w.) kulitimiza jukumu hili. Anasema:" . . .**Basi Zayd alipokwisha haja naye tulikuoza wewe ili isiwe taabu kwa waumini kuwaoa wake wa watoto wao wa kulea wanapomaliza haja nao, na amri ya Mwenyezi Mungu ni**

yenye kutekelezwa.” (*Surah al-Ahzaab*, 33:37).

Tunafikiria kwamba ndoa hii ukiachilia mbali kule kuifuta desturi isiyo sahihi, vile vile imedhihirisha mno usawa, kwa sababu Mtume (s.a.w.w.) alimwoa mwanamke ambaye hapo awali alikuwa mke wa mtumwa wake aliyepewa uungwana, na katika siku hizo ndoa ya aina hiyo vilevile ili- fikiriwa kuwa kijamii si yenye utukufu.

Hatua hii ya kishujaa ya Mtume (s.a.w.w.) ilileta maneno ya lawama kuto- ka kwa wanafiki na watu wasioona mbali nao wakawa wakizieneza habari: “Muhammad amemwoa mke wa mwanawe wa kulea!”

Ili kuzivunja fikara za aina hii, Allah Mwenye nguvu zote Aliteremsha Aya hii: “Muhammad si baba wa yeyote miongoni mwa wanaume wenu, bali ni Mtume wa Allah na hitimisho la Manabii, na Mwenyezi Mungu ni Mjuzi wa kila kitu.” (*Surah al-Ahzaab*, 33:40).

Qur’ani Tukufu haikutosheka na hilo tu. Allah alimsifu Mtume Wake (s.a.w.w.) aliyeonyesha ujasiri na ushujaa mwingi katika kuzitekeleza amri Zake, yaani Aya ya 38 na ya 39 ya *Surat al-Ahzaab*. Kiini cha Aya mbili hizi ni hiki: “**Muhammad ni kama walivyo Manabii wengine ambao waliowapelekea watu ujumbe wa Allah, naye hamwogopi yeyote yule katika kuzitekeleza amri Zake**”2

Hii ndio falsafa ya ndoa ya Mtume Muhammad (s.a.w.w.) na Bibi Zaynab. Sasa tutayachunguza kwa makini maoni ya mustashirik juu ya jambo hili.

Hadithi Ya Kuzusha Juu Ya Bibi Zaynab Ni Uwongo Mtupu

Ndoa ya Mtume (s.a.w.w.) na bibi Zaynab ni jambo la kawaida lililo huru kutokana na aina zote za utata. Hata hivyo, kwa vile baadhi ya wataalamu wa nchi za Mashariki wamelifanya tukio hili kuwa sababu ya kuwapotosha watu wapumbavu na wajinga, na kwa njia hii wamejaribu kuidhoofisha imani ya wale wasiokuwa na taarifa sahihi juu ya tabia ya Mtume (s.a.w.w.), inaonekana kuwa ni lazima kwamba tuyachunguze maelezo ya kundi hili la wataalamu wa mambo ya nchi za Mashariki na kuyafanya mambo kuwa ya dhahiri.

Kama ielewekavyo, wakoloni hawaitumii nguvu yao ya kijeshi na kiuchu- mi tu katika kuzitawala nchi za Mashariki, lakini wakati mwingine huingia kwa kupitia mlango wa elimu na utafiti, na kwa njia ya mipango iliyopangwa kwa uangalifu wanajaribu kuiweka aina mbaya zaidi ya ukoloni (yaani ukoloni wa kiakili) juu ya watu hawa.

Kusema kweli, mustashirik ni yule mkoloni wa kujieneza atendaye mambo katika njia maalum kwenye nyoyo za jamii na miongoni mwa watu wenye elimu na kuyafikia malengo yake ya kikoloni kwa kuzipumbaza akili za tabaka la wenye elimu.

Inawezekana kwamba wengi wa waandishi wa Magharibi na wapenzi wa elimu na hekima wasikubaliane na maelezo tuliyoyeleza hapo juu na kutulaumu kwa ugumu wa ushupavu wa moyo katika dini bila ya

kutumia akili, na wakafikiria ya kwamba kiburi cha kitaifa au cha kidini kimetufanya tuyatoe maoni haya. Hata hivyo, maandishi ya mustashirik na kuuficha kwao ukweli na tabia yao ya upendeleo kwenye mambo yahusianayo na historia ya Uislamu ni ushahidi wa dhahiri na ukweli uliopo kwamba, wengi wao hawakusukumwa na kiu ya elimu na kuutafuta ukweli na hivyo maandishi yao yamechafuliwa na mlolongo wa fikira zisizo za kidini wala za kitaifa.3

Jambo tunalolijadili hapa linaudhihirisha ukweli huu. Kwa dhana maalumu na ya kipekee ya watu wa Magharibi, wameipa ndoa hii lengo pekee la ambalo lilikuwa ni kufuta desturi potovu, wameipaka ndoa hii rangi ya 'mapenzi', na wakaizushia kisa kama vile wafanyavyo waandishi wa hadithi za paukwa pakawa na wasimuliaji wa hekaya, wakakihusisha na mtu aliye mtakatifu zaidi wa ulimwengu wa mwanadamu.

Kwa vyovyote vile, misingi ya ngano hizi ni zile sentensi zilizonakiliwa na Tabari4 na Ibn Athir5 na baadhi ya wafasiri wa Qur'ani kwamba, siku moja Mtume (s.a.w.w.) alibahatika kumwona Bibi Zaynab mkewe Zayd.

Zayd akahisi kwamba Mtume ameangukia kumpenda Bibi Zaynab. Kutokana na heshima ya Zayd iliyokithiri juu ya Mtume (s.a.w.w.) alikuja mbele yake na kupendekeza kumtaliki Bibi Zaynab, ili kisiwepo kizuizi kwa Mtume (s.a.w.w.) kumwoa. Mtume (s.a.w.w.) alimkataza kumtaliki mkewe kwa kurudia rudia, lakini hatimaye alimtaliki na Mtume akamwoa.

Hata hivyo, mustashirik badala ya kuchunguza historia sahihi, hawaku- tosheka hata na ngano hii ya kuzushwa tu na wameipamba mno kiasi kwamba imejitwalia umbo la hadith za '*Alfu laila u-lela*,'.

Bila shaka watu wale wanaozifahamu tabia bora zaidi za Mtume (s.a.w.w.) wameichukulia hadith ya asilia na yale mapambo yaliyotiwa humo kuwa ni uzushi na ngano halisi na wazo lililo batili kwa kuwa haiafikiani na kipimo chenye kuyahusu maisha ya Mtume (s.a.waw). Aidha, wanachuoni kama vile Fakhrur-Razi na Aahisi, wameipinga hadithi hii waziwazi na wamesema kwamba imezushwa na maadui wa Uislamu na ikaenezwa miongoni mwa waandishi wa Kiislamu.6

Yawezaje kusemwa kwamba sehemu hii ya kihistoria iliaminiwa na Tabari7 na Ibn Athir ambapo dazeni ya waandishi wamenukuu kinyume chake na kumchukulia Mtume wa Uislamu (s.a.w.w.) kuwa safi kabisa kutokana na kila aina ya uchafu.

Hata hivyo, tungalipenda kutaja kwenye kurasa hizi dalili na ishara za hadithi hii kuwa ni nyenye kughushiwa na kuidhihirisha hali hiyo kabisa kiasi cha kutohitaji maelezo ya kuihami zaidi. Ufuatao hapa chini ndio ushahidi wetu:

Hadithi iliyotajwa hapo juu ni kinyume na kauli ikubaliwayo katika Uislamu na Waislamu wenyewe, kwa sababu kama ilivyoshuhudiwa kati- ka Aya ya 37 ya Sura *al-Ahzaab*, ndoa ya Mtume (s.a.w.w.) na Bibi Zaynab ni kuipinga fikara ya Waarabu isiyo sahihi, kwamba mtu hakuruhusiwa kumwoa mtalaka au mjane wa mwanawe wa kumlea, na ndoa hii ilifanyika kwa Amri ya Allah na wala haikuwa matokeo ya

huba na mahaba.

Katika siku za awali za Uislamu hakuna yeyote aliyeupinga ukweli huu, na kama yale maelezo ya Qur'ani yangalipingana na ukweli, basi Wayahudi, Wakristo na Wanafiki mara moja wangalisimama na kuyalaumu na wangalilalamika, ambapo kwa kweli hawakuweza kulithibitisha jambo lolote lililo baya, ingawa daima walikuwa na shauku kubwa ya kupata makosa ya Mtume (s.a.w.w.).

Bibi Zaynab alikuwa ni mwanamke yule ambaye kabla ya kuolewea kwake na Zayd alipenda aolewe na Mtume (s.a.w.w.). Hata hivyo, ingawa alikuwa na mwelekeo huo, Mtume (s.a.w.w.) alisisitiza ya kwamba aolewe na yule mtumwa wake aliyempa uungwana, yaani Zayd. Kama kweli Mtume (s.a.w.w.) alipenda kumwoa hapakuwapo na kizuizi chochote katika kufanya hivyo. Basi ni kwa nini asimwoe? Kinyume na hivyo tunaona kwamba ingawa ulikuwako mwelekeo wote huo aliouona toka upande wa Bibi Zaynab, sio tu kwamba hakumpa jibu la kukubali, bali alimshauri aolewe na mtu mwingine.

Hivyo wakati maoni yao yanapokanushwa na historia, huwa hakuna nafasi ya yale mapambo yaliyotiwa na wanachuoni wa kikoloni. Na sisi tunayaamini maisha ya Mtume (s.a.w.w.) aliyeutumia muda wake hadi ikafikia miaka hamsini akiwa na mwanamke aliyekuwa mtu mzima kuliko yeye kwa miaka kumi na saba kuwa ni safi kabisa na bora kiasi cha kutoweza kuuthibitisha ukweli wa maelezo ya upinzani juu yake. Hivyo basi, sisi tunaacha kunukuu hapa maelezo ya hao Mustashirik.

Maelezo Ya Sehemu Mbili Za Aya Hiyo

Ili kukamilisha majadiliano haya tunatoa hapa chini Aya iliyoteremshwa juu ya jambo hili, pamoja na sehemu zake mbili, ambazo ndio sababu ya kusitasita na kuwa na mashaka miongoni mwa baadhi ya watu wasio na elimu ya kutosha, na kisha tutatoa maelezo yao. Yafuatayo ni maneno ya Aya hiyo: **"Na ulipomwambia yule ambaye Allah amemneemesha na wewe (nawe) umemneemesha: Shikamana na mkeo na umche Allah . . ." (*Sura al-Ahzaab*, 33:37).**

Hakuna fumbo lolote kwenye sehemu hii ya Aya lakini sehemu mbili zifuatazo zinahitaji ufafanuzi. "**Na ukaficha nafsini mwako aliyotaka Allah kuyatoa**." Hapa swali huibuka: Mtume (s.a.w.w.) alikuwa akificha nini pale alipokuwa akimshauri Zayd, ambacho Allah Alitaka kukidhihirisha? Inawezekana kudhania kwamba kile Mtume (s.a.w.w.) alichokuwa akikifanya nafsini kilikuwa kwamba, ingawa alikuwa akimkataza Zayd kumta- liki mkewe, lakini yeye alipendelea ya kwamba amtaliki Bibi Zaynab ili yeye amwoe.

Hitimisho kama hili haliwezi kuwa sahihi kwa sababu yoyote ile, kwa kuwa kama kwa siri Mtume (s.a.w.w.) alikuwa akifikiria hivyo, kwa nini Allah asiutaje ukweli huu kwa kuzipitia Aya nyingine wakati Yeye mwenyewe Allah anasema sehemu hii kwamba: Chochote kile akifichacho, Allah atakidhihirisha? Hivyo basi, wafasiri wetu wakuu wa Qur'ani tukufu wanasema kwamba maana ya kile kitu alichokificha ni ule ufunuo alioteremshiwa na Allah.

Ili kueleza dhahiri; Allah alimfunulia ya kwamba Zayd atamtaliki mkewe, naye Mtume (s.a.w.w.) atamwoa ili kuipinga ile dhana isiyo sahihi (ya kwamba ni haramu kwa mtu kumwoa mwanamke aliyekuwa kaolewa na mwanawe wa kulea). Hivyo basi, alipokuwa akimshauri Zayd ufunuo huu ulikuwa anao akilini mwake lakini aliufanya siri kwa Zayd na wengineo. Hata hivyo, kwenye hiyo aya tuliyoitaja hapo juu, Allah anamwambia Mtume (s.a.w.w.) kwamba, Yeye atayadhihirisha yale aliyonayo akilini mwake. Yaliyoelezwa hapo juu yanaungwa mkono na ukweli uliopo kwamba chini ya Aya hiyo hiyo Qur'ani tukufu inalitaja jambo hili kwa maneno haya:

وَإِذْ تَقُولُ لِلَّذِي أَنْعَمَ اللَّهُ عَلَيْهِ وَأَنْعَمْتَ عَلَيْهِ أَمْسِكْ عَلَيْكَ زَوْجَكَ وَاتَّقِ اللَّهَ وَتُخْفِي فِي نَفْسِكَ مَا اللَّهُ مُبْدِيهِ وَتَخْشَى النَّاسَ وَاللَّهُ أَحَقُّ أَنْ تَخْشَاهُ ۖ فَلَمَّا قَضَىٰ زَيْدٌ مِنْهَا وَطَرًا زَوَّجْنَاكَهَا لِكَيْ لَا يَكُونَ عَلَى الْمُؤْمِنِينَ حَرَجٌ فِي أَزْوَاجِ أَدْعِيَائِهِمْ إِذَا قَضَوْا مِنْهُنَّ وَطَرًا ۚ وَكَانَ أَمْرُ اللَّهِ مَفْعُولًا {37}

"Basi Zayd alipokwisha haja naye tulikuoza wewe ili isiwe taabu kwa waumini kuwaoa wake wa watoto wao wa kulea wanapomaliza haja nao, na amri ya Mwenyezi Mungu ni yenye kutekelezwa." **(*Surah al- Ahzaab, 33:37*).**

Kutoka kwenye sehemu hii ya Aya tuliyoinukuu hapo juu tunajifunza ya kwamba alichokuwa akikificha Mtume (s.a.w.w.) kilikuwa ni ule Ufunuo wa Alllah kwamba ili kuifutilia mbali desturi isiyo sahihi hana budi kum- woa mke wa mwanawe wa kulea yule mwanawe atakapomtaliki mke yule.

". . . . . Na ukawachelea watu, hali Allah ndiye Mwenye haki zaidi ya kumchelea; . . " Kifungu hiki ni sehemu ya pili isiyo na utata zaidi inapolinganishwa na ile ya kwanza, kwa sababu ili kuikomesha desturi iliyokuwapo kwenye mazingira yaliyochafuliwa kwa miaka kadhaa au zaidi, (yaani ndoa ya mwanamke ambaye hapo mwanzo aliolewa na mwana wa kulea) kwa kawaida kuliandamana na ugumu wa kiakili ambao uliondolewa kwenye moyo wa Mtume (s.a.w.w.) kwa mazingatio ya amri za Allah. Kama Mtume (s.a.w.w.) alihisi wasiwasi au alikuwa akihofia, ni kwa sababu alikuwa akifikiria kwamba Waarabu, waliojitenga naye, kutokana na ujinga na mawazo machafu watasema: 'Mtume amelichagua jambo la aibu,' ingawa kwa kweli, si aibu kitu.

---

1. Rejea kwenye Usudul Ghabah; Al-Isti'aab na al-Isabaah chini ya neno Zayd.
2. Maelezo ya hizi Aya mbili ni haya: "Si kosa kwa Nabii katika yale ambayo Mwenyezi Mungu amemlazimisha, ndiyo kawaida ya Mwenyezi Mungu kwa wale waliopita zamani, na amri ya Mwenyezi Mungu ni kipimo kilichokadiriwa. Wale wanaofikisha ujumbe wa Mwenyezi Mungu na kumwogopa Yeye wala hawamwogopi yeyote isipokuwa Mwenyezi Mungu, na Mwenyezi Mungu ndiye atoshaye kuhesabu." (Surah al-Ahzaab, 33:38-39).
3. Kwa maelezo zaidi rejea kitabu 'al-Mustashriqun'
4. Tarikhut-Tabari, Juz. 2.
5. Tarikhul Kamil, Juz. 2, uk.121.

6. Mafaatil Ghayb Razi, Juz. 15, na Ruhul Ma'aani, sura ya 22, uk. 23–24.
7. Tunasikitika kusema kuwa mwanahistoria huyu wa kale amechangia sehemu kubwa kuwapa mustashrik fursa ya kumkejeli na kumshusha daraja Mtume (s.a.w.w.), hiyo ni kutokana na kitabu chake cha historia kilicho muhimu katika ulimwengu wa Kisuni kujaa ngano na uzushi usiovumilika. Ikimbukwe hata kadhia hizi za hivi punde za waandishi wa Denmaki kumchora Mtume kikatuni ni matunda ya waandishi kama hawa. Mwanahistoria huyu ndiye chimbuko la wazo la kuwepo kwa Abdallah bin Saba, mtu wa kufikirika aliyefanywa chambo cha kuwatusi na kuwadhalilisha na kuwatuhumu waisilamu halisi – Mhariri.

Sura Ya 37: Vita Vya Ahzaab

Katika vita hivi majeshi ya Waarabu waabudu masanamu na Wayahudi walikusanyika dhidi ya Uislamu na, baada ya kuunda ushirikiano wa kijeshi wenye nguvu, waliuzingira mji wa Madina kwa kipindi cha mwezi mmoja hivi. Kwa kuwa makabila na makundi mbalimbali yalishiriki kwenye vita hivi na kwa kuwa Waislamu walichimba handaki kuuzunguka mji wa Madina, ili kumzuia adui asiingiye humo, vita hivi viliitwa vita vya Ahzaab, yaani vita vya makundi. Vile vile vinaitwa Vita vya Khandaq, yaani vita vya handaki.

Wale waliochochea vita hivi walikuwa ni viongozi wa kabila la kiyahudi la Bani Nuzayr na vile vile kundi la Bani Waail. Lile pigo kali walilolipata wale Wayahudi wa Bani Nuzayr kutoka kwa Waislamu na jinsi walivyoutoka mji wa Madina kwa kulazimishwa na wakaenda kuishi Khaybar, viliwafanya wapange mpango madhubuti kwa ajili ya kuupindua msingi wa Uislamu. Na kwa kweli, walipanga mpango wa hatari mno na wakawakabili Waislamu pamoja na makabila mbalimbali. Tukio hili halikuwa na kifani kwenye historia ya Waarabu.

Mpango wao ulikuwa kwamba viongozi wa kabila la Bani Nuzayr, kama vile Salam bin Abil Haqiq na Hay bin Akhtab walifika Makka pamoja na baadhi ya watu wa kabila la Waa'il na baada ya kuwasiliana na machifu wa Waquraishi, aliwaambia: "Muhammad amekufanyeni ninyi na sisi kuwa shabaha zake na amewalazimisha Wayahudi wa Bani Qaynuqa' na Bani Nuzayr kuitoka nchi yao. Ninyi Waquraishi hamna budi kuamka na kuomba msaada kutoka kwa marafiki zenu nasi tunao wapiganaji wa panga wa kiyahudi mia saba (Bani Quraydha) watakaojitokeza upesiupesi kukusaidi– eni. Wayahudi wa Bani Quraydha wamefanya kwa dhahiri mapatano ya kiulinzi na Muhammad lakini tutawashauri kuyatupilia mbali mapatano yale na kujiunga nanyi".1

Machifu wa Waquraishi walionyesha ukweli wao na kuchoka kupigana na Waislamu, lakini majigambo ya hawa watu wawili yaliwavutia na wakaukubali mpango wao. Hata hivyo, kabla ya kuthibitisha kukubali kwao, waliwauliza wale viongozi wa Wayahudi hivi:
"Ninyi ni watu wa Kitabu na muwafuasi wa Vitabu vilivyofunuliwa nanyi mnao uwezo wa kutosha wa kubainisha baina ya haki na batili, Mnatambua ya kwamba hatuna tofauti yoyote na Muhammad ila kwa

sababu ya dini yake tu iliyotofauti na yetu. Sasa, hebu tafadhalini tuelezeni ukweli, ni ipi kati ya dini hizi mbili ambayo ni bora, dini yetu au ni ile yake iliyosimamia kwenye msingi wa Allah Aliye Mmoja tu na kuyavunja masanamu na kuyabomoa mahekalu ya masanamu?"

Hebu tuone ni jibu gani watu hawa waliojifikiria kwamba ni wenye kuliunga mkono fundisho la Upweke wa Allah na washika bendera wa itikadi ya Upweke wa Mungu walilowapa wale watu wa kundi la wajinga na wasio na walimu, waliwatambua kuwa wao ni watu walioelimika na kuliweka tatizo lao mbele yao.

Bila ya aibu waliwajibu hivi: "Ibada ya masanamu ni bora kuliko dini ya Muhammad. Hamna budi kubakia imara kwenye dini yenu na msionyeshe mwelekeo japo ulio mdogo sana kwenye dini yake." 2

Hili lilikuwa ni doa la aibu mno kuhusiana na tabia za wayahudi, waliofanya uso wa historia ya dini ya Kiyahudi ambao tayari ulikuwa umeshafanywa kuwa mweusi na kuwa mweusi zaidi. Kosa lao hili lilikuwa lisilosameheka kabisa kiasi kwamba waandishi wa Kiyahudi walizidhihirisha huzuni zao nyingi juu ya jambo hili. Dakta Israeli anaandika kwenye kitabu chake kiitwacho *History of the Jews and Arabia* (Historia ya Wayahudi na Waarabu), hivi: "Haikuwa sahihi kwamba Wayahudi watende kosa la aina hii japo Waquraishi wangalikataa maombi yao. Aidha, haikuwa sahihi hata kidogo vilevile kwamba waombe ulinzi wa waabudu masanamu, kwa sababu kufanya hivyo hakuafikiani na mafundisho ya Taurati."3

Kusema kweli hii ndio sera ya wanasiasa wa siku hizi waliojitwalia ili kuyafikia malengo na madhumuni yao. Kwa nguvu sana wanaamini kwamba ili mtu kufikia lengo lake lazima atumie njia zote zinazokubalika na zisizokubalika, na kwa kweli kwa mujibu wa fikra zao kufanikiwa kwa lengo hufanya vitu visivyo kubalika kukubalika kwao. Qur'ani Tukufu inasema hivi:

"Je, huwaoni wale waliopewa fungu katika Kitabu, wanaamini sanamu na shetani, na wakiwasema wale waliokufuru kuwa; Wao wameongoka zaidi katika njia kuliko walioamini." (*Sura al–Nisa*, 4:51).

Maneno ya watu hawa waitwao wanachuoni yaliwavutia wenye kuyaabudu masananu. Kwa hiyo, wakaonesha kukubaliana kwao na ule mpango wao na vilevile wakaweka muda wa kwenda Madina.

Watu wale ambao waliokuwa na shauku ya kuanzisha vita walitoka mji wa Makka huku nyoyo zao zikiwa zimefurahi sana, na kwanza wakaenda Najd kuonana na watu wa kabila la Ghatfaan waliokuwa maadui wakuu wa Uislamu. Mbali ya kabila la Ghatfaan, koo za Bani Fazalah, Bani Murrah na Bani Asja walilikubali ombi lao chini ya sharti ya kwamba, baada ya kupata ushindi wapewe mapato ya mwaka mmoja ya Khaibar. Hata hivyo, jambo hili halikukomea hapo, kwa sababu Waquraishi waliwasiliana na marafiki zao Bani Asad na kuwaomba wajiunge na ushirika huu wa kivita. Bani Salim na Bani Asad walilikubali ombi hilo na katika siku iliyowekwa makabila yote haya yalitoka sehemu mbalimbali za Uarabuni ili kuuzingi– ra na kuuteka mji wa Madina. 4

Idara Ya Upelelezi Ya Waislamu

Kuanzia siku ile Mtume (s.a.w.w.) alipotulia mjini Madina, daima alikuwa akituma watu wajanja kwenye sehemu mbalimbali ili wapate kumwarifu kuhusu hali iliyokuwapo kwenye sehemu zile pamoja na matendo ya watu waliokiishi kwenye sehemu za nje za eneo la Waislamu. Wale watoa habari walimwarifu ya kwamba ushirikiano wa kijeshi ulio na nguvu mno umeundwa dhidi ya Uislamu na watu wale wangaliweza kuja kuuzingira mji wa Madina kwenye siku maalum. Upesi sana Mtume (s.a.w.w.) aliiarifu halmashauri ya ushauriano ili iweze kufanya uamuzi, wakiyazingatia matokeo machungu ya Vita vya Uhud.
Baadhi ya watu walipendelea kuji- hami kwa ndani ya ngome na kupigana kutoka kwenye minara na sehemu za juu badala ya kwenda nje ya mji kumkabili adui. Hata hivyo mpango huu haukutosheleza, kwa sababu kundi kubwa la mashujaa wa Uarabuni lenye maelfu ya askari, lingaliweza kuzibomoa zile ngome na minara na kuwazidi nguvu Waislamu. Hivyo basi lilikuwa jambo muhimu kuchukua hatua za kuthibitisha kwamba adui hafaulu kufikia mji wa Madina.

Salman Farsi, aliyekuwa na ujuzi kamili wa mbinu za kivita za Wairani akasema: “Huko Iran watu wanapotishiwa kushambuliwa na maadui, wanachimba handaki lenye kina kirefu kuuzunguka mji na kwa kufanya hivyo wakaweza kuwazuia maadui kuuingia mji ule.

Hivyo basi, ingelifaa kuzihami sehemu zile za Mji wa Madina ambazo zaweza kushambuliwa kwa urahisi kwa kuzichimbia handaki na kuweza kumzuia adui kwa njia hiyo kwenye maeneo hayo.

Sambamba na handaki hilo ijengwe minara na vibanda vya kungojea zamu kwenye kingo za handaki hilo kwa ajili ya ulinzi na maadui wazuiwe wasilipite handaki hilo kwa kuwatupia mishale na kuwavurumishia mawe kutoka kwenye minara na hizo ngome.”5

Ushauri alioutoa Salman ulikubaliwa na watu wengi na mpango huu wa ulinzi ulisaidia sana katika usalama wa Waislamu. Mtume (s.a.w.w.) akifuatana na baadhi ya watu, alizikagua sehemu zote zilizo rahisi kushambuli- wa na akaziwekea alama zile sehemu zilizohitaji kuchimbwa handaki.

Iliamuliwa kwamba lichimbwe handaki tangu Uhud hadi Ratij, na ili kudumisha utaratibu mwema kila watu kumi walipewa dhiraa arobaini. Mtume (s.a.w.w.) mwenyewe alipiga sururu ya kwanza kabisa ardhini na kuchim- ba, wakati Sayyidna Ali (a.s.) akijishughulisha na kuutupa udongo nje ya handaki lile. Uso na paji la uso la Mtume (s.a.w.w.) lilikuwa likitoka jasho, na alikuwa akisema: “Maisha ya kweli ni maisha ya Akhera. Ee Allah! Waghufirie Muhajiriin na Ansar!”

Kwa kujishughulisha kwake na kazi hii, Mtume (s.a.w.w.) alionyesha sehemu ya mpango wa Uislamu na kuifanya jamii ya Kiislamu kuelewa kwamba kamanda wa jeshi na kiongozi wa jamii hanabudi kuzivumilia taabu kama wengine na kuwaondolea watu mzigo wao. Kazi ya Mtume (s.a.w.w.) ilizaa shauku isiyo kifani miongoni mwa Waislamu wote, bila ya kusalia yeyote yule, walianza kufanya kazi mno kiasi kwamba Wayahudi waliofanya mapatano na Waislamu nao walitoa msaada kwa kutoa vifaa.6

Waislamu walikuwa na shida mno ya chakula katika siku zile na familia zilizokuwa na uwezo zilikuwa zikiwapa msaada wale askari wa Uislamu.

Uchimbaji wa handaki lile ulipokuwa mgumu kutokana na kutokea kwa mawe makubwa walimwendea Mtume (s.a.w.w.) ambaye yeye mwenyewe aliivunja miamba mikubwa kwa pigo kubwa.

Urefu wa handaki hili uliweza kukisiwa kwa kuichukua idadi ya wale wafanyakazi. Kwa mujibu wa kauli maarufu idadi ya Waislamu katika siku zile ilikuwa ni 3,000 na kama kuchimba dhiraa arobaini kulifanywa na watu kumi, urefu wa handaki lile utakuwa ni dhiraa 12, 000 na upana wake ulikuwa mkubwa sana kiasi kwamba wapanda wanyama werevu na wazoefu hawakuweza kulipita wakiwa kwenye migongo ya farasi.7

Maelezo Maarufu Ya Mtume (S.A.W.W.) Kuhusiana Na Salman

Wale wafanyakazi walipokuwa wakitawanywa ulizuka mzozo baina ya Muhajirina na Ansar kuhusiana na Salman. Kila mmoja wa pande hizo mbili ulidai kwamba Salman alitokana nao.

Katika hali ile Mtume (s.a.w.w.) aliumaliza mzozo ule kwa kutoa amri yenye maamuzi na kusema: “Salman yu mmoja wa watu wa nyumba yangu.”8

Mtume alitumia mchana na usiku kandoni mwa ukingo wa handaki lile hadi ile kazi ilipomalizika. Hata hivyo wanafiki hawakuifanya kazi ile kwa kutoa udhuru, nyakati fulani fulani waliondoka kwenda majumbani mwao bila hata ya kumuaga Mtume (s.a.w.w.) ambapo wale waumini wa kweli walibakia wakijishughulisha na kazi yao kwa nia madhubuti, na waliacha kufanya kazi kwa sababu njema na baada ya kupata ruhusa kutoka kwa yule kamanda, na kurejea kazini wakati udhuru ule ulipomalizika, jambo hili limesimuliwa katika Aya ya 63 ya *Suratun–Nur.*

Jeshi La Waarabu Na Wayahudi Lauzingira Mji Wa Madina

Jeshi la Waarabu lilipiga kambi kama kundi la wadudu na nzige kwenye ukingo wa lile handaki lenye kina kirefu lililochimbwa na Waislamu kiasi cha siku sita tu kabla ya kuwasili kwao. Walitegemea kulikabili jeshi la Uislamu chini ya mlima Uhud, lakini walipofika jangwa la Uhud hawakuona dalili yoyote ya Waislamu hapo. Hivyo waliendelea hadi walipoufikia ukingo wa handaki lile.

Walishangazwa mno kuliona lile handaki kandokando mwa zile sehemu za mji wa Madina zilizokuwa rahisi kuzishambulia na wote wakasema: “Muhammad kajifunza mbinu hizi za vita kutoka kwa Mwirani. Kwa kuwa Waarabu hawana uzoefu wa aina hii ya mbinu za kivita.”

Idadi Ya Askari Wa Hayo Majeshi Mawili

Lile jeshi la Waarabu lilikuwa na askari zaidi ya 10,000. Mwanga wa panga zao kutoka nyuma ya lile

handaki uliyashangaza macho. Kufuatana na ilivyonukuliwa na Maqrizi katika '*al–Imt?*' Waquraish peke yao walipiga kambi kwenye ukingo wa lile handaki na askari 4000, wapanda farasi mia tatu na ngamia 1500, na kabila la Salim lilijiunga nao mahali paitwapo Murruz Zahraan wakiwa na watu 700.

Kabila la Bani Fazaarah walikuwa na watu 1000 na kabila la Bani Ashja na Bani Murrah walikuwa na watu 400 kila moja, na makabila mengine ambayo idadi yao ilizidi watu 10,000 walipiga kambi kwenye sehemu nyingine.

Waislamu hawakuzidi elfu tatu na sehemu waliyopigia kambi yao ilikuwa chini ya mlima Sala' iliyokuwa sehemu iliyoinuka. Sehemu hii ililitawala lile handaki kikamilifu pamoja na sehemu zake za nje na matendo yote na

mienendo ya jeshi viliweza kuonekana kwa dhahiri kutoka kwenye sehe– mu ile. Baadhi ya Waislamu waliwekwa kulinda ile minara na vile vibanda vya kulindia na kuitawala ile mienendo ya watu kwenye lile handaki, nao walimzuia adui asilivuke lile handaki kwa njia ya ngome za kimaumbile na za kutengeneza.

Jeshi la Waarabu lilikaa kwenye upande wa pili wa handaki kwa kipindi cha takriban mwezi mzima na katika kipindi hicho si zaidi ya watu wachache walioweza kulivuka handaki lile. Na wale waliojaribu kuvuka handaki lile walirudishwa nyuma kwa njia ya mawe maalum (kombeo au teo) yaliyokuwa yakitumika kwenye zama zile badala ya risasi za siku hizi.

Katika kipindi hiki Waislamu walipata matukio ya kijasiri ya kuvutia pamoja na Waarabu hawa wenye kuchupa mipaka kama ilivyohifadhiwa kwenye historia. 9

Ukali Wa Majira Ya Baridi Na Upungufu Wa Chakula

Vita vya Ahzaab vilitokea wakati wa majira ya kipupwe. Mji wa Madina ulikabiliwa na ukame katika mwaka ule na hali ya njaa ilikuwepo mjini mle. Kiasi cha chakula walichokuwa nacho lile jeshi la Waarabu hakikutosheleza kuwaruhusu kuendelea kukaa pale zaidi ya hapo, kwa kuwa hawakufikiria kamwe kwamba wangeliweza kuzuiwa kwenye ukingo wa lile handaki kwa kipindi cha mwezi mzima kamili. Kinyume na hivyo walikuwa na uhakika kwamba kwa shambulio moja tu wangeliweza kuwashinda wale wapiganaji wa Kiislamu na kuwaua wote kwa panga.

Wale waliowasha moto wa vita hivi (yaani Wayahudi) waliitambua hali hii mbaya, baada ya siku chache tu walielewa kwamba kwa kadiri muda ulivyoendelea kupita uamuzi wa makamanda wa jeshi utadhoofika na watapatwa na ukali wa yale majira ya baridi na upungufu wa malisho na vyakula. Hivyo basi, ikawajia fikara ya kuomba msaada wa Bani Quraydha waliokuwa wakiishi mjini Madina, ili waweze kuwasha moto wa vita ndani ya mji ule na hivyo kuifungua njia kwa jeshi la Waarabu kuingia mjini humo.

Hay Bin Akhtab Awasili Kwenye Ngome Ya Bani Quraydhah

Bani Quraydha walikuwa Wayahudi pekee waliokuwa wakiishi Mjini Madina pamoja na Waislamu kwa amani kamili na utulivu na waliyaheshimu yale mapatano waliyofanya na Mtume Muhammad (s.a.w.w.).

Hay bin Akhtab alihisi kwamba ushindi utapatikana kwa kuomba msaada kwa ajili ya jeshi la Waarabu kutoka ndani ya mji wa Madina.

Aliamua kuwachochea Bani Quraydha kuyakana yale mapatano waliyoyafanya na Waislamu ili yaanze mapigano baina yao na hizi ghasia za ndani zingaliweza kuleta ushindi kwa jeshi la Waarabu. Kwa mpango huu akilini mwake, aliiendea ngome ya Bani Quraydha na kujitambulisha. Ka'ab aliyekuwa chifu wa Bani Quraydha aliamrisha kwamba lango la ile ngome lisifunguliwe.

Hata hivyo, Hay alisisitiza na kuomba na akasema kwa sauti kuu: "Ewe Ka'ab! Je, hulifungui lango kwa sababu unachelea mkate wako na maji yako (yaani kwa sababu unachelea kwamba itakubidi kunilisha). Sentensi hii iliangaza juu ya ukarimu na utu wa chifu aliyekubaliwa na watu wote kama vile Ka'ab. Hivyo ilimhimiza kuruhusu kwamba lile lango lifunguliwe kwa ajili ya Hay.

Huyu mwanzilishi wa vita alikaa karibu na mwanadini mwenzie na akazungumza naye kwa maneno haya; "Nimekuletea neno la heshima na ukuu kwako. Machifu wa Waquraishi watukufu wa Uarabuni na wafalme wa Ghitfaan wenye silaha za kutosha, wamepiga kambi kwenye ukingo wa handaki ili kumwangamiza adui wetu sote (Mtume s.a.w.w) nao wamenipa ahadi ya kwamba hawatarejea makwao."

Ka'ab alijibu hivi: "Ninaapa kwa Mwenyezi Mungu, Mwenye nguvu zote kwamba wewe umeleta aibu na fedheha. Kwa maoni yangu, jeshi la Waarabu ni kama wingu lililo na mvua lenye kuunguruma lakini halinyeshi mvua.

Ewe mwana wa Akhtab! Ewe mwanzilishi wa vita! Iweke mikono yako mbali nasi. Sifa njema za Mtume Muhammad zinatuzuia kuyakana yale mapatano tuliyoyafanya naye. Hakuna tulichokiona kwake ila ukweli, uaminifu na unyofu. Sasa vipi tunaweza kumsaliti?"

Akiwa kama mpanda ngamia stadi amtiishaye ngamia mkaidi kwa kuikunakuna nundu yake, Hay bin Akhtab alizungumza mambo mengi mno kwa Ka'ab kiasi kwamba hatimaye alikubali kuyakana yale mapatano. Vile vile Hay alimwahidi Ka'ab kwamba kama jeshi la Waarabu halitamshinda Muhammad, yeye (Hay) mwenyewe atakuja pale ngomeni na kushiriki katika hatima ya Ka'ab.

Ka'ab aliwaita machifu wa Wayahudi mbele ya Hay na kuiarifu halmashauri ya ushauriano na akawataka watoe imani yao, wote wakasema: "Unaweza kuamua lolote lile unaloana kuwa linafaa nasi tutakutii."10

Zubayr Bata, aliyekuwa mzee alisema: "Nimesoma kwenye Taurati kwamba katika siku za baadae, Mtume atainuka kutoka Makka. Atahajiria Madina. Dini yake itaenea ulimwenguni kote na hakuna jeshi

litakalopata ushindi dhidi yake. Kama Muhammad ndiye Mtume yule jeshi hili halitamshinda.” Mara moja yule mwana wa Akhtab akasema: “Yule Nabii atatoka miongoni mwa Bani Israeli, ambapo Muhammad yu dhuria wa Isma’il; amewakusanya watu hawa karibu yake kwa njia ya udanganyifu na uchawi.”

Alizungumza mno juu ya jambo hili kiasi kwamba alifaulu kuwafanya waamue kuyaasi yale mapatano. Vile vile alitaka apewe ile karatasi yenye yale mapatano yaliyofanywa baina ya Mtume Muhammad (s.a.w.w.) na Bani Quraydha na akalipasua vipande vipande machoni pao. Kisha akasema: “Sasa jambo hili limeshamalizika. Hamna budi kuwa tayari kupigana vita.”11

Mtume (S.A.W.W) Atambua Kuvunjwa Kwa Mapatano Na Bani Quraydhah

Mtume (s.a.w.w.) aliarifiwa na watumishi wake stadi kuhusu kuvunjwa kwa mapatano na Bani Quraydha katika wakati huu mgumu. Aliingiwa na wasiwasi mno kutokana na jambo hili. Mara moja akamtuma Saad bin Mu’aaz na Sa’da bin Ubadah waliokuwa askari mashujaa wa Uislamu na machifu wa makabila ya Aws na Khazraji kwenda kupata taarifa sahihi. Vile vile aliwaelekeza ya kwamba kama usaliti wa Bani Quraydha ukionekana kwamba ni kweli wamweleze jambo hilo kwa kutumia neno la siri (code–word) la ‘Azal na Qaarah’ (Majina ya makabila mawili yaliyowakaribisha wahubiri wa Kiislamu nchini mwao kisha wakavikatilia mbali vichwa vyao), na kama wakibakia kuwa madhubuti kuhusiana na yale mapatano, basi wayapinge mashtaka yale waziwazi.

Wote wawili walikwenda kwenye lango la ngome ya Bani Quraydha pamoja na watu wengine wawili. Kwenye mkutano wao wa awali na Ka’ab hakuna walichokisikia kutoka kwake ila lugha ya matusi na chafu. Mmoja wao akasema kwa msukumo wa kimuujiza; “Ninaapa kwa Jina la Allah! Jeshi la Waarabu litaondoka nchini humu na Mtume ataizingira ngome hii na atavikata vichwa vyenu na ataufanya wakati kuwa mgumu kwa kabila lenu.”

Kisha walirejea upesi upesi na wakamwambia Mtume (s.a.w.w.): “Azal na Qaarah!” Mtume (s.a.w.w.) akasema kwa sauti kuu ‘Allah Akbar’ (Allah Yu Mkubwa)! Enyi Waisilamu! Kuna biashara njema kwa ajili yenu kwamba ushindi uko karibu.” Sentensi iliyoudhihirisha ushujaa kamili na busara za huyu kiongozi mkuu wa Uislamu, ilitamkwa ili kuthibitisha kwamba moyo wa Waislamu usidhoofike kwa kusikia habari za kuvunjwa kwa mapatano na watu wa Bani Quraydha.12

Mwanzo Wa Uasi Wa Bani Quraydhah

Mpango wa awali wa Bani Quraydha ulikuwa kwamba hatua ya kwanza iwe ni kuuteka nyara mji wa Madina na kuwaogofya wanawake na watoto wa Waislamu waliojificha kwenye nyumba zao. Hivyo basi waliutekeleza mpango huu mle mjini Madina pole pole.

Kwa mfano watu mashujaa wa Bani Quraydha walianza kwenda huko na huko mjini mle kwa njia ya

kisirisiri. Walifanya hivi sana kiasi kwamba Safiyah bint wa Abdul Muttalib akasema:
“Nilikuwa nikikaa nyumbani mwa Hasan bin Thabit na mwanawe Hasan na mkewe nao walikuwa wakiishi nyumbani humo. Mara kwa ghafla nilimwona Myahudi akitangatanga kuizunguka ngome yetu katika hali isiyoeleweka. Nilimwambia Hasan: “Dhamira ya mtu huyu si nzuri.

Amka umfukuze.” Hasan akasema: ‘Ewe bint wa Abdul Muttalib sina moyo wa kutosha kuweza kumwua nami nachelea kwamba kama nikitoka nje ya ngome hii nitapatwa na madhara.’ Hivyo mimi mwenyewe niliamka nikafunga kibwebwe, nikaokota kipande cha chuma na kumwua Myahudi yule kwa pigo moja tu.’”

Yule mtu aliyeteuliwa na Waislamu kukusanya taarifa alimwarifu Mtume (s.a.w.w.) kwamba Bani Quraydha wamewaomba Waquraishi na Ghatfaan kuwapatia askari elfu mbili watakaoingia Madina ndani ya ngome na kuuteka nyara mji ule. Taarifa hii ilifika wakati Waislamu walipokuwa wakiulinda ule ukingo wa lile handaki ili adui asiweze kulivuka. Mara moja Mtume (s.a.w.w.) aliwateuwa maafisa wawili ambao ni Zayd bin Harithah na Maslamah bin Aslam pamoja na askari mia tano kuulinda mji na wakiwa wanaitamka takbir’ “Allahu Akbar” (Allah ni Mkubwa) wawazuie Bani Quraydha wasitende uasi ili wanawake na watoto wakae kwa raha kwa kuisikia ile Takbir.13

Mapambano Baina Ya Imani Na Ukafiri

Wakati ule tukio la vita vya Ahzaab lilipotokea waabudu masanamu na Wayahudi walikuwa wameshapigana vita mbalimbali dhidi ya Uislamu. Hata hivyo vita vyote hivyo vilikuwa ni vita maalumu vilivyokuwa vya jamii au kundi moja tu, navyo havikuwa na sifa ya ujumla ya kuihusisha Rasi nzima ya Uarabuni kwenye vita dhidi ya Uislamu. Hata hivyo, kwa kuwa hawakufaulu kuiangusha ile dola mpya ya Uislamu, ingawa walizitumia nguvu zao zote, lakini kwenye tukio hili jeshi la mchanganyiko lenye watu wa makabila mbalimbali lilikusanyika ili kuumaliza Uislamu. Tukizungumzia kimethali, waliwatupia Waislamu mshale wao wa mwisho kwenye podo lao. Hivyo basi, baada ya kutumia fedha nyingi, na vile vile kuwaomba watu wengine wasaidie, walikusanya jeshi kubwa ili kwamba kama Waislamu wasipochukua hatua za tahadhari katika kuuhami mji wa Madina, waweze kupata ushindi wa rahisi dhidi yao, na kwa njia hiyo waweze kulifikia lengo lao. Kwa lengo hili, vile vile walikuja na mpiganaji mkuu wa Bara Arabuni (Amr bin Abdiwad) ili kuweza kuyatatua matatizo yote kupitia nguvu za mkono wake.

Katika maelezo haya, katika siku za vita vya Ahzaab na hasa wakati wa mapambano baina ya wale wapiganaji wawili wa ushirikina na Uislamu, hapo ukafiri na Uislamu vilikabiliana. Pambano hili lilikuwa ni baina ya Ukafiri na Imani (Uislamu).

Moja ya sababu za kushindwa kwa jeshi la Waarabu ni lile handaki lililochimbwa kwenye njia yao. Jeshi la adui lilijaribu usiku na mchana kulivuka handaki lile, lakini kila mara lilikabiliwa na mashambulizi makali ya wale walinzi, kama alivyopanga Mtume (s.a.w.w.).

Majira makali ya baridi ya mwaka ule na upungufu wa chakula na malisho viliutishia uhai wa jeshi la

Waarabu na wanyama wao. Hay bin Akhtab (aliyeanzisha vita ile) alipata tende kiasi cha shehena ishirini za ngamia kutoka kwa Wayahudi wa Bani Quraydha lakini tende hizo zilinyakuliwa na Waislamu na kugawanywa miongoni mwa askari wa Uislamu.14

Siku moja Abu Sufyani alimuandikia Mtume (s.a.w.w.) barua ifuatayo: “Nimekuja na jeshi kubwa ili kuipindua dini yako. Lakini nifanye nini? Kwa kuwa inaonekana kwamba umekufikiria kupambana nasi kuwa ni jambo lenye kuchukiza na hivyo ukachimba handaki baina yetu na wewe.

Mimi sijui umejifunza mbinu hii ya kijeshi kutoka kwa nani, bali lazima nikueleze kwamba mpaka pale nitakapopigana vita vya kumwaga damu kama ile ye Uhud sitarejea (nyumbani).”

Mtume (s.a.w.w.) alimrudishia jibu hili: “Kutoka kwa Muhammad Mtume wa Allah kwenda kwa Abu Sufyani bin Harb ... Umejifaharisha tangu zamani na kudhania ya kwamba unaweza kuizima nuru ya Uislamu. Hata hivyo, hunabudi kutambua ya kwamba wewe ni dhaifu mno kuweza kufanya hivyo. Utarejea hivi karibuni baada ya kushindwa na hapo baadaye nitakuja kuyavunja masanamu makubwa ya Waquraishi mbele ya macho yako.”

Jibu kwa barua hii ambayo ilikuwa ishara ya uamuzi imara wa mwandishi, ilituama moyoni mwa kamanda wa jeshi la adui kama mshale. Kwa vile watu wale waliuamini ukweli wa Mtume Muhammad (s.a.w.w.) nyoyo zao zilidhoofika. Hata hivyo, ingawa hali ilikuwa hivyo, hawakukata tamaa juu ya kuziendeleza juhudi zao. Usiku mmoja Khalid bin Walid alijaribu kulivuka lile handaki akiwa na kikosi maalumu. Hata hivyo, ilimbidi kurudi nyuma kutokana na uangalifu wa askari mia mbili wa Uislamu waliokuwa wakihudumia chini ya uongozi wa Usayd Khidhr.

Mtume (s.a.w.w.) hakudharau kuziimarisha nyoyo za askari wa Uislamu japo kwa muda mfupi tu, na aliwapa moyo kwa hotuba zake zenye kuwachochea na zivutiazo ili kuulinda uhuru wa dini yao. Siku moja aliugeuza uso wake kwa wale askari na maafisa kwenye mkutano mkubwa sana na baada ya kuomba dua fupi aliwahutubia akisema: “Enyi askari wa Uislamu! Simameni imara mbele ya jeshi na kumbukeni kwamba Pepo iko chini ya kivuli cha panga zile zilizofutwa katika njia ya ukweli na haki.”15

Baadhi Ya Wapiganaji Wa Jeshi La Waarabu Wavuka Lile Handaki

Wapiganaji watano: ‘Amr bin Abdiwad, Ikrimah bin Abi Jahl, Hubayrah bin Wahab, Nawfal bin Abdullah na Ziraar bin Khatab walivalia mavazi yao ya kijeshi na wakiwa wamesimama mbele ya jeshi la Bani Kananah, walisema kwa fahari isiyo kifani; “Jitayarisheni na kupigana. Leo mtatambua ni nani walio wapiganaji wa kweli wa jeshi la Waarabu.” Kisha wakawapanda farasi wao na kuliruka lile handaki mahali fulani palipokuwa na upana mdogo kidogo. Wapiganaji hawa watano walikwenda mbali kuliko wenzao na hawakuweza kufikiwa na mishale ya askari waliokuwa wakililinda lile handaki. Hata hivyo, ile sehemu waliyovukia mara moja ilizungukwa na kuzuiwa ili askari wengine wa jeshi la Waarabu wasiweze kuvuka.

Mahali waliposimama hawa wapiganaji watano waliokuja kwa ajili ya mapigano ya mtu kwa mtu palikuwa baina ya lile handaki na mlima Sal'a (Makao makuu ya jeshi la Uislamu). Wale wapiganaji wa Kiarabu walikuwa wakicheza na farasi wao kwa fahari isiyo na kifani na majivuno, nao walikuwa wakiwaita wapinzani wao kwa njia ya vidokezo na ishara.16

Miongoni wa watu hawa watano, yule aliyekuwa maarufu zaidi kwa ushujaa na ustadi wake alijitokeza mbele, na kwanza alimwita mpinzani wake ajitokeze wapigane. Kila alipoitoa sauti yake na haja yake ya kumpata mpinzani ilipogonga kwenye uwanja ule, na kuzitetemesha nyoyo, hakupata jibu. Kimya cha Waislamu kilimchosha naye akasema: "Wako wapi wale wanaodai Pepo? Kwani ninyi Waislamu hamsemi kwamba wale wanaouwawa kutoka miongoni mwenu watakwenda Peponi na wale wanaouawa kutoka miongoni mwetu watakwenda Motoni? Hakuna hata mmoja wenu aliyeko tayari kunipeleka motoni au yeye kwenda Peponi mikononi mwangu?" Vile vile alitunga beti fulani fulani za shairi juu ya jambo hili, ambazo maana ya ule wa kwanza ni hii; "Nimechoka kupiga makelele na kumtaka mpinzani wangu ajitokeze (ili tupigane mapambano ya mtu kwa mtu) na sauti yangu imenikauka."

Ilikuwa kimya kabisa kwenye lile jeshi la Waislamu katika kuzijibu kelele za 'Amr ingawa kila mara Mtume (s.a.w.w.) alikuwa akitaka kwamba mtu mmoja aamke na kuwaondolea Waislamu uasi wa mtu yule, lakini hakuna aliyekuwa tayari kupigana naye ila Sayyidna Ali bin Abi Talib (a.s.).17

Hivyo basi, halikuwapo lolote jingine la kufanya ila kwamba tatizo hili litatuliwe kupitia kwa shujaa Sayyidna Ali (a.s.). Mtume (s.a.w.w.) alimpa upanga wake, akamfunga kilemba maalum kichwani mwake na akamwombea du'a kwa maneno haya: "Ee Allah! Mlinde Ali kutoka pande zote. Ewe Mola wangu! Ubaydah bin Harith alichukuliwa kutoka kwangu katika siku ya Badr na Simba wa Allah Hamza alichukuliwa kwenye vita vya Uhud. Ee Mola Wangu! Mlinde Ali kutokana na kupatwa na madhara kutoka kwa adui." Kisha akaisoma Aya ya Qur'ani Tukufu ifuatayo: **" . . . Ee Mola wangu! Usiniache peke yangu Nawe ndiye mbora wa wanaorithi."**18 **(*Sura al-Anbiya*, 21: 89).**

Sayyidna Ali (a.s.) alikwenda upesi iwezekanavyo ili kufidia ule muda wa kuchelewesha kulikokwisha kufanywa. Wakati huo Mtume (s.a.w.w.) aliitamka sentensi ya kihistoria ifuatayo: "Imani kamili inaukabili ukafiri kamili." Sayyidna Ali (a.s.) alitunga *rajaz* (beti za tenzi) ambazo mfuatano mzuri wa mwenendo wake na vina vyake viliafikiana na vile vya mpinzani wake, na akasema: "Usifanye haraka, kwa sababu mtu mwenye nguvu amekwishafika uwanjani ili akupe jibu."

Mwili mzima wa Sayyidna Ali (a.s.) ulifunikwa na deraya na macho yake yalikuwa yakiangaza kupitia kwenye kofia ya chuma. Amr alitaka kumtambua yule mpinzani wake. Alimwuliza Sayyidna Ali (a.s.): "Ni nani wewe?" Sayyidna Ali (a.s.) aliyekuwa maarufu, kwa sauti ya waziwazi alimjibu hivi; "mimi ni Ali, mwana wa Abu Twalib." Amr akasema: "Mimi sitaimwaga damu yako, kwa sababu baba yako alikuwa mmoja wa marafiki zangu wa tangu zamani. Mimi namshangaa binamu yako aliyekuleta kwenye uwanja wa vita akiwa na uhakika mwingi mno kuwa ninaweza kukuokota kwa ncha ya mkuki wangu na kukuning'iniza baina ya ardhi na mbingu ili kwamba uwe mwenye hali ya kutokufa wala kutokuwa hai."

Ibn Abil Hadid anasema: “Kila mwalimu wangu wa historia (Abul Khayr) alipokuwa akiielezea sehemu hii alikuwa akisema: Kwa kweli Amr alikuwa akiogopa kupigana na Ali, kwa sababu alikuako kwenye Vita ya Badr na ya Uhud naye aliuona ushujaa wake. Hivyo basi, yeye alitaka kumvunja moyo Ali asipigane naye.”

Sayyidna Ali (a.s.) akasema: “Usijali kuhusu kifo changu. Katika hali zote mbili (yaani kama nikiuwa au nikiuwawa) nitabarikiwa na makazi yangu yatakuwa Peponi, lakini wewe katika hali zote hizo, moto unakusubiri.” Amr alitabasamu na akasema: “Ewe Ali! Mgawo huu si wa haki. Vyote viwili, pepo na moto ni vyako.”

Sayyidna Ali (a.s.) alimkumbusha kwamba siku moja yeye (Amr) aliubandika mkono wake juu ya kitambaa kinachoifunika Ka’aba Tukufu (kiswa) na kumwahidi Allah kwamba wakati shujaa yeyote atakapompa ushauri wa aina tatu kwenye uwanja wa vita ataukubali ushauri mmojawapo. Hivyo Sayyidna Ali (a.s.) alimshauri kwamba asilimu. Akajibu: “Ewe Ali! Liache hilo kwa kuwa haliwezekani.” Kisha Sayyidna Ali (a.s.) akasema: “Acha kupigana na umwache Muhammad peke yake.” Akajibu: “Ni aibu kwangu mimi kulikubali hilo, kwa sababu kesho washairi wa Uarabuni watanidhihaki na kudhania kwamba nilifanya hivyo kwa ajili ya hofu.” Hapo Sayyidna Ali akasema “Mpinzani wako hana mnyama wa kupanda. Hivyo wewe nawe huna budi kushuka kutoka juu ya farasi wako ili tuweze kupambana.” Akasema: “Ewe Ali! Huu ni ushauri usio na maana, nami sikufikiria kwamba Mwarabu ataniomba ombi kama hilo.”19

Mapambano Baina Ya Mabingwa Wawili Hao Yaanza

Mapambano makali yalianza baina ya wale mabingwa wawili na wote wawili walifunikwa mno na vumbi kiasi kwamba watazamaji hawakutambua ni nini kilichokuwa kikiendelea. Waliweza kuisikia migongano ya panga tu. Amr aliulenga upanga wake kichwani mwa Sayyidna Ali (a.s.) na ingawa Sayyidna Ali (a.s.) aliweza kuikinga dharuba ile kwa ngao yake maalum, hata hivyo kichwa chake kilijeruhiwa. Na hata hivyo alipata nafasi na kumpiga ‘Amri dharuba kali miguuni. Matokeo yake ni kwamba mguu mmoja au miwili yote ya ‘Amr ilikatwa naye akaanguka chini. Sauti ya Takbir ilisikika mle mwenye vumbi, jambo lililoashiria ushindi wa Sayyidna Ali (a.s.). Mandhari ya kuanguka kwa ‘Amri pale chini yalijenga hofu kuu zaidi nyoyoni kwa wale mashujaa wengine waliokuwa wamesimama nyuma yake, kiasi kwamba walianza kuwaendesha farasi wao bila ya kupenda wakielekea lile handaki, na wote isipokuwa Nawfal, walirejea kambini mwao. Ngamia wa Nawfal alitumbukia mle handakini. Wale waliowekwa kwenye ule ukingo wa handaki wakaanza kumpiga mawe, hata hivyo alisema kwa sauti kuu; “Kumwua mtu namna hii ni kinyume na kanuni za ushujaa. Hebu mmoja wenu na ashuke ili tupigane.”Sayyidna Ali (a.s.) akatumbukia kwenye lile handaki na kumuua.

Woga ukalishika jeshi zima la washirikina, na Abu Sufyani aliogopa zaidi kuliko yeyote yule mwingine. Alifikiria kwamba Waislamu watavikata kata viungo vya maiti ya Nawfal ili kulipa kisasi cha Hamza. Hivyo alimtuma mtu mmoja kwenda kuinunua maiti ya Nawfal kwa dinar elfu kumi. Hata hivyo, Mtume

(s.a.w.w.) alisema: “Wapeni maiti yao na kwenye dini ya Uislamu hairuhusiwi kuchukua bei ya maiti.”

Thamani Ya Pigo Hili

Ingawa kwa madaha Sayyidna Ali (a.s.) alimuuwa adui wa Uislamu aliyetisha, lakini kwa kweli aliwahuisha wale watu waliokuwa wakitetemeka kuzisikia ngurumo za ‘Amr zenye kuzipasua pasua nyoyo, na vile vile aliliogofya lile jeshi lenye nguvu la askari elfu kumi lililodhamiria kuimalizia mbali ile Dola changa ya Uislamu. Thamani ya kujitoa mhanga huku kungelitambulika kama ushindi (angekosekana Ali) ungeangukia kwenye fungu la ‘Amr.

Wakati Sayyidna Ali (a.s.) alipopata heshima ya kujitokeza mbele ya Mtume (s.a.w.w.), Mtume (s.a.w.w.) aliitathmini ile faida ya lile pigo alilompiga nalo ‘Amr, kwa maneno haya: “Thamani ya kujitoia mhanga huku ni bora kuliko matendo mema yote ya wafuasi wangu, kwa sababu matokeo ya kushindwa kwa yule mpiganaji mkuu wa ukafiri, Waislamu wamekuwa wenye kuheshimika na jamii ya makafiri imeshuka cheo na kufedheheka na kunyongea.”20

Roho Nzuri Sana

Deraya ya ‘Amr ilikuwa na bei kubwa sana, lakini Sayyidna Ali (a.s.) alikuwa na roho nzuri mno kiasi cha kutoweza kuigusa, ingawa Khalifa wa pili alimlaumu kwa kutoivua mwilini mwa ‘Amr. Dada yake ‘Amr alipolitambua tukio lile alisema:21 “Katu mimi sihuzuniki kuuawa kwa kaka yangu, kwa sababu aliuawa mikononi mwa mtu mwenye roho nzuri sana. Kama isingalikuwa hivyo, ningalitiririkwa na machozi maishani mwangu.”22

Jeshi La Waarabu La Gawanyika

Lengo la majeshi ya Waarabu na Wayahudi katika kupigana dhidi ya Uislamu halikuwa moja. Wayahudi walikuwa wakichelea kuongezeka daima kwa kuenea kwa Uislamu, ambapo Waquraishi walisukumwa na uadui wao wa tangu kale dhidi ya Uislamu na Waislamu.

Ghatfaan na Fazarah na makabila mengineyo, walishiriki kwenye vita hivi kwa sababu ya mapatano ya Khaybar ambayo Wayahudi waliwaahidi.

Hivyo basi, lengo la hili kundi la mwisho lilikuwa la kimaada na kama lengo lao lingaliweza kufikiwa kupitia kwa Waislamu, wao wangeweza kurejea makwao kwa furaha kuu, hasa kwa vile ukali wa majira ya baridi, upungufu wa chakula na mazingira marefu ya mji wa Madina yamewasikitisha na wanyama wao walikuwa ukingoni mwa kifo.

Hivyo basi, Mtume (s.a.w.w.) alikiteua kikundi cha watu kufanya mapatano na machifu wa makabila tuliyoyataja hapo juu chini ya masharti ya kwamba Waislamu walikuwa tayari kuwapa theluthi moja ya matunda ya Madina, ili mradi tu wajitenge na majeshi ya Ahzaab (makabila) na warejee kwenye maeneo

yao. Wale wawakilishi wa Mtume (s.a.w.w.) waliandika mapatano na wale machifu wa yale makabila na wakamletea ayatie saini. Hata hivyo, Mtume (s.a.w.w.) aliliweka jambo hili mbele ya maafisa wawili shujaa, ambao ni Sa'ad bin Mu'aaz na Sa'ad bin Ubadah.

Wote kwa pamoja walisema kwamba kama mapatano haya yanafanyika kwa mujibu wa amri ya Allah yatakubaliwa na Waislamu, lakini kama yanafanyika kutokana na maoni ya Mtume mwenyewe, na hivyo wanaombwa kutoa maoni yao, wao wanafikiria kwamba mpango huo ukomee hapo hapo na usisainiwe. Kuhusu sababu yao ya kutoukubali mpango ule, walisema kwamba; "Katu sisi hatukuwahi kulipa ushuru kwa makabila haya na hakuna lolote miongoni mwao lithubutilo kuchukua japo tunda moja ya tende kutoka kwetu kwa nguvu na lazima.

Na kwamba sasa tumesilimu kwa rehema za Allah na chini ya mwongozo wako na tumekuwa watukufu na wenye kuheshimiwa kwa njia ya Uislamu, suala la sisi kuwalipa wao ushuru wowote ule halipo tena. Tunaapa kwa jina la Allah! Tutayajibu madai yao yasiyo na msingi kwa panga zetu hadi jambo hili liamuliwe kwa Amri ya Allah."

Mtume (s.a.w.w.) alisema: "Sababu ya mimi kufikiria juu ya mapatano ya aina hii ni kwamba nimeona kwamba mmekuwa shabaha (dango) ya jeshi la Waarabu nanyi mlikuwa mkishambuliwa kutoka pande zote. Hivyo basi mimi nilifikiria kwamba tatizo hili litatuliwe kwa njia ya kujenga mgawanyiko miongoni mwa maadui. Hata hivyo, sasa kwa vile msimamo wenu thabiti umedhihirika mimi ninauzuia hitimisho la mapatano haya na ninakuambieni – nayaaminini yale niyasemayo kwamba Allah hatamfedhehesha Mtume Wake na ataitimiza ahadi Yake kuhusu ushindi wa imani na Upweke wa Allah juu ya ushirikina. Hapo Sa'ad bin Mu'aaz akayafuta maneno ya mapatano yale kwa amri ya Mtume (s.a.w.w.) na akasema: "Waabudu masanamu wanaweza kufanya vyovyote vile wapendavyo. Sisi si watu wa kulipa ushuru."23

Sababu Zilizoligawa Jeshi La Waarabu

Katika Vita vya Ahzaab, ingawa Waarabu walileta jeshi kubwa kiasi hiki, walishindwa kulifikia lengo kutokana na kugawanyika kwa jeshi. Zifuatazo hapa chini ndizo sababu zilizozaa kugawanyika kwa lile jeshi la Waarabu:

1. Sababu ya kwanza ya ushindi wa Waislamu kwenye vita hivi ilikuwa ni mazungumzo baina ya wawakilishi wa Mtume (s.a.w.w.) na wale machifu wa makabila ya Ghatfaan na Fazarah. Kwa sababu, ingawa mapatano haya hayakuthibitishwa pale mwishoni, kule kuyaasi na kuyakataa vilevile hakukutangazwa. Kwa njia hiyo, makabila yale yakashindwa kujua lipi ni lipi kuhusiana na wale marafiki zao, hivyo waliendelea kusubiri kupata taarifa za mapatano na kila walipotakiwa kufanya mashambulizi ya ujumla (ya watu wote) waliyakataa matakwa hayo kwa sababu moja au nyingine kwa tegemeo la kufikiwa kwa kamilisho la mapatano yale.

2. Watu wengi walikuwa wameweka matumaini yao juu ya kufaulu na ushindi kwa 'Amr, yule mpiganaji

mwenye nguvu nyingi wa Uarabuni. Matokeo yake ni kwamba, alipouawa, hofu kali sana iliwaingia. Ilikuwa hivyo hasa, kwa sababu baada ya ‘Amr kuuawa wapiganaji wengine walikimbia kutoka kwenye ule uwanja wa vita.

3. Na’im bin Mas’ud aliyesilimu muda mfupi tu kabla ya vita hivi alifanya kazi kubwa sana katika kujenga mtengano baina ya makabila. Aliunda mpango bora zaidi kijasusi usio na upungufu wowote wa akili kuliko yale matendo ya majasusi wa siku hizi. Kidogo ulikuwa bora zaidi na wenye uwezo wa kutoa matokeo mazuri zaidi.

Na’im alikuja mbele ya Mtume (s.a.w.w.) na kusema: “Nimesilimu hivi karibuni nami nina uhusiano wa kirafiki na makabila yote haya, lakini wao hawajatambua kusilimu kwangu. Kama ziko amri zozote zile upendazo kunipa, nitazitekeleza.” Mtume (s.a.w.w.) akamwambia: “Fanya jambo liwezalo kuwagawa watu hawa” Yaani hakuna ubaya wowote kama ukifanywa mpango na ikapatikana dawa ya kuyasalimisha malengo yaliyo bora zaidi.

Na’im alilifikiria jambo lile kwa muda hivi. Kisha kwanza kabisa aliliendea kabila la Bani Quraydha ambao kwa kweli wao walikuwa kwenye safu ya tano ya adui, wao walikuwa wakiwatishia Waislamu kutoka kwenye mlango wa nyuma. Aliwasili kwenye ngome ya Bani Quraydha na kuilezea huba yake na urafiki wake kwao na akayatamka kila aina ya mambo yaliyoweza kumfanya wamwamini.

Kisha akaongeza kusema: “Hali yenu ni tofauti na ile ya marafiki zenu (yaani Waquraishi na Ghatfaan), kwa kuwa Madina ni maskani ya wanawake wenu na watoto wenu na mali zenu zote ziko hapa na hamwezi hata kidogo kuhamia mahali popote pale pengine, ambapo vituo vya maisha na biashara vya haya makabila yaliyojirafikisha, yaliyokuja kupigana dhidi ya Muhammad viko nje ye Madina na mbali na mji huu. Kama wakishinda vita hivi, watakuwa wamelifikia lengo lao, lakini kama wakishindwa mara moja watatoka na kuyaendea makazi yaliyopo mbali kiasi cha kutoweza kufikiwa na Muhammad. Hata hivyo, hamna budi kutambua kwamba kama makabila haya hayatashinda na wakarejea makwao wakiiacha vita, mtaachwa kwenye hali ya kutiishwa na Waislamu.

Sasa mnafikiria kwamba, kwa vile mmejishirikisha na makabila haya, ni bora kwamba muushikilie uamuzi huu. Hata hivyo, ili kuhakikisha kwamba makabila haya hayakuacheni peke yenu wakati wa vita na kurudi makwao, hamna budi kuwashika baadhi ya watu wao watukufu machifu wakawa ni dhamana ili kwamba hali itakapokuwa ngumu wasikuacheni na walimalize jambo hilo, kwa sababu, kwa njia hiyo watalazimika kupigana na Muhammad hadi mwisho ili watu wao waachiliwe.”

Maoni ya Na’im yalikubaliwa na watu wote, naye alitosheka kwamba maneno yake yalitoa athari zilizohitajika juu yao. Kisha aliiacha ngome yao na kwenda kwenye kambi ya yale makabila. Machifu wa Waquraishi walikuwa marafiki zao wa tangu kale. Hivyo basi, wakati wa mazungumzo yake na machifu wale, alisema:

“Bani Quraydha wameaibika sana nao ni wenye kujuta kwa kuyavunja kwao mapatano baina yao na Muhammad na sasa wanataka kulisahihisha jambo hilo. Hivyo basi, wameamua kuwachukua baadhi ya

watu wenu ili wawe dhamana na wampe Muhammad watu hao. Kwa njia hii, watauthibitisha uaminifu wao, na Muhammad atawauwa watu wenu mara moja. Wameshalijadili jambo hilo na Muhammad nao wamemthibitishia kwamba tangu sasa hadi mwishoni mwa maisha yao watamuunga mkono na Muhammad naye ameukubali mpango wao.

Hivyo basi, kama Wayahudi wakitaka dhamana kutoka kwenu, msikubali hata kidogo. Hamna budi kutambua kwamba matokeo ya kitendo cha aina hiyo yatakuwa ya hatari. Uthibitisho wa dhahiri wa ukweli huu ni kwamba kama kesho mkiwataka washiriki kwenye vita na kumshambulia Muhammad kwa nyuma, mtawaona kwamba hawatakubali hata kidogo kufanya hivyo, na watatoa udhuru wa kila aina."

Kisha akaiendea kambi ya Ghatfaan na kuzungumza nao kwa njia maalum. Alisema: "Ninyi watu wa kabila la Ghatfaan mu ndugu zangu. Sifikirii kwamba mtanilaumu kwa haya niyasemayo.

Nitazungumza nanyi juu ya jambo fulani bali nataka mnithibitishie kwamba hamtalizungumza kwa mtu yeyote. Wote walimthibitisha kuwa yu mtu mkweli na rafiki yao. Kisha aliwaeleza kwa kirefu yale aliyokwisha kuwaeleza Waquraishi na akawaonya juu ya matendo ya Bani Quraydha na akasema: "Msiwape jibu la kuyakubali matakwa yao kwa hali yoyote ile iwayo."

Alitekeleza wajibu wake vizuri sana. Kisha akaja kwenye kambi ya Waislamu kwa siri na kuyaeleza mazungumzo yote haya mbele ya jeshi la Uislamu (yaani kwamba Wayahudi walitaka kuichukua dhamana kutoka kwenye majeshi ya Waarabu ili kuwapa Waislamu). Bila shaka lengo la kuyatangaza maongezi haya lilikuwa kwamba, jambo lile livuke lile handaki na kuyafikia masikio ya Waarabu.

Wawakilishi Wa Waquraishi Waitembelea Ngome Ya Bani Qurayzah

Abu Sufyani katika usiku wa kuamkia Jumamosi aliamua kumaliza jambo hili. Machifu wa Waqurashi na Ghatfaan waliwatuma wawakilishi wao kwenye ngome ya Bani Quraydha na kuwaambia: "Huu si ukanda wa makazi yetu na wanyama wetu wanakufa. Kesho hamna budi kuwashambulia Waislamu kwa mlango wa nyuma ili tuweze kulimaliza jambo hili." Yule chifu wa Bani Quraydha akajibu akasema: "Kesho ni Jumamosi na sisi Wayahudi hatufanyi kazi yoyote katika siku hiyo kwa sababu baadhi ya jadi zetu walifanya kazi katika siku hii nao wakaangukiwa na ghadhabu ya Mungu. Zaidi ya hapo, tuko tayari kushiriki kwenye mapigano pale tu baadhi ya watu wenu watukufu watakapokuwamo kwenye ngome yetu wakiwa ni dhamana, ili kwamba muweze kupigana hadi mwisho ili kuthibitisha kuachiliwa kwao na msije kutuacha bila ya marafiki."

Wale wawakilishi wa Waquraishi walirejea na kuwaeleza wale machifu wa makabila juu ya hali ile. Wote wakasema: "Na'im alikuwa sahihi katika kuzieleza huruma zake kwetu. Bani Quraydha wanataka kutuhadaa." Wale wawakilishi wa Waquraishi waliwasiliana na machifu wa Bani Quraydha na kusema: "Haiwezekani kwetu sisi kuwatoa watu wetu watukufu na kukupeni ninyi ili wawe dhamana nasi hatuko tayari kukupeni japo mtu wetu mmoja tu ili awe dhamana. Kama mkielekea kuwashambulia Waislamu,

fanyeni hivyo kesho nasi tutakusaidieni kwa uwezo wetu wote.”

Maneno ya wale wawakilishi wa Waquraishi na hasa kule kusema kwao kwamba hawakuwa tayari kumtoa japo mtu mmoja ili awe dhamana kuliwafanya Bani Quraydha waamini kwamba yale yote aliyoyasema Na’im yalikuwa sahihi. Yaliithibitisha hofu yao kwamba Waquraishi walikuwa wakitazama mbali na kama hawakufaulu kwenye jambo lile, watarejea nyumbani na kuwaacha watiishwe na Waislamu.”24

Sababu Ya Mwisho

Sababu nyingine ambayo kwa kweli inaweza kuitwa msaada wa Allah ilioongezwa kwenye sababu zile tulizozitaja hapo juu na kuyatawanyisha yale makabila. Sababu hii ilikuwa kwamba kwa ghafla hali ya hewa iliingiwa na dhoruba na hewa ikawa baridi mno. Badiliko la hali ya hewa lilikuwa kali mno kiasi kwamba mahema yaling’olewa, vyungu vilivyokuwa vikipikiwa chakula vilipinduliwa, taa zilizimika na moto uliokuwa ukiwaka ulitawanywa jangwani mle. Hali ilipofikia kiasi hicho, Mtume (s.a.w.w.) alimtuma Hudhayfah kulivuka lile handaki na kupata taarifa za adui.

Anasema: “Niliweza kufika karibu na Abu Sufyani na nikamwona akiwahutubia makamanda wa jeshi. Alikuwa akisema hivi: ‘Mahali hapa tulipopigia kambi si mahali pa maskani yetu. Wanyama wetu wanakufa na upepo na dhoruba havikuyabakisha mahema, vivuli na moto kwa ajili yetu. Bani Quraydha nao hawakutusaidia. Ni bora kama tukiondoka hapa.” Kisha alimpanda ngamia wake ambaye magoti yake yalikuwa yamefungwa na akaanza kumpiga kwa kurudia rudia. Maskini mtu huyu alikuwa na hofu mno ya kutatizwa kiasi kwamba hakutambua kwamba magoti ya yule ngamia yalikuwa yamefungwa.

Ilikuwa bado alfajiri haijaingia pale jeshi la Waarabu lilipoondoka kwenye sehemu ile na hakuna yeyote aliyeonekana pale tena”.25

---

1. Maghaazil–Waaqidi, Juz. 2, uk. 441.
2. Siiratu Ibn Hishamu, Juz. 2, uk. 214; Tarikhut–Tabari, Juz. 2, uk. 233.
3. Hayaatu Muhammad.
4. Maghaazil–Waaqidi, Juz. 2, uk. 443.
5. Tarikhut–Tabari Juz. 2, uk. 224.
6. Maghaazil–Waaqidi, Juz. 2, uk. 445.
7. Siiratu Ibn Hishamu, Juz. 2, uk. 220. Maghaazil– Waaqidi, Juz. 2, uk. 453.
8. Maghaazil– Waaqidi, Juz. 2, uk. 446; Siiratu Ibn Hishamu, Juz. 2, uk. 224.
9. Siiratu Ibn Hishamu, Juzuu 1, uk. 238.
10. Maghaazil–Waaqidi, Juz. 2, uk. 455–456.
11. Bihaarul Anwaar, Juzuu 2, uk. 223.
12. Maghaazil– Waaqidi, Juz. 2, uk. 458–459.
13. Siiratul–Halabi, Juz. 2, uk. 335.
14. Siiratul–Halabi, Juz. 2, uk. 345.
15. Siiratu–Halabi, Juz. 2, uk. 349.

16. Tarikhut–Tabari, Juz. 2, uk. 239; Tabaqaatul– Kubraa. Juz. 2, uk. 86.
17. Waaqid anasema: “Kilikuwepo kimya kikali miongoni mwa Waislamu wakati Amr alipokuwa akimwita mpinzani wake wa mapambano ya mtu na mtu”. Maghaazil, Juz. 2, uk. 470.
18. Sura al–Anbiya, 21: 89
19. Bihaarul Anwaar, Juz. 20, uk. 227.
20. Bihaar An’waar, Juz. 20, uk. 216; Mustadrik Hakim, Juz. 3, uk. 32.
21. Na inasemekana kuwa dada huyu alimwomboleza kaka yake kwa beti hizi: “Laiti aliyemuuwa Amru angekuwa si huyu aliyemuuwa, basi ningelia milele maadamu bado nipo duniani. Lakini aliyemuuwa ni mtu asiyekuwa na mfano, na baba yake alikuwa akimwita: Wa pekee asiye na mfano.”
22. Mustadrik Hakim, Juz. 30, uk. 33
23. Siiratu Ibn Hishamu, Juzuu 1, uk. 223; Bihaar Anwaar, Juz. 20, uk. 252.
24. Siiratu Ibn Hishamu, Juz. 2. uk. 229–231; Tarikhut–Tabari, Juz. 2, uk. 242– 243.
25. Tarikhut–Tabari, Juz. 2, uk. 244.

Sura Ya 38: Hatua Ya Mwisho Ya Madhara

Katika mwaka wa kwanza wa kuwasili kwa Mtume (s.a.w.w.) mjini Madina aliandika mkataba muhimu na sheria za msingi kwa ajili ya mji wa Madina na vitongoji vyake ili kukomesha mifarakano na tofauti za ndani, na Wayahudi na makabila ya Aws na Khazraji wote kwa ujumla walikubali kulihami eneo hili. Tayari wasomaji wameshasoma vifungu vya sheria na maelezo kamili ya mkataba huu. Aidha, vile vile alifanya mapatano mengine na Wayahudi wa Madina. Mapatano haya yalitiwa saini na makundi yote ya Wayahudi kwa ujumla.

Ilikubaliwa kwamba kama wakimfanyia Mtume (s.a.w.w.) madhara yoyote, au masahaba zake au wakawapa silaha au wanyama wa kupanda maadui zao, Mtume (s.a.w.w.) atakuwa huru kisheria kuwauwa, kuzichukuwa mali zao na kuwateka wanawake na watoto wao.

Hata hivyo mapatano haya yalivunjwa na kutupiliwa mbali na makundi yote ya Wayahudi katika njia tofauti. Bani Qaynaqaa’ walimuuwa Mwislamu, Bani Nuzayr walipanga mpango wa kumuuwa Mtume (s.a.w.w.) na hivyo basi, akawalazimisha kuihama nchi yao na kwenda kuishi nje ya eneo la Waislamu. Ama kuhusu wale Bani Quraydha, wao walishirikiana kwa moyo mmoja na jeshi la Waarabu katika kuudhuru Uislamu. Sasa hebu na tutazame jinsi Mtume (s.a.w.w.) alivyowaadhibu Bani Quraydha.

Kabla ya kucha kwa siku ile, kikosi cha mwisho cha jeshi la makabila kiliitoka nchi ya Madina wakiwa wenye hofu mno. Ingawa dalili za uchovu na ulegevu zilijidhihirisha nyusoni mwa Waislamu, Mtume (s.a.w.w.) aliamrishwa na Allah kulimaliza jambo la Bani Quraydha. Mwadhini aliadhini na Mtume (s.a.w.w.) akasali sala ya adhuhuri pamoja na Waislamu.

Kisha kwa amri ya Mtume (s.a.w.w.) yule mwadhini alitangaza akisema: “Waislamu lazima wakaisali sala yao ya alasiri kwenye eneo la Bani Quraydha.” Kisha Mtume (s.a.w.w.) alimpa Sayyidna Ali (a.s.)

bendera.

Askari mashujaa wakatoka wakiwa chini ya uamiri jeshi wake na wakaizingira ngome ya Bani Quraydha. Mlinzi wa ngome ile akatoa taarifa ya matendo ya jeshi la Waislamu kwa wakazi wa ngome ile. Milango ya ngome ile ikafungwa mara moja, lakini ikaanza vita baridi kwa kule kuwasili kwa jeshi la Waislamu.

Wayahudi wa Bani Quraydha walimtusi Mtume (s.a.w.w.) kupitia madirishani na minarani mwa ngome ile. Yule mshika bendera wa jeshi, Sayyidna Ali (a.s.) alikuwa Madina kumzuia Mtume (s.a.w.w.) asiikaribie ngome ile ili asiyasikie yale maneno machafu ya Wayahudi.

Hivyo Mtume (s.a.w.w.) alimwambia Sayyidna Ali (a.s.) kwamba, wao Wayahudi wakimwona wataacha kuyatumia maneno ya matusi. Hivyo, Mtume (s.a.w.w.) akaikaribia ngome ile na akazungumza nao kwa ukali kidogo na akasema: “Je Mwenyezi Mungu hakukufedhehesheni ninyi?”

Aina hii ya ukali na hasira za Mtume (s.a.w.w.) vilikuwa ni vitu visivyo kifani kwa Wayahudi. Hivyo basi ili kumtuliza Mtume (s.a.w.w.) walisema upesi upesi: “Ewe Abul Qaasim! Wewe hukuwa mwepesi wa kughadhibika kiasi hicho!” Maneno haya yalizituliza mno hasira za Mtume (s.a.w.w.) kiasi kwamba aligeuka nyuma bila ya kukusudia na joho lake likaanguka chini kutoka mabegani mwake.1

Mashauriano Ya Mayahudi Ndani Ya Ile Ngome

Hay bin Akhtab Nuzayri, aliyeViwasha vita Vya Ahzaab alishiriki kwenye majadiliano haya, kwa sababu kufuatana na ahadi aliyomuahidi Ka’ab, yule chifu wa Bani Quraydha, yeye hakwenda Khaybar baada ya kutawanyika kwa makabila na badala yake alikuwa kwenye ile ngome ya Bani Quraydha. Yule chifu wa jamii ile alitoa maazimio matatu na kuwataka watu kuchagua lolote lile miongoni mwao. Alisema:

1. Sisi sote tusilimu, kwa sababu utume wa Muhammad ni ukweli uliodumishwa na kuthibitishwa na watu wote, na Taurat nayo inauthibitisha.

2. Tuwauwe wanawake na watoto wetu na kisha tutoke humu kwenye ngome na kupigana na Waislamu kwa mkono ulio huru. Kama tukiuawa hatutakuwa na chochote cha kututia wasiwasi na kama tukishinda tunaweza kujipatia tena wanawake na watoto.

3. Usiku huu ni usiku wa kuchea Jumamosi, Muhammad na masahaba zake watafikiria kwamba Wayahudi hawafanyi jambo lolote kwenye usiku wa kuchea Jumamosi na katika siku ya Jumamosi. Hivyo tujinufaishe na utovu wao wa tahadhari na tuwashambulie wakati wa usiku.”

Ile kamati ya ushauri iliyakataa maazimio yote matatu na kusema: “Hatutaikana dini yetu na Taurati, na maisha yetu nayo hayatakuwa na raha baada ya wanawake na watoto wetu (kuuawa).

Ama kuhusu azimio la tatu haliwezi kutekelezeka kutokana na itikadi za dini yetu kwa sababu, iwapo tutafanya hivyo, tunaweza kupasika na ghadhabu ya Mungu kama vile ilivyotokea kwa nyumati zilizopita

kutokana na kutoipa heshima ipasikayo siku ya Jumamosi.”2

Hotuba za wanakamati ni mwongozo wetu katika kuzielewa fikara zao. Kulikataa kwao azimio la kwanza kwaonyesha kwamba walikuwa watu wakaidi na wenye uadui, kwa sababu kama kweli waliuamini utume (kama ilivyoelezwa na chifu wao) kumpinga kwao hakukuwa na maana yoyote ila ukaidi.

Ama kuhusu lile azimio la pili, mazungumzo yaliyofanyika miongoni mwao yaonyesha kwamba walikuwa watu wakatili na wenye nyoyo ngumu kwa sababu kuwauwa wanawake na watoto wasio na kosa, hakuwezekani bila ya kuwa na moyo mgumu mno.

Inapasa kuzingatia kwamba wajumbe wa kamati ya ushauri walilikataa azimio hili kutokana na ukweli uliopo kwamba, maisha yao hayatakuwa yenye furaha bila ya wanawake na watoto. Hakuna hata mtu mmoja aliyeuliza ni kosa gani walilolitenda watu hawa wasio na msaada ambalo kutokana nalo wanauawa, na vipi wao mababa wenye huruma na wakarimu, waweze kulitenda tendo hili wakati katu Mtume (s.a.w.w.) asingaliwauwa kama angalipata mamlaka juu yao?

Azimio la tatu laonyesha kwamba hawakuitathmini barabara nguvu ya kiroho ya Mtume (s.a.w.w.) na ujuzi wake wa mbinu za vita na kanuni za ulinzi, na wakafikiria ya kwamba Mtume wa Uislamu hatachukua tahadhari ya lazima kwenye usiku na siku ya Jumamosi – na kwamba vile vile hata kuhusu adui kama wale Wayahudi, watu walio maarufu kwa hadaa zao na hila.

Kuchunguza tukio la Ahzaab kunathibitisha kwamba walikuwa wako watu wachache tu waliokuwa werevu na wenye busara miongoni mwa jamii hii, au sivyo wangaliuhami uhai wao kwa njia ya kidiplomasia bila ya kujishirikisha na kundi lolote lile (yaani la Uislamu au la ukafiri). Kusema kweli wangalibakia kuwa watazamaji tu wa mapigano yale baina ya Mtume (s.a.w.w.) na jeshi la Waarabu, na upande wowote ule ushindao, uhai wao na nguvu zao vingelibakia.

Hata hivyo, kwa bahati mbaya walidanganywa na wepesi wa kuzungumza wa Hay bin Akhtab na wakajiunga na jeshi la Waarabu, na mkosi wao ukawa mkali mno pale ambapo baada ya kushirikiana na jeshi la Waarabu kwa kipindi cha mwezi mmoja, wakakataa kuwasaidia Waquraishi, na waliponaswa kwenye ule mpango wa Na’im bin Mas’ud waliwapelekea ujumbe Waquraishi ya kwamba hawatawasaidia kupigana dhidi ya Mtume (s.a.w.w.) mpaka Waquraishi wawape baadhi ya watu wao watukufu wawe dhamana.

Kufikia hapa, watu hawa wapumbavu walizipoteza kabisa fahamu zao njema. Hawakutambua kwamba, upande mmoja wameshamwasi Mtume (s.a.w.w.), na hivyo kama upande mwingine wakikataa uhusiano na Waquraishi na ikatokea jeshi la Waarabu likajihisi kuwa ni dhaifu na kurejea makwao na kuacha vita, basi wao (Bani Quraydha) watatiishwa na Waislamu.

Kama wangalipanga mpango sahihi wa kisiasa, mara moja wangalivunja uhusiano wao na jeshi la Waarabu na moja kwa moja wakadhihirisha majuto yao kwa kuyaasi yale mapatano baina yao na

Waislamu, ili waweze kubakia salama kutokana na hatari ya uwezekano wa kushinda kwao (wao Waislamu). Hata hivyo, waliangukia kwenye windo la bahati mbaya kwa vile walikataa uhusiano wao na Waquraishi na vile vile hawakujiunga na Waislamu.

Baada ya kuondoka kwa jeshi la Waarabu, Mtume (s.a.w.w.) hakuweza kuwaacha Bani Quraydha kwa sababu wao (jeshi la Waarabu) katika wakati utakaowafaa wangelirejea tena wakiwa na zana zitoshelezazo na hatimaye kuuteka mji wa Madina na kuuhatarisha uhai wa Uislamu kwa ushirikiano na Bani Quraydha watakaokuwa ufunguo wa ushindi na kushindwa kwa Waislam, na kwa sababu hii walichukuliwa kuwa ni maadui wa ndani. Kwa sababu hii utatuzi wa suala hili la Bani Quraydha na kumalizika kwa jambo lao kulikuwa jambo lihusulo uhai wa Waislam.

Usaliti Wa Abu Lubabah

Baada ya kuzingirwa, Wayahudi wa Bani Quraydha walimwomba Mtume (s.a.w.w.) awapelekee Abu Lubabah wa kabila la Aws ili waweze kumtaka ushauri.

Abu Lubabah alikuwa tayari kaishafanya mapatano ya urafiki na Bani Quraydha. Alipowasili kwenye ngome ile wanaume na wanawake walimkusanyikia huku wakilia na kusema; “Je, ni sahihi kwamba tusalimu amri bila ya masharti yoyote?” Abu Lubabah akawajibu akasema: “Ndio.” Hata hivyo alifanya ishara kwa mkono wake kuelekea kwenye koo lake iliyokuwa na maana ya kwamba kama wakifanya hivyo, watakatwa vichwa vyao.

Abu Lubabah alitambua ya kwamba Mtume hatavumilia kuwapo hai kwa jamii ile iliyokuwa adui hatari zaidi kwa Uislam. Hata hivyo, alijuta mno kuyasaliti maslahi makubwa ya Uislamu na Waislamu na kuzifunua siri zao. Hivyo aliitoka ngome ile akiwa anatetemeka na mwenye wasiwasi na akaenda moja kwa moja hadi msikitini. Pale akajifunga kwenye moja ya nguzo za msikiti na akaweka nadhiri ya kwamba kama Allah asipomghufiria, atautumia muda wa maisha yake uliosalia katika hali ile. Wafasiri wa Qur’ani Tukufu wanasema kwamba Aya ifuatayo hapa chini ilifunuliwa kuhusiana na usaliti wa Abu Lubabah: **“Enyi mlioamnini! Msimfanyie khiyana Mwenyezi Mungu na Mtume na msikhini amana zenu na hali mnajua.”** (***Sura al-Anfal, 8:27***).

Taarifa juu ya Abu Lubabah zilimfikia Mtume (s.a.w.w.). Akasema: “Kama angalinijia kabla ya kuweka nadhiri, ningalimwombea msamaha na Allah angalimsamehe, lakini sasa hana budi kusubiri hadi ataposamehewa na Allah.”

Mkewe alikuwa akija wakati wa sala na kufungua zile kamba alizojifungia kwenye ile nguzo. Na baada ya kusali alimfunga tena kwenye nguzo ile. Baada ya siku sita Malaika Mkuu Jibril alikuja mapema wakati wa asubuhi na Aya ifuatayo, wakati Mtume (s.a.w.w.) alipokuwa nyumbani kwa Bibi Ummu Salamah:

وَآخَرُونَ اعْتَرَفُوا بِذُنُوبِهِمْ خَلَطُوا عَمَلًا صَالِحًا وَآخَرَ سَيِّئًا عَسَى اللَّهُ أَنْ يَتُوبَ عَلَيْهِمْ ۚ إِنَّ اللَّهَ غَفُورٌ رَحِيمٌ {102}

"Na wengine waliokiri dhambi zao na wakachanganya vitendo vizuri na vingine vibaya, huenda Allah akapokea toba zao, hakika Allah ni Mwingi wa kusamehe, Mwenye kurehemu." **(*Sura al-Taubah, 9:102*).**

Macho ya Bibi Ummu Salamah yaliuangukia uso wa Mtume (s.a.w.w.) wakati akiwa na tabasamu midomoni mwake. Mtume (s.a.w.w.) alimwambia Bibi huyu: "Allah Amesamehe dhambi ya Abu Lubabah. Amka na uwafikishie watu habari hii njema." Mkewe Mtume (s.a.w.w.) alipowapasha habari watu juu ya habari hizi njema walikimbilia kwenda kumfungua, lakini Abu Lubabah akasema: "Ingalifaa kama yeye Mtume mwenyewe angalifungua kamba zangu." Baadae Mtume (s.a.w.w.) alifika mle msikitini kusali sala ya Alfajiri na akamfungua kamba zile na kumwacha huru.3

Hadithi ya Abu Lubabah ni yenye mafundisho. Kosa lake lilitokana na hisia zake zisizo za busara. Kulia kwa wanaume na wanawake walio wahaini kulimnyima uwezo wake wa kujitawala na hivyo akazifunua siri za Waislamu. Hata hivyo, nguvu za imani yake na kumcha Allah zilikuwa kubwa zaidi kuliko vile na hivyo akatubia mno kwa yale aliyoyatenda kiasi kwamba lile wazo la kuzisaliti siri zile lisipite tena akilini mwake.

Hatima Ya Kundi La Tano

Siku moja Shaas bin Qays alishuka kutoka kwenye ngome akiwa yu mwakilishi wa Wayahudi na akaonana na Mtume (s.a.w.w.). Alimwomba Mtume (s.a.w.w.) aliruhusu kabila la Bani Quraydha lichukue vitu vyao kama walivyofanya Wayahudi wengine na watoke Madina. Hata hivyo, Mtume (s.a.w.w.) hakuikubali rai yake na akasema: "Wasalimu amri bila ya masharti yoyote." Shaas akaisahihisha rai yake na akasema: "Bani Quraydha wako tayari kuwapa Waislamu mali zao na kutoka Madina." Mtume (s.a.w.w.) alikataa kuikubali rai ile pia. 4

Sababu ya Mtume (s.a.w.w.) kutoikubali rai ile ilikuwa dhahiri kabisa, kwa sababu ulikuwako uwezekano wa kwamba, kama lilivyofanya kabila la Bani Nuzayr, watu hawa nao watakapokuwa mbali na Waislamu wangaliweza kuwakabili Waislamu katika njia ya hatari kwa kushirikiana na jeshi la Waarabu wenye kuyabudu masanamu na wangaliweza kuwa sababu ya mauaji zaidi. Hata hivyo, kwa sababu hii Mtume (s.a.w.w.) hakukubaliana na Shaas, aliyerejea kule ngomeni na kuilezea hali ya mambo kwa wakuu wa kabila lile.

Hatimaye Bani Quraydha waliamua kusalimu amri kwa Waislamu bila ya masharti yoyote, au kufuatana na ilivyoelezwa na baadhi ya wanahistoria, wakauukubali uamuzi wa Sa'ad bin Muaaz, waliyekuwa tayari wameshafanya mapatano naye kwa lengo hili, malango ya ngome ile yakafunguliwa. Hivyo Amir

wa Waumini akaingia ngome ile akifuatana na kikosi maalum na kuwanyang'anya silaha Wayahudi wote. Kisha akawaweka kizuizini ndani ya nyumba moja ya Bani Najjar hadi baadae hatima yao ilipoamuliwa.

Kama walivyotendewa Wayahudi wa Bani Qaynaqaa' waliotiwa kizuizini na jeshi la Waislamu hapo awali, walivyosamehewa kwa maombezi ya Bani Khazraj na hasa Abdullah Ubayy, na Mtume (s.a.w.w.) akajiepusha kuimwaga damu yao, watu wa Bani Aws nao walimshikilia Mtume (s.a.w.w.) kwa lengo la kushindana na Bani Khazraji, kwamba kwa vile Bani Quraydha walifanya mapatano nao, angaliweza kuwasamehe.

Hata hivyo, Mtume (s.a.w.w.) hakulikubali ombi lao na akasema: "Ninamwachia Sa'ad bin Mu'aaz mzee na chifu wenu wa Bani Aws atoe uamuzi. Lolote alisemalo nitalikubali." Wale wote waliokuwapo pale waliukubali kwa moyo mmoja upendeleo ule wa Mtume (s.a.w.w.).
Zaidi ya hapo Bani Quraydha wenyewe vile vile walikubali kukubaliana na uamuzi wa Sa'ad Mu'aaz. Kutegemeana na ilivyonukuliwa na Ibn Hishamu na Shaykh Mufid, ni kuwa Wayahudi wa Bani Quraydha walimpelekea ujumbe Mtume (s.a.w.w.) kwamba Sa'ad bin Mu'aaz aliamue jambo lao. 5

Katika siku zile mkono wa Mu'aaz ulikuwa umejeruhiwa kwa kupigwa mshale, naye alikuwa kalazwa kitandani kwa ajili ya matibabu kwenye hema la mwanamke mmoja aliyeitwa Zamidah aliyekuwa stadi wa upasuaji. Mtume (s.a.w.w.) alikuwa akienda pale mara kwa mara kumtazama.

Vijana wa Bani Aws walikwenda na kumleta yule chifu wa kabila lao mbele ya Mtume (s.a.w.w.) kwa taratibu maalum. Sa'ad alipofika, Mtume (s.a.w) alisema: "Ninyi nyote hamna budi kutoa heshima zenu kwa chifu wenu." Wale wote waliokuwapo pale walisimama ili kuonyesha heshima yao kwa Sa'ad. Wale waliofuatana na Sa'ad nao walirudia mle njiani kumwomba kwamba awatendee wema Bani Quraydha na awaokoe kutokana na kifo.

Hata hivyo, kinyume na tukio lote hili, alitoa uamuzi wake kwamba askari wao wote wauwawe, mali zao zigawanywe miongoni mwa Waislamu na wanawake na watoto wao wafanywe kuwa mateka.6

Uchunguzi Juu Ya Uamuzi Wa Busara Wa Sa'ad Bin Mu'aaz

Hakuna shaka juu ya ukweli kwamba kama mapenzi ya hakimu yatazishinda fikira na akili zake, kile chombo cha kisheria huvurugika na utaratibu mzima katika jamii hupatwa na mvurugiko.

Mapenzi ni kama njaa ya uwongo ambayo huonesha madhara na vitu vibaya kuwa vyenye manufaa na faida, wakati ambapo, kwa kutenda juu ya mapenzi hayo masilahi ya maelfu ya watu pamoja na ustawi wa jamii nzima utakuwa umevunjwa.

Mapenzi na hisia za Sa'd bin Mu'z, hali ya kuhuzunisha ya wanawake na watoto wa Bani Quraiyza, hali ya masaibu ya wanaume wao ambao walikuwa kizuizini na fikira ya jumla ya Bani Awsi ambao kwa umakini walisisitiza kwamba hakimu apuuze kosa lao, mambo yote haya yalihitaji kwamba hakimu

aliyeteuliwa na pande zote angetoa hukumu yake juu ya masilashi ya wachache (Bani Quraydha) badala ya upendeleo kwa masilahi ya wengi (Waislamu kwa ujumla), na angewaachia huru wahalifu wa Bani Quraydha kwa kisingizio fulani, au angalau kuwapunguzia adhabu kwa kadiri iwezekanavyo au kutenda juu ya moja ya ushauri uliotajwa hapo juu.

Hata hivyo, mantiki, akili, uhuru na kujitegemea kwa hakimu, na kuyaheshimu maslahi ya watu wote, vyote hivi vilimuongoza kwenye njia ambayo hatimaye aliitumia na akautoa uamuzi wake kwa kuwakata vichwa askari, kuzinyakua mali zao na kuwateka wanawake na watoto wao. Aliufikia uamuzi wake huo kwa kuzizingatia hoja zifuatazo:

Kipindi fulani hapo awali Wayahudi wa bani Quraydha walifanya mapatano na Mtume (s.a.w.w.) chini ya masharti ya kwamba kama wakipigana dhidi ya maslahi ya Uislamu na Waislamu au wakiwasaidia maadui wa Uislamu na kufanya ghasia au kuwachochea watu kupigana dhidi ya Waislamu, wao (Waislamu) watakuwa na haki ya kuwauwa. Hakimu huyu alikuwa na maoni ya kwamba kama akiwaadhibu kwa mujibu wa masharti ya mapatano yale hatakuwa ametenda kinyume na misingi ya haki.

Watu hawa kwa kuyavunja yale mapatano waliuweka mji wa Madina kwenye hali ya hatari kwa muda fulani hivi ukiwa chini ya kivuli cha mikuki ya kijeshi ya Waarabu na wameingia kwenye nyumba za Waislamu na kuwatisha.

Na kama Mtume (s.a.w.w.) asingalichukua hatua ya tahadhari ya kabla na asingalipeleka kikosi kutoka kwenye makao makuu ya jeshi kwenda kwenye sehemu ya ndani zaidi ya mji ili kudumisha amani na utulivu, kulikuwa na uwezekano mkubwa kwamba Bani Quraydha wangalifaulu kuutekeleza mpango wao. Katika tukio lile wangaliwauwa Waislamu, kuzinyakua mali zao na kuwachukua mateka wanawake na watoto wao. Sa'ad bin Mu'aaz alifikiria kwamba kama akitoa hukumu hiyo dhidi yao, hatakuwa ametenda kinyume na ukweli na haki.

Sa'ad bin Mu'aaz aliyekuwa chifu wa kabila la Aws, alikuwa kafanya mapatano na Bani Quraydha nao walikuwa na uhusiano mwema wa kirafiki baina yao. Hivyo basi inawezekana kwamba alikuwa akiitambua sheria ya adhabu ya Wayahudi. Maelezo ya Taurati ya Wayahudi ni haya: "Utakaposongea karibu ya mji kwenda kupigana juu yake, ndipo utakapowapigia ukelele wa amani.

Itakuwa utakapokujibu kwa amani na kukufungulia, ndipo watu wote watakapoonekana humo watakufanyia kazi ya shokoa na kukutumikia. Na kwamba hautaki kufanya amani nawe, laki– ni utafanya vita juu yako, ndipo uuhusuru; na Bwana Mungu wako autiapo mkononi mwako, mpige kila mume aliyemo kwa makali ya upanga; lakini wanawake na watoto, na wanyama wa miji, na vilivyo mjini, vyote navyo ni nyara zake zote, uvitwae viwe mateka kwako; nawe utakula nyara za adui zako alizokupa Bwana Mungu wako. (Kumbukumbu la Torati, 20:10–14.

Inawezekana Sa'd alifikiria kwamba kama yeye aliyeteuliwa kuwa hakimu na pande zote mbili, angaliwaadhibu waasi kwa mujibu wa sheria ya dini yao wenyewe, angekuwa hakutenda jambo lolote

jingine zaidi ya utekelezaji wa haki.

Tunafikiria kwamba sababu kuu iliyomfanya Sa'd bin Mu'aaz atoe uamuzi wake huu, ni kwamba ameona kwa macho yake kwamba Mtume (s.a.w.w.) amewasamehe watu wa Bani Qaynaqaa' kwa maombezi ya Bani Khazraji na ametosheka na kuwapeleka uhamishoni tu nje ya mazingira ya Madina. Watu hawa walikuwa bado hawajaitoka ile nchi ya Kiislamu kabisa pale Ka'ab Ashraf alipokwenda Makka na kutoa yale machozi ya mamba kwa ajili ya wale waliouawa kwenye Vita vya Badr na hakupumzika hadi alipowatayarisha Waquraishi kwa ajili ya vita. Kwa matokeo ya jambo hili vita vya Uhud vilipiganwa. Kwenye vita vile askari sabini wa Uislamu walikufa kishahidi. Hali kadhalika Bani Nuzayr walisamehewa na Mtume (s.a.w.w.).

Hata hivyo, katika kuitikia ishara hii ya huruma waliunda urafiki wa kijeshi na Waarabu na wakaleta vita vya Ahzaab. Na laiti si ule ustadi wa Mtume (s.a.w.w.) na mpango wa kuchimba handaki, Uislamu ungaliangamizwa na maelfu ya Waislamu wangaliuawa.

Sa'ad bin Mu'aaz aliyaona matendo yote haya. Uzoefu wa siku zilizopita haukumruhusu azidiwe nguvu na mapenzi, kwa sababu kulikuwa hakuna shaka kuhusu ukweli kwamba wakati huu wangaliunda ushirikiano wenye nguvu zaidi na wangaliuhatarisha usalama wa kile kituo kikuu cha Uislamu kwa kuyachochea majeshi ya Waarabu kuamka dhidi ya Waislamu pamoja na kuunda mipango mingine. Hivyo basi, aliuchukulia uhai wa kundi hili kuwa ni wenye madhara kabisa kwa jamii ya Waislamu.

Kama sababu hizi zisingelikuwako ingalikuwa muhimu mno kwa Sa'ad bin Mu'aaz kuyaheshimu maoni ya watu wote juu ya jambo hili, kwa sababu chifu wa kabila huhitaji sana kuungwa mkono na watu wake, na kuwaudhi na kuyakataa mapendekezo na maombi yao ni jambo lenye madhara mno kwake. Hata hivyo, aliyafikiria maombi yote haya kuwa kinyume na maslahi ya Waisalamu, na matokeo yake ni kwamba, alizitii kanuni za matumizi ya akili na hoja.

Uthibitisho wa kuona kwake mbele kwa ndani zaidi na hukumu yake ikubalikayo kuwa ya kiakili, ni kwamba wakati wao (Wayahudi) walipokuwa wakichukuliwa kwenda kunyongwa, waliyasema yale yaliyokuwa nyoyoni mwao. Macho ya yule aliyeviwasha vita vile, Hay bin Akhtab yalimwangukia Mtume (s.a.w.w.) wakati ule na akasema: "Mimi sijutii kuwa kwangu adui kwako. Hata hivyo, yeye ambaye Allah anataka amfedheheshe, amefedheheka".7
Kisha aliwageukia watu na kusema: "Msiwe na wasiwasi kutokana na Amri ya Allah. Hatimaye Allah amehukumu mateso na fedheha kwa ajili ya Bani Israeli."

Kutoka miongoni mwa wanawake, mmoja wao aliuawa kwa sababu alimuuwa Mwislamu kwa kumvurumishia jiwe la kijaa mwilini mwake. Na miongoni mwa wale waliohukumiwa kifo, mtu mmoja ambaye ni Zubayr Bata alisamehewa kwa mapendekezo ya Mwislamu mmoja aliyeit– wa Thabit bin Qays, hata wanawake wake na watoto waliachiwa huru na mali yake ilirejeshwa kwake. Watu wanne kutoka miongoni mwa Bani Quraydha walisilimu. Nyara za vita ziligawanywa miongoni mwa Waislamu baada ya kutoa katika hiyo, sehemu moja ya tano (Khums) iliyoangukia kwenye fungu la Idara ya fedha

ya Waislamu. Askari wapanda wanyama walipewa mafungu matatu kila mmoja na wale watembeao kwa miguu walipewa fungu moja kila mmoja. Mtume (s.a.w.w.) alimpa khumsi ya nyara zile Zayd kwa maelekezo ya kwamba aende Najd na kupata farasi, silaha na masrufu ya vita kutokana na bei ya fungu lile.

---

1. Siiratu Ibn Hishamu, Juz. 2. uk. 234; Tarikhut–Tabari, Juz. 2, uk. 245–246.
2. Siiratu Ibn Hishamu, Juz. 2. uk 235.
3. Siiratu Ibn Hishamu, Juz. 2. uk. 237.
4. Maghaazil– Waaqidi, Juz. 2, uk. 501.
5. Irshad Mufid, uk. 50.
6. Siiratu Ibn Hishamu, Juz. 2. Uk. 240, Maghaazil– Waaqidi, Juz. 2, uk. 510.
7. Tarikhut–Tabari, Juz. 2, uk.250.

Sura Ya 39: Matukio Ya Mwaka Wa Tano Na Sita Hijiriya

Mwaka wa Tano wa hijiriya ulikuwa bado haujamalizika pale mashambu– lio ya makabila yaliporudishwa nyuma na uasi wa Bani Quraydha nao ukakomeshwa. Mji wa Madina na viunga vyake ukaja kabisa chini ya utawala wa Waislamu. Misingi ya ile Dola changa ya Uislamu iliimarika na utulivu wa kiasi fulani ulianza kuweko kwenye zile nchi za Kiislamu. Hata hivyo utulivu huu ulikuwa wa muda tu. Ilikuwa muhimu kwamba Mtume (s.a.w.w.) aendelee kuyaangalia mambo ya maadui na kukomesha mapatano yote ya kufanya mabaya dhidi ya Uislamu, tangu mwanzoni kabisa kwa msaada wa majeshi yawezayo kupatikana.

Utulivu uliokuwako kwenye mazingira ulitoa fursa ya kuwaadhibu baadhi ya wale watu waliowasha vita vya Ahzaab na kisha wakaenda nje ya mamlaka ya Waislamu baada ya yale makabila kuvunja kambi. Hay bin Akhtab aliyekuwa mmoja wa watu wale aliyefanya machocheo ya kwanza katika vita vya Bani Quraydha, alikuwa miongoni mwa Wayahudi walionyongwa kwenye ile adhabu ya Bani Quraydha, lakini rafiki yake Sall?m bin Abi Haqiq alikuwa akiishi Khaybar. Ulikuwa ni ukweli uliokubalika kwamba mtu huyu wa hatari hatatulia mpaka pale atakapoyachochea tena makabila kuamka dhidi ya Waislamu, hasa kwa sababu Waarabu waabudu masana– mu walikuwa wako tayari kupigana vita dhidi ya Uislamu na kama gharama za vita zingethibitishwa, hali ya vita vya Ahzaab ingeliweza kurudiwa tena.

Akiyazingatia mambo haya, Mtume (s.a.w.w.) aliwateua watu mashujaa wa kabila la Khazraji kuwaondoshea mbali Waislamu mtu huyu mfidhuli na mkorofi. Hata hivyo, kazi hii iliwekewa masharti ya kwamba wasiinyanyase familia yake. Wale mashujaa wa Khazraji walifika Khaybar wakati wa usiku na

wakayafunga kwa nje malango ya nyumba zilizokuwa zikipakana na ya Sall?m, ili kwamba kama ikiwapo kelele yoyote ile majirani zake wasiweze kuzitoka nyumba zao. Kisha kwa kutumia ngazi waliifikia gorofa ya kwanza ya nyumba ile aliyokuwa akiishi Sall?m. Waligonga mlango, mkewe akatoka na kuwauliza walikuwa ni akina nani. Wakajibu: “Sisi ni Waarabu na tunayo shughuli fulani na chifu. Tunahitaji nafaka.”

Mkewe Sall?m alidanganyika kwa maelezo yale, akaufungua mlango bila ya kuthibitisha na akawaongoza chumbani kwa Sall?m, ambaye ndio kwamba amelala. Ili kuzuia kila aina ya makelele, walikiin– gia chumba kile upesi sana, wakaufunga mlango na kuyamalizia mbali maisha ya mtu huyu wa hatari na mfisadi aliyewanyima Waislamu amani yao ya kifikara kwa muda mrefu sana. Kisha wakashuka upesi upesi na kujificha kwenye sehemu ya kuingizia maji, nje ya ngome ile.

Vilio vya mkewe Sall?m viliwaamsha majirani na wote wakaanza kuwafuata wale mashujaa wa Khazraj wakiwa wameshika taa mikononi mwao. Hata hivyo, ingawa walitafuta sana lakini hawakuziona dalili zao zozote zile na hatimaye walirejea majumbani mwao. Ushujaa wa Waislamu wale ulikuwa mkubwa sana kiasi kwamba mmoja wao alijitolea kwenda miongoni mwa Wayahudi kwa kujificha ili akapate taarifa za matokeo ya yale waliyoyafanya (yaani wao Waislamu), kwa kuwa walikuwa wakidhania kwamba Sallaam alikuwa hado yu hai.

Alikwenda na kuingia kwenye kundi la Wayahudi wakati walipokuwa wamemzunguka Sall?m, na mkewe alikuwa akitoa taarifa kamili ya yale yaliyotokea, na kwa ghafla aliutazama uso wa Sall?m na akasema: “Kwa jina la Mola wa Wayahudi! Ameshafariki dunia!” Yule Mwislamu aliyekwenda pale kupata taarifa alirejea na kuwaambia wenzie juu ya ile hali ya mambo. Hivyo wakayatoka mafícho yao na kurejea Madina. Huko wakamweleza Mtume (s.a.w.w.) yale yote yaliyotokea.1

Kikundi Cha Waquraishi Chaenda Ethiopia

Kikundi cha Waquraishi waonao mbali walitishika mno na maendeleo ya daima ya Uislamu hivyo walikwenda Ethiopia ili wakaishi huko. Walifikiria kwamba, kama mwishowe Muhammad atapata mamlaka juu ya Rasi yote ya Uarabuni, basi watakuwa tayari wameshakuwa salama kule Ethiopia na kama Waquraishi watashinda watarudi maskani mwao.

Amr bin Aas alikuwa mmoja wa watu wa kikundi hiki kilichotoka Hijaz kwenda Ethiopia kikiwa na zawadi nyingi. Kuwasili kwao kulitukia pamoja na kuwasili kwa mjumbe wa Mtume (s.a.w.w.) aliyeitwa Amr bin Umayyah aliyeleta ujumbe wa Mtume (s.a.w.w.) kuhusiana na Ja’far bin Abi Talib na Muhajiriin wengine. Ili kuupata upendeleo wa machifu wa Waquraishi, ‘Amr bin Aas aliwaambia wenzie: “Ninakwenda kuomba kukutana na Mfalme wa Ethiopia pamoja na zawadi zangu maalum nami nitaiomba idhini ya kukatwa kwa kichwa cha mjumbe wa Muhammad.”

Alifika kwenye baraza la kifalme na akakunja goti moja ili kuonyesha heshima kwa mfalme, kufuatana na desturi za kale. Mfalme alizungumza naye kwa upole na akasema: “Je, mmeniletea zawadi zozote zile

kutoka nchini mwenu?” akajibu akasema: “Ndio, Jalali Mfalme.” Kisha akaziwakilisha zawadi zile na akasema: “Jalali Mfalme! Yule mtu aliyetoka hapa barazani kwako hivi karibuni yu mjumbe wa mtu aliyewauwa wazee na mashujaa wetu. Litakuwa jambo la faraja mno kwetu kama nitaruhusiwa kukikata kichwa chake ikiwa ni hatua ya kulipiza kisasi.”

Maneno ya ‘Amr bin Aas yalimkasirisha mno Negus kiasi kwamba bila ya kupenda alijipiga kofi la nguvu mno usoni mwake kiasi kwamba karibuni aivunje pua yake. Kisha kwa ghadhabu akasema: “Je, unaniomba nimsalimishe kwako mjumbe wa mtu aliyeshukiwa na Malaika Mkuu, kama alivyokuwa akimshukia Nabii Musa, ili umuue? Ninaapa kwa jina la Allah! Yeye yu mkweli na atawashinda maadui zake.” Amri bin Aas anasema: “Nilipoyasikia maneno haya nilipatwa na mwelekeo wa kwenye dini ya Mtume Muhammad lakini sikulidhihirisha jambo hili kwa wale wenzangu.”2

Kuzuia Kurudiwa Kwa Matukio Machungu

Tukio chungu na lisilopendeza la Raji’, ambalo matokeo yake ni kwamba familia za Azal na Q?rah waliotokana na kabila la Bani Lihyan waliwauwa watu wa kikundi cha wahubiri wa Uislamu kwa njia ya kikatili na ya woga kabisa, na hata kuwakamata watu wawili waliokuwa hai na kuwauza kwa Waquraishi wenye mamlaka ambao waliwanyonga, ikiwa ni hatua yao ya kulipiza kisasi, liliwahuzunisha mno Waislamu na kuisimamisha misafara ya kikundi cha wahubiri. Sasa kwa kuwa vile vizuizi vyote likuwa vimeondolewa kutoka kwenye ile njia ya Waislamu na ghasia zilizosababishwa na yale makabila ya Waarabu na Wayahudi nazo zimekomeshwa, Mtume wa Usilamu (s.a.w.w.) alifikiria kwamba sasa inafaa kuwaadhibu Bani Lihyan ili kwamba makabila mengine yazingatie wajibu wao na wasije wavisumbue vikundi vya wahubiri wa Kiislamu.

Katika mfunguo tano (Jumadiul Awwal) mwaka wa sita Mtume (s.a.w.w.) alitoka mjini Madina akamteuwa Ibn Ummi Maktum kuwa mwakilishi wake.
Hakumwarifu mtu yeyote yule juu ya lengo lake. Kwa kuwa aliche– lea kwamba Waquraishi na Bani Lihy?n watautambua mpango wake. Hivyo basi, akaishika njia ya Kaskazini iliyokuwa ikienda Shamu, na baada ya kusafiri kwa umbali fulani hivi, akabadili njia yake na akapiga kambi mahali paitwapo Ghar?n palipokuwa nchi ya Bani Lahy?n. Hata hivyo, maadui wale walilitambua lengo lake na wakakimbilia vilimani.

Shambulio hili la silaha na kufedheheshwa kwa adui lilikuwa na athari za kisaikolojia, hatimaye waliogopa mno na kufadhaika.

Ili kulifikia lengo lake, Mtume (s.a.w.w.) alifanya hila za kijeshi na yeye mwenyewe alikwenda na watu mia mbili kutoka pale Ghar?n hadi Asfaan mahali palipo karibu na Makka. Kisha akapeleka watu kumi kwenye mpaka wa Makka (Kiraa’ul Ghamim) katika wadhifa wa kikundi cha watalii katika hali ambayo mwenendo wa askari wa Uislamu na uoneshaji wa nguvu yao uweze kuonekana kwa Makureishi. Baada ya hapo alitoa amri ya kuvunja kambi na kurejea Madina.

Jabir bin Abdulah anasema kwamba baada ya kurejea kutoka kwenye vita hivi, Mtume (s.a.w.w.) alisema: “Najikinga kwa Allah kutokana na usumbufu wa safari, taabu za usafiri na matukio yasiyopendeza kwenye maisha ya kimali na kifamilia ya mwanadamu.”3

Vita Ya Ziqarad

Siku chache tu baada ya kurejea kwa Mtume (s.a.w.w.) mjini Madina, Uyainah bin Hisn Faz?ri alinyakua kundi la ngamia lililokuwa likilisha kwenye malisho ya Madina, akamuua mchungaji wao na kumteka mwanamke wa Kiislamu na akaenda naye. Salamah Aslami aliyekuwa katoka mji wa Madina kwa ajili ya kuwinda alilishuhudia tukio hili. Mara moja alikwenda kwenye kichuguu cha Sala na kuwaita Waislamu waje wasaidie na akasema: “W? Sab?h?” (Waarabu walikuwa wakiitamka sentensi hii walipokuwa wakihitaji msaada). Kisha akawafuatia wale wanyang’anyi na kwa kuwatupia mishale aliweza kuwazuia wasikimbie.

Mtume (s.a.w.w.) alikuwa mtu wa kwanza kumsikia Salamah akiomba msaada. Mara moja akawapeleka baadhi ya masahaba zake kuwafuatilia wanyang’anyi wale. Mapigano madogo yalitokea baina yao. Kwenye mapigano hayo Waislamu wawili na watu watatu wa upande wa wanyang’anyi waliuwawa. Hata hivyo, Waislamu walifaulu kurudisha sehemu kubwa ya ngamia wale kutoka kwa wale wanyang’anyi pamoja na kumpata yule mwanamke wa Kiislamu. Hata hivyo yule adui alijificha kwenye ukanda wa kabila la Ghatfaan. Mtume alikaa kwenye sehemu itwayo ‘Ziqarad’ kwa mchana mmoja na usiku. Ingawa askari wapanda wanyama wa Madina walishikilia kwamba yule adui afuatiliwe, lakini Mtume (s.a.w.w.) hakulifikiria jambo hilo kuwa ni lenye kufaa kutendwa na akarejea Madina.4

Nadhiri Isiyokubalika

Yule mwanamke aliyetetewa hadi akaachiliwa na wale wanyang’anyi alikuja mbele ya Mtume (s.a.w.w.) na kusema: “Nilipokuwa nikichukuliwa mateka pamoja na wale ngamia (alimsoza kidole ngamia mmoja wa Mtume s.a.w.w) niliweka nadhiri ya kwamba kama nikitoka mkononi mwa adui yule nitamchinja ngamia huyu.” Mtume (s.a.w.w.) akamwambia huku akitabasamu: “Umeamua kumpa malipo mabaya kiasi gani ngamia huyu! Alikupatia uhuru wako nawe unataka kumwua?” Kisha akalifafanua jambo lile na kusema: “Nadhiri yenye kuihusu dhambi au iwekwayo kuhusiana na kitu kilicho mali ya mtu mwingine hairuhusiwi. Kwa nadhiri yako hiyo ulimweka ngamia wangu. Hivyo si wajibu juu yako kuitekeleza nadhiri yako.”5

---

1. Siiratu Ibn Hishamu, Juz. 2. uk. 274–275.
2. Siiratu Ibn Hishamu, Juz. 2. uk. 276–277.
3. Tarikhut–Tabari, Juz. 2, uk. 254; Maghaazil–Waaqidi Juz. 2, uk. 535.
4. Tarikhut–Tabari, Juz. 2, uk. 255; Maghaazil–Waaqidi Juz. 2, uk. 255.
5. Siiratu Ibn Hisham, Juz. 2, uk. 280;

Sura Ya 40: Matukio Ya Mwaka Wa Sita Hijiriya

Katika mwaka wa sita hijiriya uwezo wa kijeshi wa Waislamu ulikuwa na nguvu ya kuonekana hivi, kiasi kwamba vikosi vyao maalum viliweza kuziendea sehemu zilizo karibu na Makka bila kipingamizi kisha vilirejea. Hata hivyo, nguvu hizi za kijeshi hazikukusanywa kwa lengo la kuteka nchi za makabila au kuzinyakua mali zao.

Kama washirikina wasingeliwanyima Waislamu uhuru wao, Mtume (s.a.w.w.) asingelinunua japo upanga mmoja na asingelipeleka japo askari mmoja. Hata hivyo, kwa kuwa Waislamu na vikundi vyao vya wahubiri walikuwa daima wakitishwa na maadui, Mtume (s.a.w.w.) kwa kila hali na kwa kimaadili alilazimika kuiimarisha nguvu ya kiulinzi ya Uislamu.

Sababu hasa ya vita hivi vilivyotekea hadi kwenye mwaka wa sita hijiriya, na kusema kweli, hadi dakika ya mwisho ya uhai wa Mtume (s.aw.w.) zilikuwa zifutazo:Kuyajibu mashambulizi ya kutisha yaliyofanywa na wale waabudu masanamu, (kama vile Vita vya Badr, Uhud na Vita vya Handaki).

Kuwaadhibu madhalimu waliowaua Waislamu au vikundi vya wahubiri wao katika majangwa au katika sehemu za mbali, au wale waliovunja mapatano waliyoyafanya baina yao na Waislamu. Kwenye kundi hili ni vile vita vyilivopiganwa dhidi ya makabila ya Wayahudi na ile moja iliyopiganwa dhidi ya Bani Lihy?n.

Kuyeyusha ile shauku iliyokuwa ikipikwa miongoni mwa makabila yaliyotaka kukusanya majeshi na kuushambulia mji wa Madina. Mapigano mengi madogo yalitokea kutokana na sababu hii.

Vita Vya Bani Mustaliq

Bani Mustaliq walikuwa ni tawi la Khuz?'?h waliokuwa majirani wa Waquraishi. Taarifa zilifika Madina kwamba Harith bin Abi Zir?r (chifu wa kabila lile) amedhamiria kuuzingira mji wa Madina. Kama alivyofanya katika matukio mengine, Mtume (s.a.w.w.) aliamua kuuzuia ufisadi huu, hivyo basi akaliendea kabila la Bani Mustaliq akifuatana na masahaba zake na kuwakabili karibu na kisima cha Marysi'. Mapigano yalianza baina ya pande mbili. Ushujaa wa Waislamu na woga ulioyashika makabila ya Waarabu juu ya jambo hili uliwafanya maadui kutawanyika baada ya mapigano madogo madogo ambayo ndani yake watu wao kumi na kwa makosa Mwislamu mmoja, waliuwawa. Matokeo ya vita hivi ni kwamba, ngawira nyingi ziliangukia kwenye fungu la jeshi la Uislamu na wanawake wa maadui nao walichukuliwa mateka.1

Nukta zenye mafunzo za vita hivi ni sera alizozifuata Mtume (s.a.w.w.) baada ya vita, akiyazingatia matukio ya vita hivi.

Hata hivyo, mifarakano ilizuka baina ya Muhajiriin na Ansar kwa mara ya kwanza kabisa, lakini laiti si

kupatikana busara za Mtume (s.a.w.w.) umoja wao ungalivunjika kutokana na tamaa ya mali ya baadhi ya watu wasioona mbali.

Sababu ya tukio hili ilikuwa kwamba, baada ya kwisha kwa vita vile Waislamu wawili, mmoja akiitwa Jahj?h bin Mas'ud (Muhajir) na mwingine akiitwa Sin?n Juhani (Ansar) waligombana kuhusu maji. Kila mmoja aliwaita watu wake ili wamsaidie, matokeo ya miito hii ya kuomba msaada yangelikuwa kwamba Waislamu wapigane wenyewe kwa wenyewe mahali palipokuwa mbali kutoka kwenye makao yao makuu, na kwa kufanya hivyo wangeliumalizia mbali uhai wao wenyewe. Mtume (s.a.w.w.) alilitambua tukio lile na akasema: "Waacheni hawa watu wawili wenyewe. Mwito huu wa msaada wenye kuchukiza unaofanana na masazo ya kisirani cha ujinga bado haujatoka kutoka nyoyoni mwao.
Watu hawa wawili hawana ujuzi wa mpango wa Uislamu na hawajui ya kwamba Uislamu huwachukulia Waislamu wote kuwa ni ndugu wao kwa wao na kila mwito wenye kuleta mifarakano ni kinyume na dini ya Upweke wa Allah."2

Mnafiki Mmoja Apepea Miali Ya Mfarakano

Kwa njia hii Mtume (s.a.w.w.) alizizuia tofauti na akayazuia makundi hayo mawili yasishambuliane. Hata hivyo, Abdullah bin Ubayy mmoja wa wanafiki wa Madina aliyekuwa na mfundo usio kifani dhidi ya Uislamu naye alikuwa akishiriki kwenye vita vile kwa sababu tu ya kupata fungu la ngawira, aliudhihirisha uadui na unafiki wake na akawaambia wale waliomkusanyikia hivi: "Yote haya ni matokeo ya matendo yetu wenyewe.

Tumewapa amani Muhajiriin nchini mwetu na tukawahami kutokana na maadui zao. Hali yetu inalandana na methali maarufu isemayo; 'Mlishe mbwa wako naye atakuuma' Naapa kwa jina la Allah! Tutakaporejea Madina itakuwa muhimu kwamba watu wenye nguvu na watukufu (wa Madina wawatoe wale walio dhaifu (yaani Muhajirin)."

Maneno ya Abdulah mbele ya watu ambao akilini mwao mlikuwa bado mmejibanza moyo wa kundi la Uarabu na fikara za zama za Ujinga, yalikuwa na athari zenye madhara juu yao na iliwezekana kwamba umoja wao uhatarike kabisa.

Hata hivyo, kwa bahati nzuri Mwislamu mmoja aliyekuwa na moyo aliyeitwa Zayd bin Arqam aliyekuwa pale, naye aliyajibu maneno yake ya kishetani kwa nguvu zote na akasema: "Ninaapa kwa jina la Allah! Wewe ndiwe mtu uliye duni na uliyefedheheka. Wewe ndie mtu asiyefaidi cheo chochote kile, japo kilicho kidogo sana miongoni mwa ndugu zake. Kinyume chake, Mtume Muhammad yu mwenye kuheshimika miongoni mwa Waislamu na nyoyo zao zimejawa na huba juu yeke."

Kisha alitoka pale na kumjia Mtume (s.a.w.w.) na kumwarifu juu ya maneno ya uchochezi ya Abdullah. Ili kuonyesha kwamba maneno ya Abdullah hayakumkasirisha, Mtume (s.a.w.w.) aliyakataa maneno ya Zayd mara tatu na kusema: "Pengine wewe umekosea. Pengine hasira zimekufanya useme hivyo. Inawezekana kwamba yeye anakufikiria kuwa u duni na mjinga na wala hakuwa na maana nyingine."

Hata hivyo, Zayd aliukanusha uwezekano wa aina zote hizo na kusema: “Hapana; nia yake ilikuwa kuleta tofauti na kuwasha mifarakano.”

Khalifa wa Pili alimwomba Mtume (s.a.w.w.) amruhusu amuue Abdullah. Hata hivyo Mtume (s.a.w.w.) alimjibu hivi: “Si sahihi kufanya hivyo kwa sababu watu watasema kwamba Muhammad anawauwa marafiki zake.”3

Abdullah aliyafahamu yale mazungumzo ya Zayd bin Arqam na Mtume (s.a.w.w.). Upesi sana alikuja mbele ya Mtume (s.a.w.w.) na kusema: “Katu mimi sikuyasema maneno hayo.” Baadhi ya watu waliokuwa pale walimtakia mema nao walimuunga mkono na kusema kwamba: Zayd amekosea katika kuyanukuu maneno yake.

Hata hivyo jambo hili halikuishia pale, kwa sababu utulivu wa muda ni kama kitulizo katika dhoruba. Yule kiongozi mtukufu wa Uislamu alitaka kufanya jambo fulani litakaloweza kuyafanya yale makundi mawili husika walisahau kabisa jambo hili. Ili kufikia hatima hii, aliwaamrisha watu waondoke ingawa wakati ule haukuwa muda wa kuondokea.

Usayd alimjia Mtume (s.a.w.w.) na kusema: “Huu si muda ufaao kuondoka. Nini sababu ya amri hii?” Mtume (s.a.w.w.) alimjibu akisema: “Je, wewe huifahamu kauli ya Abdillah na kile alichokiwasha?” Usayd aliapa na kusema: “Ewe Mheshimiwa Mtume! Nguvu iko mikononi mwako. Unaweza kumtoa nje. Wewe ni kipenzi mwenye kuheshimiwa. Aliye duni na aliyefedheheshwa ni yeye. Kuwa mwenye huruma kwake kwa kuwa yeye yu mtu aliyeshindwa. Kabla ya kuhamia kwako Madina Aws na Khazraj walikubaliana kumfanya Mtawala wa Madina na walikuwa wakifikiria kukusanya vito vya thamani ili aweze kutengenezewa taji la kumtawazia. Hata hivyo, kwa kuchomoza nyota ya Uislamu cheo chake kilipatwa na mabadiliko na watu wakamwacha. Na anakufikiria kuwa ndiwe sababu ya yote haya.”

Ilitolewa amri ya kuondoka na askari wa Uislamu waliendelea kutembea kwa zaidi ya masaa ishirini na manne, nao hawakutua mahali popote pale ila kwa ajili ya kusali tu. Siku ya pili hali ya hewa ilikuwa yenye joto sana na wote walikuwa wameshapoteza nguvu yao kiasi cha kutoweza kuendelea zaidi na safari, na hapo ilitolewa amri ya kupiga kambi. Mara tu baada ya kushuka kwenye wanyama wao wa kupanda, wote walilala kwa sababu ya uchovu na kumbukumbu zote za uchungu ziliondoka akilini mwao. Hivyo basi, kwa mpango huu mifarakano yao ilipungua.4

Mgongano Baina Ya Imani Na Hisia Za Askari Mmoja

Mwana wa Abdulah bin Ubay alikuwa Mwislamu mchamungu. Kwa mujibu wa mafundisho matakatifu ya Uislamu, alikuwa na huruma zaidi kwa baba yake kuliko yeyote mwingine, ingawa yeye baba mtu alikuwa mnafiki. Alipata kutambua kuhusu yale aliyoyatenda baba yake na akafikiria ya kwamba Mtume (s.a.w.w.) atamuuwa. Hivyo akamwambia Mtume (s.a.w.w.): “Kama imeamuliwa kwamba baba yangu anyongwe, mimi mwenyewe niko tayari kuitekeleza hukumu hiyo nami naomba kazi hiyo asipewe yeyote mwingine.

Ninaomba hivi kwa sababu ninachelea kwamba, kutokana na hisia za Kiarabu na mielekeo ya mvuto wa mtoto kwa baba yake, ninaweza kuipoteza nguvu yangu ya kujitawala na nikamuuwa mtu yule amnyongae baba yangu na kwa kufanya hivyo nikaipaka mikono yangu damu ya Mwislamu na matokeo yake yakawa ni kuyaharibu maisha yangu."

Maelezo ya mtu huyu ni midhihiriko iliyo bora zaidi ya imani. Kwa nini mtu huyu hakumwomba Mtume (s.a.w.w.) kumsamehe baba yake? Hakufanya hivyo kwa sababu alijua chochote kile alichokifanya Mtukufu Mtume kilikuwa kikiendana na amri ya Allah swt. Hata hivyo huyu mwana wa Abdullah alijikuta akiwa kwenye mashaka ya kisaikolojia. Mvuto wa huba ya mtoto kwa baba na kanuni za utu wema barani Arabia vilimhimiza kumlipiza kisasi myongaji wa baba yake, na kuwa kufanya hivyo akawa ameimwaga damu ya Mwislamu. Kwa upande mwingine, huba ya amani kwenye ukanda wa Uislamu ilimfanya afikiri kwamba ilikuwa muhimu kwamba baba yake auawe.

Ili kuushinda mgongano uliomo akilini mwake, aliichagua njia ya tatu ili kwamba yale maslahi ya Uislamu yaliyo bora zaidi yabakie katika hali ya usalama na vile vile upenzi kwa baba yake usipatwe na madhara. Na ile njia ya tatu ilikuwa iwe ya kwamba yeye mwenyewe aitekeleze amri ya kunyongwa kwa baba yake. Ingawa kitendo hiki ni chenye kuadhibu na kuupasua moyo, lakini ile nguvu ya imani na kujitolea kwa ajili ya mapenzi ya Allah hutoa faraja kwa kiasi fulani.

Hata hivyo, Mtume mwenye huruma alimwambia: "Hakuna jambo la aina hiyo linalodhamiriwa, nami nitakuwa mpole kwake."

Maelezo hayo yalienea miongoni mwa Waislamu nao wote walishangazwa na ukuu wa kiroho wa Mtume (s.a.w.w.). Manyunyu ya mikanusho na makemeo alinyunyuziwa Abdullah. Alifedheheka mno mbele ya macho ya watu kiasi kwamba baada ya hapo hakuna tena aliyemsikiliza.

Katika matukio haya Mtume (s.a.w.w.) aliwafunza Waislamu mafunzo yenye kumbukumbu kwa daima na akazidhihirisha baadhi ya sera za kisiasa za Uislamu zenye busara. Baada ya tukio hili, yule kiongozi wa wanafiki hakuwa na mvuto tena na alichukiwa na akadharauliwa na watu kwenye mambo yote. Safari moja Mtume (s.a.w.w.) alimwambia Umar: "Uliomba ruhusa yangu umuue. Wale watu ambao katika siku ile wangelishitushwa na kuuwawa kwake na wakaamka na kumwunga mkono, leo hii wanamchukia mno kiasi kwamba kama nikitoa amri ya kumyonga, watamuuwa palepale."

Mtume (S.A.W.W) Amuoa Juwayriyah

Mtume (s.a.w.w.) alimwoa binti wa Harith, kiongozi wa waasi. Katika vitabu mbalimbali vya maisha ya Mtume (s.a.w.w.) maelezo tofauti tofauti juu ya ndoa hii hutolewa. Hata hivyo, matokeo ya ndoa hii yalikuwa kwamba uhusiano usiovunjika ulidumishwa baina ya Mtume (s.a.w.w.) na jumuiya hii na wengi wa wanawake wa kabila hili waliokuwa wametekwa na Waislamu waliachiliwa bila ya masharti yoyote ikiwa ni ishara ya heshima kwa uhusiano baina yao na Mtume (s.a.w.w.). Ndoa hii ilikuwa ndoa iliyobarikiwa kwa sababu ilitoa matokeo ya kuachiliwa kwa wanawake mia moja.5

1. Tarikhut-Tabari, Juz. 2, uk. 260.

2. Maelezo ya Suhayli juu ya Siiratu Ibn Hisham.

3. Kuchunguza maisha ya khalifa wa Pili kunaudhihirisha ukweli uliopo kwamba katu hakuzidhihirisha nguvu zake kwenye uwanja wa vita na daima alikuwa kwenye mistari ya nyuma. Hata hivyo, kila alipokamatwa adui, alikuwa mtu wa kwanza kumwomba Mtume (s.a.w.w.) amruhusu amwue. Ifuatayo hapa chini ni baadhi ya mifano ya aina hii: (i.) Mmoja wa mifano ya aina hii ulikuwa kwamba alitaka kumwua Abdullah Mnafiki. (ii.) Muda mfupi kabla ya kutekwa kwa mji wa Makka alimwomba Mtume (s.a.w.w.) ampe ruhusa akidengue kichwa cha Haatib bin Abi Balti'ah aliye kuwa akiwafanyia ujasusi waabudu masanamu katika jeshi la Waislamu. (iii) Wakati Abbas, ami yake Mtume (s.a.w.w.) alipomleta Abu Sufyani kwenye kambi ya Wasilamu, yeye (Khalifa wa Pili) alimwomba Mtume (s.a.w.w.) amruhusu amwue (yaani Abu Sufyani) mara moja.

4. Tarikhut-Tabari, Juz. 2, uk. 261-262; Majma'ul Bayaan, Juz. 10, uk. 292-295.

5. Siiratu Ibn Hisham, Juz. 2, uk. 264.

Sura Ya 41: Safari Ya Kidini Na Kisiasa

Mwaka wa sita ulikuwa ukimalizikia na matukio yake yote machungu na matamu pale kwa ghafla Mtume (s.a.w.w.) alipoiota ndoto yenye kupendeza kwamba Waislamu walikuwa wakizifanya ibada za Hajj kwenye Masjidu'l-Haram. Aliwasimulia masahaba zake ndoto hii nao wakaichukulia kuwa ni ndege njema kwa Waislamu kwa kuwa karibuni tu watalifikia lengo lao lililokuwa likiwatia kiherehere mno nyoyoni mwao.1

Mtume (s.a.w.w.) aliwaamrisha Waislamu wajitayarishe kuifanya safari ile ya kwenda Hijja na pia aliyaalika makabila ya jirani waliokuwa bado ni washirikina kufuatana na Waislamu kwenye safari ile. Vile vile alitangaza katika sehemu zote za bara Arabu kwamba Waislamu watakwenda Makka katika mwezi wa Dhil Qa'ad.

Safari hii ya kiroho, ukiachilia mbali kule kuwa kwake na faida za kiroho, vile vile ilikuwa na kiwango fulani ya faida za kijamii na kisiasa. Ilikifanya kuwa bora zaidi cheo cha Waislamu kwenye Rasi ya Uarabuni nayo ikawa njia ya kuuenezea Uislamu miongoni mwa Waarabu kutokana na mambo yafuatayo:

1. Makabila ya Waarabu waliyokuwa washirikina yalikuwa yakidhania kwamba Mtume (s.a.w.w.) alikuwa akizikana itikadi na ibada zao zote zile za kitaifa na zile za kidini ikiwa ni pamoja na Hijja na 'Umrah, ibada zilizokuwa kumbukumbu ya jadi zao, na kwa sababu hii walimwogopa Mtume (s.a.w.w.) na dini yake. Kushiriki kwa Mtume (s.a.w.w.) na masahaba zake kwenye ibada ya Hija na 'Umrah kwenye safari hii kungeweza kuipunguza ile hofu na wasiwasi akilini mwa baadhi ya makabila ya Waarabu washirikina, na kuwadhihirishia kivitendo kuwa, sio tu kwamba Mtume (s.a.w.w.) hakuipinga Hija ya Nyumba ya Allah na ibada ya Hija, jambo lililo moja ya ibada zao za kidini na kumbukumbu zao za kitaifa, bali anaifikiria kuwa ni tendo lililo wajibu.

Aidha, vile vile alikuwa akijitahidi kama alivyofanya jadi wake Nabii Isma'il (a.s.) katika kuzihuisha na kuzihifadhi ibada hizi. Kwa njia hiii, aliweza kuyavutia kwake yale makabila yaliyoufikiria Uislamu kuwa ni wenye kuzipinga kabisa kumbukumbu zao za kitaifa na kidini na aliweza kuipunguza hofu yao.
2. Kama Waislamu wakifaulu kuitekeleza Hija na kuweza kuyatekeleza majukumu yao ya kidini kwa uhuru kabisa kwenye Masjidu'l–Haram, mbele ya macho ya Waarabu washirikina, kitendo hiki kitakuwa ni chanzo kikuu cha kuuhubiri Uislamu, kwa sababu kwenye majira ya Hajj washirikina na Waarabu kutoka kwenye sehemu zote za Penisula ile watakusanyika mjini Makka na wakati wa kurejea makwao, watazichukua taarifa juu ya Waislamu. Kwa njia hii, ujumbe wa Uislamu utazifikia sehemu zote hizo ambazo Mtume (s.a.w.w.) hakuweza kuzipelekea wahubiri na utakuwa na athahri zake pale.

3. Mtume (s.a.w.w.) aliwakumbusha watu wa Madina juu ya ule mwezi mtakatifu na akasema: "Tunakwenda kwenye Hija ya Nyumba ya Allah." Vile vile aliwaamrisha Waislamu kutochukua silaha yoyote ile ila upanga ambao kwa kawaida msafiri aliuchukua anaposafiri. Matendo yake haya yaliwafanya watu wengi wasiokuwa Waislamu wauelekee Uislamu, kwa sababu, kinyume na propaganda walizokuwa wakizifanya Waquraishi dhidi ya Uislamu, waliona kwamba kama walivyo watu wengine, Mtume (s.a.w.w.) naye aliyachukulia mapigano kwenye miezi hii kuwa ni haramu na ilikuwa katika kuipendelea kama miezi mitakatifu ya amani.

Mtume (s.a.w.w.) alifikiria kwamba, kama Waislamu wakifaulu katika wakati ule watakuwa wameifikia moja ya shauku zao kubwa (yaani kuzitekeleza ibada za 'Umrah na Hija), na wale waliokuwa mbali kutoka maskani mwao wataweza kukutana na ndugu na marafiki zao. Na kama wakikumbwa na kizuizi, Waquraishi watakipoteza cheo chao kwenye ulimwengu wa Kiarabu, kwani wawakilishi wa makabila yasiyounga mkono upande wowote (ule wa Waislamu wala ule wa Waquraishi) wataona jinsi Waquraishi watakavyowatendea Waislamu.

Watashuhudia Waisilamu walitaka kufanya 'Umrah na Hija ilihali hawakuwa wamechukua silaha zozote zile ila ile silaha ya msafiri, na ingawa Masjidu'l–Haram na ibadi za Hija ni kwa Waarabu wote, na Waquraishi ni wadhamini tu wa Haram ile, lakini waliwazuia. Hivyo basi, hapo unyoofu wa Waislamu na uonevu wa Waquraishi vitadhihirika, na Waquraishi hawataweza kujiunga na makabila mengine dhidi ya Uislamu na kuunda ushirika, kwa sababu watakuwa wamewazuia Waislamu mbele ya maelfu ya mahujaji kuzifaidi haki zao za halali.

Mtume (s.a.w.w.) alizifikiria faida na hasara za jambo hili na akawaamrisha watu waanze safari. Akavaa Ihr?m mahali paitwapo Dhul– Hulayfah pamoja na watu 14002 au 16003 au 18004 na ngamia sabini waliotiwa alama maalumu kwa ajili ya kuchinja, na kwa nia hiyo wakalidhihirisha lengo la safari ile.

Watu wa idara ya usalama wa Mtume (s.a.w.w.) walitangulia mbele ili kwamba kama wakipambana na adui humo njiani, waweze kumuarifu Mtume (s.a.w.w.). Kwenye sehemu fulani karibu na Asf?n mtu mmoja wa kabila la Khuzaa'i, aliyekuwa mmoja wa wale watu wa usalama wa Mtume (s.a.w.w.) alimjia Mtume na kumuarifu hivi: "Waquraishi wameitambua safari yako. Wameyakusanya majeshi yao na wameapa kwa majina ya Laat' na Uzza' kwamba watazuia kufika kwako mjini Makka.

Wazee na watu maarufu wa Waquraishi wamekusanyika mahali paitwapo Zi Tuwaa (mahali fulani kariubu na Makka) ili kuzuia maendeleo ya safari ya Waislamu, wamempeleka kamanda wao shujaa Khalid bin Walid mahali paitwapo Kiraa'ul Ghamim jangwa lililoko kiasi cha kilomita kumi na tatu hivi kutoka Asfaan pamoja na askari wanaopanda farasi mia mbili nao wamepiga kambi hapo5 ili kuwazuia Waislamu wasiingie Makka, au sivyo watayatoa maisha yao katika kulifikia lengo hili."

Baada ya kuisikia taarifa ile Mtume (s.a.w.w.) alisema: "Ole wao Quraishi. Vita vimewamaliza! Ningelipendelea kwamba wangaliniacha nishughulike na makabila mengine yenye kuyaabudu masanamu.
Ikiwa wao (yaani yale makabila mengine) yakishinda dhidi yangu, Waquraishi wangelikuwa wamelifikia lengo lao, na kama nikipata ushindi dhidi ya makabila hayo, wao (Waquraishi) wangelipigana nami kwa majeshi yao waliyoyaweka akiba. Ninaapa kwa jina la Allah! Nitaziendeleza juhudi zangu kwa ajili ya kuihubiri itikadi ya Upweke wa Allah hadi Allah aifanye dini ishinde au niutoe uhai wangu kwa ajili ya kulifikia lengo hili."

Kisha aliomba muongoza njia wa kuwaongoza (yaani Mtume na masahaba zake) katika njia ambayo haitawapambanisha na Khalid. Mtu mmoja wa kabila liitwalo Aslam alilichukua jukumu la kuuongoza msafara ule na akaupitisha kwenye njia ya mabonde yenye mashimo shimo na kuwafanya watue mahali paitwapo Hudaybiyah. Ngamia wa Mtume (s.a.w.w.) alipiga magoti mahali pale naye Mtume (s.a.w.w.) akasema: "Huyu mnyama ametua mahali hapa kwa amri ya Allah ili kwamba jukumu letu lidhihirike." Kisha akawaamrisha wote washuke na kukita mahema yao.

Wapanda farasi wa Waquraishi walilijua lengo la Mtume (s.a.w.w.) na wakajisogeza karibu na Waislamu. Kama Mtume angalipenda kuendelea na safari yake basi ingelimlazimu kuzitawanya safu za wapanda farasi wa Waquraishi na kuimwaga damu yao. Lakini wote walikuwa wanafikiria kwamba hakuwa na lengo lolote jingine ila kufanya Hija ya Ka'abah Tukufu.

Mahali hapa ugomvi na kumwaga damu kungeleta pigo kwenye ile nafasi na madai ya makusudio ya amani ya Mtume (s.a.w.w.). Zaidi ya hapo, hata kule kuwaua hawa wapanda farasi kusingelikiondoa kizuizi kile kwenye njia yake kwa sababu daima vikosi vingine vilikuwa vikiletwa na Waquraishi na suala hili halikuwa likiufikia mwishilizo wake. Mbali na hili, Waislamu hawakuwa na silaha zozote zile zaidi ya zile silaha za wasafiri na halikuwa jambo lifaalo kujitia kwenye mapigano kwenye hali ile. Kinyume na hivyo ilifaa kulitatua suala hili kwa njia ya mazungumzo.

Kutokana na sababu hizi, Mtume (s.a.w) aliwageukia masahaba wake baada ya kushuka kwenye mnyama wake na akasema: "Kama leo hii Waquraishi wanataka kitu chenye kuimarisha mafungamano ya udugu nitawapa na nitaishika njia ya upatanisho."6

Maneno ya Mtume (s.a.w.w.) yaliyafikia masikio ya watu na maadui nao waliyatambua. Hivyo Waquraishi waliwatuma watu kwa Mtume (s.a.w.w.) kwenda kupata taarifa sahihi.

Wawakilishi Wa Quraishi Waja Na Kukutana Na Mtukufu Mtume (S.A.W.W)

Waquraishi waliwatuma wawakilishi wengi kwa Mtume (s.a.w.w.) ili kupata taarifa juu ya lengo la kuchukua kwake safari ile. Budayl Khuzaa'i na baadhi ya watu wa kabila la Khuza'ah walionana na Mtume (s.a.w.w.) wakiwa ni wawakilishi wa Waqureishi. Mtume (s.a.w.w.) aliwaambia: "Sikuja kupigana. Nimekuja kufanya Hija ya Ka'abah." Wale wawakilishi walirejea na kuwaarifu Waquraishi kuhusu ile hali. Hata hivyo wale Waquraishi wasiosadiki hawakuyakubali maneno yao na wakasema: "Tunaapa kwa jina la Mungu! Japo awe kaja kwa ajili ya Hija ya Ka'abah hatutamruhusu aingie Makka."

Kisha Mikraz akiwa yu mwakilishi wa Waquraishi alikutana na Mtume (s.a.w.w.). Vile vile naye alirudi na kuyathibitisha yale aliyoyasema Budayl, lakini Waquraishi hawakuziamini taarifa alizozitoa.

Ili kuumaliza mgongano huu walimtuma Hulyas bin 'Alqamah kwa Mtume (s.a.w.w.) aliyekuwa mpiga mishale mkuu wa Uarabuni.7 Alikuwa bado yu mbali kidogo pale Mtume (s.a.w.w.) alipomwona na kusema: "Mtu huyu anatokana na kabila safi na lenye uchamungu. Watoeni kafara wale ngamia mbele yake ili atambue kwamba hatukuja kupigana, na kwamba hatuna lengo lolote jingine ila kufanya Hija ya Ka'abah".
Hulays aliwaona wale ngamia sabini waliokuwa na njaa kali kiasi kwamba walikuwa wakila sufi zao wenyewe kwa wenyewe. Alirudi kutoka mahali pale hata bila ya kuonana na Mtume (s.a.w.w.). Aliwahutubia Waquraishi kwa nguvu na kusema: "Sisi hatukufanya mapatano hata kidogo nanyi ili muwazuie mahujaji wa Ka'abah kufanya Hija. Muhammad hana lolote ila kufanya Hija.

Naapa kwa jina la Yule Mwenye nguvu zote, Aliyeutawala uhai wangu! Kama mkimzuia Muhammad asiingie (Makka), mimi pamoja na watu wote wa kabila langu ambao wengi wao ni wapiga mishale tutakutoeni na kukukateni kateni vipande vipande!"

Maneno haya ya Hulays hayakupendwa na Waquraishi. Hata hivyo, wakichelea upinzani wake walishauriana juu ya jambo hili na kumwambia: "Tulia kwa uhakika. Sisi wenyewe tutalitafutia jambo hili ufumbuzi utakaoukubali wewe."

Hata hivyo, kwenye hatua ya nne walimtuma 'Urwah bin Mas'ud Saqafi ambaye kwa busara, akili na uaminifu wake walimwamini. Mwanzoni alikataa kuwawakilisha Waquraishi kwa kuwa aliona vema jinsi walivyowachukulia wawakilishi wao wa awali, lakini walimthibitishia kwamba cheo chake kwao kilithaminiwa, nao hawatamlaumu kwa kuvunja uaminifu.

Urwah bin Mas'ud alimjia Mtume (s.a.w.w.) na kusema: "Ewe Muhammad! Umejikusanyia makundi mbalimbali na sasa umeamua kuishambulia sehemu uliyozaliwa (Makka). Hata hivyo, Waquraishi watakuzuia kwa nguvu zao zote nao hawatakuruhusu kuingia mji wa Makka. Hata hivyo, mimi nachelea kwamba kesho makundi haya yatakuacha pasipo msaada wowote."

Alipomaliza kuyasema hayo, Abu Bakr aliyekuwa kasimama nyuma ya Mtume (s.a.w.w.) alimgeukia ‘Urwah na kumwambia: “Umekosea. Marafiki zake Mtume (s.a.w.w.) hawatamwacha, kwa hali yoyote ile.”

‘Urwah aliutumia ujuzi wote wa diplomasia kwenye kauli yake na akajaribu kuithibitisha nguvu ya Waquraishi na kuudhoofisha moyo wa Mtume (s.a.w.w.); na kwa lengo la kukishusha cheo cha Mtume (s.a.w.w.) alizigusa ndevu zake alipokuwa akizungumza. Mughayrah bin Shu’bah kwa kurudia rudia alipiga mkono wake na kusema: “Kuwa mwenye heshima na usiwe mtovu wa adabu kwa Mtume (s.a.w.w.).” Urwah alimwuliza Mtume (s.a.w.w.): “Ni nani huyu?”8 Mtume akasema: “Huyu ni mwana wa nduguyo, Mughayrah bin Shu’bah.” Urwah alichukizwa na akasema: “Ewe mtu mwenye hila! Jana niliinunua heshima yako.

Uliwauwa watu kumi na watatu wa kabila la Saqaf muda mfupi tu kabla ya kusilimu kwako, nami nililipa fidia ya damu kutoka mfukoni mwangu ili kuizuia miali ya vita kuwaka miongoni mwa koo za Saqaf.”

Mtume (s.a.w.w.) aliyakatisha yale mazungumzo ya ‘Urwah na akamweleza lengo la safari yake kama alivyokwisha kuwaeleza wale wawakilishi wa Waquraishi, wale wa awali. Hata hivyo, ili kutoa jibu lenye pigo kwa vile vitisho alivyovitoa ‘Urwah, Mtume alisimama na akafanya wudhu (akatawadha), Urwah akaona kwa macho yake kwamba masahaba zake Mtume hawakuruhusu japo tone la yale maji ya udhu wake kuangukia ardhini.

‘Urwah aliamka na akaufikia ule mkusanyiko wa Waquraishi. Aliwataarifu machifu wa Waquraishi waliokusanyika mahali paitwapo Zi Tuwaa juu ya mkutano wake na Mtume (s.a.w.w.) na lengo la Mtume (s.a.w.w.). Vile vile aliongeza: “Nimewaona wafalme wakuu.

Nimeziona nguvu kuu kama vile nguvu za Mtawala wa Iran, Kaisari wa Dola ya Kirumi na Mfalme wa Ethiopia, lakini sijapata kuona cheo cha yeyote yule kati yao miongoni mwa mataifa yao kilicho kikuu kama kile alichonacho Muhammad miongoni mwa wafuasi wake.

Nimeona kwa macho yangu kwamba hawakuliruhusu japo tone moja la maji aliyotawadhia kuanguka ardhini, nao waliligawana miongoni mwao likiwa ni tabaruk (yaani zawadi takatifu iletayo mibaraka). Kama unywele wake mmoja ukianguka huuokota mara moja. Hivyo basi, machifu wa Waquraishi hawana budi kuifikiria hii hali ya hatari.”9

Mtume Wa Uislam (S.A.W.W) Amtuma Mwakilishi Wake

Mazungumzo ambayo wawakilishi wa Waquraishi waliyafanya na yule kiongozi mkuu wa Uislamu hayakutoa matokeo mema yeyote. Mtume (s.a.w.w.) aliweza kufikiria vyema kwamba wale wawakilishi wa Waquraishi hawakuweza kuufikisha ukweli kwa wazee wa Waquraishi au hawakufanya hivyo waziwazi kwa kuchelea kukemewa. Hivyo aliamua kumpeleka mwakilishi wake atakayewaeleza Waquraishi lengo lake hasa la kuifanya safari ile, ambalo halikuwa lolote jingine ila Hija ya Ka’abah.

Khirash mtu hodari wa kabila la Khuzaa'ah, aliteuliwa kwa kazi hii na Mtume (s.a.w.w.) alimtoa ngamia kwa ajili yake. Khir?sh alikutana na kundi la Waquraishi na akaifanya ile kazi aliyopewa. Hata hivyo, kinyume na ilivyotegemewa, na pia kinyume na desturi ya mataifa ya ulimwengu kwamba balozi yu huru kabisa kutokana na madhara, wao (Waquraishi) waliikata miguu ya ngamia wake na walikuwa karibu wamuuwe, lakini uhai wake uliokolewa kwa njia ya wale wapiga mishale wa Uarabuni. Kitendo hiki kiovu kilithibitisha kwamba Waquraishi hawakuwa na nia ya kulimaliza jambo hili kwa njia ya amani na kwamba walikuwa wakielekea kwenye mapigano.

Mara baada ya tukio hili watu hamsini wenye uzoefu kutoka miongoni mwa Waquraishi walitumwa kwenda kandokando ya sehemu ambayo Waislamu wamepiga kambi na ikiwezekanza wazinyakue mali zao na kuwateka baadhi yao. Hata hivyo, mpango wao huu ulishindwa na kinyume chake watu wale walitekwa na kuletwa mbele ya Mtume (s.a.w.w.). Ingawa waliwatupia Waislamu mishale na kuwavurumisha mawe, lakini Mtume (s.a.w.w.) aliwaelekeza Waislamu kuwaachia huru wote. Hivyo, kwa mara nyingine tena aliuthibitisha ukweli wake na akadhihirisha ya kwamba hakuwa na nia ya kupigana.10

Mtume (S.A.W.W) Ampeleka Mwakilishi Mwingine

Ingawa yalikuwako yote hayo, lakini Mtume (s.a.w.w.) hakukata tamaa ya amani, naye kwa uaminifu kabisa alitaka kulitatua tatizo lile kwa njia ya mazungumzo na kwa kuzibadili fikira za Waquraishi. Safari hii alitaka kumpeleka mwakilishi ambaye hajaimwaga damu ya Waquraishi. Hivyo Ali, Zubayr na wapiganaji wengine wa Uislamu waliowahi kupambana na wapingaji wa Waquraishi na Waarabu na kuwauwa baadhi yao, hawakufaa kuwa wawakilishi. Mwishowe aliamua kumtuma Umar bin Khatab kwa lengo hili, kwa kuwa hadi katika siku ile alikuwa bado hajamwaga japo tone moja la damu ya waabudu masanamu. Hata hivyo, Umar alitoa udhuru wa kutoweza kulibeba jukumu lile na akasema: "Mimi nina waogopa11

Waquraishi kwa kuwa nayachelea maisha yangu, na mjini Makka hakuna mtu yeyote wa familia yangu awezaye kunisaidia. Hata hivyo, mimi nampendekeza Uthman bin Aff?n mwenye uhusiano wa karibu zaidi na Abu Sufyani naye anaweza kuufikisha ujumbe wako kwa machifu wa Waquraishi."

Hivyo, Uthman akapewa jukumu lile na akaondoka kwenda Makka. Alipokuwa njiani alikutana na Ab?n bin Sa'id bin Aas na akaingia mjini Makka chini ya ulinzi wake.

Ab?n alimwahidi kwamba hakuna yeyote atakayemwingilia mpaka pale atakapoufikisha ule ujumbe wa Mtume (s.a.w.w.) waziwazi. Hata hivyo, Waquraishi waliujibu ujumbe ule wa Mtume (s.a.w.w.) kwamba wao wameamua kwa kiapo kwamba hawatamruhusu Muhammad kuuingia mji wa Makka kwa nguvu, na kwa sababu ya kiapo hiki mazungumzo yoyote yahusuyo kuingia kwa Waislamu mjini Makka hayana mjadala tena. Walimruhusu Uthman kufanya Tawaaf ya Ka'abah, lakini yeye alikataa kufanya hivyo ikiwa ni ishara ya heshima kwa Mtume (s.a.w.w.). Walichokifanya Waquraishi kuhusiana na Uthman ni kwamba walimzuia asirejee na huenda lengo lao lilikuwa kwamba wakati ule wangeliweza kupata

ufumbuzi wa tatizo lile.12

Mkataba Wa Ridhwaan

Waislamu walipatwa na fadhaa kubwa kutokana na kuchelewa kurejea kwa Uthman. Kisha ulipatikana uvumi kwamba Uthman ameuawa. Kusikia hivyo, Waislamu waliwakwa na ghadhabu nao wakataka kulipiza kisasi. Ili kuiimarisha dhamira yao ile, Mtume (s.a.w.w.) alisema: “Sitaitoka sehemu hii hadi nilimalize jambo hili.”

Katika wakati huu ambao hatari ilikuwa karibu sana, na Waislamu hawakuwa na silaha, Mtume (s.a.w.w.) aliamua kuchukua viapo vya utii kutoka kwa Waislamu na akakaa chini ya mti kwa lengo hili. Masahaba zake wote walimshika mkono ikiwa ni ishara ya kiapo na wakaapa kwamba wataihami ile dini takatifu ya Uislamu hadi mwishoni mwa uhai wao. Hii ndio ile suluhu ya Ridhwaan iliyotajwa katika Qur’ani Tukufu kwa maneno haya:

لَقَدْ رَضِيَ اللَّهُ عَنِ الْمُؤْمِنِينَ إِذْ يُبَايِعُونَكَ تَحْتَ الشَّجَرَةِ فَعَلِمَ مَا فِي قُلُوبِهِمْ فَأَنْزَلَ السَّكِينَةَ عَلَيْهِمْ وَأَثَابَهُمْ فَتْحًا قَرِيبًا {18}

“Bila shaka Allah amewawia radhi waumini walipofungamana nawe chini ya mti, na Alijua yaliyomo nyoyoni mwao. Basi akateremsha utulivu juu yao, na akawapa ushindi wa karibu.” **(*Sura al-Fath, 48:18*).**

Baada ya kula kiapo cha utii kwa Mtume (s.a.w.w.) jukumu la Waislamu likawa wazi. Imma Waquraishi wawaruhusu kuingia Makka na kufanya Hija ya Ka’abah au waupinge ukaidi wa Waquraishi kwa gharama ya uhai wao.

Mtume (s.a.w.w.) alikuwa akifikiria hili wakati Bwana Uthman alipotokea kwa mbali, na jambo hili lenyewe lilikuwa ni utangulizi wa amani aliyoitamani mno Mtume (s.a.w.w.) na kusema: “Tatizo katika njia ya Waquraishi ni kiapo walichokiapa na mwakilishi wa Waquraishi atafanya mazungumzo nawe kuhusu ufumbuzi wa tatizo hili.”

Suhayl Bin ‘Amr Aonana Na Mtume (S.A.W.W)

Suhayl bin ‘Amr alitumwa na Waquraishi na maagizo maalum ili kuumaliza ule ugomvi kwa njia ya mapatano tutakayoyasoma baadae. Macho ya Mtume (s.a.w.w.) yalipomwangukia Suhayl, alisema: “Suhayl amekuja kufanya mapatano ya amani baina yetu na Waquraishi.” Suhayl akaja akakaa. Akasema kila aina ya vitu, na kama alivyo mwanadiplomasia stadi aliuamsha mwelekeo wa Mtume (s.a.w.w.) katika kuyatimiza mambo fulani fulani. Alisema: “Ewe Abul Qaasim! Makka ni Haram na makao makuu ya heshima yetu. Ulimwengu wa Kiarabu unafahamu kwamba wewe umepigana dhidi

yetu. Kama ukiingia Makka katika hali iliyopo hivi sasa, iliyoandamana na nguvu, na uwezo, utaufanya unyonge wetu na utovu wetu wa msaada utambulike kwenye ulimwengu mzima wa Kiarabu. Kesho makabila yote ya Kiarabu watafikiria kuichukua nchi yetu.

Ninakuomba kwa jina la Mungu kuufikiria ufalme unaoshirikiana nasi, na vile vile uikumbuke heshima ya mji wa Makka na ambao vile vile ndio sehemu uliyozaliwa."

Suhayl alipokuwa akiyasema haya, Mtume (s.a.w.w.) aliyaingilia mazungumzo yake na akasema: "Unalenga nini?" Suhayl akajibu: " Machifu wa Waquraishi wana maoni ya kwamba mrudi Madina mwaka huu na muiahirishe Hija hadi mwaka ujao.

Mwaka ujao Waislamu wataweza kufanya Hija kama makabila yote mengine ya Uarabuni, kwa masharti ya kwamba hawakai mjini Makka kwa zaidi ya siku tatu na wasilete silaha yoyote nyingine ila zile ambazo kwa kawaida huchukuliwa na msafiri."

Matokeo ya mazungumzo baina ya Mtume (s.a.w.w.) na Suhayl ni kwamba, iliamuliwa kwamba yafanywe mapatano ya ujumla na marefu baina ya Waislamu na Waquaishi. Suhayl alikuwa akiudhihirisha ukali usio kifani kuhusiana na yale masharti na maelezo ya mapatano yale, na katika nyakati fulani fulani ilionekana kwamba mapatano yale ya amani yatavunjika. Hata hivyo, kwa kuwa pande zote mbili zilitaka amani na maafikiano, ule uelekeo wa mazungumzo ulikuwa ukishikwa kila mara.

Ingawa yalikuwako yote hayo kuhusu ukali wa Suhayl, yale mapatano yalikamilika na iliamuliwa kwamba maelezo yake yaandikwe katika makala mbili na makala hizo zisainiwe na pande zote mbili.

Kama ilivyoandikwa na wanahistoria wengi, Mtume (s.a.w.w.) alimwelekekeza Sayyidna Ali (a.s.) kuyaandika mapatano haya ya Amani, na akasema: "Andika kwa jina la Allah, Mwingi wa rehema, Mwenye kurehemu," na Saidina Ali (a.s.) aliandika hivyo.

Suhayl akasema: "Mimi siifahamu sentensi hii. Andika hivi: "Kwa jina Lako, Ee Allah!" Mtume (s.a.w.w.) aliikubali ile sentensi iandikwe kama ilivyotamkwa na Suhayl. Sayyidna Ali (a.s.) aliandika hivyo. Kisha Mtume (s.a.w.w.) alimwamrisha Sayyidna Ali (a.s.) aandike: "Huu ni mkataba ambao Muhammad Mtume wa Allah, ameufanya na Suhayl mwakilishi wa Waqurashi."

Suhayl akasema: "Sisi hatuutambui rasmi utume wako na kama tungalikutambua kuwa u Mtume tusingelipigana vita dhidi yako. Huna budi kuandika jina lako na lile la baba yako na huna budi kutokitia cheo hiki kwenye mapatano haya."

Baadhi ya Waislamu hawakukubali kwamba Mtume (s.a.w.w.) akubaliane na Suhayl kiasi kile.

Hata hivyo, Mtume (s.a.w.w.) alilikubali hata hilo kwa kuzingatia maslahi yaliyo makubwa zaidi yatakayoelezwa hapo baadae, na akamwamrisha Sayyidna Ali (a.s.) afute kifungu cha maneno kisemacho: "Mtumbe wa Allah."

Katika hatua hii Sayyidna Ali (a.s.) aliona uzito na akasema kwa heshima na taadhima: “Haitowezekana kwangu mimi kulichukua uhuru wa kukifuta cheo chako cha ‘Mjumbe’ na ‘Mtume’ kutoka karibu na jina lako takatifu.” Mtume (s.a.w.w.) alimwamrisha Sayyidna Ali (a.s.) kukiweka kidole cha Mtume (s.a.w.w.) kwenye neno lile ili aweze kulifuta yeye mwenyewe.

Sayyidna Ali (a.s.) akakiweka kidole cha Mtume (s.a.w.w.) juu ya neno lile na akakifuta cheo cha Mjumbe wa Allah.”13

Upole na moyo aliouonyesha Mtume (s.a.w.w.) katika kuyaandika mapatano haya havina kifani ulimwenguni. Kwa vile hakuvutiwa na fikara za kiulimwengu na mwelekeo wa majisifu, na alitambua kwamba ukweli haubadiliki kwa kuandika jambo lolote lile au kulifuta, ili kuhakikisha kwamba amani inapatikana, yeye alishika msimamo wa upatanisho na akayakubali maoni ya mpinzani wake ingawa alikuwa mkali kiasi kile.

Historia Inajirudia Yenyewe

Mwanafunzi wa kwanza na maarufu zaidi wa mafundisho ya Mtume wa Uislamu (s.a.w.w.), naye pia alikabiliwa na fadhaa ya aina ileile, na kutokana na jambo hili mwanafunzi huyu Sayyidna Ali (a.s.) aliye mfano halisi wa Mtume (s.a.w.w.), kwa sababu fulani fulani amekuwa mfano halisi wa sifa zake zilizofanana na zake (s.a.w.w.) katika hatua mbalimbali. Wakati Amirul–Mu’minin (a.s.) alipotoa udhuru kuhusu kuyafuta yale maneno ‘Mtume wa Allah’ (s.a.w.w.) alimgeukia na kumwarifu kuhusu siku zake za baadae zilizofanana mno na zile zake (s.a.w.w.) kwa maneno haya; “Kizazi cha jamii hii kitakuita kwenye kitendo kama hiki nawe utakubali chini ya uonevu mkubwa.”14

Sayyidna Ali (a.s.) alilikumbuka jambo hili hadi katika Vita vya Siffin na wafuasi wenye fikara ndogo wa Imamu Ali (a.s.) walivutiwa na matendo ya kiudanganyifu ya askari wa Sham waliokuwa wakipigana chini ya uongozi wa Muawiyah na ‘Amr bin Aas na wakamshauri akubali kufanya Amani.

Ulifanyika mkutano wa kuandika mapatano ya amani. Katibu wa Amirul– Mu’minin (a.s.) aliyeitwa Ubaydullah bin Abi Raafi’ alielekezwa na Amirul–Mu’minin (a.s.) kuyaandika yale mapatano ya Amani kwa maneno haya; “Haya ndio mambo yaliyokubaliwa na Ali, Amirul–Mu’minin.”

Hapa ‘Amr bin Aas (aliyekuwa mwakilishi rasmi wa Muawiyah na jeshi la Sham) alimgeukia yule Katibu wa Sayyidna Ali (a.s.) na kusema: “Andika jina la Ali na baba yake, kwa sababu kama hapo awali tungalimtambua kuwa yu Amir wa Waumini, tusingelipigana naye kabisa”. Majadiliano juu ya jambo hili yalirefushwa. Amirul–Mu’minin (a.s.) hakuwa tayari kutoa udhuru wowote kwa wale marafiki zake wajinga. Sehemu ya siku ilitumiwa katika kutoafikiana kwa pande hizi, mpaka kutokana na msisitizo wa mmoja wa maafisa wake mwenyewe, aliruhusu kwamba kile kifungu cha maneno kisemacho: ‘Amirul–Mu’minin’ kifutwe. Kisha akasema: “Allah Yu Mkubwa! Huku ni kuiangalia kwa mbali Hadith ya Mtume (s.a.w.w.)” Baada ya hapo alilirudia lile tukio la Hudaybiah mbele ya watu na aliyoambiwa na Mtume (s.a.w.w.) wakati ule.15

Hati Ya Mapatano Ya Hudaybiyah

Waquraishi na Waislamu wamekubaliana kwamba hawatapigana au kushambuliana kwa kipindi cha miaka kumi, ili kwamba usalama wa jamii na amani ya watu wote iweze kudumishwa kwenye sehemu mbalimbali za Uarabuni.

Kama mtu kutoka miongoni mwa Quraishi atautoka mji wa Makka bila ya ruhusa ya wazee wake na akasilimu na akajiunga na Waislamu, ni lazima Muhammad amrudishe kwa Waquraish. Hata hivyo, iwapo mmoja wa Waislamu atakwenda kwa Waquraishi, hawatalazimika kumrudisha kwa Waislamu. Waislamu na Waquraishi watakuwa huru kufanya mapatano na kabila lolote wapendalo.

Mwaka huu Muhammad na masahaba zake warudi Madina kutoka pale Hudaybiyah. Hata hivyo, kwenye miaka ifuyatiayo, watakuwa huru kuingia Makka na kufanya Hija ya Ka'abah, chini ya sharti la kwamba hawatakaa mjini Makka kwa zaidi ya siku tatu na kwamba hawatachukua silaha yoyote zaidi ya zile azichukuazo msafiri. 16

Kwa mujibu wa mapatano haya, Waislamu waishio Makka wako huru kuzitekeleza ibada zao za kidini na Waquraishi hawatakuwa na haki ya kuwatesa au kuwalazimisha kuikana dini yao au kuidhihaki dini yao.17
Watia saini wa mapatano haya wanakubali kuziheshimu mali za watu wa upande wa pili na kuepuka udanganyifu na hila dhidi ya wenzao na kuziweka nyoyo zao huru kutokana na mfundo dhidi ya wenzao. Uhai na mali za Waislamu wafikao Makka kutoka Madina vitaheshimiwa.18

Haya ndio maneno ya mapatano ya amani ya Hudaybiyah yaliyokusanywa kutoka kwenye vitabu mbali mbali. Mapatano haya yaliandikwa katika makala mbili. Baadhi ya watu kutoka miongoni mwa Waquraishi na Waislamu waliyashuhudia mapatano haya ambayo baada ya hapo, nakala moja alipewa Suhayl na nyingine akapewa Mtume (s.a.w.w.).19

Bishara Njema Ya Uhuru

Bishara njema ya uhuru kama ilivyo kwenye mapatano haya ilimfikia kila mtu. Ingawa kila kifungu cha mapatano haya kinastahili kujadiliwa, sehemu iliyo nyeti yenye kuhitaji kufikiriwa sana ni kifungu cha pili kilichoamsha hasira za baadhi ya watu katika siku ile. Ingawa masahaba wa Mtume (s.a.w.w.) walikuwa na wasiwasi kutokana na ubaguzi huu na waliyatamka maneno yasiyostahili kusemwa kuhusiana na ule uamuzi uliochukuliwa na kiongozi kama vile Mtume wa Uislamu (s.a.w.w.). Lakini kifungu hiki kikiwa bado ni chenye kuangaza kinaionyesha namna ya fikira ya Mtume (s.a.w.w.) katika mambo ya uhubiri wa Uislamu. Inaonyesha kikamilifu heshima kuu ambayo huyu kiongozi mkuu aliitoa kwenye kanuni za uhuru.

Katika kuujibu ukanusho uliotolewa na baadhi ya masahaba wa Mtume (s.a.w.w.) kuhusu ni kwa nini wawasalimishe wakimbizi waliotoka kwa Waquraishi ambapo wao Waquraishi hawawajibiki

kuwasalimisha watu wao, alijibu akisema: “Kama Mwislamu anatwaa ushirikina, na akaikimbia bendera ya Uislamu, na akayapendelea mazingira ya waabudu masanamu na dini isiyo ya kibinaadamu badala ya yale mazingira ya Uislamu na Upweke wake Allah, inaonyesha kwamba hakusilimu kwa moyo wote, na imani yake haikupata msingi ustahilio na uwezao kuyatosheleza maumbile yake, na Mwislamu wa aina hiyo, hana faida kwetu. Na kama tukimsalimisha mkimbizi atokaye kwa Waquraishi, ni kwa sababu hii kwamba sisi tumetosheka kwamba Allah atawapatia njia ya wokovu wao.”20

Mustakabali wa baadae ulithibitisha kwamba utabiri wa Mtume (s.a.w.w.) juu ya jambo hili (kwamba Allah Atawapatia njia ya wokovu wao) ulikuwa sahihi kabisa, kwa sababu mara tu baada ya hapo, wao Waquraishi wenyewe waliomba kifungu hiki kifutwe kutokana na matukio mengi yasiyopendeza waliyobidi kuyakabili kwa sababu ya kifungu hiki.

Kifungu hiki kilikuwa ni jibu lenye kunyamazisha kwa udhaifu wa wengi wa mustashirik wanaosisitiza kwamba sababu ya kuendelea kwa Uislamu ilikuwa ni matumizi ya upanga. Hawawezi kustahimili kuona kwamba utukufu wa Uislamu umo kwenye ukweli wa kwamba katika kipindi kifupi sana ulienea kwenye maeneo mengi ya ulimwenguni. Hivyo basi, kutokana na malengo ya ubinafsi, na kwa lengo la kuzitia sumu akili, wanalazimika kusema kwamba sababu ya maendeleo ya Uislamu ilikuwa ni nguvu za mabavu.

Mapatano haya ya amani yalifanyikiwa katika siku za awali za Uislamu mbele ya kiongozi mkuu wa Uislamu, kama yanavyoakisi moyo wa Uislamu na mafundisho matakatifu na misingi ya ubinadamu iliyomo kwenye sheria zake zote. Ni uonevu mkuu kwamba tulazimike kusema kuwa Uislamu umeenezwa kwa nguvu ya upanga.

Kwa mazingatio ya kifungu cha tatu, kabila la Khuzaa’ah lilifanya mapatano ya ulinzi na Waislamu na kabila la Bani Kinanah waliokuwa maadui wa Bani Khuza’ah wa tangu kale, waliamua kufanya ushirikiano baina yao na Waquraishi.

Juhudi Za Mwisho Katika Kuhifadhi Amani

Utangulizi wa mapatano ya amani na maandishi yake unaonyesha dhahiri kwamba sehemu yake kubwa ilikuwa na mwelekeo wa kielimu, na sababu zilizomfanya Mtume (s.a.w.w.) ayakubali mapatano haya na kukubali kukifuta kifungu cha maneno kisemacho: ‘Mtume wa Allah’ na kule kuanza kwake na maneno: Kwa jina lako, Ee Allah (kwa kuwa ulikuwa ndio mtindo katika zama za ujinga); ilikuwa kwamba alitamani mno kuidumisha amani Barani Arabu.

Na alipokubali kwamba wakimbizi wa Kiislamu kutoka miongoni mwa Waquraishi wasalimishwe kwa watawala wa serikali ya waabudu masanamu, ilitokana na ukaidi mkubwa wa Suhayl. Hivyo kama Mtume (s.a.w.w.) asingelikubaliana na Suhayl katika jambo hili, kwa mtazamo wa kuzihami haki za kundi hili (yaani wakimbizi wa Kiislamu kutoka miongoni mwa Waquraishi) na kuziheshimu fikira za kawaida zilizokuwa kinyume cha ubaguzi katika kule kuwasalimisha wale wakimbizi, bila shaka amani ya

jumla ingelihatarika na hii baraka kuu ingelipotea.

Hivyo basi, kwa nia ya kulifikia lengo lililo kuu na tukufu zaidi, Mtume (s.a.w.w.) alilivumilia shinikizo na matakwa yote haya ili kwamba ile fursa kuu ya kuhakikisha amani hii isipotee, juu ya hali ambayo usumbufu wote huu ulikuwa ni kitu kidogo mno. Na kama angaliyajali maoni ya kawaida na haki za kundi lile, basi Suhayl kutokana na ukaidi wake angelianzisha cheche za vita.

Tukio lifuatalo ni ushahidi wa dhahiri wa jambo hili: Majadiliano kuhusiana na maneno yaliyomo kwenye Mkataba wa amani yalimalizika na Sayyidna Ali (a.s.) alikuwa akishughulikia uandishi wake, ambapo kwa ghafla Abu Jandal bin Suhayl, mtoto wa yule mwakilishi wa Waquraishi katika kufanya yale mapatano ya amani, alitokea mahali pale akiwa kafungwa minyororo miguuni. Watu wote walishangazwa na kufika kwake pale, kwa kuwa tangu muda mrefu alikuwa kafungwa na kutiwa minyororo na baba yake. Alikuwa ni mfungwa asiye na hatia, ila kosa lake pekee lilikuwa kwamba kasilimu na alikuwa akichukuliwa kuwa yu mmoja wa wafuasi wa Mtume (s.a.w.w.). Kutokana na mazungumzo yaliyofanyika karibu na jela yake alifahamu kwamba Waislamu wamewasili Hudaybiyah.21 Hivyo basi, alifaulu kutoroka mle jela kwa hila maalum na akawasili katikati ya Waislam kwa kutwaa njia iliyochepuka kupitia milimani.

Macho ya Suhayl yalipomwona mwanawe alikasirika mno kiasi kwamba, akiwa kajawa na hasira kubwa, alimpiga kofi kubwa mno usoni mwake. Kisha alimgeukia Mtume (s.a.w.w.) na kusema: “Huyu ni mtu wa kwanza ambaye ni lazima arejee Makka kwa mujibu wa hiki kifungu cha pili cha mapatano haya.” Maana yake ilikuwa kwamba, Abu Jandal kwa vile yu Mquraishi aliyeukimbia mji wa Makka hana budi asalimishwe kwao.

Hakuna kuukana ukweli uliopo kwamba dai la Suhayl halikuwa na haki wala lenye msingi, kwa sababu yale mapatano yalikuwa bado hayajamalizwa kuandikwa na kutiwa saini na pande zihusikazo. Je, vipi mshirika wa mkataba anaweza kuyategemea mapatano ambayo bado hayajapitia kwenye hatua zake za mwisho? Kwa sababu hii Mtume (s.a.w.w.) alimwambia Suhayl: “Mapatano yetu bado hayajatiwa saini.” Suhayl akajibu akasema: “Kwa sababu hiyo, mimi ninautupilia mbali mchakato wote huo na kuufanya kuwa batili na usio na faida.” Alikuwa mkaidi mno kwenye jambo hili kiasi kwamba Mikraz na Huwaytab, watu wawili waliokuwa wakuu wa Waquraishi walichukizwa mno na ukali wake. Mara moja wakamtoa Abu Jandal kutoka kwa baba yake, wakamwingiza kwenye hema na kumwambia Mtume (s.a.w.w.): “Ewe Muhammad! Hivi sasa Abu Jandal yuko kwenye ulinzi wako.”

Walitaka kuumaliza mzozo ule kwa njia hii lakini kung’ang’ania kwa Suhayl kuliukwamisha mpango wao. Aliyashikilia maneno yake na akasema: “Kutegemeana na maoni ya maafikiano yetu, tayari mapatano yameshafanyika.”
Mtume (s.a.w.w.) alilazimika kufanya juhudi za mwisho katika kuihifadhi misingi ya amani kitu kilichokuwa na faida mno kwa uhubiri wa Uislamu. Hivyo basi, alikubali kule kurejea Makka kwa Abu Jandal pamoja na baba yake. Ili kumfariji yule Mwislamu aliyetiwa minyororo na aliyetakiwa kusalimishwa kwa makafiri mbele ya mamia ya Waislamu mashujaa, alisema: “Ewe Abu Jandal! Kuwa

mwenye subira.

Tulipenda kwamba baba yako akutoe na akuweke mikononi mwetu kwa njia ya huba na upendo. Sasa, kwa vile hajapenda kufanya hivyo, huna budi kuwa na subira na uvumilivu na huna budi kutambua kwamba Allah atakufungulia njia ya kuachiliwa, wewe na wengineo walio kwenye kifungo."

Mkutano ule ukafikia ukomo. Zile nakala za mapatano zikasainiwa. Suhayl na marafiki zake wakaondoka kwenda Makka na Abu Jandal naye akaenda Makka akiwa chini ya ulinzi wa Mikraz na Kuwaytab. Kwa nia ya kuimaliza ile hali ya kuwa kwenye Ihr?m, Mtume (s.a.w.w.) alimchinja ngamia wake na kunyoa nywele za kichwa chake na wengineo nao wakafanya vivyo hivyo.22

Tathmini Ya Mkataba Wa Amani Wa Hudaybiyah

Mapatano ya amani yalifanyika baina ya Mtume wa Uislamu (s.a.w.w.) na viongozi wa ushirikina, na baada ya kukaa pale Hudaybiyah kwa muda wa siku kumi na tisa Waislamu wakarejea Madina na wale waabudu masanamu wakarejea Makka.

Zilitokea tofauti na kutoafikiana baina ya masahaba wa Mtume (s.a.w.w.) wakati wa kuandikwa kwa yale mapatano na vilevile baada ya hapo. Kundi moja miongoni mwao waliyafikiria mapatano yale kuwa ni yenye faida kwa Uislamu, na kundi jingine ambalo watu wake waliweza kuhesabika kwa vidole vya mkono, waliukadiria kwamba uko nje ya malengo yake. Hivi sasa ni karne ya kumi na nne tangu yafanyike mapatano yale, tumeamua kuyatathmini kwa jinsi isiyo ya upendeleo na iliyo ya hakika, na tutaimalizia Sura hii baada ya kuzidokeza zile tofauti zilizotajwa hapo juu. Maoni yetu ni kwamba, haya mapatano ya amani yalithibitika kuwa ni yenye manufaa kabisa kwa Uislamu na kuufanya ushindi wake kuwa wa mwisho. Zifuatazo hapa chini ndizo hoja ambazo tungelitaka kuzitoa:

1. Vita zilizokuwa zikiendelea na mashambulizi ya Waquraishi na uchochezi wao wa ndani na wa nje tuliotaja kwenye maelezo ya vita za Uhud na Ahzaab hayakuacha nafasi ya muda kwa upande wa Mtume (s.a.w.w.) kuweza kuhubiri Uislamu miongoni mwa makabila mbalimbali, pamoja na maeneo yaliyo nje ya Bara Arabuni pia, na wakati huu wenye thamani ulitumika karibuni wote katika kujihami na kuibatilisha mipango miovu ya adui. Hata hivyo, baada ya kufanywa kwa haya mapatano ya amani, Waislamu na yule kiongozi wao mkuu waliondolewa ile hatari kutoka kwenye eneo la Kusini, na sasa uwanja umeshatayarishwa kwa uhubiri wa Uislamu kwenye nchi nyingine.

Athari za mapatano haya ya amani zilidhihirika baada ya miaka miwili, kwa sababu pale mapatano ya Hudaybiyah yalipokuwa yakifanyika Mtume (s.a.w.w.) alifuatana na watu 1400, lakini miaka miwili baadae, alipokuwa akienda rasmi kuuteka mji wa Makka watu wengi kiasi cha elfu kumi walikwenda pamoja naye chini ya kivuli cha bendera ya Uislamu na tofauti hii ya dhahiri katika idadi ya watu waliofuatana naye, ilikuwa ni matokeo ya mapatano ya Hudaybiyah. Hii ilitokana na ukweli uliopo kwamba hapo awali, watu wengi hawakuweza kujiunga na Waislamu kutokana na kuwaogopa Waquraishi. Lakini pale Waquraishi walipoanza kutambua kuwako kwa Uislamu na kuyaacha huru

makabila kujiunga nao, ule woga uliokuwamo akilini mwa watu wa makabila mengi ulitoweka na Waislamu wakawa kwenye hali ya kuweza kuuhubiri Uislamu kwa Uhuru kabisa.

2. Faida ya pili waliyoipata Waislamu kutokana na mapatano haya ilikuwa kwamba lile pazia la chuma waliloliweka wale waabudu masanamu baina ya mtu wa kawaida na dini ya Uislamu liliondolewa, na matokeo yake yakawa kwamba kufanya safari za mjini Madina kukawa huru.

Watu wakawa na mawasiliano zaidi na Waislamu katika nyakati za misafara ya kwenda Madina na wakaweza kuyafahamu mafundisho matakatifu ya Uislamu.

Walishangazwa walipoiona nidhamu na utaratibu mwema miongoni mwa Waislamu na uaminifu wao katika ibada na utii kwa Mtume wa Uislamu (s.a.w.w.). Usafi wa Waislamu na utawadhaji katika nyakati za sala, safu zao zilizopangwa vizuri, hotuba za Mtume (s.a.w.w.) zenye kuathiri na kuzivutia nyoyo na Aya tamu za Qur'ani Tukufu, pamoja na urahisi na ufasaha wake, viliwavutia upesi sana kwenye Uislamu. Waislamu walisafiri kwenda Makka na kwenye viunga vyake kwa ajili ya shughuli mbalimbali, baada ya kufanywa kwa mapatano yale, walikutana na ndugu na marafiki zao wa kale, wakawalingania Uislamu miongoni mwao na wakawafundisha maadili, sheria na kanuni, na vitu vilivyo halali na vilivyo haramu katika dini hii.

Na jambo hili lenyewe likawa chanzo cha idadi kubwa ya viongozi wa ushirikina kama vile Khalid bin Walid na 'Amr bin Aas kujiunga na Waislamu kabla ya kutekwa kwa mji wa Makka. Kwa kweli aina hii ya maarifa ya watu juu ya Uislamu ilijenga msingi wa kutekwa kwa Makka na ikawa sababu ya hiki kituo kikuu cha ibada ya masanamu ulimwenguni kuangukia chini ya utawala wa Waislamu. Matokeo yake ni kwamba, watu walisilimu kwa idadi kubwa. Ushindi huu mkuu ulikuwa matokeo ya mawasiliano ya karibu zaidi, kuondoka kwa hofu kutoka nyoyoni na ulinganiaji wa Uislamu miongoni mwa waabudu masanamu bila ya mgogoro au kipingamizi.

3. Mawasiliano ya karibu na Mtume (s.a.w.w.) wakati wa kuyafanya ule mkataba kuliondoa kutoelewa kwingi kutoka kwenye akili za viongozi wa ushirikina, kwa sababu uadilifu bora zaidi wa Mtume (s.a.w.w.) na upole na uvumilivu wake vilivyo kinyume cha ukaidi wa lile kundi la pili vilimthibitisha kuwa yu chemchem ya maadili ya hali ya juu zaidi ya kibinadamu.

Bila kujali ukweli kwamba amepata taabu sana kutoka kwa Waquraishi, bado moyo wake ulikuwa umejawa na hisia za upendo wa kibinadamu. Waquraishi walishuhudia ya kwamba katika kufanya mkataba ule na kuvikubali vifungu vyake vya kulazimishwa, alitofautiana na maoni ya idadi kubwa ya masahaba zake mwenyewe na akaipendelea heshima ya Haram na Ka'abah, na sehemu ya kuzaliwa kwake (Makka) kuliko mwelekeo wa kundi lake.

Tabia hii iliitangua ile propaganda ya kinyume iliyokuwa ikifanywa juu ya mwenendo wa Mtume (s.a.w.w.) na ilithibitisha kwamba alikuwa rafiki wa binadamu na mtu wa amani, ambaye asingeweza kuonyesha mfundo na uadui kwa maadui zake, japo itokee kupata nafasi ya kuitawala Arabia nzima. Hata hivyo hatuwezi kukana ukweli uliopo kwamba, kama Mtume (s.a.w.w.) angelijitia kwenye vita katika

siku ile angeliweza kushinda kama ilivyoelezwa na Qur'ani Tukufu, na maadui zake wangelikimbia: **"Na lau makafiri wangelipigana nanyi basi bila shaka wangeligeuza migongo, kisha wasingelipata mlinzi wala msaidizi." (*Sura al-Fath*, 48:22).** Hata hivyo, alidhihirisha hisia za huruma na huba kwa wanadamu kwa upole wake na kuzibatilisha propaganda za kinyume dhidi yake.

Kutokana na mwanga wa hoja hizi wasomaji hawana budi kuutambua utukufu wa kauli ya Imamu wetu wa Sita, Imamu Ja'far Sadiq (a.s.) juu ya mapatano haya ya amani. Anasema: "Katika kipindi cha uhai wa Mtume (s.a.w.w.) hakuna tukio lililokuwa na faida zaidi kuliko yale mapatano ya Amani ya Hudaybiyah."

Matukio yaliyofuatia yalithibitisha kwamba kuyakataa mapatano haya pamoja na maneno yake kulikofanywa na masahaba wachache wa Mtume (s.a.w.w.) ambao kiongozi wao alikuwa Bwana 'Umar bin Khatab23 hakukuwa na msingi hata kidogo. Wanahistoria wametoa maelezo kamili ya maneno ya wale walioyakataa.24

Faida ya mapatano haya ilidhihirika kutokana na ukweli uliopo kwamba Mtume (s.a.w.w.) alikuwa bado hajawasili Madina pale ilipofunuliwa Sura al-Fath, iliyowaashiria Waislamu, na ikayaita mapatano haya ya Amani ya Hudaybiyah kuwa ni ushindi katika Jihad. Inasema: **"Bila shaka Tumekupa ushindi ulio wazi." (Sura al-Fath, 48:1).**

Waquraishi Wasisitiza Kufutwa Kwa Kifungu Kimoja Cha Mkataba

Hata hivyo, mara tu baada ya haya, matukio machungu yaliwalazimisha Waquraishi kumwomba Mtume (s.a.w.w.) kukifuta kifungu cha pili cha ule Mkataba wa Amani. Kilikuwa ni kifungu kilekile kilichowaudhi masahaba zake Mtume (s.a.w.w.) na ambacho yeye amekikubali kutokana na ukaidi usio kifani wa Suhayl. Kifungu hiki kinasema hivi:

"Kama mtu kutoka miongoni mwa Quraishi atautoka mji wa Makka bila ya ruhusa ya wazee wake na akasilimu na akajiunga na Waislamu, ni lazima Muhammad amrudishe kwa Waquraishi. Hata hivyo, iwapo mmoja wa Waislamu atak- wenda kwa Waquraishi, hawatalazimika kumrudisha kwa Waislamu."

Kifungu hiki kiliamsha hasira za baadhi ya watu katika siku ile, lakini Mtume (s.a.w.w.) alikikubali kwa moyo mmoja na kusema: "Allah Ataifungua njia kwa ajili ya faraja ya Waislamu wanyonge walio wafungwa wa Waquraishi."

Njia ya faraja hiyo na sababu ya kufutwa kwa kifungu hiki ilikuwa kama ifuatavyo: Mwislamu mmoja aliyeitwa Abu Basir aliyekuwa kafungwa na waabudu masanamu kwa kipindi kirefu aliweza kutorokea Madina.

Watu wawili wakuu walioitwa Azhar na Akhnas walimwandikia barua Mtume (s.a.w.w.) na kumkumbusha

kwamba kufuatana na kifungu cha pili cha mkataba, Abu Basir hana budi kurudishwa kwao. Walimpa mtu mmoja anayetokana na kabila la Bani ?mir barua ile, ambaye alifuatana na mtumwa wao na kumwomba ampe Mtume (s.a.w.w.) barua ile.

Kufuatana na yale mapatano aliyoyafanya, Mtume (s.a.w.w.) alimwambia Abu Basir: “Huna budi kurejea kwa watu wako na katu si sahihi kwamba tufanye ukaidi dhidi yao. Mimi ninao uhakika kwamba Allah Mwenye nguvu zote atafanya njia ya kukuachia wewe na wengine.”

Abu Basir akasema: “Je unanitoa na kuniweka mikononi mwa waabudu masanamu ili wanifanye niikane dini ya Allah?” Hata hivyo, Mtume (s.a.w.w.) aliirudia tena ile sentensi tuliyoitaja na hatimaye akamkabidhi Abu Basir kwa wale wawakilishi wa Waquraishi.

Kisha wale watu watatu waliondoka kwenda Makka. Walipofika mahali paitwapo Zil–Hulayfah,25 yule Abu Basir aliegemea kwenye ukuta kutokana na uchovu. Kisha akamwomba yule mtu wa kabila la Bani ?mir kwa njia ya kirafiki, ampe upanga wake ili autazame. Ule upanga ulipofika mikononi mwake, upesi sana alimuuwa yule ‘?mir. Yule mtumwa akakimbia kwa woga. Akarejea Madina na kumwambia Mtume (s.a.w.w.): “Abu Basir amemwua yule mwenzangu.” Mara tu baada ya hapo Abu Basri naye akafika na kuisimulia hadithi yake na kusema: “Ewe Mtume wa Allah! Wewe umeyatekeleza mapatano uliyoyafanya. Hata hivyo, mimi siko tayari kujiunga na watu wenye kuifanyia mzaha dini yangu.”.

Baada ya kuyatamka maneno hayo alikwenda Pwani ya bahari iliyokuwa njia ya misafara ya Waquraishi na kwenda kukaa mahali paitwapo Eis. Waislamu wa Makka walipata taarifa za kisa cha Abu Basir na kiasi cha watu sabini miongoni mwao wakaenda kujiunga naye. Hawa Waislamu sabini ambao maisha yao yalifanywa na Waquraishi kuwa ya taabu, waliamua kuiteka nyara misafara ya kibiashara ya Waquraishi au kumwua yeyote yule waliyeweza kumkamata.
Waliitekeleza mipango yao kwa ustadi kiasi kwamba Wakureishi hawakuweza kuvumilia, kutokana na usumbufu ule walimwandikia barua Mtume (s.a.w.w.) akifute kifungu kile kwa mapatano ya pande zote mbili na amuite Abu Basir na wenzie warudi Madina. Mtume (s.a.w.w.) alikifuta kifungu kile kwa maafikiano ya watu wote na akawaamrisha wale wakimbizi waliokuwa wakiishi pale Eis warejee Madina.26

Kitendo hiki kilitoa faraja kubwa kwa watu wote kwa ujumla na Waquraishi walitambua kwamba waumini wa kweli hawawezi kufanywa mateka daima na lilikuwa ni jambo la hatari kumweka mtu wa aina hiyo katika hali ya kuwa mateka, kwa sababu wakati wowote ule apatapo nafasi ya kutoroka atataka kulipiza kisasi.

Wanawake Wa Kiislamu Hawaku Salimishwa Kwa Waquraishi

Mapatano ya Hudaybiyah yalisainiwa. Ummi Kulthumu, binti wa Uqbah bin Abi Mu’ayt, alikuja Madina kutoka Makka. Kaka zake walioitwa Amm?rah na Walid walimwomba Mtume (s.a.w.w.) amrudishe kwao kwa mujibu wa kifungu cha pili cha mapatano yale. Mtume (s.a.w.w.) aliwajibu akisema: “Wanawake

hawakujumlishwa kwenye kifungu hicho kwa kuwa kifungu kile kinawahusu wanaume tu."[27] Nayo Sura al-Mumtahinah inaidhihirisha hali hii kuhusiana na wanawake. Inasema:

"Enyi mlioamini! Watakapokufikieni wanawake walioamini wanao- hama, basi wajaribuni, Allah ndiye Ajuaye zaidi imani yao, kama mki- jua kuwa wao ni waumini basi msiwarudishe kwa makafiri. Hawa si halali kwao, wala wao si halali kwao, na warudishieni mali walizotoa. . . ." (Surah al-Mumtahinah, 60:10).

Hii ndio hadithi ya Hudaibiyah. Kama matokeo ya amani yaliyoletwa na mapatano haya, Mtume (s.a.w.w.) alikuwa kwenye nafasi ya kuwasiliana na wafalme na watawala wa ulimwenguni kote na kuwafikishia mwito na Utume wake kwa wanadamu wote.

---

1. Majma'ul Bayaan, Juz. 9, uk. 126.
2. Siiratu Ibn Hisham, Juz. 2, uk. 309.
3. Rawzatul-Kaafi, uk. 322.
4. Majma'ul Bayaan, Juz. 2, uk. 488.
5. Bihaarul Anwwar, Juz. 20, uk. 330.
6. Tarikhut-Tabari, Juz. 2, uk. 270-272.
7. Kufuatana na ilivyonukuliwa na Tabari (Juz. 2, uk. 276) Hulays alikuja kuo- nana na Mtume (s.a.w.w.) baada ya Urwah Saqafa kuonana naye.
8. Inaelekea kwamba watu waliomzunguka Mtume (s.a.w.w) walizificha nyuso zao.
9. Siiratu Ibn Hisham, Juz. 2, uk. 314; Tarikhut-Tabari, Juz. 2, uk. 274-275.
10. Tarikhut-Tabari, Juz. 2, uk. 278.
11. Mwenye macho haambiwi tazama, bali hali halisi yamsukuma kutaka kuujua uko wapi huo ushujaa wa Umar? – Mhariri.
12. Tarikhut-Tabari, Juz. 2, uk. 278-279.
13. Irshad Mufid, uk. 6; A'laamul Waraa, uk. 106; Bihaarul Anwar, Juz. 20, uk. 368; lakini Tabari alikosea kuhusu jambo hili naye ameeleza kwamba Mtume (s.a.w.w.) yeye mwenyewe aliliandika Jina Lake.
14. Tarikh, Juz. 2, uk. 138; Bihaarul Anwaar, Juz. 20, uk. 353.
15. Tarikhul Kamil, Juz. 3, uk. 162.
16. Siiratu Halabi, Juz. 3, uk. 24 na vitabu vingine.
17. Bihaarul Anwwar, Juz. 20, uk. 353 na vitabu vingine.
18. Majma'ul Bayaan, Juz. 9, uk. 117.
19. Siiratu Halabi, Juz. 3, uk. 25-26.
20. Siiratu Halabi, Juz. 3, uk. 12; Bihaarul Anwwar, Juz. 20, uk. 312.
21. Mahali hapa Hudaybiyah pako umbali wa kilometa kumi hadi kumi na nne hivi kutoka Makka na ardhi yake kubwa ni sehemu ya Haraam.
22. Tarikhut-Tabari, Juz. 2, uk. 281; Bihaarul Anwwar, Juz. 2, uk. 352 na Siiratu Ibn Hisham, Juz. 2, uk. 281.
23. Imepokewa ndani ya vitabu vya historia vya kisuni kuwa kutokana na Mtume kukubali sharti lile la Suhayl la kufuta neno "Mtume wa Allah" Umar bin Khatab alisema: "Hakuna siku niliyokuwa na shaka na utume wa Mtume kama siku hii."- Mhariri.
24. Siiratu Ibn Hisham, Juz. 2, uk. 316.
25. Hii ni sehemu iliyoko kiasi cha kilomita kumi au kumi na moja kutoka Madina. Watu huvaa Ihraam hapa waendapo Makka.
26. Maghaazil al-Waaqidi, Juz. 2, uk. 624; Tarikhut-Tabari Juz. 2, uk. 284.
27. Siiratu Ibn Hisham, Juz. 2, uk. 323.

Sura Ya 42: Matukio Ya Mwaka Wa Saba Hijiriya

Mkataba wa Amani wa Hudaybiyah ulimwondolea Mtume (s.a.w.w.) wasiwasi kutoka kwenye sehemu ya kusini mwa Makka na hivyo basi, kikundi kutoka miongoni mwa machifu wa Uarabuni kilivutiwa na Uislamu. Katika wakati ule aliitumia nafasi hii na akaanza kuwaandikia barua watawala wa zama zile, machifu wa makabila na viongozi wa kidini wa Wakristo, na kuwabalighishia dini yake watu wa mataifa yaliyokuwa yakiishi katika zama zile. Ilikuwa ni dini ambayo katika wakati ule ilikuwa imekwenda hatua moja mbele kutoka kwenye kuamini tu, na imejitwalia umbo la dini ya ulimwengu mzima na iliweza kuwaleta wanadamu wote chini ya bendera ya Upweke wa Allah na mafundisho matukufu ya kijamii na maadili.

Hii ilikuwa ni hatua ya kwanza aliyoichukua Mtume (s.a.w.w.) baada ya mgogoro wa miaka kumi na tisa na Waquraishi wakaidi. Na kama wale maadui wa ndani wasingelimshughulisha katika vita vya umwagaji damu, basi angeliyabalighishia Uislamu yale mataifa yaishio mbali na Uarabuni mapema zaidi. Hata hivyo, mashambulizi ya kutisha ya Waarabu yalimlazimisha kuitumia sehemu kubwa ya muda wake katika kuuhami Uislamu.

Barua alizoziandika Mtume (s.a.w.w.) kwa wafalme, wana wa wafalme, machifu wa makabila, viongozi mashuhuri wa kidini na kisiasa, zilitoa mwanga juu ya njia za ubalighishaji wake wa dini. Leo tunayo maandiko ya barua 185 alizoziandika Mtume (s.a.w.w.) Kwa ajili ya kuubalighisha au kuwaita watu kwenye Uislamu au kwa njia ya mapatano na mikutano.

Wanachuoni wa hadithi na wanahistoria wamezihifadhi kwenye kumbukumbu zao.1 Barua zote zaonyesha kwamba njia za kuwaita watu na kuubalighishia Uislamu alizozifanya Mtume (s.a.w.w.) ni zile za kimantiki wala si zile za vita na upanga. Mtume (s.a.w.w.) alipojihisi kuwa katika usalama kutokana na mashambulizi ya Waquraishi aliifanya sauti yake iwafikie wakazi wa ulimwenguni kote kwa kuwapelekea barua na mubalighiina.

Ujumla Wa Utume (Kwa Watu Wote)

Baadhi ya watu wajinga huutuhumu na kuutilia shaka utume wa Mtume wa Uislamu (s.a.w.w.) ulioletwa kwa ajili ya watu wote duniani kote, nao huziiga zile nyimbo tamu ziimbwazo na baadhi ya waandishi wa kukodiwa ambao kiongozi wao ni mtaalamu mmoja wa nchi za Mashariki aitwaye Sir William Muir, asemaye: “Wazo la ujumbe wa Muhammad kuwa dini ya ulimwengu mzima lilizuka baadae, na kuanzia kwenye mwanzo wa utume wake hadi alipokufa Muhammad aliwaita kwenye Uislamu Waarabu tu, naye hakuifahamu sehemu yoyote ile zaidi ya Uarabuni.”

Mwandishi huyu wa Kiingereza ameifuata mbinu ya ajabu iliyo ngeni kwa watu wa taifa lake. Bila kujali Aya nyingi zithibitishazo kwamba Mtume (s.a.w.w.) aliwaita kwenye itikadi ya Upweke wa Allah na

Utume wake watu wote, yeye Sir William Muir anauficha mwito wa Mtume (s.a.w.w.) na anasema kwamba ulikusudiwa Waarabu tu. Hapa chini tunanukuu baadhi ya Aya za Qur'ani Tukufu zenye kuonyesha kwamba Utume wa Mtume wa Uislamu (s.a.w.w.) umekusudiwa kwa watu wote:

قُلْ يَا أَيُّهَا النَّاسُ إِنِّي رَسُولُ اللَّهِ إِلَيْكُمْ{158}

"Waambie: Enyi watu! Hakika mimi ni Mtume wa Allah kwenu nyote...
(*Surah al A'raaf, 7:158*).

Hapa hatuna budi kutambua kwamba watu wanaotajwa hapa si Waarabu tu bali ni wanadamu wote.

وَمَا أَرْسَلْنَاكَ إِلَّا كَافَّةً لِلنَّاسِ بَشِيرًا وَنَذِيرًا وَلَٰكِنَّ أَكْثَرَ النَّاسِ لَا يَعْلَمُونَ {28}

***"Na Hatukukutuma ila kwa watu wote uwe mtoaji wa khabari njema na mwonyaji, lakini watu wengi hawajui."* (*Sura al-Saba, 34:28*).**

إِنْ هُوَ إِلَّا ذِكْرٌ لِلْعَالَمِينَ {27}

***"Hiyo siyo ila ni ukumbusho kwa walimwengu."* (*Sura al-Takwir, 81:27*).**

وَمَنْ يَبْتَغِ غَيْرَ الْإِسْلَامِ دِينًا فَلَنْ يُقْبَلَ مِنْهُ وَهُوَ فِي الْآخِرَةِ مِنَ الْخَاسِرِينَ {85}

***"Na anayetaka dini isiyokuwa ya Kiislamu, basi haitakubaliwa Kwake, na yeye katika Akhera atakuwa ni miongoni mwa wenye hasara."* (*Sura Al-Imran, 3:85*).**

Aya hii inazitangua dini zote isipokuwa Uislamu tu na inawawajibisha wanadamu wote kuufuata Uislamu tu

لِيُنْذِرَ مَنْ كَانَ حَيًّا وَيَحِقَّ الْقَوْلُ عَلَى الْكَافِرِينَ {70}

***"Ili amwonye aliye hai na neno litimie juu ya makafiri."* (*Sura, Yasin, 36:70*)**

هُوَ الَّذِي أَرْسَلَ رَسُولَهُ بِالْهُدَىٰ وَدِينِ الْحَقِّ لِيُظْهِرَهُ عَلَى الدِّينِ كُلِّهِ وَلَوْ كَرِهَ الْمُشْرِكُونَ {33}

***"Yeye ndiye Aliyemtuma Mtume wake kwa mwongozo na kwa dini ya haki ili ishinde dini zote, ingawa washirikina watachukia."* (*Sura Tawbah, 9:33*).**

Sasa tunamwuliza huyu mwandishi Mwingereza, vipi anasema kwamba wazo la Uislamu kuwa dini ya ulimwengu mzima lilikuja baadae, ingawa miito kwa watu wote inadhihirishwa kwenye aya hizi? Je, mtu anayo haki ya kutia shaka juu ya utume wa Mtume (s.a.w.w.) kuwa wa ulimwengu mzima ingawa zipo aya hizi na nyinginezo, na wapo wajumbe waliotumwa kwenye nchi za mbali na maneno ya barua za Mtume (s.a.w.w) zilizomo mwenye kumbukumbu za kurasa za historia? (baadhi ya zile barua za asilia alizozipeleka kwa watu mbalimbali wa sehemu za mbali zinapatikana na zinayapamba majumba ya kumbukumbu ya ulimwengu).

Yule mwandishi Mwingereza anasema kwa ufidhuli usio wa aibu kwamba Muhammad hakuwa na ujuzi wa sehemu yoyote ile zaidi ya Uarabuni (Hijaz) ingawa alikwenda Shamu pamoja na ami yake alipokuwa na umri wa miaka kumi na sita na wakati wa utu uzima wake alifanya biashara kwa niaba ya Bibi Khadija na alikuwa akifuatana na misafara ya biashara.

Hakuma shaka kwamba wakati tunaposoma katika vitabu vya historia kwamba, Alexander Mmakedonia alitaka kuwa mtawala wa ulimwengu, au Napoleon alikuwa na shauku ya kujenga dola ya ulimwengu mzima, hatushangazwi hata kidogo, lakini pale mustashirik wanaposikia kwamba Mtume wa Uislamu (s.a.w.w.) kwa amri ya Allah amewaita watawala wawili wakubwa ulimwenguni kote (ambao walikuwa na uhusiano wa kibiashara na Waarabu) wasilimu, wao pamoja na ukaidi wao wote na shaka zisizo na msingi wowote, wanasema kwamba hili ni jambo lisilowezekana.

Ujumbe Wa Utume Wapelekwa Sehemu Za Mbali

Kama yalivyo mambo yote yaliyo muhimu, suala la kuwalingania watawala wa sehemu mbalimbali kwenye Uislamu nalo liliwekwa mbele ya halmashauri kubwa ya ushauri ili lijadiliwe. Siku moja Mtume (s.a.w.w.) aliwaambia masahaba zake: "Kesho asubuhi mhudhurie nyote ili mnipe ushauri wenu juu ya jambo muhimu sana.

"Katika siku iliyofuatia aliwahutubia masahaba zake baada ya sala ya Alfajiri, alisema: "Wausieni waja wa Allah kutenda mema. Allah Ameiharimisha Pepo kwa yule aliye mlinzi wa mambo ya watu, lakini asijitahidi kuwaongoza na kuwaonyesha njia iliyonyoka. Lazima msimame na kuupeleka ujumbe wa Uislamu kwenye nchi za mbali na lazima mfanye wanadamu waisikie sauti ya Upweke wa Allah. Hata hivyo, msinipinge kama vile wanafunzi wa Nabii Isa (a.s.) walivyompinga."

Mtume (s.a.w.w.) aliulizwa kuhusu jinsi wale wanafunzi wa Nabii Isa walivyompinga. Alijibu akisema:

“Kama mimi nifanyavyo, yeye naye ali– watuma watu wakiwa wajumbe wake kwenye sehemu mbalimbali. Kutoka miongoni mwao wale waliowajibika kwenda masafa mafupi waliitii amri yake, lakini wale waliolazimika kwenda masafa marefu walimwasi.”

Baada ya hapo Mtume wa Uislamu (s.a.w.w.) aliwatuma watu sita walio hodari kwenda sehemu mbalimbali pamoja na barua ambazo ndani yake utume wake kwa watu wote ulidhihirishwa. Hawa mabalozi wa mwongo– zo walikwenda Iran, Byzantum (Dola ya Kikristo ya Shamu/Syria) Ethiopia, Misrii, Yamamah, Bahrain, na Hira (Jordan) katika siku ile ile.

Zile barua za Mtume (s.a.w.w.) zilipoandikwa na makatibu maalum, watu waliokuwa na ujuzi wa tabia njema za mabaraza ya kifalme ya zama zile walimshauri Mtume (s.a.w.w.) kwamba azitie muhuri, kwa sababu watawala mbalimbali hawakujisumbua kuzisoma barua zisizotiwa saini, (na katika siku zile, saini zilitiwa kwa njia ya muhuri).

Kwa lengo hili, uli– tayarishwa muhuri wa duara wa fedha, kama alivyoagiza Mtume (s.a.w.w.) mwenyewe na sentensi *“Muhammad Rasulillah”* Muhammad mjumbe wa Allah ilikatwa juu ya muhuri ule. Ukataji wa sentensi hii ulikuwa wa utaratibu huu kwamba neno ‘Allah’ lilikuwa juu, neno ‘Rasul’ lilikuwa katikati na neno ‘Muhammad’ lilikuwa chini. Utaratibu na uhodari huu ulitumika ili kuzuia kuiga na udanganyifu. Msomaji alitakiwa kwanza kuisoma ile saini kuanzia chini hadi alifikie neno ‘Allah’ (*Muhammad Rasuli Allah*). Hakutosheka na hilo tu, kila baada ya kuigandisha bahasha ya ile barua kwa nta maalumu (badala ya gundi ya ‘lac’ itumikayo siku hizi), alipiga muhuri juu yake.2

Hali Ya Dunia Wakati Wa Uwasilishaji Mwaliko Wa Jumla

Katika nyakati zile nguvu kuu ya ulimwengu ilikuwa mikononi mwa dola mbili kubwa na ushindani na vita baina yao viliendelea kwa muda mrefu. Vita baina ya Iran na Urumi zilianza katika zama za Waakimenia (*Achemenias*) na ziliendelea hadi katika kipindi cha Wasasani. Wakati ule upande wa Mashariki ulitawaliwa na Mtawala wa Kiirani na Iraq, Yaman na sehemu ya Asia ndogo zilihesabiwa kuwa ni sehemu za pembeni na makoloni ya Iran. Kisha ile Dola ya Kirumi iligawanyika pande mbili (ambazo ni upande wa Magharibi na Mashariki).

Kwa kuwa katika mwaka wa 395 Masihiya Theodosius The Great, yule Mtawala wa Kirumi, aliigawa dola yake baina ya wanawe wawili na hivyo akafanya kuwako kwa nchi mbili kwa majina ya dola ya Urumi ya Mashariki na Dola ya Urumi ya Magharibi; Ile dola ya Magharibi ilipinduliwa katika mwaka 476 Masihiya. Hata hivyo, ile dola ya Urumi ya Mashariki iliyokuwa na mji wake mkuu wa Constantinople na ambayo vilevile ilizitawala nchi za Shamu na Misri ilizishika hatamu za siasa za ulimwengu mikononi mwake katika wakati wa kuanza kwa Uislamu. Iliendelea kuwako hadi kwenye mwaka wa 1453 Masihiya wakati mji wa Constantinople ulipotekwa na Sultani Muhammad II Faatih. Hapo kuwako kwa dola hii kukakoma na ikavunjwa kabisa.

Arabia ilikuwa imezungukwa na hizi dola kuu mbili. Hata hivyo, kwa vile ardhi yake haikuwa na rutuba,

na wakazi wake walikuwa mabedui walikuwa wametawanyika, hakuna yoyote kati ya dola hizi mbili iliyoonyesha mwelekeo wa kuliteka Bara hili.

Fahari, udhalimu wao na vita baina yao pia vilizizuia dola hizi kuyatambua maendeleo na mabadiliko ya kisiasa kwenye eneo hili, na katu hawakuona kwamba taifa lililo mbali kabisa kutoka kwenye ustaarabu lingeliweza kuzikomesha dola zao kwa nguvu ya imani yake, na kwamba yale maeneo yaliyoangukia kwenye giza kutokana na udhalimu wao yataangazwa na alfajiri angavu ya Uislamu. Kama wangeliupata utambuzi wa kuwako kwa nuru hii iangazayo, wangeliizimisha katika hatua yake ya awali kabisa.

Mjumbe Wa Uislamu Katika Nchi Ya Kirumi

Kaisari, yule Mfalme wa Kirumi, alikula kiapo kwa Mungu kwamba, kama akishinda vita dhidi ya Iran, atatoka kwenye makao yake makuu (Constantinople) na kwenda Yerusalemu kwa miguu kufanya Hija ya sehe– mu ile Takatifu, ikiwa ni ishara ya kutoa shukrani zake kwa ule ushindi mkuu. Baada ya kupata ushindi alikitekeleza kiapo chake na akaenda Yerusalem kwa miguu.

Dihyah bin Kalbi alitumwa na Mtume (s.a.w.w.) kuipeleka barua yake kwa Kaisari. Alikuwa kaishafanya safari nyingi kwenda Shamu, naye alikuwa na ujuzi kamili wa sehemu mbalimbali za ukanda ule. Sura yake ya kuvutia, na tabia tukufu vilimfanya astahiki kabisa kulibeba jukumu hili lililo muhimu zaidi.

Kabla ya kutoka Shamu kwenda Constantinople akiwa kwenye mmoja wa miji ya Shamu uliotiwa Busra3 alitambua kwamba Kaisari amekwenda Yerusalem. Hivyo basi, upesi sana akaonana na Harith bin Abi Shamir, gavana wa Busra na kumweleza kuhusu ile kazi muhimu aliyonayo.

Mwandishi wa *Tabaqaatul–Kubra* anaandika hivi:4 “Mtume (s.a.w.w.) alikuwa kamwelekeza Dihyah kumkabidhi barua ile yule mtawala wa Busra ili kwamba yeye ampe Kaisari. Inawezekana kwamba maelezo haya yalitolewa kwa kuzingatia kwamba yeye Mtume (s.a.w.w.) alitambua juu ya safari ya Kaisari au kwa sababu hali na uwezekano wa Dihyah ulikuwa na kikomo na safari yake ya kwenda Constantinople haikuwa huru kutokana na matatizo na shida. Hata hivyo, yule balozi wa Mtume wa Uislamu (s.a.w.w.) aliwasiliana na yule Mtawala wa Busra. Yule gavana alimwita mtu mmoja aliyeitwa Addi bin Haatim na kumwamrisha afuatane na yule balozi wa Mtume (s.a.w.w.) hadi Yerusalem na kumpa Kaisari ile barua ya Mtume (s.a.w.w.).

Yule balozi ilikuwa aonane na Kaisari mjini Hams. Aliomba kuzungumza na Kaisari na akaomba kwamba uwekwe muda maalum wa kuzungumza naye. Maafisa wahusika wakamwambia: “Itakubidi umsujudie Kaisari mara moja, kwa sababu kama hukufanya hivyo hatakusikiliza na hataipokea barua yako.” Dihyah, yule balozi wa Mtume wa Uislamu (s.a.w.w.) mwenye hekima, akasema: “Nimeichukua taabu yote hii katika kuja hapa kuzikomesha hizi desturi zisizo sahihi. Nimeelekezwa na Mtume kwamba nimwambie Kaisari kwamba kumwabudu mwanadamu hakuna budi kukoma na hakuna apasaye kuabudiwa ila Allah, Mwenye nguvu zote. Basi vipi mimi niliye na jukumu na itikadi hii nitaweza kuyakubali maoni yenu na kumsujudia mtu yeyote asiye Allah?”

Uthabiti, uimara na hoja zenye nguvu za balozi huyu zilipendwa mno na wale wafanyakazi wa baraza la mfalme. Mfuasi mmoja wa mfalme aliyekuwa mwema akamwambia Dihyah: “Iache hiyo barua kwenye meza maalum ya Mfalme kisha urejee. Hakuna aigusaye barua iliyoko juu ya meza ile ila Kaisari mwenyewe. Kaisari atakapoisoma atakuita.” Dihyah akamshukuru mtu yule kwa kumpa mwongozo ule, akaiacha ile barua kwenye ile meza na akarejea.

Kaisari akaifungua ile barua. Neno la kwanza la barua ile: *Bismillah’* (kwa jina la Allah) lilimvutia na akasema: “Katu sijapata kuiona barua ya aina hii ila ya Suleimani.” Kisha akamwita mkalimani wake ili amsomee ile barua na kumtafsiria. Yule mkalimani aliitafsiri ile barua ya Mtume (s.a.w.w.) kama ifuatavyo: “Hii ni barua itokayo kwa Muhammad bin Abdullah kwenda kwa Hercules Mkuu wa Urumi. Amani na iwe juu ya wafuasi wa mwongozo. Ninakulingania kwenye dini ya Uislamu. Silimu ili usalimike. Allah Atakulipa thawabu mbili (thawabu kwa kuamini kwako wewe mwenyewe na thawabu kwa kule kuamini kwa walio chini yako). Hata hivyo, kama ukiugeuzia uso wako Uislamu, utawajibika kwa dhambi za ‘Waarisiyani’5

“Halikadhalika. Enyi watu wa Kitabu! Tunakuiteni kwenye neno lililo sawa baina yetu, yaani tusimwabudu yeyote ila Allah. Tusimfanye yeyote kuwa mshirika wake. Baadhi yetu nao wasiwafanye wengine kuwa miungu wao. Na (ewe Muhammad!) Watakapoikaidi dini ya kweli, sema: Shuhudieni ya kwamba sisi ni Waislamu.”

Kaisari Afanya Uchunguzi Juu Ya Mtume (S.A.W.W)

Yule mtawala wa Kirumi mwenye hekima alifikiria kwamba huenda mwakilishi wa barua ile alikuwa ni yule Nabii Aliyeahidiwa, Muhammad, aliyezungumziwa kwenye Injili na Taurati. Hivyo basi, aliamua kupata taarifa kamili juu ya Mtume (s.a.w.w.). hivyo alimwita mkuu wa idara ya utawala na kumwambia: “Fanya utafiti kamili kwa kupitia Shamu. Inawezekana kwamba ukaweza kupata baadhi ya jamaa au ndugu wa Muhammad au watu wengine wanaozifahamu habari zilizopita za mtu huyu ili niweze kupata taarifa kutoka kwao.”

Kwa bahati katika siku zile Abu Sufyani na watu wengine kutoka miongoni mwa Waquraishi walikuwa wamefika Shamu kwa ajili ya biashara. Yule mwakilishi wa Kaisari alionana nao na akawachukua wote hadi Yerusalemu. Walichukuliwa na kupelekwa wakaonane na Kaisari. Kaisari akawauliza: “Je, yuko yeyote miongoni mwenu aliye na uhusiano na Muhammad?” Abu Sufyani akajisoza kidole na kusema: “Yeye na mimi tunatokana na kabila moja na koo zetu zinakutana kwa jadi wetu wa nne (Abdi Munaf).”Kaisari akaamrisha kwamba Abu Sufyani asimame kwa kumwelekea na wale wengine wasimame mgongoni kwake ili kwamba kama akiwa na upendeleo katika majibu yake mara moja waeleze kosa au uwongo wake. Baada ya kuufanya mpango huu, Kaisari alimwuliza Abu Sufyani maswali yafuatayo ambayo Abu Sufyani aliyajibu kwa uhakika kama ifuatavyo:

Kaisari: Unajua nini kuhusu jadi zake Muhammad?

Abu Sufyani: Yeye anatokana na familia tukufu.

Kaisari: Je, alikuwapo yeyote kutoka miongoni mwa jadi zake aliyetawala watu?

Abu Sufyani: Hapana.

Kaisari: Je, Kabla ya kudai kwamba yu Mtume, alikuwa akijiepusha na uwongo au la?

Abu Sufyani: Hakuna shaka kwamba Muhammad alikuwa mtu mkweli.

Kaisari: Ni daraja lipi la watu wamuungao mkono na kumwamini?

Abu Sufyani: Watu watukufu wako dhidi yake na watu wa kawaida na watu daraja la chini ndio wafuasi wake waaminifu.

Kaisari: Je, wafuasi wake wanaongezeka?

Abu Sufyani: Ndio.

Kaisari: Je, mtu yeyote kutoka miongoni mwa wafuasi wake amepata kugeuka na kuwa mwenye kuikana dini yake?

Abu Sufyani: Hapana.

Kaisari: Je, alipokuwa akipigana dhidi ya maadui zake, alikuwa akishindwa?

Abu Sufyani: Katika baadhi ya nyakati alikuwa akishinda na katika nyakati nyingine alishindwa.

Kaisari akamwamrisha mkalimani amwambie Abu Sufyani na wenzie kwamba kama maelezo haya ni sahihi, yeye (Muhammad) bila shaka atakuwa ni yule Nabii wa mwisho aliyeahidiwa. Kisha akaongeza kusema: “Ninayo taarifa kwamba Nabii wa aina hii atatokea, lakini mimi sikufikiria kwamba atatokana na kabila la Waquraishi.

Hata hivyo, mimi niko tayari kutoa heshima zangu kwake na kuinawisha miguu yake ikiwa ni ishara ya heshima na hivi karibuni mamlaka na utukufu wake utazikamata nchi za Kirumi.”

Mpwawe Kaisari alisema: “Katika barua ile, Muhammad ameandika jina lake juu ya jina lako, lakini bado hajaadhibiwa kutokana na uchochezi wake huu.”

Kaisari akasema kwa ghadhabu: “Inafaa kwamba jina la mtu yule ambaye Malaika mkuu Jibriil amemshukia lilitangulie langu?”

Abu Sufyani anasema: “Upendeleo wa ndani zaidi wa Kaisari juu ya Muhammad ulizaa minong’ono mle barazani nami nikashikwa na wasiwasi kutokana na kukuwa kwa hasira zake kwamba isije ikawa kwamba cheo cha Muhammad kikawa juu zaidi kiasi kwamba taifa la kirumi likaanza kumwogopa.

Ingawa pale ulipoanza uulizaji wa maswali nilijaribu kumtweza Muhammad mbele ya Kaisari na nikamwambia kwamba Muhammad alikuwa mdogo kuliko vile alivyokwisha kusikia juu yake, lakini Kaisari hakuyasikiliza maelezo yangu yenye kuvunja heshima, na akasema: “Yajibu tu yale maswali ninayokuuliza.”6

Barua Ya Mtume (S.A.W.W) Yamvutia Kaisari

Kaisari hakutosheka tu na ile taarifa aliyoipata kutoka kwa Abu Sufyani lakini aliandika barua juu ya jambo lile kwa mmoja wa wataalamu wa Urumi. Yule mtaalamu alijibu kwa kuandika hivi: “Huyo ndiye yule Nabii anayengojewa na ulimwengu.” Kaisari alitayarisha mkutano mkubwa kwenye moja ya majumba ya watawa ili ajue jinsi machifu wa Kirumi wafikiriavyo, na baada ya kuisoma ile barua ya Mtume (s.a.w.w.) mbele yao, alisema: “Je, mnakubali kwamba niiridhie dini yake?” Mara moja yakatokea machafuko makubwa mno kwenye mkutano ule kiasi kwamba upinzani wa watu ulimwogofya Kaisari kuhusu uhai wake.

Mara moja akaamka kutoka kwenye kiti chake kilichokuwa kwenye sehemu iliyoinuka na akawahutubia watu wake, akisema: “Kwa kuliweka lengo hili mbele yenu nilitaka kukujaribuni. Uthabiti na unyoofu wenu katika dini ya Nabii Isa umeuibua upendo na furaha yangu juu yenu.”

Kaisari akamwita Dihyah na akampa heshima. Aliandika jibu la Barua ya Mtume (s.a.w.w.) na vilevile akapeleka zawadi fulani fulani kupitia kwa Dihyah. Katika barua yeke ile alionyesha imani na utii wake kwake.7

Balozi Wa Mtume (S.A.W.W) Awasili Iran

Yule Balozi wa Mtume (s.a.w.w.) alipoondoka kwenda kwenye baraza la nchi ya Iran, mtawala wa nchi ile iliyo pana mno alikuwa ni Khusro Perviz. Yeye alikuwa mtawala wa pili baada ya Anushirwan ambaye alikikalia kiti cha enzi miaka thelathini na miwili kabla ya kuhajiri kwa Mtume (s.a.w.w.) na ilimbidi kuyakabili matukio mengi, machungu na matamu kwenye kipindi kile. Katika utawala wake Khusro Perviz nguvu ya Iran ilikuwa kwenye hali ya kuyumba kabisa. Kwenye wakati fulani Iran ilipenya katika Asia Ndogo na kuieneza mamlaka yake hadi karibu na Constantinople na Msalaba wa Nabii Isa (a.s.) uliokuwa kitu kitakatifu zaidi miongoni mwa Wakristo aliuchukua na kuupeleka kwenye mji wake mkuu, Taisfun (Madaa’in).

Yule mtawala wa Kirumi aliomba amani na akampeleka balozi kwenye baraza la Iran kufanya mapatano ya Amani. Sasa mipaka ya Iran ililingana na mipaka ya nchi za Waakimeni.

Kisha, hata hivyo Iran ikafika kwenye ukingo wa maanguko kutokana na sera mbaya, fahari iliyokithiri na maisha ya kibadhilifu ya mtawala. Zile nchi zilizotekwa zikaponyoka moja baada ya nyingine na majeshi ya maadui yakafika ndani zaidi ya Iran (yaani Dastgards karibu na Taisfun). Matokeo yake yakawa kwamba Khusro Perviz akalazimika kukimbia kutokana na kuwaogopa Warumi. Kitendo hiki cha aibu

kwa upande wake kiliiamsha ghadhabu ya taifa na hatimaye aliuawa na mwanawe mwenyewe aliyeitwa Shirviyah.

Wanahistoria huyachukulia maanguko ya Iran kuwa ni matokeo ya fahari, kujipendelea na maisha ya anasa ya mtawala. Kama angaliukubali ujumbe ulioletwa na yule balozi wa Amani, utukufu wa Iran ungalisalia kwenye usalama na amani.

Kama ile barua ya Mtume (s.a.w.w.) haikuleta mvuto uliohitajika akilini mwa Khusro Perviz, basi hali hii haikutokana na kitu chochote kibaya katika barua ile au kwa sababu yule mtu aliyeileta alifanya kosa. Bali kusema kweli fikara zake za ajabu na kujipendelea kulikokithiri havikumruhusu kuufikiria mwito wa Mtume (s.a.w.w.) japo kwa kitambo tu. Matokeo yake ni kwamba, japo kabla ya mkalimani kuimalizia barua ile, alipiga makelele na baada ya kuinyakua barua ile, aliipasua vipande vipande. Yafuatayo hapa chini ndio maelezo kamili ya tukio lile: Mwanzoni mwa mwaka wa saba Hijiriya8 Mtume (s.a.w.w.) alimteua mmoja wa maafisa wake mashuja aliyeitwa Abdullah Huzafah Sahmi Qarashi kupeleka barua kwa Khusro Pervis akimlingania kwenye Uislamu. Hapa chini tunaona ile barua ya Mtume (s.a.w.w.):

“Kwa jina la Allah, Mwingi wa Rehema, Rahim. Hii ni barua itokayo kwa Muhammad Mjumbe wa Allah, kwenda kwa Kisra Mkuu wa Iran. Amani na iwe juu yake yule autafutaye ukweli na akaidhihirisha imani yake juu ya Allah na juu ya Mtume Wake na akashuhudia ya kwamba hakuna mungu ila Allah na kwamba hana mshirika, na yule aaminiye kwamba Muhammad yu mja na Mtume wake. Kwa Amri ya Allah, ninakuita (uje) Kwake. Amenituma kwa ajili ya mwongozo wa watu wote ili kwamba niwaonye wote dhidi ya ghadhabu Yake na niwafikishie makafiri onyo la mwisho. Silimu ili kwamba uwe salama. Na kama ukikataa kusilimu, utawajibikiwa na dhambi.”9

Yule Balozi wa Mtume (s.a.w.w.) aliwasili kwenye baraza la Iran. Khusro Perviz aliamrisha kwamba ile barua ichukuliwe kutoka kwake. Lakini yule balozi akasema kwamba lilikuwa ni jambo muhimu kwamba ampe mfalme barua ile yeye mwenyewe, na kisha akaiwasilisha kwake. Khusro Perviz alimwita mkalimani naye akaitafsiri hivi:

“Hii ni barua itokayo kwa Muhammad Mjumbe wa Allah, kwenda kwa Kisra mkuu wa Iran. . . Yule mkalimani alikuwa bado hajamaliza kuisoma barua ile wakati yule mtawala wa Iran alipofadhaika mno, akapiga ukelele kwa sauti kuu, akaichukua ile barua kutoka mikononi mwa yule mkalimani akaipasua vipande vipande na akasema kwa sauti kuu: “Hebu mtazame mtu huyu! Ameliandika jina lake mwenyewe kabla ya jina langu.” Mara moja akaamrisha kwamba Abdullah atolewe nje ya Ikulu. Abdullah akatoka mle Ikulu akampanda farasi wake na akaondoka kurejea Madina. Alipofika huko alimwarifu Mtume (s.a.w.w.) jambo lile. Mtume (s.a.w.w.) alichukizwa mno kupata tarifa za utovu wa heshima aliouonyesha Khusro, na dalili za ghadhabu zilijitokeza usoni mwake. Alimlaani Khusro kwa maneno haya: “Ee Mola! Uvunje ufalme wake vipande vipande.”10

Maoni Ya Uwongo Ya Yaa'qubi

Kinyume na ukweli ukubaliwao na wanahistoria wengi, Yaa'qubi katika historia yake anasema hivi: "Khusro Perviz aliisoma ile barua ya Mtume (s.a.w.w.) na akampelekea zawadi ya manukato ya miski na nguo za hariri kupitia kwa yule balozi wake zikiwa ni ishara ya heshima kwake.
Mtume akayagawa manukato yale na akasema kwamba: "Hariri haikuwafaa wanaume." Vile vile alisema: "Nguvu ya Uislamu itaingia katika nchi zake na amri ya Allah itatimizwa hivi karibuni."11

Hata hivyo, hakuna yeyote miongoni mwa wanahistoria anaye kubaliana naye, ila Ahmad bin Hanbal anayeandika kwamba Khusro Perviz alipeleka zawadi kwa aijili ya Mtume (s.a.w.w.).12

Khusro Perviz Awasiliana Na Mtawala Wa Yemen

Nchi yenye rutuba ya Yaman iko upande wa Kusini mwa mji wa Makka na daima watawala wake wamekuwa wakitawala wakiwa ni vibaraka wa Wafalme wa Kisasani. Mtawala wa Yaman katika siku zile alikuwa ni Bazan na yule Mfalme wa Kisasani aliandika barua kwa jinsi ya majivuno ya majisifu hivi: "Nimearifiwa kwamba mtu mmoja kutoka miongoni mwa Waquraishi wa Makka anadai kwamba yu Mtume. Wapeleke maafisa wako wawili walio mashuja kwake ili wakamtie kizuizini na kumleta kwangu."13

Ibn Hajr ameeleza kwenye kitabu chake *al–Isabah* kwamba Khusro Perviz alimwamrisha Bazan kwamba hao maafisa wawili hawana budi wamshawishi Mtume arejee kwenye dini ya jadi zake na kama akikataa kufanya hivyo, akatwe kichwa chake na kipelekwe kwake.

Barua hii yaonyesha dhahiri ujinga wa mtawala wa wakati ule, hakuweza hata kujua kwamba yule mwenye kudai utume kahajiri kutoka Makka kwenda Madina miaka sita kabla ya pale. Vilevile hakutambua kwamba haikuwezekana kumtia kizuizini kwa kuwatuma maafisa wawili, au japo kumwita aende Yaman mtu ambaye aliyedai kuwa yu Mtume kwenye nchi ambayo ushawishi wake umeenea mno kiasi kwamba alikuwa akiwatuma mabalozi kwenye mabaraza ya watawala wa ulimwengu.

Kama alivyoamrishwa na makao makuu, yule Mtawala wa Yaman aliwapeleka huko Hijaz maafisa wawili mashujaa na wenye nguvu walioitwa Firoz na Kharkhusrah. Kwanza walionana na Mquraish mmoja mjini Taa'if.

Aliwaongoza na akasema: "Mtu mnayehitaji kuonana naye, siku hizi yuko Madina." Hapo wakaenda Madina na wakajifikisha mbele ya Mtume (s.a.w.w.) wakampa Mtume (s.a.w.w.) barua ya Bazan na kusema: "Kufuatana na amri tuliyopewa kutoka makao makuu, tumetumwa tukuchukue twende nawe Yaman, nasi tunafikiri kwamba Bazan atamwandikia barua Khusro Perviz kuhusiana nawe na atafanya yale ayasemayo, au sivyo, kwa vyovyote vile vita itaanza baina yako na sisi na nguvu ya Kisasani itazibomoa nyumba zenu na kuwauwa watu wenu."

Mtume (s.a.w.w.) aliyasikiliza maneno yao kwa utulivu kamili. Kabla ya kuwapa jibu aliwakaribisha wasilimu. Hakuzipenda sura zao kwa vile walifuga masharubu marefu na akawaambia: “Mola wangu ameniamrisha kwamba nifuge ndevu zangu na kuyafanya masharubu yangu kuwa mafupi.”14

Maafisa hawa walitishwa mno na ukuu, haiba na utulivu wa Mtume (s.a.w.w.) kiasi kwamba alipowakaribisha wasilimu, walikuwa wakitetemeka. Kisha akawaambia: “Mnaweza kwenda leo hii. Nitakuarifuni uamuzi wangu kesho.”Wakati uleule ulikuja ufunuo na Malaika Mkuu ukimwarifu Mtume (s.a.w.w.) kuhusu kuuawa kwa Khusro Perviz.

Katika siku iliyofuatia wale maafisa wa Yaman walipokuja kwa Mtume (s.a.w.w.) aliwaambia: “Mola wa ulimwengu ameniarifu kwamba yalipopita masaa saba ya usiku uliopita, Khusro Perviz kauawa na mwanawe (Shirviyah) ambaye hivi sasa kakalia kiti cha enzi.”

Ule usiku ambao Mtume (s.a.w.w.) aliuainisha ulikuwa usiku wa kuchea Jumanne, mwezi 10, Jumadiul Awwal, 7 Hijiriya.15 Wale wawakilishi wa Bazan walishangazwa sana kusikia hivyo na wakasema: “Jukumu la yale uliyoyasema ni kubwa zaidi kuliko dai la utume lililomkasirisha yule mfalme wa Kisasani. Hatuna la kufanya ila kumtaarifu Bazan juu ya jambo hili. Atapeleka taarifa kuhusu jambo hili kwa Khusro Perviz.”

Mtume (s.a.w.w.) akasema: “Mimi nitafurahi sana kama mkimweleza juu ya jambo hili na vile vile mwambieni kwamba dini na mamlaka yangu vitazifikia nchi hizo ambazo farasi waendao mbio huzifikia na kama yeye akisilimu nitamwachia nchi hizo zilizo kwenye utawala wake hivi sasa.” Kisha ili kuwashawishi wale watu wawili waliotumwa na Bazan, Mtume (s.a.w.w.) aliwapa mkanda wa bei ghali uliotariziwa kwa dhahabu na fedha na ambao alipewa zawadi na machifu fulani wa makabila. Wote wawili walitosheka kabisa na wakamwacha na wakarejea Yaman. Walipofika kule walimweleza Bazan ule ujumbe wa Mtume (s.a.w.w.).

Bazan akasema: “Kama taarifa hizi ni sahihi, bila shaka yeye yu Mtume wa Allah kweli na hana budi kutiiwa.” Wakati ule ule alipokea barua kutoka kwa Shirviyah yenye maneno haya: “Fahamu ya kwamba nimemuua Khusro Perviz. Ghadhabu ya taifa imenifanya nimuue kwa sababu amewauwa watu watukufu (wa Uajemi–Iran) na kuwatawanya wazee. Mara tu uipatapo barua yangu huna budi kupata kiapo cha utii kwa ajili yangu kutoka kwa watu, na mpaka pale upatapo amri nyingine kutoka kwangu usiwe mkali kwa yule mtu adaiye kwamba yu Mtume na ambaye baba yangu alitoa amri dhidi yake.”

Ile barua ya Shirviyah ilitoa njia ya kusilimu kwa Bazan na watumishi wa serikali wote waliokuwa Wairan. Bazan alimwandikia barua Mtume (s.a.w.w.) na kumwarifu kuhusu kusilimu kwake pamoja na wale watumishi wa serikali.

Mjumbe Wa Uislamu Awasili Misrii

Misrii ilikuwa chanzo cha ustaarabu wa kale, makao makuu ya ufalme wa Mafarao (Mafirauni) na makao

makuu ya serikali ya Wakibti (Madhehebu ya Kikristo ya KiMisrii). Tangu mwanzoni mwa Uislamu huko Hijaz, Misrii ilipoteza nguvu na uhuru wake. Maqauqis ameukubali ugavana wa Misrii kutoka kwa Mfalme wa Kirumi kwa kulipwa dinar milioni kumi na tisa kwa mwaka.

Hatib bin Abi Balta'ah alikuwa mpanda wanyama shujaa na mzoefu naye alihusika na tukio maarufu la historia ya Uislamu. Yeye alikuwa mmoja wa wale watu sita waliotumwa kuzipeleka zile barua za kimialiko za Mtume (s.a.w.w.) kwenda kwa watawala wa ulimwenguni. Mtume (s.a.w.w.) alimwamrisha kuipeleka barua ifuatayo kwa Maqauqis, Mtawala wa Misri: "Kwa jina la Allah, Mwingi wa Rehma, Rahimu. Hii ni barua itokayo kwa Muhammad bin Abdillah kwenda kwa Maqauqis mkuu wa Wakibti. Amani na iwe juu ya wafuasi wa ukweli. Ninakulingania kwenye dini ya Uislamu. Silimu ili usalimike (kutokana na ghadhabu ya Allah). Silimu ili Allah Mwenye Nguvu zote akulipe thawabu mbili. Na kama ukiugeuzia mbali uso wako kutoka kwenye Uislamu utawajibikiwa na dhambi za Wakibti pia.

"Enyi watu wa Kitabu! Tunakuiteni kwenye neno lililo sawa baina yetu, yaani tusimwabudu yeyote ila Allah. Tusimfanye yeyote kuwa mshirika wake. Baadhi yetu wasiwafanye wengine kuwa miungu wao. Na (ewe Muhammad) Watakapoikaidi dini ya kweli, sema: "Shuhudieni ya kwamba sisi ni Waislamu."16

Yule balozi wa Mtume wa Uislamu (s.a.w.w.) aliondoka kwenda Misri na akapata taarifa ya kwamba wakati ule, yule mtawala alikuwa akiishi kwenye kasri ndefu mjini Alexandria, mji ulioko kwenye ukingo wa mto. Hivyo akaenda Alexandria na akaliingia jahazi.
Habib akapokewa kwenye baraza la kifalme, mfalme akaifungua ile barua na akayafikiria maneno yaliyokuwamo katika barua ile kwa kitambo fulani. Kisha akakiinua kichwa chake na kuzungumza na yule balozi wa Uislamu kwa maneno haya: "Kama kweli Muhammad yu Mtume wa Allah kwa nini wapinzani wake waliweza kumtoa kwenye sehemu aliyozaliwa na ni kwa nini alilazimika kuishi Madina? Kwa nini asiwalaani ili kwamba waangamizwe na Allah?"

Yule balozi wa Uislamu aliye mtu mwenye akili na mjuzi wa mambo, alijibu akasema: "Nabii Isa (a.s.) alikuwa ni Mtume wa Allah nawe pia wamtambua kuwa alikuwa hivyo. Basi kwa nini hakuwalaani wana wa Israeli walipopanga kumwua ili kwamba Allah angeliwaangamiza?"

Yule Mtawala ambaye hakulitegemea jibu la haraka kiasi kile alikubaliana na hoja za kimantiki zenye nguvu za yule balozi na akamsifu akisema: "Vizuri sana! Wewe ni mtu mwenye hekima na umeuleta ujumbe utokao kwa mtu mwenye hekima na elimu nyingi."17

Yule balozi alitiwa moyo na mapokezi mazuri aliyopewa na yule Mtawala wa Misri na kwa lengo la kutaka kumkaribisha asilimu, alisema hivi: "Kabla yako, mtu mmoja (Farao) aliitawala nchi hii; aliwatesa watu kwa muda mrefu. Allah alimwangamiza ili kwamba maisha yake yawe somo kwa ajili yako. Hata hivyo, lazima ujitahidi kwamba maisha yako kama yalivyokuwa yake yasije yakawa somo kwa wengine.

"Mtume wetu anawalingania watu kwenye dini safi. Waquraishi walifanya kampeni dhidi yake na Wayahudi nao walimpinga kwa chuki isiyo kifani. Watu walio karibu yake ni Wakristo. Ninaapa kwa uhai wangu kwamba kama vile Nabii Musa bin Imran alivyowatabiria watu juu ya Nabii Isa (a.s.) naye

ameutabiri Utume wa Muhammad (s.a.w).

“Ninakulingania kwenye dini ya Uislamu na kitabu chetu kilichofunuliwa (Qur’ani) kama vile ulivyowaitia watu wa Taurati kwenye Injili. Kila taifa liusikiao mwito wa Mtume ni lazima limfuate. Na sasa kwa vile niishaufanya mwito huu wa Mtume (s.a.w.w.) kufika nchini mwako, inafaa kwamba wewe na watu wa taifa la Wa–Misri muifuate dini yake. Katu mimi sikuzuieni kuifuata dini ya Nabii Isa (a.s.). Ila tu ninakuambieni kwamba ifuateni dini yake lakini muelewe kwamba utaratibu uliokamilika wa dini ya Nabii Isa (a.s.) ni huu Uislamu wenyewe.”18

Mkutano wa yule balozi na mtawala wa Misri ulimalizika, lakini yule Maqauqis hakumpa jibu la mwisho. Hivyo ilikuwa muhimu kwamba Hatib asubiri kwa muda fulani zaidi ili apate jibu la kupeleka kwa Mtume wa Uislamu (s.a.w.w.). Siku moja yule Maqauqis alimwita na akafanya mkutano naye katika sehemu ya faragha ya Kasri lake, na akamwuliza kuhusu mpango na dini ya Mtume (s.a.w.w.). Yule balozi akajibu akasema: “Yeye anawalingania watu kumwabudu Allah tu.

Anaamrisha kwamba watu wasali mara tano kwenye nyakati za mchana na usiku, na pia wafunge kwenye mwezi wa Ramadhani. Pia lazima wafanye Hijja kwenye Nyumba ya Allah na watimize ahadi zao, waambae kula mfu na kunywa damu . . .” Hatib aliyamalizia maneno yake kwa kuzieleza tabia tukufu za Mtume (s.a.w.w.).

Yule mtawala wa Misri akamwambia: “Hizi ni dalili za utume. Nilijua kwamba Nabii wa mwisho bado hajaja. Hata hivyo, nilikuwa nikidhania kwamba atatokea, lakini si katika Hijaz bali nchini Shamu, nchi iliyokuwa kitovu cha kutokea kwa Mitume. Lakini, ewe balozi wa Muhammad! Huna budi kutambua kwamba kama nikisilimu Wakibti hawatashirikiana nami. Ninategemea kwamba mamlaka ya Mtume huyu yatapanuka hadi yafike Misri na masahaba zake watakuja nchini mwetu na kupata ushindi juu ya majeshi ya nchi hii na juu ya itikadi za uwongo. Na ninapendelea kwamba uyafanye mazungumzo haya kuwa siri na asiyajue Mkibti yeyote.”19

Maqauqis Amwandikia Barua Mtume (S.A.W.W)

Yule mtawala wa Misri alimwita katibu wake wa Kiarabu na kumwamrisha aandike barua iendayo kwa Mtume (s.a.w.w) kama ifuatavyo: “Hii ni barua iendayo kwa Muhammad bin Abdullah, itokayo kwa Maqauqis chifu wa Wakibti. Amani na iwe juu yako! Nimeisoma barua yako, nimeyaelewa yaliyomo humo na kuutambua ukweli wa mwito wako.

Nilijua kwamba atatokea Mtume, lakini nilifikiria kwamba atainukia katika nchi ya Shamu. Nimekukaribisha kuwasili kwa balozi wako.”

Kisha kwenye barua ile anazitaja zawadi alizompelekea Mtume (s.a.w.w.) na akaishilizia barua ile kwa maneno: “Amani naiwe juu yako.”

Heshima aliyoionyesha yule Maqauqis kwa Mtume (s.a.w.w.) kwenye barua yake na kwa kuandika jina

la Muhammad mwanzoni, na zile zawadi za thamani alizompelekea Mtume (s.a.w.w.) na yale makaribisho aliyompa yule balozi wake, vyaonyesha kwamba aliukubali mwito wa Mtume (s.a.w.w.) kwa siri lakini kwa kukipenda kwake cheo chake cha utawala, kulimzuia kuidhihirisha imani yake.

Kutoka Misri, Hatib alifika Shamu akiwa chini ya ulinzi wa kikundi cha watu walioteuliwa na Maqauqis. Hapo Shamu aliwaruhusu watu wale warejee na yeye akaendelea na safari kurudi Madina pamoja na msafara. Akaifikisha ile barua ya Maqauqis kwa Mtume (s.a.w.w.) na vile vile akaufikisha ujumbe wake. Mtume (s.a.w.w.) akasema: “Hakusilimu kutokana na woga kwa ajili ya utawala wake, lakini utawala wake na mamlaka vitamalizika hivi karibuni.”

Balozi Wa Uislamu Aingia Ethiopia

Ethiopia iko kwenye ncha ya mwisho ya Afrika ya Mashariki. Eneo lake ni kilometa za mraba 18,000 na mji wake mkuu wa siku hizi ni mji wa Adis Ababa. Watu wa nchi za Mashariki walifika nchini humu kwa zaidi ya karne nzima kabla ya Uislamu.

Kufika kwao huku kulianzia na mashambulizi ya jeshi la Kiirani kwenye zama za Utawala wa Anushirw?n na ukafikia ukubwa wake kwa kuhamia humo wale Waislamu waliotoka Makka kuja Ethiopia.

Wakati Mtume (s.a.w.w.) alipoamua kuwatuma wajumbe sita wenye sifa nzuri na mashujaa kwenye sehemu za mbali kuwa mabalozi kwa ajili ya kuubalighisha utume wake wa ulimwengu mzima ili ufahamike kwa watu wa ulimwenguni kote, alimteuwa ‘Amr bin Umayyah kwenda Ethiopia pamoja na barua yake na kuupeleka ujumbe wake kwa Negus, mtawala mwadilifu wa nchi ile. Hii haikuwa barua ya kwanza ambayo Mtume (s.a.w.w.) alimwandikia yule Mtawala wa Ethiopia.

Hapo awali aliandika barua pia kuhusiana na Muhajiriin akimwomba Negus kuwahurumia. Maneno ya barua ile yamehifadhiwa katika historia.20 Wakati mwingine hutokea kuchanganyikiwa baina ya hizi barua mbili (yaani baina ya ile ya kuwatambulisha wale Muhajiriin kwa Negus, na ile ya Mtume (s.a.w.w.) kuubalighisha utume wake kwa ulimwengu mzima), na maneno ya barua zote hizi yamechanganyika.

Pale Mtume (s.a.w.w.) alipompeleka balozi wake kule Ethiopia akiwa na barua, baadhi ya wahajiri wa Kiislamu walikuwa bado wakiishi pale, ambapo wengine walikuwa tayari wamesharejea na kuishi Madina, nao walikuwa wameusifu uadilifu wa yule mtawala mkuu wa nchi ile na huruma zake kwa raia zake. Hivyo basi, kama tukiona aina fulani ya mwelekeo, huruma, na upole kwenye maneno ya barua aliyoandika Mtume (s.a.w), akimwandikia mtawala yule, ni kwa sababu alizitambua fikira za Negus. Katika barua alizowaandikia watawala wengine aliwaonya kuhusiana na wakati wa ghadhabu ya Allah na akawaambia kwamba kama hawatasilimu, basi dhambi za wale watakaoacha kusilimu kutokana na hofu vilevile zitaandikwa kwenye hesabu zao. Hata hivyo, hakuna jambo la aina hii lililosemwa kwenye barua ifuatayo, aliyoandikiwa Negus: “Kwa jina la Allah, Mwingi wa rehema, Rahim. Hii ni barua itokayo kwa Muhammad Mjumbe wa Allah kwenda kwa Negus Mfalme wa Ethiopia. Amani na iwe juu yako.

Ninamhimidi Allah ambaye hakuna mungu ghairi Yake. Yeye ndiye Allah aliyetakasika kutokana na kila aina ya upungufu na makosa; salama kutokana na ghadhabu Yake. Anaona na kuishuhudia hali ya waja wake.

“Ninashuhudia ya kwamba Nabii Isa Bin Maryam ni roho ya Allah na ‘neno’ (la Allah) lililokaa kwenye tumbo la uzazi la Maryam mchamungu, Allah alimuumba kwenye tumbo la uzazi la mama yake bila ya baba kwa Nguvu ile ile aliyomuumbia Adamu bila ya wazazi.

“Ninakuita kwa Allah Aliye Mmoja tu, Asiye na mshirika, na ninakutaka umtii na kuifuata dini yangu. Mwamini Allah aliyeniteuwa kuishika kazi ya utume. Mfalme wa Ethiopia, huna budi kutambua kwamba mimi ni Mtume wa Allah. Ninakuita wewe na askari zako kwa Allah, Mwenye nguvu zote, kwa kuileta barua hii na balozi wangu nitakuwa nimeshalitekeleza jukumu langu zito lililonikalia, na nimekushauri. Amani na iwe juu ya wale waufuatao mwongozo.”21

Mtume (s.a.w.w.) aliianza barua hii kwa ile salamu ya Kiislamu ya *Salaamu Alayk* na kutuma salaam zake binafsi kwa yule Mfalme wa Ethiopia. Hata hivyo, katika barua nyingine (zilizopelekwa kwa Kisra – Mtawala wa Iran, Kaisari–Mtawala wa Urumi na Maqauqis – mtawala wa Misri) anaanza na salaam ya ujumla (Amani naiwe juu ya wafuasi wa mwongozo). Katika barua hii alipeleka salamu za mtu binafsi kwa mtawala wa Ethiopia na hivyo akampa ubora juu ya wale watawala wengine wa ulimwenguni, katika zama zile.

Katika barua hii zimetajwa baadhi ya sifa kuu za Allah, Mwenye nguvu zote zionyeshazo Upweke na Ukuu wake. Baada ya hapo Mtume (s.a.w.w.) analizungumzia suala la ‘Uungu’ (Nabii Isa kuwa mungu), jambo ambalo ni uzushi wa fikara zilizooza za kanisa, na anaukanusha uzushi huu kwa hoja zinazotajwa kwenye Qur’ani. Ama kuhusu Nabii Isa kuzaliwa bila ya baba, analieleza tukio hili kwa kufanya ulinganisho na kuzaliwa kwa Adamu na akathibitisha kwamba kama kuzaliwa bila ya baba kutakuwa ni hoja ya mtu kuwa mwana wa Mungu, hoja hiyo hiyo haina budi kutumika kwa ajili ya Adamu, ambalo Wakristo hawana itikadi ya aina hiyo juu yake. Mwishoni mwa barua ile anatoa ushauri kumpa yeye (Negus) na kwa njia hiyo anakidhihirisha cheo chake mwenyewe.

Mazungumzo Baina Ya Yule Balozi Na Negus

Baada ya kwisha kwa taratibu zilizokuwa muhimu yule balozi wa Uislamu alipokewa kwenye baraza la kifalme la yule Mtawala wa Ethiopia. Alizungumza na mtawala yule hivi: “Ni wajibu wangu kuuwasilisha ujumbe wa Mtume (s.a.w.w.) kwako, na tabia zako zilizo safi nazo zahitaji kwamba uusikilize uwasilishaji wangu.

Ewe Mtawala mwadilifu wa Ethiopia! Huruma zako kwa wahajiri wa Kiislamu haziwezi kusahauliwa na hisia zako hizi zimetufurahisha mno kwamba tunakuhesabu kuwa u mmoja wetu. Nasi tunayo imani juu yako, kama kwamba sisi ni marafiki zako. Kitabu chako cha mbinguni ni ushahidi thabiti na usiokatalika. Kitabu hiki ni mwamuzi bora zaidi asiyefanya dhulma na huyu ni hakimu mwadilifu, anaushuhudia utume

wa Mtume wa Uislamu (s.a.w.w.). Kama ukimfuata huyu Mtume wa ulimwengu mzima na Mtume wa Mwisho wa Allah, utaipata baraka kubwa; au sivyo, utakuwa kama Wayahudi walioikataa dini ya Nabii Isa iliyoitangua dini ya Nabii Musa (a.s.) na wakaendelea kuifuata ile dini iliyotanguliwa. Na dini ya Uislamu inazitangua dini za awali kama vile dini ya Nabii Isa na kwa maana nyingine kwamba inazitimiza."

Yule Mtawala wa Ethiopia alimjibu yule balozi wa Mtume wa Uislamu (s.a.w.w.) kwa maneno haya: "Ninamshuhudia ya kwamba yeye ndiye yule Nabii angojewaye na watu wa Kitabu na ninaamini ya kwamba, kama vile Nabii Musa alivyowaarifu watu kuhusu utume wa Isa, Nabii Isa naye alizieleza dalili za Mtume wa Mwisho. Mimi niko tayari kuutangaza utume wake mbele ya hadhara. Hata hivyo, kwa kuwa bado mazingira hayajakuwa tayari kwa tangazo hili, na vilevile nguvu zangu hazitoshelezi, ni muhimu kwamba uwanja uhitajikao hauna budi kutayarishwa ili kwamba nyoyo za watu zitumiwe kwenye Uislamu.

Kama ingaliwezekana kwangu Mimi ningaliharakisha kumfikia huyo Mtume wenu mara moja."22 Kisha aliandika barua ya kumjulisha Mtume (s.a.w.w.).

Negus Amwandikia Barua Mtume (S.A.W.W)

"Kwa jina la Allah, Mwingi wa rehema, Rahimu. "Hii ni barua iendayo kwa Muhammad, Mtume wa Allah kutoka kwa Negus. Baraka ya yule Mmoja ambaye hakuna mungu ila Yeye tu na Salaam za yule mmoja Aliyeniongoza kwenye Uislamu ziwe juu yako. Nimeisoma barua yako ihusianayo na Utume na sifa za kibinadamu za nabii Isa (a.s.). Ninaapa kwa jina la Mola wa Mbingu na ardhi kwamba kila ulilolisema ni sawa kabisa nami sina tofauti kuhusiana na itikadi hii japo iliyo ndogo. Vilevile nimeutambua ukweli wa dini yako nami nimewapa wahajiri Waislamu huduma zifaazo. Kwa njia ya barua hii ninashuhudia ya kwamba wewe ni Mtume wa Allah na mtu mkweli ambaye utume wake umethibitishwa na Vitabu vya mbinguni. Nimekwisha kuzitekeleza ibada za Kiislamu na kula kiapo cha utii kwako mbele ya binamu yako (Ja'far bin Abu Twalib).

"Ninamtuma mwanangu R?rh? mbele ya hadhara yako tukufu ili aufikishe ujumbe wangu na kusilimu kwangu. Nami ninasema dhahiri kwamba mimi siwajibikiwi na yeyote ila mimi mwenyewe. Hivyo basi, kama ukiniamuru nitafika mbele yako. Amani na iwe juu yako, Ewe Mtume wa Allah."23

Barua Za Mtume (S.A.W.W) Kwa Watawala Wa Shamu Na Yamamah

Inawezekana kwamba kupanuka kwa matangazo ya Uislamu aliyoyafanya Mtume wa Uislamu (s.a.w.w.) kwa watawala mbalimbali kukafikiriwa na baadhi ya wanasiasa wa zama zile kuwa ni kitu kilicho kinyume na upole. Hata hivyo, jinsi muda upitavyo, imethibitika kwamba Mtume (s.a.w.w.) hakuwa na njia nyingine ya kufanya.

Kwanza, kule kuwapeleka wale mabalozi sita kwenye sehemu mbalimbali za ulimmwengu na pia wakiwa na barua thabiti na zenye kuvutia kuliifunga njia ya shaka kwa wapinzani wa siku zijazo. Baada ya Mtume (s.a.w.w.) kukitenda kitendo hiki kikuu, siku hizi hakuna yeyote awezaye kutia shaka juu ya mwito wake huu kuwa wa ulimwengu mzima. Aidha, ukiziachilia mbali zile aya zilizoshushwa juu ya jambo hili, kule kuwapeleka wale mabalozi ni uthibitisho mkubwa wa Uislamu kuwa dini ya ulimwengu mzima.

Pili, watawala wa zama zile ukimwachilia mbali Khusro Perviz aliyekuwa mtu mwenye kiburi na dhalimu, kwa ujumla walivutiwa na mwito ule na zile barua. Walionyesha kuwaheshimu wale wawakilishi wa Mtume (s.a.w.w.), na kule kutokea kwa Nabii wa Kiarabu kukawa jambo la kujadiliwa kwenye uwanja wa dini. Barua hizi ziliwaamsha wale waliokuwa wamelala, ziliwapa mshtuko mkali wale watu wasiosikiliza na kuzikoroga mno akili za mataifa yaliyostaarabika ili kwamba waweze tena kufanya mijadala na utafiti juu ya yule Nabii aliyeahidiwa wa Taurati na Injili, na wakuu wa dini wa wakati ule waweze kujua hii dini mpya kwa njia mbalimbali.
Kwa sababu hii, wengi wa viongozi wa dini mbalimbali za zama zile walikuja Madina, katika siku za mwishoni mwa uhai wa Mtume (s.a.w) na hata baada ya kufariki kwake dunia na wakajifunza dini hii kwa karibu zaidi.

Katika sura zilizotangulia tumeeleza kwa kirefu taswira zilizotolewa na zile barua za Mtume (s.a.w.w.) kwa watawala wa Urumi, Iran na Misri. Sasa tumeshayaona matokeo ya barua yake kwa Negus.

Baada ya mwakilishi wa Mtume wa Uislamu (s.a.w.w.) kumpa Negus zile zawadi ili awape wakuu wa dini wa Ethiopia, aliwapeleka makasisi thelathini wenye maarifa mengi mjini Madina ili waweze kujifunza maisha yaliyo rahisi na ya uchamungu ya Mtume (s.a.w.w.) kwa karibu zaidi, na ili wasije wakadhania kwamba yeye naye (s.a.w.w.) alikuwa na madaraka kama ya wafalme wa zama zile.

Wale watu waliotumwa na yule Mfalme wa Ethiopia walikutana na Mtume (s.a.w.w.) na wakamwuliza kuhusu itikadi yake juu ya Nabii Isa (a.s.).

Mtume (s.a.w.w.) aliwaeleza itikadi yake juu ya Nabii Isa (a.s.) kwa kuisoma Aya ifuatayo:

إِذْ قَالَ اللَّهُ يَا عِيسَى ابْنَ مَرْيَمَ اذْكُرْ نِعْمَتِي عَلَيْكَ وَعَلَىٰ وَالِدَتِكَ إِذْ أَيَّدتُّكَ بِرُوحِ الْقُدُسِ تُكَلِّمُ النَّاسَ فِي الْمَهْدِ وَكَهْلًا ۖ وَإِذْ عَلَّمْتُكَ الْكِتَابَ وَالْحِكْمَةَ وَالتَّوْرَاةَ وَالْإِنجِيلَ ۖ وَإِذْ تَخْلُقُ مِنَ الطِّينِ كَهَيْئَةِ الطَّيْرِ بِإِذْنِي فَتَنفُخُ فِيهَا فَتَكُونُ طَيْرًا بِإِذْنِي ۖ وَتُبْرِئُ الْأَكْمَهَ وَالْأَبْرَصَ بِإِذْنِي ۖ وَإِذْ تُخْرِجُ الْمَوْتَىٰ بِإِذْنِي ۖ وَإِذْ كَفَفْتُ بَنِي إِسْرَائِيلَ عَنكَ إِذْ جِئْتَهُمْ بِالْبَيِّنَاتِ فَقَالَ الَّذِينَ كَفَرُوا مِنْهُمْ إِنْ هَٰذَا إِلَّا سِحْرٌ مُّبِينٌ {110}

“Allah Atakaposema: Ewe Isa mwana wa Mariam! Kumbuka neema Yangu juu yako na juu ya mama yako, pale nilipokutia nguvu kwa Roho Takatifu, ukazungumza na watu katika utoto na utu uzima. Na nilivyokufunza kuandika na hekima na Taurati na Injili. Na ulipofinyanga udongo mfano wa umbo la ndege, kwa idhini Yangu, kisha ukapuliza ndani yake, mara akawa ndege kwa idhini Yangu, na ulipowaponyesha vipofu na wakoma kwa idhini Yangu, na ulipowafufua wafu kwa idhini Yangu na nilipokukinga na wana wa Israeli ulipowajia na hoja zilizo wazi, na wakasema waliokufuru miongoni mwao: Haya si lolote ila ni uchawi mtupu.” (***Surat al- Ma’ida, 5:110***).

Maneno ya Aya tuliyoinukuu hapo juu yaliwatia wasiwasi mno kiasi kwamba walianza kutiririkwa na machozi machoni mwao bila ya kupenda. Watu hawa walioteuliwa na Negus wakarejea Ethiopia baada ya kujifunza kwa makini ule mwito wa Mtume (s.a.w.w.) na kumweleza mfalme yale waliyoyaona na kuyasikia. Yeye naye alijawa na machozi machoni mwake kama wale makasisi.24

Ibn Athir ameisimulia hadith ya wale makasisi waliotumwa na Negus kwa jinsi nyingine. Anasema: “Makasisi wote hawa walikufa maji baharini na Mtume (s.a.w.w.) alimpelekea mfalme barua ya rambirambi.” Hata hivyo, maneno ya barua aliyoizungumzia haionyeshi hata kidogo kwamba Negus alipatwa na msiba wowote wa aina hiyo.25

Barua Ya Mtume (S.A.W.W) Kwa Mwana Wa Mfalme Wa Waghassaani

Waghassani walikuwa ni familia ya kabila la Qaht?ni liitwalo Azd lililokuwa likiishi nchini Yeman kwa muda mrefu, na mashamba yao yalikuwa yakinyweshewa na bwawa la Ma’rib. Bwawa hili lilipoharibiwa walilazimika kuitoka sehemu ile na kuja Shamu. Nguvu na ushawishi wao uliufunika ule wa wenyeji na hatimaye walianzisha Dola iliyoitwa Ghass?niyah. Walitawala kwenye eneo hili chini ya ufalme wa Wafalme wa Urumi, na Uislamu ulipouvunja utaratibu wao, watu thelathini na wawili kutoka miongoni mwao walikuwa wametawala katika sehemu za Golan, Yarmuk na Dameski.
Miongoni mwa wale mabalozi sita waliopelekwa kwenye nchi kubwa kuubalighisha ujumbe wa utume huu wa ulimwengu mzima, wa tano wao alikuwa ni Shujaa’ bin Wahab, aliyekwenda kwenye Dola ya Ghass?niyah kuipeleka barua ya Mtume (s.a.w.w.) kwa mfalme wao, aliyeitwa Harith bin Abi Shamir mjini Ba’uzah. Yule balozi alipoingia nchi ya Harith alitambua ya kwamba yule mtawala alikuwa akijishughulisha na matayarisho ya mapokezi ya Kaisari aliyekuwa akija kutoka Constantinople kwenda Yerusalem kwa miguuu ikiwa ni ishara ya shukrani kwa kupata ushindi dhidi ya adui yake, Iran.

Katika ile hali Shujaa’ bin Wahab ilimbidi asubiri kwa muda fulani kabla ya kupata muda wa kuweza kukutana na yule mtawala. Kupatikana kwa wakati ule kulimsaidia kujenga alijenga urafiki na H?jib (Mkuu wa maazimisho), naye akamwarifu juu ya sifa za Mtume (s.a.w.w.) na juu ya Uislamu. Maneno yenye kuvutia na kupenya moyoni yalileta mabadiliko yasiyo kifani katika fikara za yule H?jib kiasi kwamba alianza kutiririkwa na machozi machoni mwake na kusema: “Nimejifunza Injili kwa makini na humo nimezisoma sifa za Mtume nami basi natamka dhahiri kwamba mimi ninamwamini. Hata hivyo,

ninamwogopa Harith kwamba asije akaniuwa. Na Harith naye anamwogopa Kaisari na hata kama akiyaamini maneno yako, hataweza kuitangaza imani yake, kwa sababu yeye pamoja na jadi wa familia hii wamekuwa vibaraka wa Kaisari."

Shujaa' alipopata nafasi ya kufika barazani kwa mtawala alimwona akiwa ameketi kwenye kiti cha enzi na kuvaa taji. Akaitoa ile barua ya Mtume (s.a.w.w.). Barua ile iliandikwa hivi: "Kwa jina la Allah, Mwingi wa rehema, Rahimu. "Hii ni barua itokayo kwa Muhammad Mtume wa Allah kwenda kwa Harith bin Shamir. Amani na iwe juu ya wafuasi wa ukweli na viongozi wa waumini wa kweli. Ewe Harith! Ninakuitia kwa Allah Aliye Mmoja tu, Asiye na mshirika. Kama ukisilimu dola yako itaendelea kuwapo."

Maneno yaliyoko mwishoni mwa barua ile yaliyotishia kuangamia kwa ufalame wake kutokana na kushindwa kwake kuamini (Upweke wa Allah na utume wa Mtume s.a.w.w) yalimuudhi Harith naye akasema: "Hakuna awezaye kuniondolea mamlaka yangu. Ni lazima mimkamate huyu Mtume anayeamka." Kisha ili kumvutia yule balozi aliamrisha kwamba jeshi lifanye gwaride mbele yake ili kwamba yule balozi wa Mtume (s.a.w.w.) aweze kuiona nguvu yake ya kijeshi kwa karibu zadi.

Kwa njia ya kutoa huduma iliyozidi kiasi chake kwa serikali ya Kirumi yeye naye alimwandikia barua Kaisari na akimweleza uamuzi wake wa kutaka kumkamata Mtume wa Uislamu (s.a.w.w.). Kwa bahati, barua hii ilimfikia Kaisari wakati Dihyah Kalbi, yule balozi mwingine wa Mtume (s.a.w.w.) alipokuwa kwenye baraza la Kaisari na yule mtawala wa Kirumi alipokuwa akifikiria juu ya Uislamu. Yule Kaisari alikasirishwa na ile shauku kuu ya yule Mtawala wa Kighass?ni na akamjibu kwa kumwandikia hivi: "Achana na wazo lako hilo, na tuonane mjini Ailyaa."

Hata hivyo, kufuatana na methali isemayo: "Watu huifuata njia ya mtawala wao" jibu la Kaisari liliubadilisha msimamo wa Harith na hivyo akampa yule balozi wa Mtume (s.a.w.w.) joho la heshima, na kabla ya kuondoka na kurejea Madina alimwambia: "Nitolee salaam zangu kwa Mtume wa Uislamu na mwambie kwamba mimi ni mmoja wa wafuasi wake halisi." Hata hivyo, Mtume (s.a.w.w.) hakulipa muhimu wowote lile jibu lake la kidiplomasia, na akasema: "Hivi karibuni mamlaka yake yataporomoka." Harith alifariki dunia kwenye mwaka wa 8 Hijiriya yaani mwaka mmoja tu baada ya tukio hili.26

Balozi Wa Sita Wa Mtume (S.A.W.W) Aenda Yamamah

Yule balozi wa sita wa Mtume (s.a.w.w.) alikwenda Yamamah, nchi iliyokuwako baina ya Najd na Bahrain, na hatimaye kuifikisha barua yake kwa mtawala wa sehemu ile aliyeitwa Hamza bin Ali Hanaf. Maneno ya barua ya Mtume yalikuwa haya yafuatayo:
"Kwa jina la Allah. Amani na iwe juu ya wafuasi wa mwongozo. Huna budi kutambua kwamba dini yangu itaenda Mashariki na Magharibi hadi kwenye pembe ya mbali zaidi ya dunia. Silimu ili kwamba ubakie kuwa salama na mamlaka na ufalme wako viendelee kuwako."

Kwa vile yule mtawala wa Yamamah alikuwa Mkristo, balozi aliyeteuliwa kwa sehemu ile alikuwa ni mtu aliyepata kuishi nchini Ethiopia kwa muda mrefu naye alikuwa na ujuzi kamili juu ya hoja na ibada za

Ukristo. Mtu huyu alikuwa ni Salit bin ‘Amr ambaye alihajiri Ethiopia chini ya amri ya Mtume (s.a.w.w.) wakati Waislamu walipokuwa wakiteswa vikali na waabudu masanamu wa Makka.

Mafundisho matukufu ya Uislamu na mawasiliano yake na watu wa matabaka mbalimbali katika safari zake vimemfanya kuwa shujaa na mwenye nguvu mno kiasi kwamba alimvutia yule mtawala wa Yamamah kwa maneno yake na akamwambia: “Yu mwenye kuheshimiwa yule aliyebarikiwa imani na uchamungu. Watu walioko chini ya uongozi wako katu hawatashindwa. Ninakuita kwenye kitu kilicho bora zaidi na ninakuzuia kutokana na matendo yaliyo maovu zaidi. Ninakuitia kwenye kumuabudu Allah na ninakuzuia kutokana na kumtii shetani na kuyafuata majaribu na tamaa mbaya. Matokeo ya kumwabudu Allah ni kuipata Pepo na yale ya kumfuata shetani ni kutiwa kwenye Moto (wa Jahanamu). Kama ukitenda kinyume na nilivyosema, basi huna budi kusubiri hadi ukweli ukudhihirikie.”

Uso wa yule Mtawala wa Yamamah ulionyesha kwamba maneno ya yule balozi yamejenga mvuto mwema akilini mwake. Aliomba muda wa kuufikiria ule utume wa Mtume (s.a.w.w.). Kwa bahati njema mmoja wa Maaskofu wakuu wa Urumi alipata kufika nchi ya Yamamah katika wakati ule naye yule mtawala wa Yamamah akalipeleka suala lile mbele yake. Yule Askofu akasema: “Kwa nini umeacha kumtambua?” Akajibu: “Ninachelea ufalme wangu na mamlaka yangu.” Yule Askofu akasema: “Ni bora kwako kumfuata huyo ndiye yule Nabii wa Kiarabu ambaye kuja kwake kumetabiriwa na Kristo na imeandikwa kwenye Injili kwamba Muhammad yu Mtume wa Allah.”

Ushauri alioutoa yule Askofu ulimshawishi yule mtawala. Alimwita yule balozi aichukue barua itokayo kwake na ampelekee Mtume (s.a.w.w.). Barua ile ilisema hivi: “Umeniita kwenye dini iliyo bora zaidi.

Mimi ni mshairi mzungumzaji fasaha na msemaji wa jumuiya yangu, nami ninacho cheo miongoni mwa Waarabu chenye kutambuliwa na watu wote. Mimi niko tayari kuifuata dini yako, kwa sharti la kwamba unaniruhusu nipate fungu katika vyeo vya juu vya kidini.”

Hakutosheka na hilo tu bali vilevile alituma ujumbe wake kwenda mjini Madina ukiongozwa na mtu aliyeitwa Muj?’ah bin Murarah ili waweze kuufikisha ujumbe wake kwa Mtume (s.a.w.w.) na kumwambia kwamba iwapo cheo hiki cha kidini atakishika yeye baada ya kufariki dunia kwa Mtume (s.a.w.w.), yuko tayari kusilimu na kumsaidia, bali iwapo sivyo hivyo, atapigana vita. Wajumbe wa ujumbe huu walifika mbele ya Mtume (s.a.w.w.) na wakasilimu bila ya masharti. Ama kuhusu yule mtawala wa Yamamah, alijibu ujumbe wake kwa kusema hivi: “Kama imani yake ina masharti, haifai kwa utawala na kuirithi nafasi yangu, na Allah Atanilinda kutokana na madhara yake.”27

Barua Nyingine Za Mtume Wa Uislamu (S.A.W.W)

Barua alizoziandika Mtume (s.a.w.w.) akiwaita wana wa wafalme, wafalme, na wakuu wa dini kwenye Uislamu ni nyingi kuliko hizi tulizozitaj hapo juu. Hata katika siku zetu hizi wanachuoni watafiti wamenukuu vitabuni mwao barua ishirini na tisa za miito aliyoipeleka. Hata hivyo, kwa ajili ya kupunguza ukubwa wa kitabu hiki, tutatosheka na hizi tulizozitaja hapo juu.

1. Wanachuoni wakuu wa Uislamu wamezikusanya hizi barua za Mtume (s.a.w.w.) kwa kadiri walivyoweza. Vitabu viwili vifuatavyo ni vyenye thamani mno juu ya jambo hili:
Al–Wasaa'iqus Siyasah' cha Profesa Muhammad hamidullah Hyderabadi, Profesa wa chuo Kikuu cha Paris.
Makaatibur Rasul' cha mwanachuoni wa zama zilezile, Ali Ahmadi.
2. Tabaqaatul–Kubra, Juz. 1, uk. 258; Siiratu Halabi, Juz. 3, uk. 271.
3. Busra yalikuwa ni makao makuu ya Gavana wa jimbo la Haraam. Jimbo hili lilihesabiwa kuwa ni koloni la Kaisari na Harith bin Abi Shimar na watawala wa familia ya Waghassaani walilitawala jimbo hili wakiwa ni vibaraka wa Kaisari.
4. Tabaqaatul– Kubra, Juz. 1, uk. 259.
5. Kuna tofauti ya maoni baina ya wanachuoni kuhusu maana ya neno lihi 'Waarisiyani' Ibn Athiir anaandika kwenye kitabu chake 'Nihayah,' Juz. 1, uk. 31. 'Lina maana ya wafanyakazi wa baraza la mfalme'. Wengine wanasema kwamba lina maana ya wakulima, kwa sababu katika siku zile watu wengi walikuwa wakulima. Maoni haya yanaungwa mkono na ukweli uliopo kwamba kwenye baadhi ya nakala za barua (Tarikhul–Kamil, Jz. 2, uk. 145) neno 'Akaarin' limetu– mika badala ya neno hilo hapo juu, na 'Akar' lina maana ya mkulima. Vile vile inafikiriwa kwamba pengine 'Aris' lilikuwa jina la jumuiya iliyokuwa ikiishi kati– ka Dola ya Kirumi.
6. Tarikhut–Tabari, Juz. 2, uk. 290; Bihaarul–Anwwar, Juz. 20, uk. 378–380.
7. Tabaqaatul–Kubra, Juz. 1, uk. 259; Siiratu Halabi, Juz. 2, uk. 277; Tarikhul– Kamil, Juz. 2, uk. 44; Bihaarul Anwwar, Juz. 20, uk. 379.
8. Kufuatana na Ibn Sa'ad (Tabaqaatul– Kubra, Juz. 1, uk. 258) Mtume (s.a.w.w.) alimpeleka balozi huyu katika mwezi wa Muharam, Mwaka wa 7, Hijiriya.
9. Tabaqaatul–Kubra, Juz. 1, uk. 360; Tarikhut–Tabari, Juz. 2, uk. 295 na 296; Tarikhul–Kamil, Juz. 2, uk. 81 na Bihaarul Anwwar, Juz. 20, uk. 389.
10. Tarikhul–Kubra, Juz. 1, uk. 260.
11. Tarikhu Ya'qubi, Juz. 2, uk. 62.
12. Musnadi Ahmad, Juz. 1, uk. 96.
13. Siiratu Halabi, Jz. 3, uk. 278.
14. Tarikhul–Kamil, Juz. 2, uk. 106.
15. Tabaqaatul–Kubra, Juz. 1, uk. 260; Bihaarul–Anwwar, Juz. 20, uk. 382.
16. Siiratu Halabi, Juz. 3, uk. 280; Durrul–Mantur, Juz. 1, uk. 40 na A'ayaanis– Shi'ah, Juz. 1, uk. 142.
17. Usudul Ghaba, Jz. 1, uk. 362.
18. Siiratu Halabi, Juz. 3, uk. 28.
19. Siiratuz–Zayni Dehlaan, Juz. 3, uk. 73.
20. Tarikhut–Tabari, Juz. 2, uk. 294.
21. Siiratu Halabi, Juz. 3, uk. 279; Tabaqaatul–Kubra, Juz. 1, uk. 259.
22. Siiratu Halabi,
23. Tarikhut–Tabari, Juz. 1; Bihaarul Anwwar, Juz. 20, uk. 392.
24. A'alamal Waraa, uk. 31.
25. Usudul Ghaba, Juz. 2, uk. 62.
26. Siiratu Halabi, Juz. 3, uk. 286; Tabaqaati, Juz. 1, uk. 261.
27. Tarikhul– Kamil, Juz. 2, uk. 83; Tabaqaat Kubra, Juz. 1, uk. 262.

Sura Ya 43: Ngome Ya Khaybar: Kitovu Cha

Hatari

Kuanzia siku ile ambapo Uislamu ulianza kubalingiwa mjini Madina, Wayahudi walianza kuwa maadui dhidi ya Mtume (s.a.w.w.) na Waislamu hata zaidi ya Waquraishi, na wakaamka na makri na nguvu zao zote kuiangamiza dini hii.

Wayahudi waliokuwa wakiishi mjini Madina penyewe au viungani mwake walikutwa na balaa walilolistahili kutokana na matendo yao yenye madhara. Kikundi chao kimoja kilinyongwa, na wengineo kama vile kabila la Bani Qaynaqaa' na Bani Nuzayr walipelekwa uhamishoni kutoka mjini Madina, na wakaenda kuishi Khaybar na Wadud Qaraa'.

Wanda mpana na wenye rutuba ulioko Kaskazini mwa mji wa Madina yapata masafa ya kilomita 134 unaitwa Bonde la Khaybar, kabla ya kuanza kwa utume Wayahudi walijenga hapo ngome saba madhubuti kwa ajili ya upinzani na usalama wao. Kwa kuwa sehemu hii ilifaa sana kwa malengo ya kilimo, wakazi wake walikuwa na ujuzi kamili juu ya mambo yahusianayo na kilimo, kujikusanyia utajiri, kujikusanyia silaha na misingi ya ulinzi. Idadi ya wakazi wake ilizidi elfu ishirini na watu wengi walio mashujaa na wapenda vita waliweza kuonekana miongoni mwao.1

Kosa kubwa walilotenda Wayahudi wa Khaybar ilikuwa kwamba waliyachochea makabila yote ya Kiarabu kuivunja Dola ya Kiislamu, na kwa msaada wao wa kifedha jeshi la ushirikina lilikuja kutoka sehemu mbalimbali za Uarabuni hadi kwenye kuta za Madina. Matokeo ya kitendo hiki vita vya Ahz?b vikatokea (ambavyo maelezo yake kwa kirefu tuishayaeleza). Hatua alizozichukua Mtume (s.a.w.w.) na kujitolea mhanga kwa masahaba zake vilifanya lile jeshi la washambuliaji pamoja na Wayahudi wa Khaybar kurudi nyumbani kwao baada ya kukaa kwenye upande wa pili wa handaki lile kwa kipindi cha mwezi mzima, na hapo amani na utulivu vilirudishwa tena kwenye yale makao makuu ya Uislamu.

Mchezo mbaya uliochezwa na Wayahudi ambao hapo awali waliheshimiwa na Waislamu ulimfanya Mtume (s.a.w.w.) kuamua kukiharibu hiki kituo kikuu cha hatari na kuwanyang'anya silaha wote, kwa sababu halikuwa jambo lililowezekana kwamba watu hawa wakaidi na hatari waendelee kuwepo hapo Khaybar, kwani wangeweza tena kutumia fedha nyingi katika kuwachochea Waarabu waabudu masanamu kuasi dhidi ya Waislamu, na hadithi ya vita vya Ahzaab ingelirudiwa tena, kwa kuwa utovu wao wa uvumilivu katika mambo ya dini uliizidi mno ile huba ya Waquraishi juu ya ibada ya masanamu, na ni kwa sababu ya imani hii potofu kwamba wakati maelfu ya waabudu masanamu yakisilimu, hakuna hata Myahudi mmoja aliyeonyesha kuwako kwake tayari kuiacha dini yake.

Jambo jingine lililomfanya Mtume (s.a.w.w.) kuivunja nguvu ya Wayahudi wa Khaybar, kuwanyang'anya silaha, na kuwateua maafisa wake kuiangalia mienendo yao, ni kwamba alikuwa kaishawasiliana na wana wa wafalme, wafalme na watawala wa nchi mbalimbali za ulimwengu na amewalingania wote kwenye Uislamu kwa sauti thabiti, na katika hali hiyo halikuwa jambo lisilowezekana Wayahudi kuwa

silaha iliyo mkononi mwa Kisra na Kaisari na hatimaye wangaliweza kulipiza kisasi kwa Waislamu kwa msaada wa hawa wafalme wawili, na hivyo kuvunjilia mbali hili vuguvugu la kiroho la Kiislamu, au kuwachochea hawa wafalme wawili waasi dhidi ya Waislamu, kama vile walivyowachochea waabudu masanamu hapo awali, kwa kuwa katika siku zile Wayahudi walisimama pamoja na wafalme hawa, mmoja au mwingine katika vita baina ya Iran na Rumi, na hivyo Mtume (s.a.w.w.) aliona kwamba ni muhimu kuukomesha uovu huu tangu mwanzoni kabisa.

Huu ulikuwa ndio wakati ufaao zaidi wa kuchukua hatua hii, kwa sababu baada ya kuyafanya yale mapatano ya Hudaybiah, Mtume (s.a.w.w.) alikuwa salama kutokana na kila aina ya wasiwasi kutoka kwenye upande wa Kusini (wa Waquraishi) na akatambua kwamba kama akikikamata chama cha Wayahudi, hawatapata msaada wowote kutoka kwa Waquraishi. Ama kuhusu kuyazuia makabila mengine ya upande wa Kaskazini (kama vile familia ya Ghatf?n waliokuwa washirikina na marafiki wa watu wa Khaybar kwenye Vita vya Ahzaab) kutokana na kuwasaidia Wayahudi, alikuwa na mpango fulani akilini mwake ambao tutauzungumzia baadae.
Akisukumwa na mambo haya, Mtume (s.a.w.w.) aliwaamrisha Waislamu kuwa tayari kuviteka vile vituo vya mwisho vya Wayahudi Bara Arabuni. Aliongeza kusema kwamba ni watu wale tu waliokuwepo wakati wa kufanya mapatano ya Hudaybiyah ndio waruhusiwao kushiriki kwenye vita hivi. Ulikuwa ni mmojawapo wa nyakati za kuhuzunisha kwa Uislam. Kuhusu wale wengine (wasiokuwepo Hudaybiyah) wanaweza kushiriki kama askari wa kujitolea lakini hawapasiki na mgao wowote katika ngawira.

Mtume (s.a.w.w.) alimteua Ghayla Laythi kuwa mwakilishi wake mjini Madina. Mtume (s.a.w.w.) alimpa Sayyidna Ali (a.s.) bendera nyeupe mkononi mwake na akawaamrisha Waislamu waanze safari. Na ili msafara ule uweze kufika kule uendako upesi iwezekanavyo, alimruhusu kiongozi wa ngamia wake aliyeitwa ‘Aamri bin Akwa’ kusoma beti hizi za mashairi wakati wa kuwaswaga ngamia hao: “Ninaapa kwa jina la Allah! Kama Asingalitubariki tungelipotea, tusingeli– toa zaka wala tusingeliswali. Sisi ni taifa ambalo kama taifa (fulani) liki– tuonea au kutenda maovu dhidi yetu, hatungelilivumilia (taifa hilo). Ee Allah! Tujaalie uvumilivu na utuimarishe kwenye njia hii.”

Yanayonenwa kwenye beti hizi yalidhihirisha lengo na sababu za vita hivi. Hii ina maana ya kwamba, kwa vile wayahudi wametutesa na kutenda maovu kwenye kizingiti cha chini cha nyumba yetu, sisi tunaifanya safari hii kuikomesha hatari hii. Maneno ya beti hizi yalimridhisha mno Mtume (s.a.w.w.) kiasi kwamba alimwombea dua ‘Aamir. Ilitukia kwamba ‘Aamir alipata kifo cha ushahidi kwenye vita hivi.

Jeshi La Waislamu Laelekea Upande Usiojulikana

Mtume (s.a.w.w.) aliipenda mno mbinu ya kujificha2 katika kwenda kwa vikosi. Alitaka kwamba asiwepo mtu awezaye kuutambua mwelekeo wake ili awaingilie maadui kwa mshituko na kuyazingira makazi yao kabla ya wao kuweza kuzichukua hatua za lazima. Vilevile yalikuwa ni mawazo yake kwamba, kila mmoja wa wale maadui washirika afikirie kwamba yeye pekee ndiye lengo la Mtume (s.a.w.w.) na kwa njia hii basi, wajifiche majumbani mwao ikiwa ni hatua ya tahadhari na wasiungane.

Baadhi ya watu walifikiria kwamba pengine Mtume (s.a.w.w.) aliichukua safari ile kuelekea upande wa Kaskazini ili kuyakomesha makabila ya Ghatf?n na Fazarah waliokuwa washirika wa Wayahudi kwenye Vita vya Ahzaab.

Hata hivyo, baada ya kulifikia jangwa la Raji', aliyaelekeza majeshi upande wa Khaybar na hivyo akaukata ushirikiano baina ya hawa washirika wawili na akayazuia makabila haya yasiweze kuja kuwasaidia Wayahudi wa Khaybar. Matokeo yake yakawa kwamba, ingawa mazingira ya Khaybar yaliendelea kwa kipindi cha mwezi mzima, lakini makabila tuliyoyataja hapo juu hayakuweza kuwapa washirika wao msaada wowote.3

Yule kiongozi mkuu wa Uislamu aliendelea na safari yake akielekea Khaybar akifuatana na mashujaa 1600 waliokuwa na askari wapanda wanyama mia mbili.4 Walipofika karibu na ukanda wa Khaybar, Mtume (s.a.w.a) aliiomba dua ifuatayo iliyokuwa uthibitisho wa nia yake safi: "Ee Allah! Uliye Mola wa mbingu na kila kilichoko chini yake, na Mola wa ardhi na kila chenye kuutupia uzito wake humo!... Naomba kutoka Kwako wema wa makazi haya na wema wa wakazi wake na kila kilichomo humo na ninajikinga Kwako Wewe kutokana na uovu wake na kutokana na uovu wa makazi na kila kilichomo ndani yake."5

Dua hii iliyofanywa pia mbele ya wale mashujaa 1600 ni ushahidi wa kwamba Mtume (s.a.w.w.) hakuja kwenye nchi hii kwa ajili ya kuiteka, yaani kuitanua nchi yake au kulipiza kisasi. Kinyume na hivyo amekuja kukibomoa hiki kitovu cha hatari ambacho kingeliweza kuwa kituo kikuu cha waabudu masanamu, na lengo lake lilikuwa kwamba harakati za Uislamu zisitishwe kutoka mahali hapa. Na kama vile mheshimiwa mso- maji utakavyoona, Mtume (s.a.w.w.) baada ya kuiteka ngome hii na kuwanyang'anya silaha hawa Wayahudi, aliwarudishia mashamba yao na akatosheka na kuwapa ulinzi kamili na akawasamehe kulipa 'Jizyah' (ushuru).

Sehemu Muhimu Zachukuliwa Wakati Wa Usiku

Zile ngome za Khaybar zilikuwa na majina maalum; Na'im, Qamus, Katibah, Nastaat, Sahiq, Watih na Sulaalim. Miongoni mwa ngome hizi, wakati mwingine zilihusishwa na majina ya machifu wa ngome maalum. Kwa mfano, moja miongoni mwao iliitwa ngome ya Marhab. Ili kuzihami ngome hizi na kila mara kuweza kupata taarifa za hali ya mambo ya nje ya eneo lile, minara ya doria ilijengwa kwenye pembe za ngome zote, ili kwamba wale walinzi wawekwao kwenye minara ile waweze kutoa taarifa za mambo yatokeayo nje na kuwajulisha wakazi walio ndani ya ngome. Minara hiyo ilijengwa katika hali ambayo wakazi wake waliweza kulitawala barabara eneo lote la nje na waliweza kumpiga mawe adui kwa njia ya kombeo (teo), manati n.k.6

Idadi hii ya wakazi elfu ishirini inajumuisha watu mashujaa na wababe wa vita elfu mbili waliokuwa kwenye neema ya maji na akiba ya chakula. Ngome hizi zilikuwa madhubuti mno kiasi kwamba haikuwezekana hata kidogo kutoboa tundu ndani yake, na wale waliojaribu kuziendea walijeruhiwa au kuuawa kwa mawe waliyotupiwa kutoka kwenye ngome hizo. Ngome hizi zilihesabiwa kuwa ni ngome

madhubuti kwa ajili ya mashujaa wa Kiyahudi.

Ilikuwa lazima kwa hawa Waislamu waliokabiliwa na adui mwenye silaha za kutosha na mwenye nguvu, kutumia ustadi wa kivita wa hali ya juu zaidi na mbinu za kivita ili kuweza kuziteka ngome hizi. Jambo la kwanza kufanywa lilikuwa kwamba zile sehemu zote zilizokuwa muhimu na njia na malango yalikaliwa na askari wa Uislamu wakati wa usiku.

Kazi hii ilifanywa kwa siri mno na upesi mno kiasi kwamba hata wale walinzi waliokuwa kwenye ile minara ya doria hawakutambua. Ilipofika asubuhi wakulima wakiwa hawana walijualo kuhusu yaliyotokea usiku, walizotoka ngome zote za Khaybar wakiwa na zana za kilimo, macho yao yaliwaangukia askari mashujaa wa Uislamu ambao wakiwa na nguvu ya imani yao na ya mikono yao na silaha kali, waliwafungia kabisa njia zote, kiasi kwamba kama wangekuja hatua moja mbele wangelikamatwa.

Mandhari hii iliwaogofya mno kiasi kwamba mara moja walianza kukimbia na kusema: “Muhammad yuko hapa na askari wake.” Upesi upesi wakayafunga malango ya ngome zao kwa nguvu kabisa, na ndani ya ngome halmashauri zao za kivita zikakutana. Macho ya Mtume (s.a.w.w.) yalipoziangukia zana haribifu kama vile mabeleshi na sululu alizifikiria kuwa ni ndege njema na akayasema maneno yafuatayo ili kuziimarisha nyoyo za askari wa Uislamu: “Allah Yu Mkubwa! Na iangamie Khaybar. Tunapolishukia taifa, utakuwa ni wakati mbaya kiasi gani kwa wale walioonywa!”

Baada ya majadiliano baina yao Wayahudi waliamua kwamba wanawake na watoto wawekwe kwenye moja ya ngome zile na maghala ya vyakula yapelekwe kwenye ngome nyingine. Kisha wale mashujaa na wababe wa vita wa kila ngome wajihami wenyewe kutoka juu ya minara kwa kutumia mawe na mishale. Katika baadhi ya matukio maalumu wapiganaji wa kila ngome watoke nje ya ngome ile na wapigane na Waislamu. Wale mashujaa wa Kiyahudi hawakuuacha mpango huu hadi mwishoni mwa uadui ule na matokeo yake ni kwamba, waliweza kulizuia lile jeshi kubwa la Waislamu kwa kipindi cha mwezi mzima. Wakati mwingine ilichukuwa siku kumi kufanya juhudi za kuiteka ngome lakini lengo halikuweza kufikiwa.

Ngome Za Wayahudi Zaanguka

Sehemu iliyochaguliwa na maafisa wa Uislamu kuwa makao makuu ya jeshi katika jihadi hii ya Kiislamu haikuwa muhimu sana kwa upande wa kijeshi. Jeshi la kiyahudi lilitawala sehemu hii kikamilifu na hakikuweko kizuizi au pingamizi yoyote katika kulenga shabaha kwenye yale makao makuu ya jeshi la Waislamu. Kwa sababu hii, mmoja wa mashujaa stadi wa Uislamu aliyeitwa Hubab bin Munzir alikuja kwa Mtume (s.a.w.w.) na kusema: “Kama umepiga kambi kwenye sehemu hii kwa amri ya Allah Mwingi wa rehema, siwezi kukataa hata kidogo kwa kuwa amri ya Allah ni nje ya hoja na tahadhari zetu zote. Hata hivyo, iwapo ni jambo la kawaida ambalo maafisa wanaweza kutoa maoni yao, ninalazimika kusema kwamba sehemu hii iko mbele ya macho ya adui na mbele ya ngome ya Nataah, na kwa kuwa hakuna miti wala nyumba hapa, wapiga mishale wa ngome hii wanaweza kulenga shabaha kwenye hiki kituo cha jeshi kwa urahisi sana.”

Mtume (s.a.w.w.) akiwa yu mwenye kuyatenda mambo kwa mujibu wa moja ya kanuni muhimu mno za Uislamu (ambayo ni kanuni ya ushauriano na kuyaheshimu maoni ya wenzie), alisema hivi: “Kama ukiitaja sehemu iliyo bora zaidi ya hii nitaisogeza hapo kambi yangu.”

Baada ya kuichunguza ardhi ya Khaybar, sahaba mmoja aliyeitwa Kubab aliipendekeza sehemu iliyokuwa nyuma ya mitende, na hivyo askari na yale makao makuu ya jeshi yalihamishiwa pale. Baada ya hapo hadi ilipotekwa Khaybar, maafisa na Mtume wa Uislamu (s.a.w.w.) walikuja kwenye ngome zile kila siku kutoka mahali pale, na ulipoingia usiku wakarejea kwenye kambi yao.7

Hakuna maoni yenye kukata shauri yawezayo kuelezwa kuhusiana na maelezo kamili ya Vita vya Khaybar. Hata hivyo, kutoka kwenye vitabu vyote vya historia na vya maisha ya Mtume (s.a.w.w.) tunajifunza kwamba askari wa Uislamu walizizingira ngome zile moja baada ya nyingine na wakajitahidi kuyakata mawasiliano ya ngome iliyozingirwa, na wakaendelea kuizingira nyingine baada ya kuiteka ile ya awali.

Kutekwa kwa zile ngome zilizoungana moja baada ya nyingine kulicheleweshwa kwa njia za chini ya ardhi au ambazo mashujaa wao walifanya upinzani mgumu kuliahirishwa, ambapo zile ngome ambazo makamanda wao walitishiwa mno au ambazo uhusiano wao na ngome nyingine ulikatwa kabisa, zilitekwa kwa urahisi kabisa. Katika hali hiyo, umwagaji wa damu mdogo sana ulitendeka na mambo yalimalizwa kwa haraka.

Kufuatana na kauli ya baadhi ya wanahistoria, ngome ya kwanza ya Khaybar iliyosalimu amri kwenye majeshi ya Kiislamu baada ya juhudi kubwa na taabu ilikuwa ni ngome ya Na’im. Kutekwa kwa ngome hii iligharimu kufa kishahidi kwa Muhammad bin Maslamah Ansari mmoja wa makamanda wakuu wa Uislamu. Kwenye vita hivi askari hamsini wa Uislamu walijeruhiwa. Muhammad bin Maslamah alipigwa jiwe lililovurumishwa kutoka juu na akafariki dunia papo hapo. Hata hivyo, kufuatana na kauli ya Ibn Athir8 alifariki dunia baada ya siku tatu. Ama kuhusu wale askari hamsini waliojeruhiwa, walipelekwa kwenye sehemu fulani kwenye ile kambi iliyowekwa kwa ajili ya kufunga vidonda.9

Kikundi cha wanawake wa kabila la Bani Ghif?r walikuja pale Khaybar kwa idhini ya Mtume (s.a.w.w.) kuwasaidia Waislamu kuvifunga vidonda vyao na kuwapatia huduma zote nyingine ziruhusiwazo kwa wanawake kwenye kambi ya jeshi. Walizitoa huduma hizi kwa moyo mmoja na kwa uaminifu.10

Halmashauri iliamua kwamba baada ya kuiteka ngome ya Na’im, wale askari wa Uislamu waishambulie ngome ya Qamus. Chifu wa ngome hii alikwua Ibn Abil Haqiq.
Ikiwa ni matokeo ya kujitolea mhanga kwa wale askari wa Uislamu, ngome hii ilitekwa nayo, na Bibi Safiyah binti wa Hay bin Akhtab ambaye baadae alikuwa mkewe Mtume (s.a.w.w.) alikamatwa. Kutekwa kwa ngome hizi mbili kuliziimarisha nyoyo za askari wa Uislamu na fadhaa na woga vikawapata Wayahudi. Hata hivyo, Waislamu walikuwa kwenye mashaka makubwa mno kutokana na upungufu wa chakula, kiasi kwamba walilazimika kula nyama ya baadhi ya wanyama ambao nyama yao ilichukiza (ingawa haikua haramu). Ile ngome iliyokuwa na chakula kingi ilikuwa bado haijaingia mikononi mwa

Waislamu.

Uchamungu Mbele Ya Dhiki Hasa

Wakati mmoja Waislamu walipokabiliwa na njaa kubwa na wakawa wanaitosheleza njaa yao kwa kula nyama ya wanyama ambao nyama yao haikupendekezwa kwenye sheria ya vyakula, mchungaji mmoja aliyekuwa na uso mweusi na aliyekuwa akifanya kazi ya kuwachunga wanyama wa Wayahudi alikuja mbele ya Mtume (s.a.w.w.) na akaomba kwamba aelezwe ukweli juu ya Uislamu.

Baada ya kuyasikia maneno ya Mtume (s.a.w.w.) yenye kuvutia na yenye kupenya moyoni alisilimu mara moja na akasema: “Kondoo wote hawa wamewekwa dhamana kwangu na Myahudi. Niwafanye nini sasa wakati mawasiliano na wenyewe yamekatika?” Mtume (s.a.w.w.) alimweleza kwa maneno yaelewekayo, tena dhahiri mbele ya mamia ya askari wenye njaa kwamba: “Katika dini yangu, kuvunja ahadi ni moja ya dhambi zilizo kubwa zaidi. Ni muhimu kwamba uwapeleke kondoo wote hao kwenye lango la ngome.” Aliitekeleza amri ya Mtume (s.a.w.w.) na kisha yeye mwenyewe akarejea upesi na akashiriki kwenye vita ile na akafa kishahidi katika njia ya Uislamu.[11]

Hakuna shaka kwamba Mtume (s.a.w.w.) aliyejipatia cheo cha *al–Amin* (mwaninifu) kwenye zama za kabla ya Uislamu aliendelea kuwa mwaninifu na mkweli kwenye hali zote.

Upitaji wa makundi ya wanyama ulikuwa huru wakati wa asubuhi na vilevile wakati wa alasiri kwenye kipindi chote cha kuzingirwa na hakuna hata Mwislamu moja aliyefikiria kumchukua kondoo wa adui, kwa sababu Waislamu nao wamekuwa wanyoofu na waaminifu kutokana na mafundisho matukufu ya kiongozi wao.

Ni kwenye siku moja tu, wakati wote walipozidiwa nguvu kabisa na njaa, aliwaruhusu wakamate kondo wawili kutoka kwenye kundi moja na akawaacha wengine kwenye ngome yao. Hili pia lisingelitendeka kama wasingelilazimishwa na njaa kali kufanya hivyo. Hivyo basi, wale askari walipolalamika kuhusu njaa, Mtume (s.a.w.w.) aliinua mikono yake na akaomba, akisema: “Ee Mola! Wawezeshe askari hawa kuiteka ile ngome vilimohifadhiwa vyakula.” Hata hivyo, hakuwaruhusu kuitwaa mali ya watu mpaka pale ulipopatikana ushindi.[12]

Kwa habari zote hizi, utovu wa misingi wa kauli za baadhi ya mustashirik wa zama hizi wenye upendeleo hudhihirika, kwa sababu ili kuyatweza malengo matukufu ya Uislamu wanajitahidi kuthibitisha kwamba vita walivyopigana Waislamu vilishabahia kwenye utekaji na kukusanya ngawira, na utawala wa haki kwenye nyakati zile za kupigana vita hivi haukuzingatiwa na watu hawa.

Hata hivyo, tukio tulilolitaja hapo juu pamoja na matukio mengine ya aina hii yaliyowekwa kwenye kumbukumbu za historia huudhihirisha uwongo wa kauli hizi, kwa sababu Mtume (s.a.w.w.) hakuruhusu kwamba yule mchungaji aivunje ahadi yake na wale matajiri wake wa Kiyahudi, japo kwenye hali ngumu mno (kwa mfano pale askari wake wenye kujitoa mhanga walipokabiliwa na njaa na kifo), ingawa wakati

ule angeweza kuwanyakua kondoo wote wale.

Ngome Zatekwa, Moja Baada Ya Nyingine

Baada ya kutekwa kwa zile ngome tulizozitaja, yale majeshi yenye kuzingira yalizielekeza juhudi zao kwenye ngome za Watih na Sulaalim.[13]

Hata hivyo, yale mashambulizi ya Waislamu yalizuiwa kwa nguvu na wale Wayahudi kwa nje ya ngome, na mashujaa wa Uislamu hawakuweza kupata ushindi ingawa walikuwa nao ushupavu wa kijasiri. Idadi ya hasara walizozipata imeandikwa na mwandishi wa historia ya Uislamu Ibn Hisham chini ya orodha maalum. Walipigana na Wayahudi kwa muda wa siku kumi lakini kila siku walirejea kule kambini kwao bila ya kupata ushindi.

Katika moja ya siku hizi kumi, Bwana Abubakr aliteuliwa aende akalete ushindi. Alikuja hadi kwenye ukingo wa ile ngome akiwa amechukua ile bendera nyeupe na wale askari mashujaa wa Uislamu walikwenda chini ya amri yake. Hata hivyo, baada ya muda fulani walirudi bila kupata matokeo yoyote yale, na yule kamanda wa kile kikosi na wapiganaji wake aalimtupiana lawama kuhusika na kule kushindwa na kukimbia kutoka kwenye uwanja wa vita.

Katika siku iliyofuatiwa uamiri jeshi aliupewa Umar. Yeye naye alirudia ile hadithi ya rafiki yake, na kwa mujibu wa kauli ya Tabari,[14] aliwatishia masahaba wa Mtume (s.a.w.w.) kwa kumsifu chifu wa ngome ile aliyeitwa Marh kwa ushujaa na ujasiri wake usio kifani. Mtume (s.a.w.w.) na makamanda wa Uislamu waliudhishwa mno na jambo hili.[15] Wakati huo, Mtume (s.a.w.w.) aliwakusanya maafisa na mashujaa wa jeshi pamoja akazitamka sentensi zifuatazo zenye kuamsha ushujaa wa askari ambazo zimehifadhiwa kwenye historia:

“Kesho nitampa bendera hii yule mtu ampendaye sana Allah na Mtume Wake (s.a.w.w), na apendwaye sana na Allah na Mtume Wake, na Allah atatimiza kutekwa kwa ngome hii mikononi mwake. Yu mtu ambaye katu hajawahi kumgeuzia adui mgongo wake na haukimbii uwanja wa vita.”

Na kufuatana na ilivyonukuliwa na Tabrasi na Halabi alitumia maneno *‘Karraar Ghayr–i–Farraar’* yenye maana ya mtu amshambuliaye adui na asiyekimbia.[16] (yaani yu kinyume na wale makamanda wawili tuliwataja hapo awali)

Kauli hii, ambayo ni ushahidi wa ubora, na uwezo wa kiroho wa kamanda ambaye alikusudiwa kuwa mshindi, ilizaa hoihoi za furaha zilizoandamana na wasiwasi wa akili miongoni mwa askari na makamanda wa jeshi lile, na kila mmoja wao alikuwa akitamani[17] kwamba hii medali kuu ya kijeshi imwangukie yeye.

Giza la usiku lilienea kila mahali. Wale askari wa Uislamu wakaenda kulala na walinzi wa doria wakazishika nafasi zao kwenye sehemu za miinuko ili kuiangalia mienendo ya adui.
Hatimaye kulikucha. Wale makamanda wakamzunguka Mtume (s.a.w.w.). Wale makamanda wawili

walioshindwa pia nao walikuwapo pale wakizinyoosha shingo zao kwa kuwa wao nao walikuwa na shauku ya kutaka kujua upesi iwezekanavyo ni nani atakayepewa ile bendera tukufu.18

Ukimya wa watu waliokuwa wakisubiri kwa hamu na dukuduku ulivunjwa na maneno ya Mtume (s.a.w.w.): “Yuko wapi Ali?” Aliarifiwa kwamba alikuwa mgonjwa wa macho na alikuwa amepumzika pembeni hivi. Mtume (s.a.w.w.) akasema: “Mleteni hapa.” Tabari anasema: “Ali alipandishwa juu ya ngamia na alisaidiwa kushuka juu ya ngamia mbele ya hema la Mtume.” Sentensi hii inaonyesha kwamba maradhi ya macho yalikuwa makubwa kiasi kwamba yalimfanya kamanda asiweze kutembea. Mtume alinyoosha mkono wake mwenyewe kwenye macho yake na akamuombea. Kitendo hiki na dua hii ilikuwa na athari kama pumzi ya Nabii Isa, kwani baada ya hapo macho ya Ali kamanda mkuu wa Uislamu, hayakuwa na matatizo maishani mwake mote.

Mtume (s.a.w.w.) alimwamrisha Sayyidna Ali (a.s.) kwenda vitani. Kuhusiana na jambo hili alimkumbusha kwamba kabla ya kuanza kupigana awapeleke wawakilishi wake kwa wale machifu wa ile ngome na wawaite kwenye Uislamu. Hata hivyo, kama watakataa kusilimu, waarifu wajibu wao wawapo chini ya bendera ya Serikali ya Uislamu, yaani kwamba watalazimika kuzitoa silaha zao na kuishi maisha yaliyo huru kabisa chini ya ulinzi wa Uislamu kwa kulipa *Jizyah.*19 Hata hivyo kama watakataa kuikubali, hapo apigane nao.

Na sentensi ya mwisho aliyoitamka Mtume (s.a.w.w.) ikiwa ni mwongozo kwa Sayyidna Ali (a.s.) ilikuwa hii: “Kama Allah Mwenye nguvu zote Akimwongoza japo mtu mmoja tu kupitia kwako, ni bora kuliko kwamba wewe uwe na ngamia wenye manyoya mekundu na kuwatumia (ngami hao) katika njia ya Allah.”20 Hakuna shaka kwamba Mtume (s.a.w.w.) alifikiria kuwaonyesha wanadamu njia iliyonyooka hata katika nyakati za vita, na jambo hili laonyesha kwamba vita hivi vinapiganwa kwa ajili ya mwongozo wa watu.

Ushindi Mkuu Wa Khaybar

Wanahistoria na waandishi wa wasifu wa Uislamu wameandika kwa kirefu juu ya kutekwa kwa Khaybar, na mtu anapozisoma taarifa hizi hujifunza kiasi fulani ya habari. Hapa tunayataja yale yaliyoandikwa na waandishi wa wasifu wa Mtume (s.a.w.w.) kwa njia ya kuyasimulia matukio, na hapo baadaye tutayachunguza.

Maneno na kurasa za historia ya Uislamu ihusianayo na vita hivi yaonyesha kwamba, bila ya uhodari na kujitolea mhanga kwa Amirul- Mu’minin, isingeliwezekana kuziteka zile ngome za Wayahudi wa Khaybar. Ingawa baadhi ya waandishi wamezibadili habari fulani fulani na badala yake wameweka ngano fulani fulani, lakini bado idadi kubwa kidogo ya wanachuoni watafiti wamempa Sayyidna Ali (a.s.) sifa zipasikazo. Maelezo ya mukhtasari katika jambo hili la kihistoria kama zilivyokusanywa kutoka kwenye vitabu mbalimbali vya historia tunayatoa hapa chini:

“Ali alipoteuliwa na Mtume (s.a.w.w.) kuziteka ngome za Watih na Sulaalim, zile ngome mbili ambazo

wale makamanda wawili wa mwanzo walishindwa kuziteka na wakapigwa pigo lisilotengenezeka katika heshima ya jeshi la Uislamu kwa kuzionyesha jozi mbili za visigino zilizo safi (yaani kukimbia), alivaa deraya madhubuti na akaufunga upanga wake *Dhulfiqar* kwenye mkanda wake. Kisha akaenda kule kwenye ile ngome kwa shauku maalum imstahiliyo mpiganaji hodari awapo kwenye uwanja wa vita na akaenda akaikita ile bendera aliyopewa na Mtume (s.a.w) mahali fulani karibu na Khaybar. Wakati huo huo lile lango la Khaybar lilifunguliwa na mashujaa wa Kiyahudi wakatoka.

Kwanza kabisa Harith nduguye Marhab akaja mbele. Sauti yake yenye kuogofya, mbaya na yenye uvumi mkali iliogofya mno kiasi kwamba wale askari waliokuwa nyuma ya Ali, walisogea nyuma bila ya kupenda. Hata hivyo, Ali alisimama kwa uthabiti kwenye sehemu yake kama mlima. Mara tu baada ya hapo, Ali alimpiga dharuba Harith na akaanguka, mwili wake uliojeruhiwa ukawa umelala chini na akafa.

Kifo cha Harith kilimsikitisha mno Marhab. Akasogea mbele ili alipize kisasi cha kuuwawa kwa nduguye. Alikuja katika hali ambayo alijifunga silaha tangu miguuni hadi kwenye meno. Alivaa deraya ya Yaman mwilini mwake na alivaa kofia iliyotengenezwa kwa jiwe maalumu kichwani mwake ambayo kaifunika kwa kofia ya chuma. Kufuatana na desturi za wapiganaji wa Kiarabu wa zama zile, alizisoma beti za utenzi zifuatazo: “Milango na kuta za Khaybar zashuhudia kwamba mimi ni Marhab. Mimi ni mpiganaji mzoefu nami ninazo silaha za vita. Kama wakati ni wenye kushinda, mimi nami ni mshindi. Wapiganaji wanikabilio mimi kwenye uwanja wa vita huwapaka rangi ya damu zao”

Ali naye alisoma beti za utenzi ili kumjibu Marhab na akamweleza cheo chake yeye kama askari, na nguvu za mikono yake, na akasema: “Mimi ndiye yule mtu ambaye mama yake alimwita Haydar (Simba). Mimi ni mtu shujaa na Simba wa mapori (ya ushujaa). Nina mikono yenye nguvu na shingo yenye nguvu. (Nikiwa) kwenye uwanja wa vita huwapiga watu kwa hofu kama Simba.”

Tenzi za kujisifu toka kwenye pande zote mbili zilimalizika. Sauti za panga na mikuki ya mashujaa hawa wawili zilizovuma kama radi zilijenga hofu isiyo na kifani akilini mwa watazamaji. Mara kwa ghafla ule upanga mkali upigao dharuba wa yule shujaa wa Uislamu ulikipiga kichwa cha Marhab na kuichana ngao yake, ile kofia yake ya chuma, ile kofia ya jiwe na kich– wa chake hadi kwenye meno na hatimaye kukigawa pande mbili. Dharuba hii ilikuwa kali mno kiasi kwamba baadhi ya askari wa Kiyahudi waliokuwa wakisimama nyuma ya Marhab, walikimbia na kwenda kujificha kwenye ile ngome, na wengine waliobakia pale walipigana bega kwa bega dhidi ya Ali na wakauawa.

Ali akawafuatilia wale Wayahudi waliokimbia hadi kwenye lile lango la ngome. Katika juhudi hizi, mmoja wa askari wa Kiyahudi aliipiga ngao ya Ali kwa upanga wake nayo ikamponyoka ikaanguka chini. Upesi sana Ali akaigeukia ile ngome akalikwanyua lango lake na kulifanya ngao hadi mwishoni mwa vita vile. Na alipoitupa chini, askari kumi wa Uislamu wenye nguvu, ikiwa ni pamoja na Abu Raf’i walijaribu kuipindua chini juu, juu chini lakini walishindwa kufanya hivyo.21 Matokeo yake ni kwamba, ile ngome ambayo Waislamu walikuwa wakiisubiri kutekwa kwake kwa muda wa siku kumi, ilitekwa kwa muda mfupi. Yaa’qubi anasema:22”Lile lango la ngome ile lilitengenezwa kwa jiwe na lilikuwa na urefu wa dhiraa23 nne na upana wa dhiraa mbili.

Sheikh Mufid ameinukuu ile Hadith ya kulikwanyua lile lango la Khaybar kutoka kwa Amirul–Mu'minin, kutoka kwa watu maalum wenye kuamini– ka ya kwamba: "Nililing'oa lile lango la Khaybar na nikalifanya ngao. Baada ya kwisha mapambano yale nililiweka mithili ya daraja penye han– daki lililochimbwa na Wayahudi. Kisha nililitumbukiza ndani ya handaki." Mtu mmoja alimwuliza: "Je, ulilliona zito?" Ali alijibu: "Nililiona kuwa ni zito kama ile ngao yangu."24

Wanahistorisa wamenukuu mambo yenye kushangaza sana juu ya lile lango la ile ngome ya Khaybar na maajabu yake na ule ushujaa alioudhihirisha Sayyidna Ali (a.s.) katika kuiteka ngome ile. Ukweli ni kwamba ujasiri kama huu hauwezi kutendwa kwa nguvu ya binadamu wa kawaida. Hata hivyo, Sayyidna Ali (a.s.) amelieleza jambo hili yeye mwenyewe na hivyo basi ameziondoa shaka zote na dhana mbaya. Kwa sababu, akilijibu swali lililoulizwa na mtu mmoja, alisema: "Sikuling'oa lango lile kwa nguvu za kibinadamu. Nilifanya vile kwa nguvu niliyojaaliwa na Allah, na kutokana na imani yangu thabiti juu ya siku ya Hukumu."25

Kuugeuza Ukweli Wa Mambo

Haki inahitaji kwamba tusiwe na budi kukubali kwamba Ibn Hisham na Abu Ja'afar Tabari wametoa taarifa ndefu vya kutosha juu ya mapigano ya Sayyidna Ali (a.s.) pale Khaybar na wameeleza mambo hata yale yaliyo madogo mno juu ya tukio lile. Hata hivyo, mwishoni wameutaja uwezekano wa kimawazo tu juu ya Marhab kwamba aliuwawa mikononi mwa Muhammad bin Maslamah na wanasema: "Baadhi ya watu wanaamini kwamba Marhab aliuwawa mikononi mwa Muhammd bin Maslamah kwa sababu aliteuliwa kwa lengo lile na Mtume (s.a.w.w.) ili alipizie kisasi cha kuuwawa kwa nduguye kulikofanywa na Wayahudi wakati wa kutekwa kwa ngome ya Na'im na inawezekana kwamba alifaulu kulitimiza jukumu hili."

Uwezekano huo ni usiothibitishwa kabisa kiasi kwamba hauwezi kulinganishwa na yale maelezo sahihi na yenye kufululiza yasimuliwayo kwenye historia ya Uislamu. Aidha, matatizo fulani fulani hujitokeza kwenye ngano hii kama tutakavyoeleza hapa chini: Tabari na Ibn Hisham wameinukuu ngano hii kutoka kwa sahaba maarufu wa Mtume (s.a.w.w.) Jabir bin Abdullah, na msimuliaji wa hadith hii amelinukuu jambo hili geni kutoka kwa mtu huyu mkubwa, ambapo ukweli ni kwamba Jabir alipata heshima ya kufuatana na Mtume (s.a.w.w.) kwenye vita vyote, lakini hakuweza kushiriki kwenye vita hivi.

Muhammad bin Maslamah hakuwa shujaa vya kutosha kiasi kwamba aweze kuwa mtekaji wa Khaybar na hakupata kuonyesha uthibitisho wowote wa ushujaa maishani mwake. Kwenye mwaka wa pili wa Hijiriya aliteuliwa na Mtume (s.a.w.w.) kumwua Myahudi Ka'ab bin Ashraf, aliyekuwa akiwachochea waabudu masanamu waamke dhidi ya Uislamu baada ya vita vya Badr na kupigana tena na Waislamu.

Hata hivyo, aliogopa mno kiasi kwamba hakula wala kunywa kitu chochote kwa siku tatu mchana na usiku, na Mtume (s.a.w) akamlaumu kwa woga wake huu.

Akajibu, akisema: "Sijui kama nitafaulu katika jukumu hili au la." Mtume (s.a.w.w.) alipoona hali hii ya

mambo, aliwatuma watu wanne pamoja na yeye ili wakaumalizie mbali uasi wa Ka'ab bin Ashraf, aliyekuwa akijaribu kuufufua uadui baina ya waabudu masanamu na Waislamu. Wakaunga makri maalum kwa lengo hili na wakamwua yule adui wa Allah wakati wa usiku wa manane. Hata hivyo, kutokana na woga uliokithiri, na hofu, Muhammad alimjeruhi mmoja wa wale wenzie."26 Hakika mtu mwenye moyo wa aina hii, hangeliweza kumsukumizia nyuma yule shujaa wa Khaybar.

Yule Mtekaji wa Khaybar hakupambana na Marhab pekee na kumwua, bali baada ya kuuawa kwa Marhab, baadhi ya watu walikimbia na wengine waliingia uwanjani mmoja baada ya mwingine na kupambana naye katika mapambano ya wawili wawili. Wale mashuja wa Kiyahudi waliopigana na Sayyidna Ali (a.s.) baada ya Marhab na kuuawa ni hawa:

(i) Dawudi bin Qubus

(ii) Abil Haqia,

(iii) Abul Ba'ith

(iv) Marrah bin Marwaan

(v) Yasir Khaybari

(vi) Zajih Khaybari.

Watu sita hawa ndio waliokuwa mashujaa wa Wayahudi nje ya Khaybari nao walihesabiwa kuwa walikuwa kizuizi kikuu katika kuziteka zile ngome za Khaybar. Na wote hawa walipokuwa wakiziimba beti za tenzi na kumwita mpinzani ili aje kupigana, waliuawa mikononi mwa Amirul–Mu'minin (a.s.). Katika hali hii, hatuna budi kuamua ni nani awezaye kuwa mtekaji wa Khaybar.

Hii ni kwa sababu kama Muhammad bin Maslamah angelikuwa muuwaji wa Marhab asingelirejea kwenye ile kambi ya Waislamu baada ya kumuuwa Marhab na kuwaacha wale mashujaa waliokuwako mgongoni kwa Marhab, kwa sababu angelilazimika kupigana na watu wale pia, ambapo wanahistoria wote wanakubaliana kwamba watu hawa walipigana na Sayyidna Ali (a.s.) na waliuawa mikononi mwake.

Ngano hii ya historia ni kinyume na hadith zenye kurudiwa rudiwa zilizonukuliwa kutoka kwa Mtume (s.a.w.w.), kwa sababu alisema kuhusiana na Sayyidna Ali (a.s.) kwamba: "Nitampa bendera hii yule mtu ambaye mikononi mwake ushindi utakamilika," na katika siku iliyofuatia alimpa (yeye Sayyidna Ali – a.s) ile bendera ya ushindi. Na moja ya vizuizi vikuu katika kuupata ushindi kilikuwa ni Marhab wa Khaybar, ambaye uhodari wake umewafanya makamanda wawili wa Uislamu kuukimbia uwanja wa Vita. Sasa kama muuwaji wa Marhab angelikuwa Muhammad bin Maslamah ingelifaa tu kwamba Mtume (s.a.w.w.) angeliitamka juu yake sentensi tuliyoitaja hapo juu, na wala si juu ya saidina Ali (a.s.).

Mwanahistoria maarufu Halabi anasema: "Hakuna shaka juu ya ukweli uliopo kwamba Marhab aliuawa

mikononi mwa Ali."27 Ibn Athir anasema kwamba waandishi wa wasifu wa Mtume (s.a.w.w.) na wanahadithi wanamhesabu Sayyidna Ali (a.s.) kuwa ndiye muuwaji wa Marhab na masimulizi yenye kurudiwa rudiwa yamenukuliwa kuthibitisha ukweli huu.

Tabari na Ibn Hisham kwa kiasi fulani walisumbuliwa kimawazo na wakalitaja lile tukio la kushindwa na kurejea kwa wale makamanda wawili walioteuliwa kuiteka ngome ile kabla ya Sayyidna Ali (a.s.) kwa jinsi isiyoafikiana na maana ya ile sentensi aliyoitamka Mtume (s.a.w.w.) juu ya Sayyidna Ali (a.s.): "Yule asiyekimbia," yaani yu kamanda asiyekimbia, ambapo wale makamanda wawili wa awali, kwa hakika walikimbia na wamepaacha pale mahali pa vita. Hata hivyo, hawa waandishi wawili tuliowataja hapo juu hawakulitaja jambo hili nao wamelisimulia tukio hili kwa njia ambayo kana kwamba walilitekeleza jukumu lao kikamilifu. Lakini hawakufaulu katika kuiteka ngome ile.

Nukta Tatu Zenye Kung'ara Katika Maisha Ya Ali (A.S)

Sasa tunaimalizia maudhui hii hapa baada ya kutaja nemsi tatu za yule mtekaji wa Khaybar. Siku moja Muawiyah alimlaumu Sa'ad bin Waqqas kwa kutokumlaani Ali (a.s.), yeye alimjibu akisema: "Kila ninapozikumbuka nemsi tatu za Ali, ninatamani kwamba angalau ningekuwa na mojawapo ya hizo:

1. Siku moja Mtume (s.a.w.w.) alimteua kuwa mwakilishi wake mjini Madina na yeye mwenyewe akatoka na kwenda kwenye Vita vya Tabuk, alimwambia Ali: "Wewe kwangu unacho cheo kama kile alichokuwa nacho Harun kwa Musa ila tu kwamba hatakuwepo Mtume baada yangu."

2. Katika siku ya Khaybar Mtume alisema: "Kesho nitampa bendera yule mtu apendwaye na Allah na Mtume." Maafisa na makamanda wa Uislamu wakuu wote walikuwa na tamaa ya kuipata heshima ile. Hata hivyo, siku iliyofuatia Mtume alimwita Ali na akampa ile bendera na Allah akatujaalia ushindi ambao hasa ulitokana na kujitolea mhanga kwa Ali.

3. Ilipoamualiwa kwamba Mtume aingie kwenye Mubahilah (kulaaniana) na viongozi wa Najr?n, aliishika mikono ya Ali, Fatmah, Hassan na Hussein, na akasema: "Ee Allah! Hawa ndio watu wa Nyumba yangu."28

Mambo Yaliyoleta Ushindi

Malango ya ngome za Khaybar yalifunguliwa na Wayahudi wakasalimu amri mbele ya jeshi la Uislamu chini ya masharti maalum. Hata hivyo, hatuna budi kujua ni mambo gani yaliouleta ushindi huu, na bila shaka mambo haya yatakuwa ndiyo yaliyo makuu zaidi kwenye kisa hiki. Ushindi huu mkuu wa Waislamu ulikuwa ni matokeo ya mambo yafuatayo: Mipango na mbinu za Kijeshi.

Kujipatia taarifa na kuwa macho juu ya siri za adui. Ushujaa kamili na kujitoa mhanga kwa Sayyidna Ali, Amirul–Mu'minin (a.s.)

2. Mipango Na Mbinu Za Kijeshi

Jeshi la Uislamu lilipiga kambi mahali palipowawezesha kuyakata mawasiliano baina ya Wayahudi na marafiki zao (yale makabila ya Ghatf?n). Kwa ujumla ilikuweko idadi kubwa ya askari wapiganao kwa panga na watu wasiotishika kwenye familia za Ghatf?n, na kama wangelikuja kuwasaidia Wayahudi na wakapigana bega kwa bega pamoja nao basi kutekwa kwa ngome ya Khaybar kusingeliwezekana. Watu wa kabila la Ghatf?n walipopata taarifa juu ya jeshi la Waislamu kwenda Khaybar walikwenda upesi sana wakiwa na zana za kutosha ili wakawasaidie washirika wao.

Hata hivyo, walipokuwa njiani ziliwafikia fununu miongoni mwao kwamba wapiganaji wa Muhammad walikuwa wakija nchini mwao kwa kupitia njia isiyokuwa ile ya kawaida. Fununu hizi zilipata nguvu mno kiasi kwamba walirejea kwao walipokuwa katikati ya njia na hawakutoka tena nchini mwao mpaka ilipotekwa Khaybar na Waislamu.

Wanahistoria huihesabu fununu hii kuwa ni matokeo ya sauti ya siri. Hata hivyo, si jambo lisiliwezekana kwamba uvumi huu ulienezwa na Waislamu wa kabila la Ghatf?n, na waundaji wa uvumi huu walikuwa ni wale watu ambao kusema kweli walikuwa ni Waislamu nao walikuwa wakiishi miongoni mwa watu wa kabila lao katika vazi la makafiri na walikuwa wastadi mno katika kuibuni mbinu hii kiasi kwamba waliweza kufaulu kuyazuia majeshi ya Ghatf?n kwenda kuwasaidia washirika wao. Na kitendo hiki kilikuwa ni mfano wa vita vya Ahzaab, kwa sababu kwa matokeo ya upelezi wa Mwislamu mmoja wa kabila la Ghatf?n aliyeitwa Na'im bin Mas'ud, jeshi la makafiri lilitawanyika na akauzuia msaada wao kutoka kwa Wayahudi.

Kujipatia Taarifa

Mtume (s.a.w.w.) aliweka muhimu mkubwa sana katika kupata taarifa kuhusiana na vita. Hivyo basi, kabla ya kuizingira Khaybar alipeleka watu ishirini kwenye sehemu ile ili wawe watangulizi wakiwa chini ya uongozi wa 'Abbad bin Bashir. Watu hawa walikutana na mkazi mmoja wa Khaybar karibu na sehemu ile. Baada ya kuzungumza naye, 'Abbad alitambua kwamba alikuwa mmoja wa watu wenye taarifa kamili juu ya Wayahudi.

Hivyo akaamrisha akamatwe upesi sana na akampelekwa kwa Mtume (s.a.w.w.). Alipotishiwa kifo alizivujisha siri zote za Wayahudi. Kutokana naye ilifahamika kwamba Wayahudi wamekuwa na woga mno baada ya kupata taarifa kutoka kwa yule chifu wa wanafiki, (yaani Abdulah bin Sullul) na vile vile kwa kuwa bado hawajapata msaada kutoka kwa watu wa kabila la Ghatfan.

Katika usiku wa sita wa vita vile, kikosi cha doria cha Waislamu kilimkamata Myahudi na wakamleta mbele ya Mtume (s.a.w.w.) aliyemuuliza kuhusu hali na mambo ya Wayahudi. Alisema: "Nitakuambieni mradi tu nithibitishieni uhai wangu." Alipothibitishiwa alisema: "Usiku huu askari wa Khaybar watahama kutoka kwenye Ngome ya Nastaat kwenda kwenye Ngome ya Shiq ili wajihami kutoka pale.

Ewe Abul Qaasim! Kesho utaiteka ngome ya Nastaat.” Mtume akasema: “Kama Allah Akipenda.” Yule Myahudi akaendelea kusema: “Kwenye ngome hiyo utapata idadi kubwa ya teo, zana za kijeshi, deraya, na panga, vikiwa vimefichwa ardhini, na kwa silaha hizi utaweza kuipiga mawe ngome ya Shiq.”29

Yule kiongozi mkuu wa Uislamu hakuzitumia silaha hizi zenye uwezo wa kuleta uharibifu mkubwa, lakini zile taarifa zilizotolewa na yule mfungwa zilikuwa muhimu kwa kuwa zilieleza waziwazi kwamba ni ngome ipi ipasikayo kushambuliwa siku iliyofuatia, na ilifahamika kwamba kutekwa kwa Ngome ya Nastaat hakungalihitaji nguvu kubwa na kwamba tahadhari ilihitajika ili kuiteka ngome ya Shiq.

Baada ya kucheleweshwa kwa kutekwa kwa moja ya ngome zile kwa muda wa siku tatu Myahudi mmoja alimjia Mtume (s.a.w.w.), pengine kwa lengo la kutaka kuyaokoa maisha yake, na kusema: “Japo ukae mahali hapa kwa muda wa mwezi mzima hutaweza kuwazidi nguvu. Hata hivyo, ninaweza kukuonyesha chanzo cha maji cha ngome hii na kama ukipenda unaweza kuwakatia maji.”

Mtume (s.a.w.w.) hakuikubali rai hii, na akasema: “Hatumkatii maji mtu yeyote ili asije akafa kwa kiu.” Hata hivyo, ili kuweza kuzidhoofisha nyoyo za maadui aliamrisha kwamba upatikanaji wa maji kwa ajili yao uzuiwe kwa muda. Jambo hili liliwaogofya mno kiasi kwamba mara tu baada ya mapigano madogo walisalimu amri kwenye jeshi la Uislamu.30

3. Kujitoa Mhanga Kwa Ali (A.S)

Tumetaja kwa kifupi hapo awali kujitoa mhanga kwa Ali (a.s.) na sasa tunayanakili maneno yake mwenyewe: “Tulisimama upande wa pili wa jeshi kubwa na ngome imara za Wayahudi. Mashuja wao walitoka nje ya ngome zile na kuwaita wapinzani ili waje kupambana nao na kila siku waliua baadhi ya watu. Wakati huo Mtume (s.a.w.w.) aliniamrisha nisimame na niende kwenye ile ngome. Niliwakabili wapiganaji wao na kuwaua baadhi yao na kuwarudisha nyuma wengine. Walikimbilia kwenye ngome ile na kujificha, kisha wakalifunga lango lake. Nililing’oa lile lango kisha nikaingia ile ngome peke yangu. Hakuna aliyeweza kunipinga na kwenye jambo hili, hakuna yeyote aliyenisaidia ila Allah.”31

Hisia Za Huruma Mwenye Uwanja Wa Vita

Ilipotekwa ngome ya Qamus Bibi Safiah binti Hay bin Akhtab na mwanamke mwingine walitekwa. Bilal aliwapitisha hawa wanawake wawili karibu na maiti za Wayahudi waliouawa kwenye vita vile na akawaleta mbele ya Mtume (s.a.w.w.). Mtume (s.a.w.w.) alipopata taarifa za jambo lile aliamka akaliweka joho lake kichwani kwa Bibi Safiyah na akamtendea mambo yaonyeshayo heshima kwake na akampa mahali maalum pa kupumzikia kule kambini.

Kisha akamwambia Bilal kwa ukali: “Je, umepotewa na hisia za huruma kabisa kiasi kwamba umethubutu kuwapitisha hawa wanawake karibu na maiti za watu wao wapendwa?” Mtume (s.a.w.w.) hakutosheka na hilo tu bali alimchagua Bibi Safiyah kuwa mkewe na kumtendea hivyo akamfidia kwa kuvunjika kwake moyo.

Kutendewa wema alikotendewa Bibi huyu na Mtume (s.a.w.w.) na hisia zake Mtume (s.a.w.w.) za huruma zilikuwa na athari njema mno kwa Bibi huyu kiasi kwamba baadaye alihesabiwa kwamba alikuwa moja wa wakeze wapenzi zaidi na waaminifu, naye alilia zaidi ya watu wengine pale Mtume (s.a.w.w.) alipokaribia kufariki dunia.32

Kananah Bin Rabi' Auwawa

Tangu pale Wayahudi wa kabila la Bani Nuzayr walipofukuzwa kutoka Madina na wakaenda kuishi Khaybar walianzisha kisanduku cha watu wote kwa ajili ya mambo ya ustawi wa jamii na gharama za vita na kwa ajili ya kulipa dia kwa ajili ya wale waliouawa mikononi kwa Bani Nuzayr. Taarifa alizozipata Mtume (s.a.w.w.) zilionyesha kwamba pesa hizi zilikuwa zikitawaliwa na Kananah, mumewe Bibi Safiyah. Mtume (s.a.w.w.) alimwita Kananah na akamwuliza kuhusu kisanduku kile.

Hata hivyo, yeye alikataa kuwa na taarifa juu ya kitu kile. Hivyo, Mtume (s.a.w.w.) akatoa amri ya kwamba Kananah abakie mpaka pale zitakapopatikana taarifa zaidi juu ya kisanduku kile. Wale walioteuliwa kuzitafuta fedha zile waliendelea kufanya uchunguzi. Hatimaye mtu mmoja akasema: "Ninadhani hazina hii itakuwa imefichwa mahali pale (kwenye gofu), kwa sababu nimemwona Kananah akiitembelea sehemu ile mara kwa mara wakati ule wa vita na baada ya hapo." Mtume (s.a.w.w.) akamwita tena Kananah na akamwambia: "Inasemekana kwamba kile kisanduku kiko mahali pale (Akapataja). Kama hazina ile ikipatikana hapo utauawa." Kananah akakana tena kwamba hana taarifa yoyote juu ya jambo lile. Mtume akaamrisha sehemu ile ichimbuliwe na ile hazina ya Bani Nuzayr ikaangukia mikononi mwa askari wa Uislamu.

Sasa ikawa muhimu kumwadhibu Kananah kwa vitendo vyake. Ukiachilia mbali kuficha taarifa juu ya jambo hili (yaani kule kuelewa ilipokuwa ile hazina) vile vile Kananah alimuua afisa mmoja wa Uislamu kwa jinsi ya kiwoga (yaani alimtupia jiwe kubwa kwa ghafla kichwani mwa Mahmud bin Maslamah, aliyefariki dunia palepale). Ili kulipiza kisasi na vilevile kuwaadhibu Wayahudi ili kwamba wasije tena wakafanya hadaa na uwongo kwa serikali ya Uislamu hapo baadaye, Mtume (s.a.w.w.) alimkabidhi yule Kananah kwa ndugu wa yule afisa wa Kiislamu, na nduguye marehemu akamuua. Kananah alikuwa mtu wa mwisho kuuawa kwa kumuua afisa maafuru wa Uislamu.

Nyara Za Vita Zagawanywa

Baada ya kuziteka ngome za adui na kuwanyang'anya Wayahudi silaha na kukusanya nyara, Mtume (s.a.w.w.) aliamrisha ya kwamba nyara zote ziletwe mbele yake katika sehemu fulani maalum. Kama ilivyoamrishwa na Mtume (s.a.w.w.) mtu mmoja alitangaza miongoni mwa askari wa Uislamu: "Ni wajibu juu ya kila Mwislamu kurudisha kwenye hazina ya Umma kila nyara aliyonayo japo iwe ni uzi na sindano, kwa sababu kuvunja uaminifu ni jambo la aibu na itakuwa moto kwa upande wa roho yake katika Siku ya Hukumu."

Wale viongozi halisi wa Uislamu wamekuwa wakali mno katika mambo ya amana kiasi kwamba

wamekuhesabu kurudisha amana kuwa ni moja ya ishara ya imani, na kuvunja ahadi kuwa ni moja ya dalili za unafiki.33

Hivyo basi pale mali iliyoibiwa ilipopatikana kwenye mali zilizoachwa na askari mmoja aliyefariki dunia, Mtume (s.a.w.w.) hakumsalia askari yule sala ya maiti. Maelezo marefu ya tukio hili yako kama ifuatavyo: “Siku ya kuondoka pale Khaybar, mshale wa ghafla ulimpiga mtumwa mmoja aliyekuwa akifunga kitundu anachokalia Mtume (s.a.w.w.) juu ya mgongo wa ngamia anaposafiri, na mtumwa yule akafa palepale.

Waliteuliwa watu wa kulichunguza jambo lile. Watu wale waliifanya kazi ile lakini hawakupata jibu. Watu wote wakasema: “Na abarikiwe kupata Pepo.” Hata hivyo, Mtume (s.a.w.w.) akasema: “Mimi siafikiani nanyi juu ya jambo hili, kwa kuwa joho lililoko mwilini mwake ni sehemu ya hizi nyara za vita naye alivunja uaminifu, na litamzunguka likiwa katika hali ya moto katika Siku ya Hukumu.” Wakati ule ule mmoja wa masahaba wa Mtume (s.a.w.w.) akasema: “Nimechukua jozi moja ya vigwe vya viatu kutoka kwenye nyara bila ya ruhusa.”
Mtume (s.a.w.w.) akasema: “Virudishwe au sivyo vitafungwa miguuni mwako katika Siku ya Hukumu vikiwa katika umbo la moto!”34

Ni mahali hapa ambapo malengo ya siri ya mustashirik wenye upendeleo hudhihirika, kwa sababu, wanazisimulia vita za Uislamu kuwa ni utekaji nyara, lakini huyafumbia macho yale malengo ya kiroho, kwa kuwa aina hii ya nidhamu haiwezi kuelezeka kutoka kwenye kundi lenye kuteka nyara. Haiwezekani kwa kiongozi wa jumuia ya wateka nyara kuufanya uaminifu kuwa ni dalili ya imani imara na kuwafundisha askari wake katika hali ambayo aweze kuwazuia kuchukua japo ugwe wa kiatu kutoka kwenye mali ya umma.

Msafara Utokao Ethiopia; Nchi Ya Kumbukumbu

Kabla ya kwenda Khaybar, Mtume (s.a.w.w.) alimtuma ‘Amr bin Umayyah kwenye baraza la Negus. Lengo la kumpeleka mjumbe wake kwenye lile baraza kule Ethiopia lilikuwa kwamba aufikishe ujumbe wa Mtume (s.a.w.w.) kwa yule Mfalme wa Ethiopia na kumwomba awapatie masurufu ya safari ya Waislamu wote ili watoke Ethiopia na kurudi nyumbani. Yule Negus aliwatayarishia jahazi mbili. Zile jahazi za Muhajiriin zilitia nanga kwenye pwani ya Madina. Waislamu wakapata habari kwamba Mtume (s.a.w.w.) amekwenda Khaybar hivyo nao wakaja Khaybar bila ya kuchelewa. Wale wasafiri watokao Ethiopia walifika Khaybar wakati zile ngome zilipokuwa tayari zimeshatekwa.

Mtume (s.a.w.w.) akaenda mbele hatua kumi na sita kumlaki Ja’far bin Abu Twalib, akalibusu paji la uso wake na akasema: “Sijui ni kipi nikifurahie zaidi kukutana nawe tena baada ya kuachana kwa miaka mingi au kwa Allah kutufungulia ngome za Wayahudi kupitia kwenye mikono ya kaka yako Ali?” Kisha akaongezea kusema: “Leo ninataka kukupa zawadi” Watu wakafikiria kwamba zawadi ile itakuwa zawadi ya kimaada ya kawaida kama vile dhahabu au fedha.

Mara kwa ghafla Mtume (s.a.w.w.) akakivunja kimya kilichotanda pale na akafundisha dua ambayo hapo baadae ilifahamika kwa jina la '*Dua ya Ja'far Tayyaar*.'35

Idadi Ya Waliouwawa

Waliouawa kwa upande wa Waislamu katika vita hivi hawakuzidi watu ishirini. Waliouwawa katika upande wa Wayahudi walikuwa ni watu tisini na watatu kufuatana na ilivyoandikwa kwenye vitabu vya historia.36

Msamaha Wakati Wa Ushindi

Wakati watu wakubwa na wachamungu wanaposhinda huonyesha huba na huruma kwa wale maadui zao waliowashinda na wasio na msaada. Mara tu baada ya adui kusalimu amri wao huonyesha huruma na huepuka kumlipizia kisasi na kutokuwa na mfundo dhidi yake.

Baada ya kutekwa kwa Khaybar yule kiongozi mkuu wa Waislamu alionyesha hisia za huruma kwa watu wa sehemu ile (bila kujali ukweli wa kwamba walikitumia kiasi kikubwa cha fedha katika kuwachochea Waarabu waabudu masanamu kupigana dhidi yake na kuuweka mji wa Madina kwenye mashambulizi na uwezekano wa kuanguka), na akakubali matakwa yao kwamba wangeliweza kubakia Khaybar na wakaendelea kuyamiliki mashamba na miti ya eneo lile kwa masharti ya kwamba watalipa nusu ya mazao kwa Waislamu.37
Si hilo tu, bali kufuatana na nukuu ya Ibn Hisham mwenyewe,38 Mtume (s.a.w.w.) aliitoa rai hii mwenyewe na kwa rai hii akawapa Wayahudi uhuru wa kuendelea na kilimo, kupanda na kukuza miti.

Mtume (s.a.w.w.) angeliweza kuwakata vichwa wote au kuwatoa pale Khaybar au kuwalazimisha kusilimu. Hata hivyo, kinyume na fikira za mustashirik wenye upendeleo walio watumishi na askari wa kinadharia ya ukoloni, ambao hudhania kwamba Uislamu ulienezwa kwa ncha ya upanga, yeye Mtume (s.a.w.w.) hakutenda mambo ya aina hii bali aliwapa hifadhi na akawaruhusu kuifuata misingi, kanuni, taratibu na ibada za dini yao.

Kama Mtume (s.a.w.w.) alipigana vita dhidi ya Wayahudi wa Khaybar, hii ilitokana na ukweli uliopo kwamba Khaybar na wakazi wake ilikuwa kitovu cha hatari kwa Uislamu na daima ilishirikiana na waabudu masanamu ili kuipindua ile serikali mpya ya Waislamu.

Hivyo basi, Mtume (s.a.w.w.) alilazimika kupigana nao na kuwanyang'anya silaha ili kwamba waweze kujishughulisha na kilimo kwa uhuru kabisa na kuweza kuzitekeleza ibada zao chini ya utawala wa serikali ya Kiislamu. Au la, maisha yangalikuwa magumu mno kwa Waislamu na kuenea kwa Uislamu kungelisimama.

Kama alitwaa Jizyah kutoka kwao, ni kwa sababu ya kwamba walipatiwa ulinzi chini ya serikali ya Kiislamu na ilikuwa wajibu juu ya Waislamu kuuhami uhai na mali zao. Na kufuatana na kasma

iliyokasimiwa kwa makini, kodi iliyo wajibu kwa Mwislamu iliizidi Jizyah ambayo Wayahudi na Wakristo walitakiwa kulipa. Waislamu waliwajibika kulipa Zaka na Khumsi, na katika nyakati nyingine vilevile walitakiwa kulipa malipo kutokana na mali zao ili kutimiza mahitaji ya serikali.

Kwa kulinganishwa na hilo, Wayahudi na Wakristo ambao waliishi chini ya bendera ya Uislamu na wakazifaidi haki za pamoja na za mtu binafsi, iliwabidi walipe kwa njia ya Jazyah kama walivyofanya Waislamu kwa usalama wa bendera hii.

Utozaji wa Jizyah ya Kiislamu ni jambo lililo tofauti na kutoa ushuru. Mwakilishi wa Mtume (s.a.w.w.) aliyekuwa akiteuliwa kila mwaka kukasimia na kugawa (katika nusu mbili) mazao ya Khaybar, alikuwa mtu mchamungu na mwadilifu, aliyepata kupendwa na Wayahudi kwa kutopendelea kwake na uadilifu wake. Mtu huyu alikuwa ni Abdullah Rawaha, ambaye baadaye aliuwawa katika Vita vya Muta. Alikuwa akiyakasmia mafungu ya Waislamu kutokana na mazao ya Khaybar na wakati mwingine Wayahudi walifikiria kwamba alikuwa akikosea katika kukasimia, na akawa anatia alama ya kujulisha kwenye (lile fungu la Waislamu) zaidi (ya vile ipasikavyo kuwa). Alikuwa kila mara akisema: “Niko tayari kukirudisha kwenu kile kiasi kilichokasimiwa, na kile kilichobakia kiwe ndio mali ya Waislamu.”

Wayahudi waliusifu uadilifu wake kwa kusema: “Mbingu na nchi hutulia chini ya kivuli cha usawa na uadilifu wa aina hii.”39

Zile nyara za vita zilipokusanywa kipande cha Taurat kiliangukia mikononi mwa Waislamu. Wayahudi wakamwomba Mtume (s.a.w.w.) kwamba warudishiwe kipande kile. Mtume (s.a.w.w.) alimwelekeza yule mtu aliyekuwa akiingoza hazina ya umma kuirudisha ile sehemu ya Taurati kwa Wayahudi.

Tabia Ya Ukaidi Ya Wayahudi

Bila kujali upole huu wa hali ya juu, Wayahudi hawakuuacha ukaidi na makri zao. Waliweka mitego kwa ajili ya kumvamia Mtume (s.a.w.w.) na masahaba zake na wakapanga makri dhidi yao. Hapa tunanukuu mifano miwili ya uvunjaji wao wa ahadi:

1. Watu fulani walimchochea mwanamke mmoja aliyeitwa Zaynab, aliyekuwa mke wa mmoja wa watu watukufu miongoni mwa Wayahudi, kukitia sumu chakula cha Mtume (s.a.w.w.). Yule mwanamke akamtuma mtu aende kwa mmoja wa masahaba wa Mtume (s.a.w.w.) na kumwuliza ni sehemu gani ya nyama ya kondoo aipendayo sana? Mtume (s.a.w.w.) akamjibu kwamba chakula chake akipendacho sana ni mkono wa kondoo. Zaynab akambanika yule kondoo na nyama yote akaitia sumu, Kisha akaipeleka kwa Mtume (s.a.w.w.) ikiwa ni zawadi. Mtume (s.a.w.w.) alipoweka kinywani finyango ya kwanza alihisi kwamba ilitiwa sumu. Hivyo upesi sana akaitema.

Hata hivyo, Bishr bin Baraa’ Ma’rur, aliyekuwa akila nyama ile na Mtume (s.a.w.w.) alikula finyango nyingine zaidi. Bila ya kujua akafariki dunia baada ya muda fulani. Mtume (s.a.w.w.) aliamrisha kwamba aitwe Zaynab mbele yake. Alitoa sababu za kitoto na kusema: “Umeichafua hali ya kabila letu. Nilifikiria

kwamba kama wewe ni mtawala utakufa kwa sumu ile na kama u mtume wa Allah kweli, bila shaka utaitambua na utaacha kuila nyama ile.” Mtume (s.a.w.w.) alimsamehe vile vile hakuwatolea madai wale watu waliomchochea Zaynab kulitenda kosa lile.

Hata hivyo, kama kitu cha aina hii kingalitokea kwa mtawala mwingine asiyekuwa Mtume, angaliwaua bila ya huruma wale wakosefu au angaliwahukumu vifungo virefu.40

Kutokana na malengo haya maovu ya yule mwanamke wa Kiyahudi wengi wa masahaba wa Mtume (s.a.w.w.) nao hawakumwamini yule mwanamke wa Kiyahudi Bibi Swafiyah ambaye sasa amekuwa mkewe (s.a.w.w.), na wakafikiria ya kwamba inawezekana kwamba atajaribu kuudhuru uhai wake wakati wa usiku.

Hivyo, Abu Ayub Ansari alichukua jukumu la kulilinda hema la Mtume (s.a.w.w.) kule Khaybar pamoja na siku ya kurejea Madina, ingawa Mtume (s.a.w.w.) hakutambua ya kwamba masahaba wanamhurumia. Hivyo, Mtume (s.a.w.w.) alipotoka mle hemani asubuhi alimwona Abu Ayub akilizunguka zunguka huku akiwa ameufuta upanga mkononi mwake. Mtume (s.a.w.w.) alipouliza sababu ya kufanya vile ndipo alipomjibu: “Dalili za ushupavu wa kidini na ukafiri bado hazijafutika kutoka moyoni mwa mwanamke huyu (Swafiyah) ambaye hivi sasa yu mmoja wa wakezo, nami nina imani ndogo katika nia yake. Hivyo nilikuwa nikilizunguka zunguka hema lako tangu usiku hadi asubuhi ili kulinda uhai wako.” Mtume (s.a.w.w.) alimshukuru kwa zile hisia za huruma za huyu rafiki wake wa tangu kale na akamwombea dua.41

2. Safari moja Abdullah bin Sahl aliteuliwa na Mtume (s.a.w.w.) kuyasafirisha mapato ya Khaybar kutoka pale na kuyapeleka Madina. Alipokuwa akiifanya kazi hii alishambuliwa na kikundi cha Wayahudi ambacho hakikutambulika. Matokeo ya shambulizi hili ni kwamba shingo yake ilijeruhiwa vibaya sana. Alianguka chini na akafariki dunia. Kile kikundi cha washambuliaji kikaitupa maiti yake kwenye bwawa.

Wazee wa Kiyahudi waliwatuma watu kwa Mtume (s.a.w.w.) ili kumpasha habari za kifo kile kisichoeleweka cha wakala wake, wasichojua kimesababishwa na nani. Ndugu wa yule aliyeuwawa aliyeitwa Abdur Rahman bin Sahl alimjia Mtume (s.a.w.w.) pamoja na binamu yake na kumwarifu juu ya tukio lile. Yule ndugu wa yule marehemu alitaka kufanya mazungumzo juu ya jambo lile, lakini kwa vile alikuwa ndiye mdogo zaidi miongoni mwa wale waliokuwapo, Mtume (s.a.w.w.) aliidokeza moja ya desturi za kijamii za Uislamu na akasema: *“Kabir, Kabir”* Yaani aache watu wakubwa wazungumze kwanza.

“Kama mnaweza kumuainisha muuwaji wa Abdullah na mkaapa kwamba yeye ndiye muuwaji, mimi nitamkamata na kumweka mikononi mwenu.” Hata hivyo wao walionyesha uchamungu na unyoofu na ingawa walishikwa na ghadhabu lakini hawakuuficha ukweli na wakasema:
“Hatuwezi kumtambua yule muuwaji.” Hapo Mtume (s.a.w.w.) akasema: “Je, mnakubali kwamba Wayahudi waeleze kwa kiapo kwamba wao hawakumuuwa na kwa msingi wa kiapo hicho waachiwe huru kutokana na kifo cha Abdullah?” Hata hivyo, walijibu kwamba mapatano na viapo vya Wayahudi

haviwezi kuaminika. Katika mazingira haya Mtume (s.a.w.w.) aliamrisha iandikwe barua kwenda kwa wazee wa Wayahudi ikiwaambia kwamba maiti ya Mwislamu imepatikana kwenye eneo lao na hivyo basi wao hawana budi kulipa dia kutokana na sababu hii.

Katika jibu lao, Wayahudi waliapa kwamba katu wao hawakumuuwa Abdullah na vile vile kwamba hawamtambui yule muuwaji. Mtume (s.a.w.w.) alitambua ya kwamba jambo lile limeifikia hatua ya kukwama. Hivyo basi, ili kuzuia kurudia umwagaji damu, yeye mwenyewe alilipa dia kwa ajili ya Abdullah.42 Kwa kitendo hiki aliwaonyesha tena Wayahudi kwamba hakuwa mpenda vita na kama angelikuwa mtawala wa kawaida angelifanya tukio la Abdullah kama shati la Uthman na kuuwa idadi fulani ya Wayahudi.

Hata hivyo, kama vile Qur'ani imwitavyo, yeye alikuwa ni Mtume wa rahma na mdhihiriko wa huruma ya Allah, naye hakuuchomoa upanga wake mpaka pale alazimikapo kufanya hivyo.

Wayahudi Watolewa Khaybar

Kukithiri kwa Wayahudi hakukukomea kwenye matukio haya tu bali vilevile waliendelea kuwasumbua Waislamu kila mara kwa makri zao mbalimbali.

Mwishowe kwenye zama za Ukhalifa wa Umar mwanawe Abdullah aliyekwenda Khaybar akifuatana na watu wengine, ili kwenda kufanya mapatano, aliteswa na Wayahudi. Khalifa alipata taarifa za tukio lile na akawaza jinsi ya kulitatua tatizo lile. Hivyo, akiitegemea hadith moja ya Mtume (s.a.w.w.) iliyonukuliwa na baadhi ya watu, aliwaambia masahaba wa Mtume (s.a.w.w.): "Yeyote yule ambaye anataka kulipwa deni lake kutoka kwa watu wa Khaybar basi na afanye hivyo, kwani nitatoa amri ya kwamba watoke sehemu ile."

Mara tu baada ya hapo Wayahudi wa Khaybar walipigwa marufuku kukaa pale kutokana na kukithiri kwa matendo yao maovu waliyokuwa wakiyatenda mara kwa mara, nao wakaitoka Rasi ya Uarabuni.43

Uongo Uliothibitishwa Na Nia Yake

Mfanyabiashara mmoja aliyeitwa Hajjaj bin Il?t alikuwako pale Khaybar. Alikuwa kafanya biashara na watu wa Makka. Utukufu wa Uislamu na mapenzi na huruma alizozionyesha Mtume (s.a.w.w.) kwa taifa lake kaidi (yaani Wayahudi) viliuangaza moyo wake na akamjia Mtume (s.a.w.w.) na akasilimu. Kisha akapanga mpango ili kulipwa deni lake kutoka kwa watu wa Makka. Aliuingia mji wa Makka kupitia kwenye lango moja na akaona kwamba machifu wa Waquraishi walikuwa wakisubiri taarifa na walikuwa na shauku kuu juu ya matokeo ya Khaybar.

Wote wakamzunguka ngamia wake na wakaulizia hata bila ya subira kuhusu hali ya Muhammad, aliwajibu akisema: "Muhammad ameshindwa vibaya sana na masahaba zake wameuwawa au kutekwa. Yeye mwenyewe (Mtume) ametekwa na machifu wa Wayahudi na wameamua kumleta Makka na

kumnyonga mbele ya macho ya Waquraishi.” Taarifa hii ya uwongo iliwaridhisha sana sana.

Kisha alirejea kwa watu na kusema: “Kutokana na taarifa hii njema, ninakuombeni mnilipe deni langu mapema iwezekanavyo ili kwamba niende Khaybar mapema kuliko wafanyabiashara wengine ili niweze kununua watumwa.” Wale watu waliodanganyika wakamlipa deni lake katika muda mfupi sana.

Kuenea kwa taarifa ile kulimkera sana Abbas ami yake Mtume (s.a.w.w.) na akataka kukutana na Hajjaj. Hata hivyo, alimpiga ukope Abbas, kwa maana ya kwamba atamweleza hali halisi baadae. Muda mfupi kabla ya Hajjaj kutoka, alikutana na huyu ami yake Mtume (s.a.w.w.) kwa siri na akasema: “Nimesilimu na mimi nilipanga mpango huu ili niweze kulipwa madeni yangu tu. Taarifa zilizo sahihi ni kwamba siku niliyotoka Khaybar ngome zote zilikuwa zimeshatekwa na Waislamu na binti wa kiongozi wao aliyeitwa Hay bin Akhtab (Swafiyah) amekamatwa na amekuwa mkewe Mtume. Tafadhali ufanye ukweli huu ufahamiwe na watu baada ya siku tatu za kuondoka kwangu hapa.”

Baada ya siku tatu Abbas alivaa nguo zake nzuri zaidi, akajipaka manukato ya bei ghali zaidi na akauingia msikiti akiwa ameshika fimbo mkononi mwake na akaanza kufanya Tawaaf ya Kaabah. Waquraishi walishangazwa kuliona vazi la Abbas lililoonyesha shangwe na furaha kwa kuwa walifikiria kwamba kutokana na msiba uliomwangukia mwana wa kaka yake angalivaa nguo ya msiba. Hata hivyo, aliwaondolea ule mshangao wao kwa kusema: “Ile taarifa aliyokupeni Hajjaj ilikuwa ni ujanja wa kupata kulipwa madeni yake. Yeye amesilimu na ametoka Khaybar wakati Muhammad akiwa tayari kaishapata ushindi mkubwa, na Wayahudi wameshanyang’anywa silaha, na baadhi yao wameuwawa na wengine wamefanywa mateka.” Machifu wa Waquraishi wakasikitika sana walipoisikia taarifa hii na mara tu baada ya hapo walizipata taarifa zile zile (kutoka kwa watu wengine vilevile).44

---

1. Siiratu Halabi, Juz 3, uk. 36; Tarikhu Yaa’qubi, Juz. 2, uk. 46.
2. Wakati mwingine inasemekana kwamba, ingawa Mtume (s.a.w.w.) aliitumia mbinu hii ya kujificha kwa ukamilifu wake, yule chifu wa Wanafiki (Abdullah Sallul) aliwaarifu Wayahudi wa Khaybar juu ya mpango ule na akawashauri kwamba, zaidi ya kujihami kutoka juu ya ngome zao zile, vile vile wapigane na Waislamu nje ya ngome zao.
3. Siiratu Ibn Hisham, Juz. 2, uk. 330.
4. Amaalit–Tusi, uk. 164.
5. Tarikhul Kamil, Juz. 2, uk. 147.
6. Siraatu Halabi, uk. 38.
7. Siiratu Halabi, Juz. 3, uk. 39.
8. Usudul Ghabah, Juz. 4, uk. 334.
9. Siiratu Halabi, Juz. 3, uk. 40.
10. Siiratu Ibn Hishamu, Juz. 3, uk. 342.
11. Siiratu Ibn Hishamu, Juz. 3, uk. 344.
12. Siiratu Ibn Hishamu, Juz. 2, uk. 335.
13. Badhi ya wanahistoria wanaamini kwamba ngome hizi zilichukuliwa kwa amani kwa njia ya mapatano na tukio linalosimuliwa hivi sasa, linahusiana na ngome ya Qamus au Nastat.
14. Tarikhut–Tabari, Juz. 2, uk. 300.
15. Majma’ul Bayaan, Juz. 9, uk. 120 Siiratu Halabi, Juz. 2, uk. 43.
16. Hadithi ya kukimbia kwa wale makamanda wawili ilimhuzunisha sana Ibn Abil Hadid, mwanahistoria mkuu wa Uislamu.

Anasema mwenye Qaswida yake maarufu: “Japo nisahau kila kitu, siwezi kuisahau hadithi ya hawa makamanda wawili, kwa sababu walimwendea adui kwa panga mikononi mwao, lakini walimgeuzia adui migongo yao na wakakimbia, ingawa walijua kwamba ni haramu kuikimbia Jihadi. Waliichukua ile bendera kuu ya Uislamu na kuipeleka kwa adui yule, ingawa, kwa kweli fungu lao lilikuwa fedheha na uduni. Mtu mwepesi kutoka miongoni mwa dhuria wa Nabii Musa aliwarudisha nyuma. Yeye alikuwa yu mtu mrefu aliyekuwa akimrekebu farasi mwenye mbio.

17. Sayidna Ali (a.s.) aliopoyasikia haya maneno ya Mtume (s.a.w.w.) mle hemani, alisema kwa tamaa yenye nguvu zaidi akilini mwake: “Ee Mola! Kama ukimpa mtu hakuna wa kumnyima; na kama ukimnyima mtu yeyote hakuna wa kumpa.” (Siiratu Halabi, Juz. 3, uk. 41)
18. Maneno yaliyotumiwa kwenye Tarikhut–Tabari kwa jambo hili ni Fa tataawala Abu Bakr wa Umar.
19. Bihaarul Anwwaar, Juz. 21, uk. 28.
20. Sahih Muslim, Juz. 5, uk. 195; Sahih Bukhari, Juz. 5, uk. 22–23.
21. Tarikhut–Tabari, Juz. 2, uk. 94.
22. Tarikhu Yaaqubi, Juz. 2, uk. 46.
23. Dhiraa moja ni kama sentimita 37 hivi.
24. Al–Irshaad, uk. 59.
25. Bihaarul Anwwar, Juz.21, uk. 21.
26. Siiratu Ibn Hisham, Juz.2, uk. 65.
27. Siiratu Halabi, Juz. 3, uk. 44.
28. Sahih Muslim, juz. 7, uk. 120.
29. Siiratu Halabi, Juz. 3, uk. 41.
30. Siiratu Halabi, Juz. 3, uk. 47.
31. Khisaal, Juz. 2, uk. 16.
32. Tarikhut–Tabari, Juz. 3, uk. 302.
33. Wasaa’ilus– Shi’ah, Sura ya Jihad bin–Nafs, Hadith ya 4.
34. Siiratu Ibn Hisham, Juz. 3, uk. 339.
35. Khisaal, Juz. 2, uk. 86; Furuul Kafi, juz. 1, uk. 129.
36. Bihaarul Anwaar, Juz. 21, uk. 32.
37. Siiratu Ibn Hisham, Juz. 1, uk. 327.
38. Siiratu Ibn Hisham, Juz. 1, uk. 356
39. Siiratu Ibn Hisham, Juz. 2, uk. 354; Furu’i Kaafi, Juz. 1, uk. 405.
40. Inafahamika vema kwamba kwenye ugonjwa wa Mtume (s.a.w.w.) uliomal– izikia kwenye kifo chake, alisema: “Maradhi haya wametokana na athari za chakula kilichotiwa sumu ambacho yule mwanamke wa kiyahudi alinileta baada ya kutekwa kwa Khaybar” Ingawa Mtume (s.a.w.w.) aliitema finyango ya kwan– za, ile sumu ya hatari ilichanganyika mno na mate yake kiasi kwamba iliidhuru afya yake.
41. Siiratu Ibn Hisham, Juz. 2, uk. 339–340; Bihaarul Anwwar, Juz. 21, uk. 6.
42. Siiratu Ibn Hisham, Juz. 2, uk. 356.
43. Siiratu Ibn Hisham, Juz. 3, uk. 356.
44. Bihaarul An’war, Juzuu 21, uk. 34.

Sura Ya 44: Hadith Ya Fadak

Nchi iliyoendelea na yenye rutuba ambayo ilikuwa karibu na Khaybar na umbali wa kilometa 140 kutoka Madina na iliyokuwa ikifikiriwa kuwa ngome yenye nguvu ya Wayahudi wa Hijaz, baada ya zile ngome

za Khaybar, ilikuwa ikiitwa kijiji cha Fadak. Baada ya kuivunja nguvu ya Wayahudi wa Khaybar, Wadi'ul Qurra' na Taym?', na kuzijaza sehemu hizo kwa majeshi ya Uislamu, pengo pekee lililoachwa kwenye upande wa Kaskazini wa Madina lilikuwa ni Fadak.

Sasa Mtume (s.a.w.w.) aliona kwamba aivunje nguvu ya Wayahudi wa eneo la Fadak waliokuwa wakifikiriwa kwamba ni hatari kwa Uislamu na Waislamu. Hivyo akampeleka balozi aliyeitwa Muhit kwa wazee wa Fadak. Yush'a bin Nun aliyekuwa chifu wa kijiji kile aliipendelea amani na kusalimu amri kuliko kupigana, na hatimaye wakazi wa sehemu ile walikubali kumpelekea Mtume (s.a.w.w.) mapato ya kila mwaka na kuishi chini ya ulinzi wa Uislamu na kutofanya makri dhidi ya Waislamu. Serikali ya Uislamu kwa upande wake, ilithibitisha usalama wa eneo lao.

Kwa mujibu wa Uislamu zile sehemu zitekwazo kwa njia ya vita na nguvu za kijeshi ni mali ya Waislamu wote na utawala wake unakuwa mikononi mwa mtawala wa Kiislamu. Hata hivyo, nchi ziangukiazo mikononi mwa Waislamu bila ya kuzitumia nguvu za kijeshi huwa mali ya Mtume (s.a.w.w.) na baada ya kuondoka kwake huwa mali ya Imam (a.s.). Yeye (Mtume s.a.w au Imamu a.s) huwa na mamlaka kamili juu ya nchi hizi na anao uwezo wa kuzitoa zawadi au kuzikodisha. Na moja ya sababu zimfanyazo aweze kuzitumia mali hizi ni kwamba, aweze kuzikabili gharama za halali za jamaa zake kutokana na mali hii kwa njia ya heshima.1

Chini ya msingi huu, Mtume (s.a.w.w.) aliitoa zawadi Fadak kwa binti yake mpenzi, Bibi Fatimah Zahrah (a.s.). Kama vile ambavyo hali ya baadae itakavyoonyesha. Mtume (s.a.w.w.) alikuwa akifikiria mambo mawili pale alipoitoa mali yake hii kuwa zawadi:

1. Kama vile ambavyo mara kwa mara Mtume (s.a.w.w.) alikuwa akieleza, utawala wa Waislamu baada ya kufariki dunia kwa Mtume (s.a.w) ulikuwa ushikwe na Sayyidna Ali Amirul–Mu'minin (a.s.), na kukishika cheo hiki kunamfanya alazimike kuzikabili gharama kubwa. Hivyo basi, Sayyidna Ali (a.s.) angaliweza kuyatumia mapato ya Fadak kwa kadiri iwezekanavyo katika kukihami cheo chake. Inaweza kuonekana kwamba wale walioshika madaraka ya Ukhalifa walizitambua hatua hizi za tahadhari na hivyo basi wakawanyang'anya watu wa Nyumba ya Mtume (s.a.w.w.) ile Fadak katika siku za awali kabisa za kuyatwaa mamlaka.

2. Lilikuwa ni jambo muhimu kwamba baada ya kifo cha Mtume (s.a.w.w.) familia yake iliyokuwa na binti yake mpenzi Fatimah Zahrah (a.s.) na wanawe Hasan (a.s.) na Husain (a.s.), ingeliweza kuishi maisha ya heshima na heshima ya Mtume (s.a.w.w.) ikasalimika. Mtume (s.a.w.w.) aliitoa zawadi Fadak kwa binti yake ili kulifikia lengo hili. Wanahadithi na wafasiri wa Qur'ani wa Kishia na baadhi ya wanachuoni wa Sunni wanasema hivi:

"Ilipoteremshwa aya isemayo: **"Na mpe aliye jamaa yako haki yake, na masikini na msafiri wala usitumie ovyo kwa fujo" (Sura Israa, 17:26),** Mtume (s.aw.w) alimwita binti yake Fatimah na akampa Fadak."2 Na msimuliaji wa tukio hili ni Abu Saidi Khudri aliyekuwa mmoja wa masahaba zake Mtume (s.a.w.w.) walio maruufu sana.

Wafasiri wote wa Qur'ani wa Kishia na Kisunni wanakubaliana kwamba aya hii iliteremshwa kwa ajili ya jamaa wa karibu zaidi wa Mtume (s.a.w.w.) na maneno 'aliye jamaa' yanamhusu zaidi binti yake. Zaidi sana kiasi kwamba mtu mmoja aliye mwenyeji wa Shamu alimtaka Imam wetu wa Nne, Imamu Sajjad (a.s.) ajitambulishe mwenyewe. Imamu (a.s.) alisoma aya tuliyoitaja hapo juu ili kujitambulisha kwa mtu yule. Na ukweli huu ulifahamika vizuri mno kwa Waislamu kiasi kwamba yule mtu wa Shamu alipokuwa akikitikisa kichwa chake katika hali ya kukubali alimwambia Imamu: "Kwa uhusiano maalum ulionao kwa Mtume (s.a.w.w.), aliamrishwa na Allah kukupeni haki yenu."3

Kifupi ni kwamba wanachuoni wote wa Kiislamu wanaamini kwamba aya hii iliteremshwa kwa heshima ya Bibi Fatimah Zahraa (a.s.) na wanawe. Hata hivyo, swali ni je, wakati wa kuteremshwa kwa aya hii, Mtume (s.a.w.w.) aliitoa Fadak na kumpa binti yake? Wanachuoni wote wa Kishia wanakubaliana kwamba kwa kweli alifanya hivyo, na baadhi ya wanachuoni wa Kisuni pia wanakubaliana nao.

Wakati mfalme Maamun (wa ukoo wa Bani Abbas) alipotaka kuirudisha Fadak kwenye kizazi cha Zahra alimwandikia barua mmoja wa wanahadithi maarufu (aliyeitwa Abdullah bin Musa) ili ampe mwanga juu ya jambo lile. Yeye (Abdullah) aliiandika hadith tuliyoitaja hapo juu (ambayo kwa kweli inalielezea tukio la kuteremshwa kwa aya hii) na akampelekea. Matokeo yake yakawa kwamba yeye, yaani Mamun aliirudisha Fadak kwenye kizazi cha Fatimah.4 Na akamwandikia gavana wake wa Madina, akisema: "Mtume wa Uislamu (s.a.w.w.) aliitoa zawadi Fadak na kumpa binti yake Fatimah. Huu ni ukweli unaokubalika na hakuna tofauti kwayo miongoni mwa kizazi cha Fatimah."5

Maamun alipokikalia kiti maalum ili kusikiliza malalamiko ya watu, ombi la kwanza lilikuwa ni lalamiko moja ambalo mwandishi wake alijitambulisha kwa jina la mtetezi wa Bibi Fatimah (a.s.), Maamum alilisoma ombi lile akalia kidogo na akasema: "Ni nani huyu mtetezi wake?" Mzee mmoja alisimama na kujitambulisha kuwa ndiye huyo mtetezi. Kisha lile baraza la kisheria liligeuka na kuwa kikao cha mdahalo baina ya mzee yule na Maamun. Hatimaye Maamun alitambua kwamba ameshindwa. Hivyo alimwamrisha Jaji mkuu kuandika mkataba wenye kichwa cha habari: "Kuirudisha Fadak kwenye kizazi cha Zahra." Mkataba ule uliandikwa na ukapata idhini ya Maamun.

Katika wakati huo Da'bal Khuzaa'i aliyekuwepo pale wakati wa mdahalo ule alisimama na akazisoma beti fulani za utenzi.6

Ili kuthibitisha kwamba Fadak ilikwua ni mali ya Bibi Fatimah Zahra (a.s.) Mashia hawahitaji ushahidi ulioelezwa hapo juu, kwa sababu mtu aliye mkweli zaidi katika Uislamu, Sayyidna Ali Amirul-Mu'minin (a.s.) ameutaja ukweli huu waziwazi kwenye barua aliyomwandikia Uthman bin Hunayf, Gavana wa Basra. Anaandika hivi: "Ndio! Miongoni mwa vile vilivyoko chini ya mbingu mali ihusianayo nasi na tuliyonayo ni Fadak. Watu fulani waliona kijicho. Baadhi ya watu wakuu hawakulikataza jambo hili (la kuinyakua Fadak kutoka kwetu) kutokana na maslahi yao. Na Allah ndiye Hakim bora zaidi." Je inawezekana kutia shaka yoyote ile juu ya jambo hili baada ya kauli hii ya dhahiri?

Hadith Ya Fadak Baada Ya Mtume (S.A.W.W)

Baada ya kufariki dunia kwa Mtume (s.a.w.w.) binti yake mpenzi alizuiwa umiliki wake wa Fadak kutokana na matilaba ya kisiasa, na watendaji na wafanyakazi wa serikali walimtoa kwenye baraza la Khalifa alilokwenda kupeleka dai la Fadak. Hivyo basi aliamua kuichukua haki yake kutoka kwa Khalifa yule kwa kutumia hatua za kisheria.

Kwanza kabisa kijiji cha Fadak kilikuwa katika umiliki wake, na umiliki huu haswa ulikuwa ni dalili ya kuwa yeye ndiye mwenye mali ile. Hata hivyo, kinyume kabisa na vipimo vyote vya sheria ya Kiislamu, Khalifa yule alimuomba atoe ushahidi wakati wote ilihali tunajua kwamba mwenye kumiliki kitu hatakiwi kutoa ushahidi.

Hapo alilazimika kuwapeleka mashahidi mbele ya Khalifa ambao ni Sayyidna Ali (a.s.) na mwanamke mmoja aliyeitwa Ummi Ayman (ambaye kuhusiana naye Mtume (s.a.w.w.) alithibitisha kwamba atakwenda Peponi) na (kama ilivyonukuliwa na Bal?dhuri kwenye kitabu chake kiitwacho *Futuhul Buladn,* uk. 43), na Rabah mtumwa wa Mtume (s.a.w.w.) aliyepewa uungwana.

Hata hivyo, kutokana na maslahi fulani, yule Khalifa hakuukubali ushahidi wao na hatimaye yule binti wa Mtume (s.a.w.w.) alinyimwa mali ile ambayo baba yake alimpa ikiwa ni zawadi yake. Kwa mujibu wa Aya ya Tohara (Sura al–Ahzab, 33:33), Bibi Zahrah, Sayyidna Ali, na wana wao Hasan na Husein wamesafika kutokana na aina yote ya uchafu (ikiwemo kusema uongo), na kama aya hii itachukuliwa na kuhusishwa vilevile wake wa Mtume (s.a.w.w.) utumikaji wake (aya hii) kwa binti wake ni wa uhakika kabisa. Hata hivyo, kwa bahati mbaya hali hii ya mambo nayo ilikataliwa, na Khalifa wa wakati ule hakulikubali dai lake.7

Hata hivyo, wanachuoni wa Kishia wanaamini kwamba hatimaye Khalifa aliyakubali maoni ya yule binti wa Mtume (s.a.w.w.) na akaandika hati ionyeshayo kwamba Fadak ilikuwa ni mali yake na akairudisha kwake. Lakini alipokuwa njiani rafiki wa tangu kale wa Khalifa yule alibahatika kukutana naye na akapata kuyatambua yaliyokuwamo kwenye hati ile.

Aliichukua hati ile kutoka kwake na kuileta kwa Khalifa na kumwambia: “Kwa kuwa Ali ndiye mnufaika katika kesi hii, ushahidi wake haukubaliki, na Ummi Ayman kwa vile ni mwanamke, ushahidi wake naye hauna thamani.” Kisha akaipasua hati ile mbele ya Khalifa.8

Halabi, mwandihsi wa Kisuni wa maisha ya Mtume (s.a.w.w.) aliye maarufu sana anatoa maelezo mengine ya tukio hili, na anasema: “Khalifa alikubali umiliki wa Fatima (a.s.).

Mara kwa ghafla Umar alitokea pale na akauliza: “Hati hii ni ya nini?” Yule Khalifa akajibu akasema: “Nimethibitisha umiliki wa Fadak kwa Fatimah katika hati hii.” Umar akasema: “Wewe unahitaji mapato yatokanayo na Fadak. Kama kesho waabudu masanamu wa Uarabuni wakiamka dhidi ya Waislamu, utazikabili gharama za vita kutoka wapi?” Kisha akaishika hati ile mkononi mwake na akaipasua

pasua.”9

Hapa ndipo mahali ambapo mtu huukubali ukweli uliotajwa na mwanatheolojia mmoja wa Kishia, ambaye alisimulia kwamba Ibn Abil Hadid alisema: “Nilimwambia mwanatheolojia mmoja wa Kishia aliyeitwa Ali bin Naqi: Kijiji cha Fadak hakikuwa kikubwa sana, na sehemu ndogo kama hiyo iliyokuwa na mitende michache tu hivi, hakikuwa muhimu mno kiasi kwamba wapinzani wa Fatimah wakitamani.” Alisema katika jibu lake: “Hapa umekosea. Idadi ya mitende ya sehemu ile haikuwa kidogo kama miti iliyoko Kufah hivi sasa.

Hakika familia ya Mtume (s.a.w.w.) ilinyang’anywa ardhi hii yenye rutuba ili Ali Amirul–Mu’minin asije akayatumia mapato ya ardhi hii katika kufanya kampeni dhidi ya Khalifa; hivyo basi, sio tu kwamba walimnyima Fatimah Fadak, bali vilevile waliinyima familia nzima ya Bani Hashim na kizazi cha Abdul Muttalib haki zao za kisheria (khums; yaani 1/5 ya ngawira) kwa sababu watu ambao maisha yao wanaishi katika hali ya matatizo ya kiuchumi hawafikirii kuzibadili hali zilizopo.”10

Na kisha mwandishi huyo anainukuu sentensi tunayoinukuu hapa chini, itokayo kwa mmoja wa waalimu maarufu wa Madrasatul Gharbi Baghdad Iraq, aliyeitwa Ali bin F?ruqi. Anasema: “Nilimwambia: Je yule bintiye Mtume (s.a.w.w.) alikuwa mkweli katika kulifanya dai hilo?” Akasema: “Ndio.” Nikasema: “Je Khalifa alitambua kwamba yeye alikuwa ni mwanamke mkweli?” Akasema: “Ndio.”

Nikasema: “Kwa nini Khalifa hakumpa kile chenye kukubalika kwamba ni haki yake?” Wakati huu yule mwalimu alitabasamu na akasema kwa heshima kuu: “Kama angeliyakubali maneno yake katika siku ile, na akairudisha Fadak kwake kwa sababu ya yeye kuwa yu mwanamke mkweli, na bila ya kumtaka alete mashahidi, kesho angaliweza kabisa kukitumia cheo hiki kwa faida ya mumewe, na kusema: ‘Mume wangu Ali ana haki ya kuushika ukhalifa,’ na hapo Khalifa atalazimika kuutoa ukhalifa na kumpa Ali kutokama na kule kumtambua kwake kwamba yu mwanamke mwaminifu. Hata hivyo, ili kulikatisha dai au ugomvi wowote wa aina hii, ilimbidi amnyang’anye haki yake ikubalikayo.”11

Msingi wa kunyimwa kwa kizazi cha Bibi Fatimah (a.s.) lile dai lao la Fadak ulijengwa kwenye zama za Khalifa wa kwanza. Baada ya kufa kishahidi kwa Sayyidna Ali (a.s.) Muawiyah akazishika hatamu za serikali na akaigawa Fadak miongoni mwa watu watatu (Marw?n, Amr bin Uthman na mwanawe Yazid). Katika kipindi cha ukhalifa wa Marw?n mafungu yote matatu aliyachukua yeye na akampa zawadi mwanawe, aliyeitwa Abdul Aziz. Na yeye Abdul Aziz alimpa mwanawe aliyeitwa Umar.

Kutokana na ukweli uliopo kwamba Umar bin Abdul Aziz alikuwa mtu mnyoofu kutoka miongoni mwa Bani Umayyah uasi wa kwanza aliouondoa ulikuwa ni kurudisha Fadak kwenye kizazi cha Bibi Fatimah (a.s.). Hata hivyo, baada ya kifo chake makhalifa wa Bani Umayyah waliofuatia waliichukua tena Fadak kutoka kwa Bani Hashim na iliendelea kumilikiwa na wao hadi ulipokoma utawala wao.

Katika ukhalifa wa Bani Abbas, suala la Fadak lilitangatanga katika hali ya ajabu. Kwa mfano, Saffah alimpa Abdulah bin Hassan na baada yake Mansur Daw?niqi aliichukua, lakini mwanawe Mahdi aliirudisha kwenye kizazi cha Bibi Zahra (a.s.).

Baada yake, Musa na Harun waliitwaa kutoka kizazi cha Bibi Zahra (a.s.) kutokana na sababu za kisiasa. Maamun alipokikalia kiti cha Ukhalifa kwanza aliitoa na kuwapa wale wamiliki wa awali. Baada ya kifo chake hali ya Fadak ilisitasita tena na wakati mmoja ilirudishwa kwenye kizazi cha Bibi Fatimah (a.s.) na kisha ikachukuliwa tena kutoka kwao.

Katika kipindi cha ukhalifa wa Bani Abbas, Fadak ilijitwalia mwelekeo wa kisiasa mkubwa zaidi ikilinganishwa na mwelekeo wake usiyo na kifani. Na hata kama wale makhalifa wa kwanza walikuwa wahitaji wa mapato kutoka Fadak, makhalifa na waungwana wa baadae walikuwa matajiri sana kiasi kwamba hawakuwa wahitaji wa haja yoyote ya mapato yake.

Hivyo basi, wakati Umar bin Abdul Aziz alipoirudisha Fadak kwenye kizazi cha Bibi Fatimah (a.s.), Bani Umayah walimkemea na wakasema: “Kwa kitendo chako hicho, umewaona wale watu wawili walio watukufu (yaani Abu Bakr na Umar) kuwa wana makosa.” Hivyo basi, walimshauri kuyagawa mapato ya Fadak miongoni mwa kizazi cha Bibi Fatimah (a.s.), lakini kuubakisha umiliki wake mikononi mwake mwenyewe.12

---

1. Sura al-Hashir; 59:6,8; na kwenye vitabu vya Fiqhi (sheria za Kiislamu) jambo hili limejadiliwa kwenye sura ihusuyo Jihadi chini ya kichwa cha habari ‘Fay’.
2. Majma’ul Bayaan, Juz. 3, uk. 411; Sharh Ibn Abil Hadid, Juz. 16, uk. 248.
3. Durrul-Manthur, Juz. 4, uk. 176.
4. Majma’ul Bayaan, juz. 2, uk. 211; Futuhul Buldaan, uk. 45.
5. Sharh Nahjul Balagha cha Ibn Abil Hadid, Juz. 15, uk. 217.
6. Sharhu Nahjul Balagha cha Ibn Abil Hadid, Juz. 16.
7. Hii ina maana kwamba Qur’ani inasema Fatimah ni Mkweli asiyesema uongo – Mhariri.
8. Sharhu Ibn Abil Hadid, Juz. 16, uk. 274.
9. Siiratu Halabi, juz. 3, uk. 400.
10. Sharhu Ibn Abil Hadid, Juz. 16, uk. 236.
11. Sharhu Nahjul Balagh cha Ibn Abil Hadid, uk. 284.
12. Sharhu Ibn Abil Hadid, Juz. 16, uk. 278.

Sura Ya 45: Kadha Ya Umrah

Yalipotiwa saini yale mapatano ya Hudabiyah, Waislamu walipata haki ya kwenda Makka baada ya mwaka mmoja tangu tarehe ya kufanyika kwa yale mapatano, nao waliwajibika kutoka mjini humo baada ya kukaa siku tatu na kufanya Umrah.1 Katika siku hizo hawakuruhusiwa kuchukua silaha yoyote zaidi ya silaha ya msafiri (ambayo ni upanga).

Mwaka ulipita tangu pale yalipofanyika yale mapatano, hivyo muda ulifika kwa Waislamu kuweza

kuitumia ile fursa waliyopewa na mapatano yale, na wale Waislamu muhajiriina walioyaacha maskani yao yapata miaka saba iliyopita kwa ajili ya Uislamu na wameichagua nchi ya kigeni kuwa maskani yao, sasa wanaweza kwenda Makka tena kufanya Hija ya Ka'abah na vile vile kuwaona ndugu zao. Kwa sababu hiyo, pale Mtume (s.a.w.w.) alipotangaza kwamba wale watu walionyimwa kuitembelea Ka'abah mwaka mmoja uliopita, wajitayarishe kwenda Makka, shauku isiyo na kifani ilitokea miongoni mwao na machozi ya furaha yalitiririka mashavuni mwao. Kama katika kipindi cha mwaka mmoja uliopita Mtume (s.a.w.w.) alisafiri na watu 1300, idadi ya wale waliofuatana naye mwaka mmoja baadae ilifikia watu elfu mbili.

Watu mashuhuri miongoni Muhajirina na Ansar waliweza kuonekana miongoni mwa wale waliojitayarisha kwa safari hii. Walimfuata Mtume (s.a.w.w.) kwenye sehemu zote na walichukua ngamia themanini waliokuwa na alama za kutolewa kafara shingoni mwao. Mtume (s.a.w.w.) alivaa Ihr?m msikitini na wengineo wakamfuatia. Hivyo watu elfu mbili waliovaa Ihraam na wenye kutamka kwa dhati neno *Labbayk* midomoni mwao, waliondoka kwenda Makka.

Msafara huu ulikuwa na utukufu na heshima nyingi nao ulivutia mno kwa Waislamu pamoja na waabudu masanamu, kiasi kwamba iliwafanya waabudu masanamu kuelekea kwenye imani na ukweli wa Uislamu.

Kama tukisema kwamba safari hii ilikuwa safari ya kiuhubiri na watu hawa kwa kweli walikuwa jeshi la Uislamu, tutakuwa bado hatujatia chumvi, kwani matokeo ya kiroho ya safari hii yalitokea upesi sana na hatimaye wale maadui wakuu wa Uislamu kama vile Khalid bin Wadid, yule shujaa wa vita vya Uhud, na Amr bin Aas mwanasiasa wa Uarabuni, walipata mwelekeo wa kwenye Uislamu kutokana na kuuona utukufu huu na mara tu baada ya hapo waliipokea dini hii.

Mtume (s.a.w.w.) hakuwa na imani na Waquraishi kutokana na udanganyifu na kijicho chao. Ulikuwako uwezekano kwamba wangaliwashambulia Mtume (s.a.w.w.) na masahaba wake kwa kuwashitukizia atakapokuwa kwenye ukanda wa Makka na kumwaga damu ya baadhi yao, hasa pale ambapo wao (Waislamu) hawakuchukua silaha yoyote mbali ya zile silaha za msafiri. Hii ni kwa sababu kufuatana na masharti ya mapatano yale hawakuweza kuingia Makka wakiwa na silaha.

Ili kuondoa aina yoyote ile ya wasiwasi, Mtume (s.a.w.w.) alimteua mmoja wa maafisa wake aliyeitwa Muhammad bin Maslamah akifuatana na watu mia mbili waliokuwa na silaha zilizokuwa muhimu kama vile deraya na mikuki na walikuwa na farasi mia moja wepesi wa kukimbia ili kuutangulia ule msafara na kwenda kupiga kambi kwenye bonde la Marruz Zahraan (lililoko karibu na Haram) na kusubiri hapo hadi Mtume (s.a.w.w.) awasili. Majasusi wa Waquraishi waliokuwa wakiziangalia harakati za Mtume (s.a.w.w.), waliwaarifu machifu wa Waquraishi jambo hili.
Mikriz bin Hafs alikutana na Mtume (s.a.w.w.) akiwa yu mwakilishi wa Waquraishi na akamfikishia kutopendelea kwao kitendo kile. Mtume (s.a.w.w.) alijibu akasema: "Mimi au masahaba zangu hututafanya jambo lolote lililo kinyume na yale mapatano (yetu) na sisi sote tutaingia kwenye Haram tukiwa hatuna silaha.

Ama kuhusu afisa huyu na wale watu mia mbili wenye silaha, watabakia hapa.” Kwa kauli hii Mtume (s.a.w.w.) alimfanya yule mwakilishi wa Waquraishi atambue kwamba kama wakifanya mashambulizi ya kustukiza wakati wa usiku na kuchukua fursa isiyostahili kutokana na Waislamu kutokuwa na silaha, hili jeshi la msaada lililowekwa ukingoni mwa Haram pamoja na silaha, lingekuja upesi kuwasaidia na kuwapatia silaha mikononi mwao.

Waquraishi wakatambua umaizi wa Mtume (s.a.w.w.) na wakawafungulia Waislamu malango ya mji wa Makka. Viongozi wa waabudu masanamu na walio chini yao wakatoka mjini na kwenda kwenye vilima na vichuguu vya kaburini, ili kwamba wasionane na Mtume (s.a.w.w.) na masahaba zake na vilevile waweze kuyaona mishughuliko yao yote kwa mbali.

Mtume (S.A.W.W.) Aingia Mjini Makka

Mtume (s.a.w.w.) aliingia mjini Makka akiwa amepanda ngamia wake maalum huku akifuatana na watu elfu mbili waliomzunguka na sauti ya tamko lao, *Allahumma labbaik* ikipaa na kupiga mwangwi mji mzima. Sauti ya huu mkusanyiko teule ilivutia mno kiasi kwamba watu wote wa Makka walivutiwa nayo, na wakaanza kuwa na mvuto maalum na hisia juu ya Waislamu nyoyoni mwao. Wakati huo huo, umoja wa Waislamu ulijenga hofu isiyo kifani nyoyoni mwa waabudu masanamu.

Wakati wa kutoka kwa sauti ya neno *Labbayk* lililotamkwa na wale Waislamu, Abdullah Ram?hid aliyekuwa amezishikilia hatamu za ngamia wa Mtume (s.a.w.w.) mikononi mwake alisoma tenzi zifuatazo kwa sauti yenye kuvuma na ya kuvutia, akasema: “Enyi wana wa kufuru na kuabudu masanamu. Mpisheni njia Mtume wa Allah. Hamna budi kutambua kwamba yeye ndiye chanzo cha ustawi na wema. Ee Mola! Ninayaamini maneno yake nami ninayazingatia maamrisho Yako kuhusiana na kuutambua Utume wake.”2

Mtume (s.a.w.w.) alifanya Tawaaf ya Kaabah akiwa amepanda ngamia. Alipoifikia hatua hii aliamrisha kwamba Abdullah bin Rawaah aisome dua maalum ifuatayo na wale wengine wasome pamoja naye. Dua hiyo ni hii: “Hakuna mungu ila Allah (tu). Yeye Yu Mmoja tu na Asiye kifani. Ameitimiza ahadi Yake (Aliyoahidi kwamba Waislamu watafika kwenye Ka’abah hivi karibuni). Amemsaidia mja wake. Amelitukuza jeshi la upweke wa Allah, na kuyashutumu na kuyatupilia mbali majeshi ya kufuru na ushirikina.”

Katika siku ile vituo vyote vya hija na zile sehemu zifanyikako ibada za Umrah, ikiwa ni pamoja na mle msikitini Ka’abah, Safaa na Marwah zilikuwa chini ya utawala wa Waislamu. Sasa ibada za bidii na shauku kubwa kwenye sehemu iliyokuwa kitovu cha ibada ya masanamu na ushirikina kwa kipindi kirefu zimepiga pigo kubwa mno la kiakili kwa uongozi wa ushirikina na wafuasi wao kiasi kwamba ushindi wa Mtume Muhammad (s.a.w.w.) ulithibitika bara Arabuni kote.

Wakati wa sala ya adhuhuri ukaingia. Sasa ilikuwa muhimu kwamba Waislamu walitimize hili jukumu la Allah kwa jamaa mle msikitini na mwadhini wao atoe adhana kwa sauti kuu. Kama alivyoamrishwa na

Mtume (s.a.w.w.), Bilal yule mtumwa Mwethiopia aliyekuwa akiteswa mjini humo kwa kipindi kirefu kutokana na kusilimu kwake, alipanda juu ya paa la Kaabah na akaiweka mikono yake masikioni mwake, alitamka kwa sauti maalum zile sentensi tunazozitaja sote. Alizitamka kwenye sehemu ambayo tangazo la Upweke wa Allah na Utume wa Muhammad katika kipindi fulani lilikuwa ni kosa kubwa kwa mujibu wa makafiri wa Kiquraishi.

Sauti yake na zile thibitisho ambazo Waislamu walizifuatisha baada ya kuisikia kila sehemu ya adhana viliyafikia masikio ya waabudu masanamu na maadui wa Upweke wa Allah, na vikawatia wasiwasi mno kiasi kwamba Safwan bin Umayyah na Khalid bin Usayd wakasema: “Mungu na asifiwe kwamba jadi zetu walikufa nao hawakuisikia sauti ya huyu mtumwa Mwethiopia.”

Suhayl bin Amr alipomsikia Bilal akiyatamka maneno: *Allah Akbar* aliuficha uso wake kwa leso. Hawakupatwa na wasiwasi mno tu kutokana na sauti ya Bilal, bali walijihisi kwamba wamo katika mateso ya kiakili kutokana na vile vifungu mbalimbali vya adhana vilivyokuwa kinyume kabisa na itikadi zao walizozirithi kutoka kwa jadi zao.

Mtume (s.a.w.w.) alianza kufanya *Sai* (kutembea) baina ya vilima vya Safaa na Marwah. Kwa kuwa wanafiki na waabudu masanamu walieneza uvumi kwamba hali mbaya ya hewa Madina imewadhoofisha Waislamu, aliamua kufanya *Harwalah*3 katika sehemu ya ile *Sai,* na Waislamu nao wakamwiga. Baada ya kufanya *Sai* Waislamu waliwatoa kafara wale ngamia na wakavua Ihraam na wakanyoa nywele za vichwa vyao. Baada ya hapo Mtume (s.a.w.w.) aliamrisha kwamba watu mia mbili waende Marruz Zahran wakalinde zile silaha na zana nyingine za kijeshi ili kwamba wale watu waliokuwa wakishika kazi ile waje kwenye Haram na kufanya ibada za Umra.

Ibada za Umra zikamalizika Muhajiriin walikwenda majumbani mwao kuwasalimu ndugu zao. Vilevile waliwakaribisha baadhi ya Ansar huko majumbani kwao na hivyo wakawaonyesha fadhila kwa yale makaribisho na huduma walizotendewa na Ansar katika kile kipindi cha miaka saba.

Mtume (S.A.W.W.) Aondoka Mjini Makka

Utukufu na heshima ya Uislamu na Waislamu vilijenga hisia kali zaidi akilini mwa watu wa Makka, na wakapata ujuzi zaidi wa fikara za jumuia ya Waislamu. Machifu wa Waquraishi walitambua kwamba kule kukaa kwa Mtume (s.a.w.w.) na masahaba wake kumezidhoofisha nyoyo za watu wa Makka kuhusiana na imani yao juu ya ibada ya masanamu na uadui wa itikadi ya Upweke wa Allah, na wamejenga huba na mvuto baina ya haya makundi mawili. Hivyo ulipomalizika wakati wa mwisho wa zile siku tatu mwakilishi wa Waquraishi aliyeitwa Huwaytab alimjia Mtume (s.a.w.w.) na kumwambia: “Kipindi cha siku tatu kilichowekwa kwenye yale mapatano kwa wewe kuweza kukaa Makka kimekwisha, na hivyo basi, huna budi kutoka nchi yetu upesi iwezekanavyo.”

Baadhi ya masahaba waliona wasiwasi kutokana na ukali wa yule mwakilishi wa Waquraishi. Hata hivyo, Mtume (s.a.w.w.) si mtu achelewaye katika kuyatekeleza mapatano. Hivyo basi, Waislamu waliamrishwa

kulitoka eneo la Haram upesi sana.

Maimuna (dada yake Ummi Fazal, mkewe Abbas) alivutika mno na hamasa za Waislamu kiasi kwamba alimweleza shemeji yake Abbas, ami yake Mtume (s.a.w.w.) kwamba alikuwa tayari kuolewa na Mtume (s.a.w.w.) na akalichukulia jambo hilo kuwa ni heshima kwake. Mtume (s.a.w.w.) alimkubalia na hivyo akauimarisha uhusiano wake na Waquraishi. Mwelekeo wa mwanamke kwa mwanaume aliye na umri mkubwa kuliko wake wenyewe ni ushahidi utoshekezao wa mvuto wake wa kiroho. Vile vile Mtume (s.a.w.w.) alimwomba yule mwakilishi wa Waquraishi kumpa muda ili aweze kuifanya sherehe ya ndoa yake mle mjini Makkh na vilevile aweze kuwaalika machifu wote wa Makka kushiriki kwenye Walima. Hata hivyo, yule mwakilishi wa Waquraishi hakuikubali rai hiyo na akasema: “Sisi si wahitaji wa chakula chako.”

Mtume (s.a.w.w.) aliamrisha kwamba Waislamu waondoke Makka wakati wa adhuhuri. Alimwelekeza mtumwa wake tu aliyeitwa Abu Raafi’ kubakia pale hadi wakati wa jioni ili aje na mkewe Mtume (s.a.w.w.).4

Baada ya kuondoka kwa Waislamu, maadui wa Mtume (s.a.w.w.) walimkemea Maimuna, lakini kwa vile alikuwa kaishajenga mvuto na Mtume (s.a.w.w.) na hivyo amejitolea kuolewa naye, maneno yao hayakuwa na athari kwake. Hivyo basi, ile ahadi iliyosimama juu ya ndoto ya kweli ya Mtume (s.a.w.w.) ambayo aliifanya na Waislamu mwaka mmoja uliopita juu ya Hija kwenye Ka’abah na kufunguliwa kwa malango ya Makka kwa ajili ya Waislamu ilitimizwa, Aya ifuatayo iliteremshwa:

لَقَدْ صَدَقَ اللَّهُ رَسُولَهُ الرُّؤْيَا بِالْحَقِّ ۖ لَتَدْخُلُنَّ الْمَسْجِدَ الْحَرَامَ إِنْ شَاءَ اللَّهُ آمِنِينَ مُحَلِّقِينَ رُءُوسَكُمْ وَمُقَصِّرِينَ لَا تَخَافُونَ ۖ فَعَلِمَ مَا لَمْ تَعْلَمُوا فَجَعَلَ مِنْ دُونِ ذَٰلِكَ فَتْحًا قَرِيبًا {27}

“Bila shaka Allah Amemtimizia Mtume Wake ndoto ya haki. Bila ya shaka nyinyi mtauingia Msikiti Mtakatifu, Inshallah, kwa amani, na hali mmenyoa vichwa vyenu na mmepunguza nywele. Hamtakuwa na khofu. Na Mwenyezi Mungu anajua msiyoyajua. Basi alikupeni kabla ya haya ushindi ulio karibu.” (***Sura al-Fatih, 48:27***).

---

1. Umrah ina ibada maalum ziwezazo kufanywa wakati wowote ule wa mwaka. Tafauti na ibada za Haj ziwezazo kufanywa kwenye mwezi wa Dhil–Haj tu.
2. Siiratu Ibn Hisham, Juz. 2, uk 47.
3. Harwalah ni aina ya utembeaji wa kuchanganya zaidi ya ule wa kawaida lakini hauna kukimbia.
4. Siiratu Ibn Hishamu, Juz. 2, uk. 372

Sura Ya 46: Matukio Ya Mwaka Wa Nane Hijiriya

Mwaka wa saba wa hijiriya ukamalizika na Waislamu walifaulu kufanya Hija ya kwenye Ka'abah kwa pamoja kwa mujibu wa masharti ya Hudaybiyah. Vile vile waliweza kuziona ibada za kupendeza na kuvutia kwa manufaa ya Upweke wa Allah zikitendwa kwenye kitovu hasa cha ibada ya masanamu, kiasi cha kuweza kuzivutia kwenye Uislamu nyoyo za baadhi ya machifu wa Kiquraishi kama vile Khalid bin Walid, Amr Aas1 na Uthman bin Talhah. Mara tu baada ya hapo hawa machifu watatu walikuja Madina kwa Mtume Muhammad (s.a.w.w.) na wakaelezea mafungamano yao kwa ajili ya Mtume Muhammad na dini yake, na wakaukata uhusiano wao na Waquraishi wa Makka ambao hadi wakati ule hawakubakia kuwa chochote kile kingine isipokuwa mifupa isiyokuwa na uhai.2

Baadhi ya waandishi wa maisha ya Mtume (s.a.w.w.) wanasema kwamba Khalid na Amr bin Aas walisilimu kwenye mwaka wa 5 Hijiriya. Hata hivyo inawezekana kwa uhakika kwamba kusilimu kwao kulitokea kwenye mwaka wa 8 Hijiriya, kwa kuwa Khalid alikuwa kamanda wa kikosi cha jeshi la Waquraishi wakati wa kufanyika kwa yale mapatano ya Amani ya Hudaybiyah na wote wawili walisilimu pamoja.

Mwanzoni mwa mwaka wa 8 Hijiriya amani ilitawala katika maeneo mengi ya Hijaz na mvuto wa kuwaita watu kwenye ibada ya Mungu Mmoja ukazifikia sehemu nyingi, na ushawishi wa Wayahudi kwenye upande wa Kaskazini, na mashambulizi ya Waquraishi kutoka kwenye upande wa Kusini hayakuwatishia tena Waislamu.

Mtume (s.a.w.w.) sasa akaamua kuupanua mwito wake hadi Shamu na kufungua kituo kwa ajili ya kuupenyeza Uislamu nyoyoni mwa watu ambao wakati ule walikuwa wakiishi chini ya utawala wa mfalme wa Kirumi. Kwa ajili ya lengo hili alimtuma Harith Umayr Azd pamoja na barua kwenye baraza la mtawala wa Shamu. Katika siku zile Harith bin Shamir Ghassani alikuwa Mtawala dikteta wa Shamu, aliyetawala akiwa yu kibaraka wa Kaisari. Yule balozi wa Mtume (s.a.w.w.) aliifikia miji ya mpakani mwa Shamu na akaendelea na safari yake. Hata hivyo, Shurahbil aliyekuwa gavana wa maeneo ya mpakani alipata taarifa za kuwasili kwa yule balozi.

Alimfunga kwenye kijiji kiitwacho Muta na akafanya uchunguzi wa kina kutoka kwake. Yule balozi alikubali kwamba alikuwa na barua itokayo kwa Mtume wa Uislamu (s.a.w.w.) kwenda kwa Harith Ghassani mtawala dikteta wa Shamu. Akiivunja misingi yote ya ubinadamu na ikubalikayo duniani kote ambayo kwa mujibu wake (misingi hiyo) maisha na damu ya balozi huheshimiwa duniani kote, yule gavana aliamrisha kwamba afungwe mikono na miguu na kisha auwawe.

Mtume (s.a.w.w.) alipata taarifa za kitendo hiki kiovu cha Shurahbil. Alipatwa na wasiwasi mno kutokana na kuuwawa kwa yule balozi wake na akawapasha habari Waislamu kile kitendo kiovu cha Shurahbil na akawataka walipize kisasi dhidi ya yule gavana aliyetenda kitendo kile cha kinyama cha kumuuwa yule

balozi hata bila ya kupata ruhusa ya wakuu wake.

Msiba Mwingine Zaidi

Sambamba na kitendo hiki msiba mwingine zaidi ulitokea, hivyo ukathibitisha zaidi ile nia ya Mtume (s.a.w.w.) kuwaadhibu watu wa Shamu ambao waliutishia uhuru wa mahubiri yao na wahubiri wake na wakamuuwa mjumbe wake na wahubiri wa Uislamu kwa njia ya ukatili mno.

Tukio tulilolizungumzia hapo juu ni hili. Katika mwaka wa 8 Hijiriya, Kaab bin Umar Ghifaari alitumwa pamoja na watu wengine kumi na watano wote wakiwa ni wahubiri stadi, waende kwenye ukanda wa Zaat Atlah ulioko kwenye upande wa pili wa Waadiul Qaraa na kuwaita watu wa sehemu ile kwenye Uislamu. Wahubiri hawa walifika kwenye eneo hili na wakaifanya ile kazi waliyopewa.

Kwa ghafla wakakumbana na upinzani mkali kutoka kwa watu wale nao wakashambuliwa wote. Kile kikundi cha wahubiri kikajikuta kikiwa kimezungukwa na kundi kubwa la watu, Walijihami kishujaa na wakapendelea kufa kishahidi kuliko kufedheheka.

Ni mmoja wao tu ambaye naye alijeruhiwa na akalala miongoni mwa maiti za wale wenziwe, aliyeweza kuamka usiku wa manane na akarejea Madina. Alipofika huko alimsimulia Mtume (s.a.w.w.) tukio zima.

Kule kuwauwa wahubiri na watu wengi mno wasio na makosa kulimfanya Mtume (s.a.w.w.) aamrishe Jihadi. Hivyo basi, jeshi la askari elfu tatu lilipelekwa huko kwenda kuwaadhibu wale waasi, na wale waliozuia kuenezwa kwa Uislamu.3

Ilitowa amri ya Jihadi. Askari elfu tatu wapiganao kwa panga wakajikusanya kwenye uwanja wa kijeshi wa Madina (uitwao Jurf). Mtume (s.a.w.w.) akaja uwanjani pale yeye mwenyewe na kuwahubiria wale askari, akasema: “Hamna budi kwenda kuwaita tena watu hao kwenye Uislamu. Kama wakisilimu basi haitahitajika kulipiza kisasi cha kule kuuwawa kwa yule mjumbe, lakini kinyume na hivyo, hamna budi kuomba msaada wa Allah na kupigana dhidi yao. Ndio! Enyi askari wa Uislamu!

Piganeni Jihadi kwa Jina la Allah! Waadhibuni maadui wa Allah na maadui wenu waishio Shamu. Msiwaingilie watawa wa kiume na wa kike (masista) wanaotumia muda wao kwenye majumba ya watawala wakiwa wamejisogeza mbali zaidi kutoka kwenye Ghasia za ulimwengu. Viangamizeni vitu vyenye asili ya kishetani kwa hizi panga zenu.

Msiwauwe wanawake, watoto na wazee. Msiikate miti wala msiyabomoe majengo.4 Ndio! Enyi Mujahidiin! Kamanda wa jeshi hili ni binamu yangu Ja’far bin Abi Twalib. Kama akijeruhiwa, Zayd bin Harith ataishika bendera na kuliongoza jeshi, na kama naye akiuawa, Abdullah bin Rawaah atachukua mkanda wa jeshi. Na kama yeye naye akijeruhiwa, mnaweza kumteua kamanda wenu mkuu ninyi wenyewe.”

Hapo ilitolewa amri ya kuanza kuondoka na yeye mwenyewe Mtume (s.a.w.w.) pamoja na baadhi ya

Waislamu walilisindikiza jeshi lile hadi mahali paitwapo Thaniyatul Widaa.

Hapo wale waliowasindikiza wale askari waliwapa kwaheri na kwa mujibu wa desturi za zamani, waliwaambia: “Allah na akusaidieni mpate kurejea salama, wenye afya timamu na ngawira.”
Hata hivyo, Abdullah Rawaah aliyekuwa makamu wa pili au wa tatu wa kamanda wa jeshi lile aliusoma utenzi ufuatao: “Ninaiomba ghofira ya Allah na (kinga Yake) kutokana na mapigano makali ambayo kutokana nayo, povu la damu hububujika.”5

Kutokana na utenzi huu mtu anaweza kuitathmini vizuri sana ile nguvu ya imani na huba ya kufa kishahidi ya kamanda huyu shujaa. Wakati huo huo, watu walimwona akitokwa na machozi. Alipoulizwa ni kwa nini analia alijibu akisema: “Mimi sina haja kabisa ya huu ulimwengu, lakini nilimsikia Mtume (s.a.w.w.) akisoma ubeti huu: “Ni hukumu ya Allah isiyoepukika kwamba nyote mtawasili Motoni. Na kutoka hapo wale wachamungu waendelee na kwenda Peponi.” Hivyo basi, kuwasili kwangu Motoni ni kwenye uhakika lakini mwishilizio wa kuwasili huku sio dhahiri na haifahamiki ni kipi kitakachotokea baada ya hapo.”6

Tofauti Ya Maoni Kuhusu Kamanda Wa Kwanza

Wengi wa waandishi wa maisha ya Mtume (s.a.w.w.) wameandika kwamba yule kamanda mkuu wa jeshi lile alikuwa Zayd bin Harith mwana wa kulea wa Mtume (s.a.w.w.), na Ja’far na Abdullah walikuwa makamu wake wa pili na wa tatu, kwa utaratibu wa huku kutajwa kwa majina yao.

Hata hivyo, kinyume na maoni haya wanachuoni watafiti wa Kishia humchukulia Ja’far bin Abi Twalib kuwa ndiye kamanda mkuu wa jeshi lile na wale watu wawili wengine kuwa ni makamu wa pili na wa tatu. Sasa swali hapo ni, ni maoni yapi kati ya haya mawili yaliyo sahihi?

1. Kutokana na mtazamo wa heshima ya kijamii pamoja na uchamungu na elimu, Zayd bin Harith hakuwa sawa na Jaafar Tayyar. Ibn Athir kwenye kitabu chake *Usudul Ghabah*; anasema hivi kuhusiana na Jaafar: “Alifanana na Mtume katika tabia, umbile la mwili, na alimwamini Mtume muda mfupi tu baada ya Ali. Siku moja Abu Twalib alimwona Ali akiwa amesimama kuumeni kwa Mtume. Hapo akamwambia mwanawe Jaafar: “Wewe nawe huna budi kwenda na kusali ukiwa umesimama kushotoni kwa Mtume. “ Alikuwa kiongozi wa watu walioyaacha maskani yao kwa ajili ya dini na imani yao na wakatoka mji wa Makka kwa amri ya Mtume (s.a.w.w.) na kukimbilia Ethiopia. Yeye akiwa yu msemaji wa kikundi kile cha wahamiaji alimvutia Mfalme wa Ethiopia kwenye Uislamu kwa hoja zake zenye nguvu na zenye kupenya akilini na akauthibitisha uwongo wa wawakilishi wa Waquraishi waliotamani kurudishwa Hijaz kwa wale wahamiaji. Na kwa kuzisoma aya za Qur’ani zihusianazo na Nabii Isa (a.s.) na mama yake Mariam akazipata huruma na ulinzi wa Negus kwa ajili ya Waislamu wahamiaji kwa jinsi ambayo aliwatoa wale wajumbe wa Waquraishi barazani mwake.7

Jaafar alikuwa mtu yule aliyerejea kutoka Ethiopia wakati wa kutekwa kwa Khaybar, na Mtume (s.a.w.w.) aliposikia kurejea kwake, alikwenda mbele hatua kumi na sita kumlaki, akaiweka mikono yake

shingoni mwake, akalibusu paji la uso wake na akatokwa na machozi kwa furaha, kisha akasema: “Sijui ni kwa tukio lipi nilifurahie zaidi imma kwa ajili ya kuonana nawe baada ya kutengana kwa miaka mingi, au kwa ajili ya Allah kutufungulia ngome za Wayahudi kwa mikono ya kaka yako Ali.”

Jaafar ndiye yule mtu maarufu aliyekumbukwa na Amirul–Mu’minin (a.s.) baada ya kifo chake kwa ushujaa na uhodari wake. Sayyidna Ali (a.s.) alipopata habari kwamba Amr bin Aas amekula kiapo cha utii kwa Muawiyah na kwamba wameafikiana kwamba kama wakipata ushindi dhidi ya Sayyidna Ali (a.s.) ugavana wa Misri utapewa Amr, basi Amirul–Mu’minin (a.s.) alikosa raha na akamkumbuka ami yake Hamza na nduguye Jaafar na akasema:
“Kama watu hawa wawili wangelikuwa hai, ushindi wetu ungalithibitika.”8

Je, inaingia akilini kwamba ingawa Jaafar alikuwa nazo zile sifa maarufu ambazo baadhi yake tumezitaja hapo juu, kisha Mtume (s.a.w.w.) amteuwe Zayd kuwa kamanda wa jeshi lile na kumfanya Jaafar kuwa msaidizi wake wa kwanza?

2. Zile tenzi walizozisoma washairi wakuu wa Uislamu wakiviomboleza vifo vya hawa makamanda watatu zaonyesha kwamba kamanda mkuu alikuwa ni Jaafar na wale watu wawili wengine walikuwa wasaidizi wake. Katika kuzisikia taarifa za vifo vya hawa makamanda, Hassan Bin Thabit, mshairi wa Mtume (s.a.w) aliusoma utenzi ulionukuliwa kwenye kitabu *Siiratu Ibn Hisham*. Alisema: “Allah na awabariki wale makamanda waliouawa kwenye vita vya Muta, mmoja baada ya mwingine. Wao walikuwa ni Jaafar Zayd na Abdulah, waliokikaribisha kifo mmoja baada ya mwingine.”

Neno *tinaabi’u* lililotumika kwenye utenzi huu linaonyesha ya kwamba hawa makamanda watatu waliuawa mmoja baada ya mwingine na wa kwanza kuuawa alikuwa ni Jaafar. Shairi lililo wazi zaidi ni ule utenzi ulioandikwa na Ka’ab bin M?lik Ansari kuomboleza vifo vya wale waliouawa huko Muta. Katika utenzi huu aliainisha kamanda wa kwanza alikuwa ni Jaafar. Mshairi huyu yeye mwenyewe alishuhudia ukweli uliopo kwamba Mtume (s.a.w.w.) alimpa Jaafar ukamanda mkuu wa jeshi lile.

Anasema: “Hebu ukumbuke ule wakati askari wa Uislamu walipowekwa chini ya bendera ya kamanda wa kwanza ambaye ni Jaafar bin Abi Twalib na akatoka kwenda kupigana Jihadi.”

Beti hizi zilizoandikwa siku zilezile na bado zimesalia kuwa salama kutokana na mageuzi ya nyakati ni muhimu sana na ni ushahidi thabiti wa ukweli kwamba kile walichokiandika waandishi wa Kisuni juu ya jambo hili hakiafikiani na habari za kihistoria, na wasimuliaji wale wameyazusha masimulizi yale kwa sababu za kisiasa, na waandishi wa maisha ya Mtume (s.a.w.w.) wameyarekodi vitabuni mwao bila ya kuyathibitisha. Hata hivyo, inashangaza kwamba ingawa upo ukweli kwamba Ibn Hisham9 amezinakili tenzi hizi lakini amemchukulia Jaafar kuwa yu kamanda msaidizi wa pili.

Utaratibu Wa Vikosi Vya Kirumi Na Kiislamu

Siku zile Urumi ilikabiliwa na ghasia zisizo kifani kutokana na vita zilizokuwa zikiendelea baina yake na

Iran. Ingawa Warumi walitiwa moyo na ushindi wao juu ya Iran, vilevile waliutambua ushujaa na ujasiri wa askari wa Uislamu waliopata heshima kutokana na ushujaa wao na nguvu ya imani ya kila mmoja wao. Serikali ya kirumi ilipopata taarifa juu ya matayarisho na mwenendo wa askari wa Uislamu, Hercules na yule mtawala wa Shamu waliunda jeshi la kutisha kwenda kulikabili lile jeshi lenye nguvu la askari elfu tatu la Waislamu.

Shurahbil pekee alikusanya askari laki moja kutoka miongoni mwa makabila mbalimbali yaishiyo nchini Shamu na akaenda kule mipakani mwa nchi yake kwenda kuyazuia maendeleo ya wale mashujaa wa Kiislamu. Akiwa bado hajatosheka na hili, Kaisari naye kutokana na taarifa alizozipata kabla ya hapo, alitoka Urumi na askari laki moja na wakaenda wakapiga kambi mahali paitwapo Ma'ab ambapo ni miongoni mwa miji ya Balqaa. Walikaa hapo wakiwa ni jeshi la akiba la kuongezea nguvu.10

Ukusanyaji wa askari wote hawa ulifanywa kwenda kupigana na jeshi lililokuwa dogo sana linapolinganishwa na hilo linalokusanywa, ukusanyaji huo ulitokana na taarifa walizozipata wale makamanda wa Kirumi juu ya utekaji wa Waislamu. Isingalikuwa hivyo basi hata moja ya kumi ya jeshi hili lenye askari elfu ishirini lilitosha kabisa kuwakabili maadui wale vyovyote vile wawavyo mashujaa.

Ukweli unaopaswa kuzingatiwa hapa ni kwamba, nguvu ya haya majeshi mawili inapotathminiwa, utaona jeshi la Uislamu lilikuwa dhaifu mara nyingi sana kuliko lile la Urumi katika idadi ya askari pamoja na ujuzi wa maarifa na mbinu za kijeshi. Kutokana na kushiriki kwao kwenye vita vya muda mrefu baina ya Urumi na Iran, maafisa wa Urumi wamejipatia siri nyingi za ubora na ushindi wa kijeshi, ambapo ujuzi wa lile jeshi changa la Uislamu katika mambo haya wakati ule ulikuwa mdogo. Hivyo Waislamu hawakulingana na Warumi katika mambo ya zana na usafiri wa kijeshi.

Na jambo lililo muhimu zaidi ni kwamba lile jeshi la Waislamu lilikuwa liende kuishambulia nchi ya kigeni ambapo wale Warumi waliokuwa na zana zote hizo, walikuwa kwenye nchi yao wenyewe na walikuwa wajihami tu. Katika hali hizo, daima huwa muhimu kwamba lile jeshi lenye kushambulia liwe na zana na nguvu za kutosha kuzishinda hali zisizofaa.

Tukiyazingatia mambo haya, sasa tutaona kwamba wale makamanda wa jeshi la Waislamu walipendelea kuwa thabiti na kupigana kuliko kukimbia uwanja wa vita, na hivyo waliongeza heshima yao ya kihistoria, ingawa waliweza kukiona kifo kwa hatua chache tu.

Baada ya kuwasili mipakani mwa Shamu, Waislamu waliyatambua yale matayarisho na nguvu za kijeshi ya yule adui. Hivyo basi, upesi sana waliunda halmashauri ya ushauri ili kuweza kuamua juu ya maarifa ya kijeshi. Baadhi ya watu walikuwa na maoni kwamba jambo hilo lipelekwe kwa Mtume (s.a.w.w.) na kupata maelezo zaidi kutoka kwake. Maoni haya yalielekea kuthibitishwa, wakati uleule Abdullah Rawaahi aliyekuwa kamanda wa pili na aliyemwomba Allah kufa kishahidi katika ule wakati wa kutoka Madina aliamka na kutoa hotuba kali. Alisema: "Mmetolewa ili mlifikie lengo msilolipenda. Mmetoka Madina kukifikia kifo cha kishahidi, katika uwanja wa vita Waislamu hawategemei ubora wa idadi. Sisi tutapigana dhidi ya watu hawa katika njia ya Allah, Uislamu.

Uislamu uleule uliotufanya kuwa waheshimiwa na wastahiki. Kama tukishinda, tutaipata fahari; na kama tukifa kishahidi hilo nalo ni moja ya matakwa yetu.”

Maneno ya Abdullah yalizibadili fikara za maafisa na wale wajumbe wa halmashauri ya ushauri. Hivyo basi, iliamuliwa kwamba ili kuzitekeleza amri za Mtume (s.a.w.w.) yafanyike mapigano pale alipoamrisha Mtume (s.a.w.w.).11

Majeshi haya mawili yalikabiliana mahali paitwapo Sharaf. Hata hivyo, kutokana na kuzifikiria mbinu za kijeshi, sehemu ya jeshi la Waislamu ilirudi nyuma na kupiga kambi mahali paitwapo Muta. Jaafar bin Abu Twalib aliyekuwa kamanda mkuu wa jeshi lile, aliligawa katika sehemu tatu na akateua kamanda katika kila sehemu. Mapambano ya mtu na mtu yakaanza. Sasa ilikuwa muhimu kwa Jaafar kuishika ile bendera mikononi mwake na kuwaongoza askari wake katika mashambulizi na wakati huo huo kupigana na kujihami.

Ushujaa na uthabiti wake katika njia ya malengo yake ni dhahiri kabisa kutokana na beti za ule utenzi aliousoma pale alipokuwa akimshambulia adui. Alisema kwamba: “Ninayo furaha kwamba ile Pepo iliyoahidiwa imekuwa karibu zaidi; ile Pepo iliyo safi yenye vinwyaji baridi. Kinyume na hivyo, kuangamia kwa Urumi nako kumekaribia. Hali ya taifa kosefu kwa kufuru zake katika upande wa fundisho la Upweke wa Allah. Na ni taifa ambalo mawasiliano na uhusiano wake nasi umekatwa. Mimi ninayo dhamira ya kuwapiga pigo nitakapowakabili!”12

Yule kamanda mkuu wa Uislamu alipigana mapigano ya kijasiri dhidi ya adui. Hata hivyo, alipojikuta akiwa amezingirwa na maadui wale, na akatambua kwamba sasa kufa kwake kishahidi kulikuwa na uhakika, ili kwamba maadui wasimtumie farasi wake na vile vile watambue kwamba sasa kaishakata uhusiano na ulimwengu, alishuka kutoka kwenye farasi wake na akampiga pigo lililomfanya yule farasi asiweze kutembea, na kisha akaendelea kupigana.
Wakati ule ule kitanga chake cha kulia kilikatwa. Ili ile bendera ya Mtume (s.a.w.w.) isianguke chini, aliishika kwa kitanga chake cha kushoto na kile kitanga chake cha kushoto nacho kilipokatwa aliishika kwa mikono yake ile isiyo na vitanga. Hatimaye,baada ya kupata majeraha themanini alianguka chini na akafariki dunia.

Sasa ikafika zamu ya Zayd bin Harith, yule kamanda wa pili. Aliichukua ile bendera begani mwake na kulitekeleza jukumu lake kwa ujasiri usio kifani na hatimaye kafariki dunia kutokana na majeraha makubwa aliyoyapata.

Kisha akafuatia Abdullah Rawaah, yule kamanda wa tatu. Akaishika ile bendera mkononi mwake. Akampanda farasi wake na akaanza kuzisoma beti za utenzi wake. Katika kipindi cha yale mapigano alijiona kuwa yu mwenye njaa sana. Alipewa tonge la chakula ili aweze kuondokwa na njaa ile kwa kiasi fulani. Alikuwa bado hajakula chochote kile kutokana na kile chakula pale aliposikia sauti ya mtiririko kama kundi la maadui. Hapo akalitupa lile tonge la chakula na akaenda mbele kumkabili adui na akaendelea kupigana hadi alipokufa kishahidi.

Jeshi La Uislamu Laelemewa

Tangu pale na kuendelea kuelemewa na kutatanishwa kwa jeshi la Uislamu kulianza. Yule kamanda mkuu na wasaidizi wake wawili wameuawa. Hata hivyo, Mtume (s.a.w.w.) aliiona hali hii kwenye fikira zake kabla ya pale na tayari amewapa mamlaka wale askari kwamba, kama mambo yakitokea hivyo wamteue kamanda wao wenyewe. Kwa wakati ule Thabit bin Arqam akaiokota ile bendera, akawageukia wale askari wa Uislamu na kuwaambia: “Jichagulieni kamanda.” Wote wakasema: “Wewe na uwe kamanda wetu.” Akajibu akasema: “Mimi siko tayari kabisa kuichukua nafasi hii. Hivyo basi, hamna budi kumchagua mtu mwingine.” Kisha Thabit pamoja na Waislamu wengine wakamchagua Khalid bin Walid aliyesilimu hivi karibuni tu, na alikuwamo kwenye jeshi lile, kuwa kamanda wao.

Khalid alipoteuliwa kuwa kamanda hali ilikuwa nyeti mno. Hofu na kitisho viliwaingia Waislamu. Yule kamanda (mpya) alipanga kuzitumia mbinu za kijeshi zisizokuwa na kifani. Aliamrisha kwamba wakati wa usiku kitakapoingia kiza kila mahali, wafanye mageuzi na mabadilishano ya farasi na kwamba pia wapige makelele. Vikosi vya kulia viende kwenye nafasi ya vikosi vya kushoto na vikosi vya kushoto vije kwenye nafasi ya vikosi vya kulia, na hali kadhalika safu ya mbele ije katikati ya jeshi na safu ya katikati iende mbele. Mabadiliko haya yaliendelea hadi asubuhi.

Kufuatana na masimulizi fulani, aliamrisha kwamba kikosi cha Waislamu kisogee kwenye sehemu ya mbali wakati wa usiku na kisha kirudi wakati wa asubuhi huku kikisoma *Laailaha illallah* (hakuna mungu ila Allah). Lengo la mpango wote huu lilikuwa kwamba lile jeshi la Kirumi lifikirie kwamba jeshi la msaada limefika kujiunga na Waislamu. Kwa bahati ilitokana na dhana hii kwamba hawakuwashambulia Waislamu siku iliyofuatia na wakaambiana kwamba ikiwa Waislamu wameweza kupigana kishujaa kiasi kile walipokuwa hawana jeshi la msaada sasa watapigana kishujaa zaidi baada ya kupata jeshi la msaada.

Kutulia kwa lile jeshi la Warumi kuliwapa Waislamu nafasi ya kurejea makwao. Mafanikio makubwa waliyopata Waislamu yalikuwa kwamba walipigana dhidi ya jeshi lililoandaliwa na lenye nguvu kwa muda wa siku moja au tatu hivi. Ule mpango wa kijeshi alioutumia yule kamanda mpya ulikuwa mzuri kwa sababu uliwatoa Waislamu kwenye kifo na kuwafanya warejee Madina kwa usalama. Hivyo basi anastahili kusifiwa.13

Askari Wa Uislamu Warejea Madina

Taarifa zihusianazo na mapigano na kurudi nyuma kwa askari wa Uislamu zilikuwa tayari zimeshafika Madina kabla ya kufika kwao pale. Hivyo basi, Waislamu walitoka na kwenda kuwalaki hadi wakafika Juraf kwenye uwanja wa kijeshi wa mji wa Madina.

Ile hatua iliyochukuliwa na yule kamanda mpya ilikuwa ni mbinu ya hekima, lakini kwa kuwa haikuafikiana na mwelekeo wa Waislamu na hali yao ya ushujaa halisi, na kulelewa kwenye himaya ya imani, hawakutazamia kule kurudi nyuma kwa wale askari na hawakufikiria kitendo hiki kuwa ni chenye

rehema. Hivyo basi, waliwapokea kwa kauli mbiu zenye uchungu kama vile: “Enyi wakimbizi! Kwa nini mmeikimbia Jihadi?” Na kwa kuwatupia vumbi vichwani na nyusoni mwao.

Kitendo cha Waislamu hawa dhidi ya hiki kikundi kilikuwa cha jeuri mno kiasi kwamba baadhi ya watu walioshiriki mwenye vita ile walilazimika kujifungia majumbani mwao kwa kipindi hivi, nao hawakujitokeza mbele ya macho ya hadhara. Na walipotoka watu waliwasoza vidole na kusema: “Huyu ni mmoja wa wale watu walioikimbia Jihadi.”14

Hatua za Waislamu dhidi ya kurejea nyuma kwa wale askari wa Uislamu kulikofanyika kwa busara, ni dalili ya moyo wa ushujaa na ujasiri ambao itikadi juu ya Allah na Siku ya Hukumu imejenga na kukamilika nyoyoni mwao, na ambayo kutokana nayo, walikipendelea kifo katika njia ya Uislamu kuliko ile faida ndogo itokanayo na kule kurejea nyuma.

Ngano Badala Ya Historia

Kama vile Amirul–Mu’minin Sayyidna Ali bin Abi Twalib (a.s.) anavyofahamika miongoni mwa Waislamu kama Simba wa Mungu – *Asadullah*, baadhi ya watu waliona kuwa inafaa kuunda katika ulinganisho naye, kamanda atakayekishika cheo cha Upanga wa Allah, na mtu huyo si yeyote mwingine ila ni yule kamanda shujaa wa Uislamu, Khalid bin Walid. Hivyo basi wanasema kwamba aliporejea kutoka kwenye Vita vya Muta, Mtume (s.a.w.w.) alimpa cheo cha Upanga wa Allah.

Hakuna shaka kwamba kama Mtume (s.a.w.w.) angempa cheo hiki kwenye tukio jingine basi lisingelikuwako swali lolote juu ya jambo hili, lakini hali ya mambo ilivyo, baada ya kurejea kwa lile jeshi la Waislamu kutoka kwenye Vita vya Muuta haikufanya kuweko umuhimu wa kwamba Mtume (s.a.w.w.) ampe cheo hicho.

Je ni haki kwamba Mtume (s.a.w.w.) ampe cheo cha ‘Upanga wa Allah’ mtu anayewaongoza watu ambao Waislamu wanawaita wakimbizi na kuwapa mapokezi ya kuwamwagia vumbi vichwani na nyusoni mwao? Na hata kama akiidhihirisha sifa ya kuwa

‘Upanga wa Allah’ kwenye vita nyinginezo, lakini kwenye vita hivi hakuweza kulifikia lengo lolote zaidi ya ule mpango wake wa kijeshi ustahilio sifa, kwani vinginevyo yeye na wafuasi wake wasingalipewa sifa ya wakimbizi.

Ibn Sa’ad anaandika hivi: “Katika ule wakati wa kurudi nyuma kwa askari wa Uislamu, askari wa Kirumi waliwafuatia na kuwauwa baadhi yao.”15

Wazushi wa ngano hii ya ‘Upanga wa Allah’ vile vile wameiongeza sentensi ifuatayo ili kuiunga mkono kauli yao: “Khalid alipoushika ukamanda, aliwaamrisha askari kumshambulia adui. Yeye mwenyewe alishambulia kwa ushujaa na panga tisa zilivunjika mkononi mwake, na ikasalia ngao tu.”
Hata hivyo, wazushi wa ngano hii walisahau jambo moja nalo ni, kama Khalid na askari wake walitenda ujasiri na ushujaa wa aina ile kwenye uwanja wa vita, ni kwa nini watu wa Madina waliwaita ‘wakimbizi’

na ni kwa nini wawalaki kwa kuwamwagia vumbi vichwani mwao na nyusoni mwao, wakati wao kwa kitendo kile (yaani kama walipigana kishuja kama ilivyoelezwa hapo juu) wangewalaki kwa heshima, kwa mfano kwa kuchinja kondoo na kuwanyunyizia manukato na marashi kwenye njia yao?

Mtume Alilia Sana Kwa Kifo Cha Ja'far

Mtume (s.a.w.w.) aliangua kilio kwa kifo na shahada ya binamu yake Ja'far, alikwenda moja kwa moja kumwarifu mkewe Asmaa' bint Umays kuhusu kifo cha mumewe na pia kumpa salamu za rambirambi. Akizungumza na Asmaa, alisema hivi: "Wako wapi wanangu?" Asmaa akawaleta wana wa Jaafar, Abdulah, Awn na Muhammad mbele ya Mtume (s.a.w.w.). Alipoona uambatanaji mkubwa sana wa Mtume (s.a.w.w.) kwa wanawe, Asmaa alitambua ya kwamba mumewe mpenzi amefariki.

Akasema: "Inaonekana kwamba wanangu wamekuwa yatima, kwa sababu ya hivyo unavyowatendea." Mtume (s.a.w.w.) akalia sana wakati ule. Kisha akamwomba binti yake atayarishe chakula na kuifariji familia ya Jaafar kwa muda wa siku tatu. Hata baada ya hapo, Mtume (s.a.w.w.) aliendelea kumhuzunikia Jaafar bin Abi Twalib na Zayd bin Harith na alipoingia nyumbani mwake (Mtume s.a.w.w) aliwalilia mno.16

---

1. Waaqidi ametoa masimulizi mengine ya mvuto ya chifu huyu kuelekea kwenye Uislamu (Maghaazi, Juz. 2, uk. 743–745).
2. Tabaqaatu Ibn Saad, Juz. 7, uk. 394.
3. Tabaqaatul Kubra, juz. 2, uk. 128.
4. Maghaazil–Waaqidi, juz. 2, uk. 757.
5. Na baada ya hapo, upesi sana akausoma utenzi mwingine usemao; "Wakati watu watakapoliona kaburi au maiti yangu, ikiwa imetapakaa damu, waweze kuusifu ushujaa wangu na kujitolea mhanga kwangu na kuniombea." (Bihaarul Anwaar, juz. 21, uk. 60 na Tabaqatul Kubra, juz. 2, uk. 128).
6. Siiratu Ibn Hishamu, Juz.2, uk. 374.
7. Usudul Ghabah, Juz. 1, uk. 387.
8. Siffin Ibn Muzaahim, uk. 47.
9. Siiratu Ibn Hishamu, Juz. 2, uk. 384–387.
10. Mughaazil–Waaqid, juz. 2, uk. 760; Siiratu Ibn Hishamu, Juz. 2, uk. 375.
11. Maghaazil–Waaqid, Juz. 2, uk. 760; Siiratu Ibn Hishamu, Juz. 2, uk. 77.
12. Siiratu Ibn Hishamu, Juz. 2, uk. 378.
13. Maghaazil–Waaqid, Juz. 2, uk. 763.
14. Siiratu Ibn Hishamu, Juz. 2, uk. 382–383; Siiratu Halabi, Juz. 2, uk. 79.
15. Tabaqatul–Kubra, Juz.2, uk. 129.
16. Bihaarul Anwaar, Juz. 21, uk. 54–55; Maghaazil–Waaqidi, Juz. 2, uk. 766.

Sura Ya 47: Vita Vya Dhatus Salasil

Tangu siku ile Mtume (s.a.w.w.) alipohajiria Madina na kuufanya mji ule kuwa makao makuu ya Uislamu, daima alikuwa mwangalifu wa hali ya maadui na shauku yao na makri zao, na akaupa upatikanaji wa taarifa umuhimu ustahilio kuhusiana na matendo yao. Aliwapeleka Makka watu stadi na hodari na kwenye makabila mbalimbali ili waweze kumwarifu mapema juu ya maamuzi na mipango ya maadui.

Baada ya kuzitambua njama zao, mara kwa mara alikuwa akizikomesha palepale mwanzoni kabisa. Katika hali hiyo, mashujaa wa Uislamu walikuwa wakiwashambulia maadui kwa kuwasitukiza chini ya ukamanda wa Mtume (s.a.w.w.) au chini ya baadhi ya maafisa mashujaa wa Uislamu na kuwatawanya hata kabla ya kusogea kutoka kwenye sehemu zao. Matokeo yake yakawa kwamba, Uislamu ulisalimika kutokana na hatari za maadui, na umwagaji damu mwingi nao ulizuiwa.

Katika nyakati zetu hizi, taarifa za nguvu na kufaa kwa jeshi la adui na juu ya mipango yake ya siri kunafikiriwa kwamba ni moja ya visababisho vya ushindi, na mataifa makuu ya ulimwengu yanayo mipango mipana mno ya jinsi ya kuwafunza majasusi, kuwapeleka kwenye sehemu mbalimbali ulimwenguni na kuwatumia.

Katika Uislamu, mwongozo wa kuanzisha jambo la upelelezi ulichukuliwa na Mtume mwenyewe, na baada yake makhalifa wa Uislamu, na hususan yule Amirul–Mu'minin pia aliwapa majasusi kadhaa majukumu mbalimbali.

Na kila alipomteua mtu kuwa gavana wa sehemu fulani, aliwaamrisha baadhi ya watu kuiangalia tabia na mwenendo wake na kumpelekea taarifa (yaani kwake yeye Sayyidna Ali a.s). Amelitaja jambo hili kwenye barua zake kadhaa alizowaandikia magavana ambazo kwazo magavana hawa wamekemewa. (Tazama Barua Na. 33 na 35 kwenye *Nahjul Balaghah*).

Katika mwaka wa pili Hijiriya Mtume (s.a.w.w.) aliwapeleka watu themanini kutoka miongoni mwa Muhajiriin chini ya uongozi wa Abdullah bin Jahsh, kwa maelekezo ya kwenda kupiga kambi mahali fulani maalum na kumweleza (yeye Mtume s.a.w.w) kuhusu matendo na mipango ya Waquraishi. Kama Mtume (s.a.w.w.) hakuweza kushambuliwa kwa kushitukizwa bila ya yeye mwenyewe kujua wakati wa vita vya Uhud, na akaweza kuyaweka majeshi yake nje ya mji wa Madina kabla ya kuwasili kwa maadui, na pia kama kwenye vita vya Ahz?b aliweza kuchimba lile handaki lenye kutisha mbele ya maadui kabla ya kufika kwao pale, ni kwa sababu tu ya zile taarifa zenye maelezo kamili ambazo Waislamu, waliotumwa kwa lengo hili waliziwasilisha kwake, na kwa njia hii wakaweza kutekeleza wajibu wao wa kidini katika kuusalimisha Uislamu kutokana na kuanguka.

Njia hii ya hekima aliyoitumia Mtume (s.a.w.w.) ni mfano wenye thamani mno kwa Waislamu kuweza kuufuata, na chini ya msingi huu ni muhimu kwamba viongozi wakuu wa Uislamu wazitambue kwa ukamilifu aina zote za makri zilizo dhidi ya Uislamu ndani ya nchi za Kiislamu na vilevile katika sehemu

mbalimbali ulimwenguni. Kwa njia hii waweze kuzizima cheche kabla ya kugeuka kuwa miali na ili waweze kulifikia lengo lao. Hata hivyo, kweye zama zetu hizi jukumu hili haliwezi kutimizwa bila ya zana muhimu.

Kwenye Vita vya Dhatus-Salaasil ambavyo ndio maudhui ya mazungumzo yetu ya hivi sasa, uasi mkubwa sana ulikomeshwa kwa urahisi sana kwa kupata taarifa kamili juu ya mpango wa adui. Na kama Mtume (s.a.w.w.) asingeliitumia njia hii ya kukusanya taarifa basi angelipata hasara isiyotengezeka.Yafuatayo hapa chini ndio malezo ya tukio hili kwa urefu:

"Idara ya ujasusi ya Mtume (s.a.w.w.) ilimtaarifu kwamba kwenye Bonde la Yaabis, maelfu ya watu yalifanya mapatano ya pamoja kwamba watauangamiza Uislamu kwa nguvu zao zote na watautoa uhai wao kwa ajili ya kulifikia lengo hili au wamuue Muhammad, na afisa wake shujaa na mshindi, Ali (a.s.)." Mwanachuoni mkuu Ali bin Ibrahim Qummi anaandika hivi: "*Wahyi* ulimwarifu Mtume (s.a.w.w.) juu ya mpango wao huo."1

Lakini Shaykh Mufid mwanachuoni mtafiti mkuu anasema: "Mwislamu mmoja alitoa taarifa juu ya jambo hili kwa Mtume (s.a.w.w.) na akaitaja sehemu ya njama hiyo kuwa ni bonde la Raml"2 na akaongeza kusema kwamba makabila hayo yaliamua kufanya mashambulizi ya usiku mjini Madina na kulimaliza kabisa jambo hili kwa ukamilifu.

Mtume (s.a.w.w.) alifikiria kwamba ilikuwa muhimu kuwaarifu Waislamu juu ya hatari hii kuu. Kwenye siku hizo, neno la siri lililokuwa likitumika kwa ajili ya kuwaita watu kwenye sala au kusikiliza taarifa muhimu lilikuwa '*Assalaat Jaami'ah'* Hivyo basi, kama ilivyoamrishwa na Mtume (s.a.w.w.) mtangazaji alikwenda kwenye nafasi yake ya kutangazia iliyokuwa mahali palipoinuka kwenye paa la msikiti na kutamka ile kauli tuliyoitaja kwa sauti kuu.

Upesi sana Waislamu walikusanyika mle msikitini. Mtume (s.a.w.w.) akapanda mimbari na akazungumza mambo mengi yakiwamo haya: "Maadui wa Allah wanakuoteeni nao wameamua kukushambulieni kwa kukuvizieni wakati wa usiku. Baadhi yenu ni lazima wasimame ili kuuzuia uasi huu."

Wakati huu, kikundi cha watu kiliteuliwa kwa lengo hili, na Bwana Abubakr aliteuliwa kuwa kamanda wake. Yeye pamoja na hicho kikundi maalum waliliendea kabila la Bani Salim. Umbali ambao hawa askari wa Uislamu walisafiri ulikuwa ni pamoja na njia yenye mawe yasio ya kawaida, na eneo lenye bonde lililokuwa likikaliwa na kabila lile lilikuwa pana sana.

Wale askari wa Uislamu walipojaribu kuliingia bonde lile iliwabidi kuwakabili Bani Salim na yule kamanda wa jeshi la Uislamu hakuweza kuifikiria njia yoyote nyingine ila kwamba arudi kwa njia aliyojia.3

Mwanachuoni Ali bin Ibrahim Qummi anaandika kwenye *Tafsiir* yake hivi: "Machifu wa kabila lile la Bani Salim walipomwuliza Abubakr: "Nini lengo la msafara huu wa kijeshi?" alijibu akisema: "Mimi

nimeteuliwa na Mtume wa Allah kukubalighishieni Uislamu na kupigana dhidi yenu kama mkikataa kusilimu.” Muda uleule wale machifu wa lile kabila wakamtisha na wakamfanya aikabili idadi kubwa ya askari.

Hivyo, akawaamrisha wale askari wa Uislamu kurejea na akawarudisha Madina, licha ya ukweli kwamba walipaswa kupigana kishujaa.”

Kurejea kwa jeshi la Uislamu na pia katika hali ile inayosemekana, kulimgusa Mtume (s.a.w.w.). Sasa akakabidhi ukamanda wa jeshi hili kwa rafiki yake Abubakr, Umar. Wakati huu wale maadui walikuwa na tahadhari zaidi kuliko pale mwanzo na wakawa wamejificha kwenye mlango wa kuingilia bondeni mle nyuma ya mawe na miti. Wakati wa kuwasili kwa jeshi la Uislamu walitoka mle kwenye maficho kwa nguvu. Hivyo, yule kamanda wa jeshi alilazimika kukimbia na kurejea Madina.

Amr bin Aas, mwanasiasa mwenye hila wa Uarabuni ambaye wakati ule ndio kwanza kwamba alisilimu, alimjia Mtume (s.a.w.w.) na kusema: “Vita ni udanganyifu.” Alikuwa na maana ya kusema kwamba ushindi katika vita hautegemei ujasiri na nguvu tu, lakini vilevile unatokana na uhodari na udanganyifu ambao ni lazima utumike juu ya adui ili kupata ushindi. Aliongeza kusema: “Kama nikiruhusiwa kuwaongoza askari wa Uislamu, nitafaulu kulifikia lengo lihitajikalo.” Kwa ajili ya kulifikia lengo jema Mtume (s.a.w.w.) aliikubali rai yake lakini yeye naye kama ilivyokuwa kwa wale makamanda wa awali, alikutana na matatizo yale yale.

Sayyidna Ali (A.S.) Ateuliwa Kuwa Kamanda Wa Jeshi Lile

Kushindwa kulikoandamana kumewahuzunisha mno Waislamu. Hatimaye Mtume (s.a.w.w.) aliandaa jeshi na akamteua Sayyidna Ali (a.s.) kuwa kamanda na akampa Ali (a.s.) bendera mkononi mwake na akamwomba mkewe Bibi Fatimah (a.s.) ampe kitambaa alichokuwa akikifunga kichwani awapo kwenye hali ngumu. Yule binti yake Mtume alilia sana kumwona mumewe mpendwa akiwa anakwenda kwenye safari ya hatari mno.

Mtume (s.a.w.w.) alimfariji na akayafuta machozi machoni mwake. Kisha Mtume (s.a.w.w.) akamsindikiza Sayyidna Ali hadi kwenye Masjidul Ahzaab. Sayyidna Ali (a.s.) akampanda farasi mwenye madoa ya rangi mbili huku akiwa amevaa mavazi mawili yaliyofumwa nchini Yaman, na mkononi mwake akiuchukua mkuki uliotengenezwa Hind,4 na akatoka. Aliubadili kabisa utaratibu wa safari kiasi kwamba wale askari wakaanza kudhania kwamba alikuwa akienda Iraq. Mtume (s.a.w.w.) aliyekuwa akimtazama pale alipokuwa akiondoka, alisema: “Yeye ni kamanda mpiganaji ambaye kamwe hakimbii kutoka uwanja wa mapambano.”

Kuihusisha kauli hii makhsusia kwa Sayyidna Ali (a.s.), kunaonyesha kwamba wale makamanda wa awali sio tu kwamba wameshindwa, bali kinyume na misingi ya kijeshi ya Uislamu, kule kurudi nyuma kwao vilevile kulikuwa na maana ya kushindwa.

Siri Ya Ushindi Wa Sayyidna Ali (A.S.) Kwenye Vita Hivi

Siri ya ushindi alioupata Ali (a.s.) kwenye vita hivi inaweza kuelezwa kwa mukhtasari katika sababu tatu zifuatazo:

Hakumwezesha adui kutambua matendo yake, kwa sababu aliibadili njia yake ili kwamba, taarifa zenye kuzihusu mbinu zake zisifike kwa yule adui kupitia kwa Waarabu mabedui na makabila ya jirani. Alitenda juu ya kanuni muhimu ya kijeshi, yaani kujificha. Alisafiri wakati wa usiku na kujificha kwenye sehemu fulani wakati wa mchana na aka- pumzika. Alikuwa bado hajaufikia ule mlango wa lile bonde pale alipowaamrisha askari wote kupumzika. Na ili adui asitambue kuwasili kwao karibu na lile bonde, vile vile aliwataka wale askari wa Uislamu kuifunga midomo ya farasi wao ili milio yao isimwamshe yule adui. Alfajiri ilipoingia alisali pamoja na wafuasi wake kisha akawaamrisha wale askari waanze kuupanda ule mlima kutoka kwenye upande wa nyuma wa mlima ule, na akawaingiza kwenye lile bonde kutoka juu ya mlima.

Chini ya uongozi wa afisa shujaa na jasiri, wale askari waliendelea mbele kama mmiminiko wa maji na kuanza kuwashambulia kama radi wale maadui wakiwa bado wamelala. Baadhi yao wakauwawa na wengine wakakimbia.

Ushujaa wa Amirul-Mu'minin usio kifani, aliyewaua wapinzani saba, ulimzidi nguvu yule adui. Waliogopa sana kiasi kwamba walipojikuta wakiwa hawana uwezo wa upinzani zaidi, walikimbia huku wakiziacha ngawira nyingi sana nyuma yao.5

Yule kamanda shujaa alirejea madina na akavikwa taji la heshima. Mtume (s.a.w.w.) akifuatana na baadhi ya masahaba zake wakamlaki. Alipomwona Mtume (s.a.w.w.) alishuka kwenye mnyama wake upesi sana. Mtume (s.a.w.w.) alipokuwa akiupiga mgongo wa Sayyidna Ali (a.s.) ili kumpongeza, alimwambia: "Mpande farasi wako. Allah na Mtume Wake wamekuridhia."

Hapo machozi yakaanza kumtiririka mashavuni mwake kutokana na furaha nyingi, na kisha Mtume (s.a.w.w.) aliitamka hii kauli ya kihistoria kuhusiana na Sayyidna Ali (a.s.): "Kama si kwa kuchelea kwamba kikundi cha wafuasi wangu wanaweza wakayasema kuhusiana nawe mambo kama yale wayasemayo Wakristo kuhusiana na Nabii Isa, ningalisema mambo yahusianayo nawe, ambayo watu wangaliliona vumbi lililochini ya wayo wako kuwa ni kitu cha baraka popote pale upitapo."6

Ushujaa huu wa kujitoa mhanga ulikuwa na thamani kubwa mno kiasi kwamba Sura *al-Aadiyaat* ilifunuliwa kuhusiana na tukio hili na kiapo chake kisicho kifani na chenye kushtusha kinalenga katika kuuridhia moyo wa kijeshi na ujanadume wa wale askari mashujaa walioshiriki kwenye vita hii. Zifuatazo hapa chini ni baadhi ya aya za Sura hii: **"Naapa kwa farasi wendao mbio wakipumua. Na wakitoa moto kwa kupiga kwato zao chini. Wakishambulia wakati wa asubuhi. Huku wakitimua vumbi. Na wakijitoma kati ya kundi.." (Sura al-Aadiyaat, 100:1-5).**

Aya hizo hapo juu ni muhtasari wa tukio la vita vya Dhatus–Salasil kama lilivyoandikwa na wafasiri wa Qur'ani na wanahistoria wa Kishi'ah juu ya msingi wa wanachuoni waaminiwao. Hata hivyo, wanahistoria wa Kisunni kama vile Tabari, wametoa masimulizi mengine ya tukio hili yenye kutofautiana na yale tuliyoyaeleza hapo juu. Si jambo lisilowezekana kwamba vita mbili zote zina jina la Dhatus–Salasil na kila kundi limesimulia matukio ya moja kati ya hizo vita mbili na kuiacha ile nyingine kutokana na sababu fulani fulani.7

---

1. Tafsirul Qummi, uk. 733.
2. Inawezekana kwamba Bonde la Raml (jangwa la mchanga) na Bonde la Yaabis (jangwa kavu) ni sehemu ile ile.
3. Al–Irshaad, uk. 84.
4. Hind ni jina la mji.
5. Tafsirul Furaat, uk. 222–226; Majma'ul Bayaan, Juz. 1, uk. 528.
6. Al–Irshaad, uk. 84–86.
7. Tarikhut–Tabari, Juz. 3, uk. 30; Siiratu Halabi, Juz. 3, uk. 215; Maghaazil– Waaqidi, Juz. 2, uk. 769–774.

Sura Ya 48: Kutekwa Kwa Mji Wa Makka (Faatihu–Makkah)

Ukiachilia mbali kule kuwa moja ya matukio makuu ya historia ya Uislamu, kutekwa kwa mji wa Makka hutoa mwanga kwenye malengo na shabaha takatifu za Mtume na maadili yake ya hali ya juu sana.

Katika kipindi hiki cha historia, imani njema na uaminifu wa Mtume (s.a.w.w.) na masahaba zake kuhusiana na vifungu vya mkataba wa Hudaybiyah waliousaini, hudhihirika, na zaidi ya hapo ni kuwa kuvunja ahadi na uaminifu kwa Waquraishi kuhusiana na kufungamana na masharti ya mapatano yale hudhihirika pia.

Kuchunguza sehemu hii ya historia kunathibitisha ustadi na busara za Mtume (s.a.w.w.) na sera ya hekima aliyoitumia katika kuiteka ngome ya mwisho na iliyokuwa madhubuti zaidi.

Inaonyesha kwamba mtu huyu wa Allah ameitumia sehemu ya uhai wake kwenye moja ya vyuo vya kijeshi vilivyo vikuu zaidi, kwa sababu alipanga mipango ya kupatia ushindi kama vile afanyavyo kamanda mwenye uzoefu, katika hali ambayo Waislamu waliweza kuupata ushindi huu mkuu bila ya kazi ngumu wala shida.

Hata hivyo, huba ya Mtume (s.a.w.w.) kwa wanadamu na kuwajibika kwake na usalama wa maisha na mali ya maadui zake, nako kunadhihirishwa kwenye kipindi hiki cha historia. Kama tutakavyoona hivi

karibuni, mtu huyu mashuhuri aliyekuwa akionyesha kuona mbele kwake, aliyatupilia mbali maovu ya Waquraishi baada ya kupata ushindi na akatangaza msamaha kwa watu wote. Yafuatayo hapa chini ni maelezo kwa urefu ya tukio hili:

Katika mwaka wa sita Hijiriya, yalifanyika mapatano baina ya machifu wa Kiquraishi na Mtume wa Uislamu (s.a.w.w.) na yakasainiwa na pande zote mbili. Kufuatana na kifungu cha tatu cha mapatano yale Waquraishi na Waislamu walikuwa huru kufanya mapatano na makabila mengine kwa kadiri watakavyopenda.

Kutegemeana na kifungu hiki, kabila la Bani Khuza'ah lilifanya mapatano na Waislamu na Mtume (s.a.w.w.) alichukua jukumu la kuyahami maji yao, nchi yao, uhai wao na mali zao. Kabila la Bani Kananah waliokuwa maadui wa tangu kale wa kabila la jirani yao Bani Khuz?'ah, lilifanya mapatano na Waquraishi. Jambo hili lilitekelezwa kwa mujibu ambao kwamba udumishaji wa amani wa Bara Arabuni kwa jumla utatimia. Kwa mujibu wa mapatano ya Amani ya Hudaybiyah, yale makundi mawili (la Waislamu na marafifiki zao, na Waquraishi na marafiki zao) yasiasi moja dhidi ya jingine na vile vile wasichochee marafiki wa kundi moja kuasi dhidi ya marafiki wa kundi jingine.

Ilipita miaka miwili baada ya kufanyika kwa mapatano haya, na pande zote mbili zilitumia wakati huu kwa amani, na katika miaka iliyofuatia ya mapatano yale Waislamu waliweza kwenda kufanya hija kwenye Ka'abah kwa uhuru kabisa na wakazifanya ibada zao mbele ya maelfu ya waabudu masanamu waliokuwa kwenye kambi ya adui.

Katika mwezi wa Jamadiul–Awwal wa mwaka wa nane Hijiriya Mtume (s.a.w.w.) aliwapeleka askari wenye nguvu 3000 chini ya uongozi wa maafisa watatu wa Uislamu mashujaa kuelekea kwenye mipaka ya Shamu, kwenda kuwaadhibu watawala wa Kirumi kwa kuwaua wahubiri wa Kiislamu wasiokuwa na ulizi kwa namna ya uonevu na ukatili mkubwa. Hawa mashujaa wa Uislamu waliyaokoa maisha yao kwenye msafara huu na si zaidi ya makamanda wao watatu na askari wachache waliuawa, lakini hawakurejea na ushindi uliokuwa ukitegemewa kuletwa na Mujahidiin wa Uislamu, na kazi yao haikuwa tofauti na hali yashambulia na kukimbia.

Kuenea kwa taarifa hii kuliwashawishi Waquraishi nao wakaanza kufikiria kwamba nguvu ya kijeshi ya Waislamu imedhoofika nao wamekwisha kuupoteza moyo wa ushujaa na kujitoa mhanga.

Hivyo wakaamua kuivuruga hali ya hewa ya amani na utulivu. Katika hatua yao ya kwanza waligawa silaha miongoni mwa watu wa kabila la Bani Bakr na kuwachochea kufanya mashambulizi ya usiku dhidi ya Bani Khuz?'ah waliokuwa washirika wa Waislamu, na hatimaye kuwaua baadhi yao na kuwafunga wengine. Hata hivyo, hawakutosheka na hilo tu, bali vilevile kikosi cha Waquraishi kilishiriki kwenye yale mashambulio dhidi ya Bani Khuza'ah. Hivyo waliyavunja masharti ya mapatano ya Amani ya Hudaybiyah na wakaibadili ile amani na utulivu wa miaka miwili kuwa vita na umwagaji wa damu.

Matokeo ya mashambulizi haya ya usiku ni kwamba baadhi ya watu wa kabila hili waliokuwa wamelala wakati ule na waliokuwa wakisali, waliuawa na wengine wakafanywa wafungwa. Wachache wao

waliyatoka majumba yao na wakakimbilia Makka sehemu iliyokuwa ikihesabiwa kuwa sehemu ya amani miongoni mwa Waarabu.
Wale wakimbizi waliokwenda Makka walikwenda nyumbani kwa Budayl bin Warq?1 na kumhadithia kile kisa cha kuhuzunisha cha kabila lao.

Ili kwamba taarifa za msiba wao ziyafikie masikio ya Mtume (s.a.w.w.) walimtuma Amr Sal?m chifu wa kabila lao kwa Mtume (s.a.w.w.).

Alipowasili mjini Madina alikwenda moja kwa moja hadi msikitini na akasimama mbele ya watu, kwa sauti maalum alisoma beti za shairi zenye kuzipasua nyoyo zionyeshazo dhulma iliyotendewa kabila la Bani Khuz?'ah na maombi yao ya msaada, na akamkumbusha Mtume (s.a.w.w.) kuyaheshimu yale mapatano aliyoyafanya baina yake na wao. Alimwomba Mtume (s.a.w.w.) awasaidie na kuilipizia kisasi damu ya wale waliodhulumiwa. Mwishoni mwa shairi hili, alisema:

"Ewe Rasuli wa Allah! Wakati baadhi yetu walipokuwa kwenye ukingo wa maji ya Watiir na wengine walikuwa wakisali, Waquraishi waabudu masanamu, walioyatia saini yale mapatano ya kutoshambuliana kwa kipindi cha miaka kumi, waliwashambulia watu wetu wasio na ulinzi wala silaha wakati wa usiku wa manane na kuwaua ovyo". Aliurudia ubeti huu: "Walituchanja ambapo sisi tulikuwa Waislamu." mara nyingi kiasi cha kuibua hisia na moyo wa askari wa Waislamu wapiganaji wa panga.

Mashairi yenye kuziibua nyoyo ya chifu wa lile kabila yalikuwa na athari zake. Mtume (s.a.w.w.) alimgeukia Amr mbele ya mkusanyiko mkubwa wa Waislamu na akasema: "Ewe Amr bin Sal?m! Tukusaidieni." Jibu hili lenye maamuzi lilileta faraja ya kiakili kubwa sana kwa Amr, kwa sababu alikuwa na uhakika kwamba karibuni tu Mtume (s.a.w.w.) atalipiza kisasi ule msiba waliotiwa Bani Khuza'ah na Waquraishi waliokuwa sababu halisi ya tukio lile la kimsiba.

Hata hivyo, hakuweza kudhania kwamba kazi hii italeta kutekwa kwa mji wa Makkh na mwishilizo wa utawala wa kidhalimu wa Waquraishi.

Mara tu baada ya hapo alifika Budayl bin Waraqa kwa Mtume (s.a.w.w.) pamoja na kikundi cha watu wa kabila la Khuza'ah ili kuomba msaada. Alimwarifu Mtume (s.a.w.w.) kuhusu ushirika wa Waquraishi na Bani Bakr katika kuwapiga na kuwaua watu wa Bani Khuz?'ah, na kisha wakarejea Makka.

Uamuzi Wa Mtume (S.A.W.W.) Wawatia Waquraishi Kiwewe

Waquraishi walijuta mno kuhusiana na yale waliyoyatenda, nao walitambua ya kwamba wamewapa Waislamu udhuru wa hatari mno na wametenda tendo lililouvunja moyo wa yale mapatano na masharti yake. Kwa lengo la kumtuliza Mtume (s.a.w.w.) na kupata uthibitisho wa kuyaimarisha mapatano ya miaka kumi (na kwa mujibu wa maelezo fulani) kwa ajili ya kuyaendeleza,2 walimtuma kiongozi wao Abu Sufyani kwenda Madina ili aweze kuyaficha makosa na uasi wao kwa njia zote ziwezekanazo. Alitoka kwenda Madina na alipokuwa njiani alikutana na Budayl, yule kiongozi wa Bani Khuz?'ah mahali

paitwapo Asfan palipo karibu na Makka. Alimwuliza Badayl kama alikuwa Madina na kama amemweleza Muhammad mambo yaliyotokea karibuni.

Budayl akamweleza ya kwamba alikwenda kuwaona ndugu zake waliodhulumiwa na kuwafariji, na katu hakuwa Madina. Baada ya kuyasema hayo alirejea Makka. Hata hivyo Abu Sufyani alikivunja kinyesi cha ngamia wa Budayl na akaona humo kokwa za tende yenye sifa za tende ya Madina. Hapo akawa na uhakika kwamba Budayl alikwenda Madina kuonana na Mtume (s.a.w.w.).

Abu Sufyani akafika Madina na akaenda moja kwa moja nyumbani kwa binti yake Bibi Ummi Habibah mkewe Mtume (s.a.w.w.).
Alitaka kukaa kwenye mkeka aliokuwa akikalia Mtume (s.a.w.w.), lakini yule binti yake akaukunja. Abu Sufyani akamwambia binti yake: “Je, hukuuona mkeka huo kuwa ni wenye kunifaa au baba yako kufaa kwa mkeka huo?” Binti yake akamjibu, akasema: “Mkeka huu ni maalum kwa ajili ya Mtume, na kwa kuwa wewe ni kafiri, sipendi kwamba mtu aliye kafiri asiye tohara akae kwenye mkeka wa Mtume.”

Hivyo ndivyo hoja ya binti wa mtu aliyekwenda kinyume na Uislamu kwa kipindi kirefu cha miaka ishirini. Hata hivyo, kwa kuwa Bibi huyu mtukufu alilelewa kwenye mahadhi ya Uislamu na fundisho la Upweke wa Allah, mafungamano yao ya kiroho yalikuwa na nguvu mno kiasi kwamba aliifanya kuwa duni ile mielekeo na mivuto yote ya mtoto kwa baba yake, ikilinganishwa na nguvu yake ya kidini.

Abu Sufyani aliingiwa na wasiwasi mwingi kuhusiana na tabia za binti yake aliyekuwa kimbilio lake pekee mle mjini Madina.

Akaitoka nyumba ya binti yake na kwenda kwa Mtume (s.a.w.w.) na kuzungumza naye kuhusu kuendelezwa na kuimarishwa kwa yale mapatano ya Amani. Hata hivyo, ilimbidi kukabiliana na kimya cha Mtume (s.a.w.w.), jambo lililoonyesha kutojali kwa Mtume (s.a.w.w.) juu ya rai ile.

Abu Sufyani alionana na baadhi ya masahaba wa Mtume (s.a.w.w.) ili aweze kumwendea tena kupitia kwao, na kwa njia ile aweze kulifikia lengo lake. Lakini mawasiliano haya nayo hayakuzaa matunda. Mwishowe akaenda nyumbani kwa Sayyidna Ali (a.s.) na akazungumza naye hivi: “Wewe ndiwe mtu uliye karibu zaidi na mimi mjini humu kwa sababu u ndugu yangu. Hivyo basi, ninakuomba uniombee kwa Mtume.” Sayyidna Ali (a.s.) akamjibu akasema: “Sisi katu hatuingilii katika mambo ambayo tayari Mtume kaishafanya uamuzi.”

Baada ya kukatishwa tamaa na upande wa Sayyidna Ali (a.s.), alimgeukia Bi. Fatimah Zahra (a.s.) mkewe Sayyidna Ali na binti wa Mtume (s.a.w.w.), na akaona kwamba wanawe wawili Hasan na Husain (a.s.) walikuwa karibu naye. Ili kuuamsha mvuto wake alimwambia: “Ewe binti wa Mtume! Yawezekana kwamba unaweza ukawaeleza wanao kuwapatia watu wa Makka kimbilio na wao kuwa machifu wa Uarabuni hadi mwisho wa muda na kuwako kwa dunia.” Bibi Zahra (a.s.) aliyekuwa akiitambua nia mbaya ya Abu Sufyani, mara moja akasema: “Jambo hili liko mikononi mwa Mtume, na wanangu hivi sasa hawana cheo cha aina hiyo.”

Alirejea tena kwa Sayyidna Ali (a.s.) na kusema: “Mpendwa Ali! Hebu niongoze kwenye jambo hili.” Sayyidna Ali (a.s.) akamjibu akasema: “Hakuna njia ya kutokea kwenye tatizo hili, ila kwamba uende msikitini na kutangaza tangazo la usalama kwa Waislamu.” Akauliza: “Je, kama nikifanya hivyo, itakuwako faida yoyote ile?” Ali (a.s.) akamjibu akasema: “Si sana, lakini mimi sidhani kama kuna kitu kingine hivi sasa.”

Abu Sufyani aliyekuwa akiutambua ukweli, unyoofu na usafi wa Sayyidna Ali (a.s.) alikwenda msikitini na kuyatekeleza yale aliyokuwa akiyafikiria.

Kisha alitoka msikitini mle na akaenda Makka. Kufuatana na taarifa alizowapa wale machifu wa Waquraishi kuhusu kile alichokitenda kule Madina, vile vile aliutaja ushauri aliopewa na Ali, na akasema: “Kufuatana na ushauri niliopewa na Ali, nilikwenda msikitini na nikatangaza usalama kwa Waislamu.” Wale waliokuwapo pale wakamwambia: “Ushauri wa Ali haukuwa chochote ila ni mzaha, kwa sababu Mtume hakulisikizi tangazo lako la usalama kwa Waislamu na tangazo la upande mmoja halina faida yoyote.” Kisha wakafanya mikutano mingine zaidi ili kupata njia ya kuwatuliza Waislamu.3

Jasusi Akanaswa

Maisha yote ya Mtume (s.a.w.w.) yaonyesha kwamba daima alikuwa akijitahidi kwamba adui asalimu amri kwenye ukweli na katu hakufikiria kulipiza kisasi kwa adui au kumwangamiza. Katika vita nyingi ambazo Mtume (s.a.w.w.) alishiriki yeye mwenyewe binafsi au alituma kikosi kwenda kupigana, daima lengo lake lilikuwa kwamba mipango ya maadui iweze kushindwa, umoja wao ukome na watu wao watawanyike. Hii ni kwa sababu alitambua kuwa, vizuizi vilivyoko kwenye njia ya Utangazaji wa Uislamu vikiondolewa hoja za Uislamu zenye nguvu zitafanya mvuto wake katika mazingira huru, na kama wale watu ambao mkusanyiko wao na uundaji wa mifarakano ulizuia kupenya kwa utangazaji wa Uislamu wangelinyang’anywa silaha na kukoma kuwa katika hali ya vita na wasiweke akilini mwao matumaini ya kupata ushindi juu ya Uislamu, basi watalazimika kuvutika kuelekea kwenye Uislamu na kwa kawaida watakuwa wenye kuunga mkono Uislamu na marafiki.

Hivyo, mataifa mengi yaliyoshindwa ambayo yalizidiwa kwa nguvu za kijeshi za Uislamu, baadae yatayafikiria mafunzo yake matukufu katika mazingira ya mbali na fujo na ghasia na hatimaye yatavutika kwenye dini hii na watajishughulisha na utangazaji wa ile dini ya Upweke wa Allah.

Wakati wa kutekwa kwa mji wa Makka, jambo hili lilijitokeza katika mdhihiriko wake katika hali yake ya ukamilifu. Mtume (s.a.w.w.) alitambua kwamba, iwapo atauteka Mji wa Makka, akamnyang’anya silaha adui na akayafanya mazingira kuwa ya amani, wale watu waliokuwa maadui wake wakubwa wakati ule mara moja watakuwa waumini waaminifu wa Uislamu. Hivyo basi, ilikuwa muhimu kushinda na kumtiisha adui lakini si kumwangamiza na vile vile kuzuia umwagaji wa damu kadiri iwezekanavyo.

Ili kulifikia lengo hili takatifu (kumtisha adui bila ya umwagaji wa damu), ile kanuni ya kumshitukiza adui haina budi kufuatwa, na adui huyu hana budi kushambuliwa na kunyang’anywa silaha kabla ya kufikiria

kukusanya majeshi na kujihami. Hata hivyo, kanuni ya kushitukiza dhidi ya adui inaweza kutekelezwa wakati siri zote za jeshi la Waislamu zinapobakia kuwa salama na adui asijue kama Mtume (s.a.w.w.) ameamua kushambulia au alikuwa akifikiria tu juu ya jambo lile. Vile vile ilikuwa muhimu kwamba yule adui asiyatambue matendo na mbinu za jeshi la Waislamu.

Mtume (s.a.w.w.) aliamrisha matayarisho ya watu wote kwenda kuuteka mji wa Makka na kuitiisha ngome ya ibada ya masanamu iliyokuwa madhubuti zaidi. Lengo lake lilikuwa ni kuipindua serikali ya kidhalimu ya Waquraishi iliyokuwa kizuizi kikuu katika maendeleo ya Uislamu. Vile vile alimwomba Allah kwamba majasusi wa Waquraishi wasivitambue vitendo vya Waislamu.

Ili kuidumisha siri kamili njia zote zilizokuwa zikielekea Makka zililindwa na Waislamu walioteuliwa kwa lengo hili, na utawala madhubuti ulifanyika kuhusiana na upitaji wa watu.

Ilikuwa bado askari wa Uislamu hawajaondoka pale Malaika Mkuu Jibriil alipomwarifu Mtume (s.a.w.w.) kwamba mjinga mmoja aliyeichukua nafasi yake kwenye safu za Waislamu amewaandikia barua Waquraishi na amempa mwanamke mmoja barua ile aitwaye Sarah ili awapelekee kwa malipo ya mshahara, na kwenye barua ile baadhi ya siri za kijeshi za Uislamu ikiwa ni pamoja na shambulio lao alilokusudia kulifanya hivi karibuni dhidi ya mji wa Makka, limefichuliwa ndani ya barua hiyo.

Sarah alikuwa msichana mwimbaji wa mjini Makka ambaye katika nyakati fulani fulani, vile vile aliimba nyimbo za maombolezo kwenye hafla za maombolezo za Waquraishi. Baada ya vita ya Badr, kazi yake mle mjini Makka ililegalega kwa sababu kutokana na idadi kubwa ya watu muhimu kuuawa kwenye vita vile, Makka ilizama kabisa kwenye huzuni, na haukuwepo tena wakati wa hafla za muziki na anasa. Zaidi ya hapo, ili ghadhabu na mfundo wa Waquraishi ubakie, tamaa yao ya kulipiza kisasi isife, uimbaji wa nyimbo za huzuni ulipigwa marufuku.

Kutokana na sababu tuliyoitaja hapo juu, Sarah alikuja Madina baada ya miaka miwili tangu kupiganwa kwa vita vya Badr. Mtume (s.a.w.w.) alipomwuliza kama alishasilimu, akasema: “Hapana”. Kisha Mtume (s.a.w.w.) akamwuliza ni kwa nini kaja Madina.
Kwa swali hili alisema: “Kwa upande wa asili na nasaba, ninatokana na Waquraishi. Hata hivyo, baadhi yao wameuawa na wengine wamehamia Madina. Baada ya Vita vya Badr kazi yangu ilipungua nguvu nami nimekuja hapa kutokana na shida.” Hapo Mtume (s.a.w.w.) aliamrisha kwamba upesi sana apewe chakula na nguo kwa ajili ya baridi kadiri ihitajikavyo.

Sarah alifanyiwa matendo ya huruma sana na Mtume (s.a.w.w.), lakini kwa kupata ujira wa dinari kumi kutoka kwa Hatib bin Abi Balta’ah, aliamua kufanya ujasusi dhidi ya Uislamu na kuwapelekea Waquraishi barua yake yenye taarifa zihusuzo kuwako tayari kwa Waislamu kuuteka mji wa Makka. Mtume (s.a.w.w.) aliwaita askari watatu mashuja na kuwaamrisha waende Makka kumkamata yule mwanakme popote pale watakapomwona na kuichukua ile barua.

Watu wale waliopewa jukumu lile walikuwa ni Sayyidna Ali (a.s.), Zubayr na Miqdad. Walimkamata mwanamke yule mahali paitwapo Rauzat Khakh na wakaipekua mizigo yake kwa makini lakini

hawakupata kitu. Vile vile yule mwanamke alikataa kabisa kwamba alichukua barua yoyote ile kutoka kwa Hatib. Sayyidna Ali (a.s.) akasema: “Ninaapa kwa jina la Allah! Katu Mtume wetu hasemi uwongo. Huna budi kuitoa barua hiyo au la, tutaichukua kutoka kwako kwa njia zozote zile ziwezekanazo!”

Wakati ule Sarah alitambua kwamba Sayyidna Ali (a.s.) alikuwa askari asiyekata tamaa juu ya upekuzi ule hadi aitekeleze amri ya Mtume (s.a.w.w.). Hivyo basi alimwomba awe mbali naye. Kisha akaitoa barua ndogo kutoka kwenye msuko wa nywele zake na kumpa Sayyidna Ali (a.s.).

Mtume (s.a.w.w.) aliingiwa na wasiwasi kuona kwamba jambo lile limetendwa na mwislamu, mwenye rekodi ndefu ya huduma na aliyekuwa na shauku ya kuusaidia Uislamu hata kwenye hali ngumu. Hivyo basi alimwita Hatib na akamtaka aeleze msimamo wake. Aliapa kwa jina la Allah na Mtume Wake na akasema: “Hakuna kulegalega kulikotokea kwenye imani yangu. Hata hivyo, ninaishi peke yangu hapa Madina, na watoto wangu na ndugu zangu wanasumbuliwa na shinikizo la mateso huko Makka mikononi mwa Waquraishi. Hivyo basi, lengo langu katika kuipeleka taarifa hii lilikuwa kwamba Waquraishi wapunguze mateso wawatendeayo watu wangu.”

Udhuru alioutoa Haatib waonyesha kwamba, ili kupata taarifa kuhusiana na siri za Waislamu, machifu wa Waquraishi waliwatesa ndugu za Waislamu waliokuwa wakiishi mjini Makka na kuweka kuwa ni sharti la uhuru wao pindi wapatapo taarifa muhimu kutoka kwa ndugu zao walioko Madina.

Ingawa udhuru alioutoa Hatib haukuwa na msingi mzuri, Mtume (s.a.w.w.) aliukubali kutokana na sababu mbalimbali, ikiwa ni pamoja na huduma zake za muda mrefu alizozitoa katika njia ya Uislamu, na akamwachia.

Wakati Umar alipoomba ruhusa kutoka kwa Mtume (s.a.w.w.) kukidengua kichwa cha Hatib, Mtume (s.a.w.w.) alimjibu akisema: “Ninamwachia kwa sababu alishiriki kwenye Vita vya Badr na siku moja alikuwa ni sababu asili ya baraka za Allah.”

Hata hivyo, ili kuhakikisha kwamba tukio la aina hii halirudiwi tena, aya tisa za kwanza za *Surat al-Mumtahinah* zilifunuliwa:4 **“Enyi mlioamini! Msiwafanye adui Zangu na adui zenu kuwa marafiki .....” (Sura al- Mumtahinah, 60:1).**

Mtume (S.A.W.W.) Na Waislamu Waenda Makka

Katika kuzizingatia kanuni za mashambulizi ya kuotea, muda wa kuondoka, utaratibu na lengo la safari ile vilielezwa na Mtume (s.a.w.w.). Amri ile ilitolewa mnamo mwezi 10 kumi Ramadhani, mwaka wa nane Hijiriya, ingawa Waislamu wa Madina na viungani mwake walipewa maelezo yake mapema kabla ya hapo ili kujiweka tayari.
Katika siku ambayo Mtume (s.a.w.w.) aliondoka Madina, alimteua mtu mmoja aliyeitwa Abu Ruhm Ghifari kuwa kaimu wake mjini humo na akalikagua jeshi lake nje ya mji wa Madina. Alipokuwa kaishasafiri umbali fulani kutoka Madina aliomba maji mahali paitwapo Kadid na akafungua swaumu

yake na kisha akawaamrisha watu wote kufanya vivyo hivyo.

Wengi wao walizivunja swaumu zao, lakini wengine wakajizuia kufanya hivyo kwa kudhania kwamba kama wakifanya Jihadi wakiwa wamefunga watapata thawabu nyingi. Watu hawa wajinga hawakutambua kwamba Mtume huyo huyo ambaye aliamrisha kufunga mwezi wa Ramadhani vilevile hivi sasa ametoa amri ya kuivunja saumu yake, na kama yeye yu kiongozi wa kuelekea kwenye ustawi na ukweli, basi amri zake zote mbili zilikuwa kwa ajili ya mema ya watu na haukuwako ubaguzi kwenye amri zake.

Mtume (s.a.w.w.) alichukia alipogundua kwamba baadhi ya watu walikataa amri yake na akasema: “Watu hawa ni wenye dhambi na waasi.”5

Kuutafuta ubora kama huo na kumtangulia Mtume (s.a.w.w.) ni aina ya upotovu kutoka kwenye ukweli na kunaonyesha utovu wa imani ya watu wale juu ya Mtume (s.a.w.w.) na dini yake. Hivyo basi, Qur’ani Tukufu imewakemea watu hawa na inasema:

يَا أَيُّهَا الَّذِينَ آمَنُوا لَا تُقَدِّمُوا بَيْنَ يَدَيِ اللَّهِ وَرَسُولِهِ ۖ وَاتَّقُوا اللَّهَ ۖ إِنَّ اللَّهَ سَمِيعٌ عَلِيمٌ {1}

***“Enyi mlioamini! Msitangulie mbele ya Allah na Mtume Wake, na mcheni Allah. Hakika Allah ni Mwenye kusikia Mwenye kujua.”* (*Sura al-Hujurat, 49:1*).**

Abbas bin Abdul Muttalib alikuwa mmoja wa wale Waislamu waliokuwa wakiishi mjini Makka. Alikuwa akiishi pale chini ya ushauri wa Mtume (s.a.w.w.), naye alikuwa akimwarifu juu ya maamuzi yaliyochukuliwa na Waquraishi. Aliudhihirisha Uislamu wake baada ya Vita ya Khaybar, lakini uhusiano wake na machifu wa Waquraishi uliendelea kudumu. Aliamua kuondoka Makka akiwa ni familia ya Kiislamu ya mwisho kwenda kuishi Madina.

Ilikuwa ni kwenye siku za Mtume (s.a.w.w.) kwenda Makka pale Abbas alipoondoka Makka kwenda Madina na akakutana na Mtume (s.a.w.w.) njiani mahali paitwapo Ju’fah. Kuwepo kwa Abbas kulithibitika kuwa ni kwenye faida kwa ajili ya kutekwa kwa mji wa Makka na hivyo kulitoa faida kwa makundi yote mawili (Waislamu na Waquraishi). Inawezekana kwamba kama asingelikuwepo yeye, basi kutekwa kwa mji wa Makka kusingelitimia bila ya upinzani wa Waquraishi. Hivyo basi, inawezekana kwamba kutoka kwake mle mjini Makka kwenda madina kulifanyika kutokana na maelezo ya Mtume (s.a.w.w.) ili kwamba aweze kulifanya jukumu la kiusuluhishi kwenye tukio hili.

Kuonyesha Huruma Uwapo Mwenye Mamlaka Na Cheo

Maisha yaliyopita ya Mtume (s.a.w.w.) yenye kung’ara, tabia zake zenye kuridhisha, na ukweli na

unyoofu wake vilikuwa maarufu sana kwa watu wa familia yake na ndugu zake, kwa ujumla ni kuwa jamaa zake wote walifahamu kwamba aliishi maisha ya heshima na katu hakupata kutenda dhambi yoyote au mashambulizi au kuzungumza lolote lile lililo la uwongo. Hivyo basi, tangu siku ya kwanza ya mwito kwa watu wote, karibuni watu wote wa familia ya Bani Hashim waliuitikia mwito wake na wakajikusanya na kumzunguka kama nondo wauzungukavyo mshumaa.

Mustashrik mmoja wa Kiingereza asiye na upendeleo, ameuchukulia ukweli huu kuwa ni ishara ya usafi na uchamungu wa Mtume (s.a.w.w.) na anasema: “Kila mtu vyovyote vile awavyo mwangalifu na mwenye kujihadhari, hawezi kuwaficha watu wa familia yake na ndugu zake mambo yote ya maishani mwake.
Kama Muhammad angalikuwa na fikira na tabia mbaya, vitu hivi visingeliweza kufichikana mbele ya ndugu zake nao wasingaliweza kuvutika naye upesi sana.”6

Hata hivyo, vilevile wako watu wachache miongoni mwa Bani Hashim waliokataa kumwamini. Mbali na Abu Lahab majina ya watu wawili wa aina hiyo, Abu Sufyani bin Harith na Abdullah bin Abi Umayah, yanaweza kutajwa kuhusiana na jambo hili. Waliudhihirisha uadui na ukaidi dhidi yake na sio tu kwamba hawakumwamini lakini vilevile walikuwa kizuizi katika njia ya ukweli na kuziumiza fikara za Mtume (s.a.w.w.).

Abu Sufyani alikuwa mwana wa Harith, ami yake Mtume (s.a.w.w.) na vilevile alikuwa nduguye wa kunyonya. Kabla ya kuanza kwa Utume, Abu Sufyani alimpenda sana Mtume (s.a.w.w.) lakini akawa adui kwake baada ya hapo. Abdullah alikuwa kaka yake Ummi Salmah (aliyekuwa mke wa Mtume) na mwana wa Atik Shangazi yake Mtume (s.a.w.w.) na binti wa Abdul Muttalib.

Hata hivyo, kuenea kwa Uislamu kwenye Rasi ya Uarabuni kuliwafanya hawa watu wawili kuamua kuutoka mji wa Makka na kujiunga na Waislamu. Wakati Mtume (s.a.w.w.) alipokuwa njiani kwenda mji wa Makka, hawa wawili walikutana na jeshi la Uislamu mahali paitwapoo Thanyatul Uqaab au Nabque ‘Uqaab. Pamoja na kusisitiza kwao, lakini Mtume (s.a.w.w.) alikataa kukutana nao. Na hata pale Ummi Salmah alipowaombea kwa mapenzi, Mtume (s.a.w.w.) alikataa mapendekezo yake, na akasema: “Ni kweli kwamba Abu Sufyani yu binamu yangu, lakini amenisumbua sana. Na yule mtu wa pili ndiye mtu yule aliyeniomba mambo ya kijinga7 naye amewazuia watu kusilimu.”

Sayyidna Ali Amirul–Mu’minin (a.s.) aliyekuwa akizifahamu vizuri tabia za Mtume (s.a.w.w.) na jinsi ya kuibua mwelekeo wake, aliwaambia wale watu wawili: “Nendeni mkakae mbele ya Mtume na itamkeni ile kauli waliyoitamka nduguze (Nabii) Yusuf walipoomba msamaha (kwa ndugu yao Nabii Yusuf a.s). Nduguze Nabii Yusuf walipokuwa wakiomba radhi, walisema: “Tunaapa kwa jina la Allah! Yeye (Allah) Amekupa upendeleo juu yetu nasi tumetenda dhambi.”

Naye Nabii Yusuf alipoyasikia maneno haya, aliwasamehe akisema: “Leo hapana lawama juu yenu. Allah atakusameheni, Naye ni Mwingi wa kurehemu kuliko wote wanaorehemu.”8

Kisha Amirul–Mu’minin aliongeza kusema: “Kama mkiitamka ile kauli ya awali bila shaka atakujibuni kwa

ile kauli ya pili, kwa sababu yeye yu mtu asiyekuwa tayari hata kidogo kwamba mtu awe mkunjufu zaidi yake.”

Wale watu walifanya kama walivyoshauriwa na Sayyidna Ali (a.s.) na Mtume (s.a.w.w.) naye aliwasamehe kama alivyofanya Nabii Yusuf (a.s.). Kisha wote wawili wakalivaa vazi lihitajikalo kwa ajili ya Jihad, na wakabakia kuwa imara kwenye dini yao hadi mwishoni mwa maisha yao. Ili kuweza kufanya masahihisho ya yale aliyoyatenda huko nyuma, Abu Sufyani aliimba shairi la wasifu, ambalo ubeti wake wa kwanza ulisema: “Ninaapa kwa maisha yako! Siku nilizoichukulia bendera begani mwangu ili kwamba jeshi la Laat (sanamu lililokuwako mjini Makka) liweze kushinda dhidi ya jeshi la Muhammad, nilikuwa kama msafiri wa usiku aliyetatanishwa, anayepapasa gizani, lakini huu sasa ndio wakati ninapotakikana kuwa chini ya himaya ya mwongozo wa Mtume (s.a.w.w.).”

Ibn Hisham anaandika9 kwamba binamu yake Mtume (s.a.w.w.), Abu Sufyani bin Harith alimpelekea ujumbe Mtume (s.a.w.w.) akisema: “Kama huikubali imani yangu (yaani kusilimu kwangu) nitaushika mkono wa mwanangu mdogo na kwenda jangwani.” Na ili kuuibua mwelekeo wa huruma wa Mtume (s.a.w.w.), Bibi Ummi Salamah alisema:
“Mara kwa mara nimekusikia ukisema kwamba Uislamu huyafunika matendo ya wakati uliopita.” Kwa msingi huu, Mtume (s.a.w.w.) aliweza kukaribiwa na watu hao wawili.10

Mbinu Zenye Kuvutia Za Jeshi La Waislamu

Murruz Zahran iko kilometa chache kutoka Makka. Mtume (s.a.w.w.) alilionga jeshi lake lenye askari elfu kumi wenye nguvu hadi kwenye mpaka wa Makka ili kwamba Waquraishi na majasusi wao na mawakala wao wasiweze kutambua kwenda kwao pale.

Ili kwamba wakazi wa Makka waweze kusalimu amri bila ya upinzani na ile ngome kubwa na kituo kitakatifu kitekwe bila ya umwagaji damu, na ili kujenga hofu nyoyoni mwa wakazi wa Makka, Mtume (s.a.w.w.) aliwaamrisha Waislamu wawashe moto kwenye sehemu za miinuko. Vilevile aliamrisha kuwaogofya zaidi watu wa Makka kwa kumfanya kila mtu akoke moto wake ili ule moto na miali iangaze vilima vya jirani na sehemu za miinuko.

Waquraishi na washiriki wao walikuwa wamelala fofofo. Hata hivyo, ile miali iliyozipa sehemu zote za miinuko umbo la moto mkubwa ambao nuru yake ilizifikia nyumba za watu wa Makka, ulijenga hofu na wasiwasi nyoyoni mwao na kuzivutia fikara zao kwenye miinuko ile. Wakati ule ule machifu wa Waqurauishi kama vile Abu Sufyani bin Harb na Hakam bin Hiz?m walitoka mji wa Makka kwa ajili ya kufanya uchunguzi na wakajishughulisha na uchunguzi na ugunduzi.

Abbas bin Abdul Muttalib aliyekuwa akifuatana na Mtume (s.a.w.w.) alifikiria kwamba, kama jeshi la Waislamu likipingwa na Waquraishi watu wengi kutoka miongoni mwa Waquraishi watauwawa. Hivyo basi, aliamua kufanya kazi fulani itakayokuwa na faida kwa pande zote mbili na kuwashawishi Waquraishi wasalimu amri.

Alimpanda nyumbu mweupe wa Mtume (s.a.w.w.) na akaenda Makka wakati wa usiku wa manane ili kupitia kwa wakata miba na watema kuni aweze kuwaarifu machifu wa Waquraishi kuhusu kuzingirwa kwa Makka na jeshi la Waislamu, na kuifanya nguvu na moyo wa upiganaji vita wa Waislamu ufahamike kwao, na watambue ya kwamba wao (Waquraishi) hawana njia nyingine ila kusalimu amri. Hata hivyo, kwa mbali aliyasikia mazungumzo yafuatayo kati ya Abu Sufyani na Budayl Warq?;

Abu Sufyan: Sijawahi kuona moto mkubwa na jeshi kubwa kama hili.

Budayl bin Warqa': Hao ni watu wa kabila la Khuza'ah, waliojitayarisha kwa ajili ya vita.

Abu Sufyan: Khuz?'ah ni wachache mno kuliko kiasi cha kuweza kuwasha moto mkubwa kiasi hiki au kuunda jeshi kubwa kama hili!

Hapo Abbas akayaingilia mazungumzo yao na akamwita Abu Sufyani na kumwambia: "Ewe Abu Hanzalah!"11 Upesi Abu Sufyani akaitambua ile sauti ya Abbas na kujibu: "Ewe Abul Fazal12, umesema nini?" Abbas akasema: "Ninaapa kwa jina la Allah! Udhia wote huu umeletwa na mashujaa wa Mtume wa Allah. Amewajia Waquraishi na jeshi kubwa lenye nguvu na haiwezekani hata kidogo Waquraihi kuwazuwia."

Maneno ya Abbas yalimfanya Abu Sufyani atetemeke kwa nguvu mno. Akiwa mwenye hali ya woga, alimgeukia Abbas na kusema: "Wazazi wangu wawe fidia kwako! Dawa hasa ni nini?" Abbas akamjibu akasema: "Dawa iliyopo ni kwamba, wewe ufuatane nami hadi kwa Mtume (s.a.w.w.) na uombe usalama kwake, au sivyo uhai wa Waquraishi wote utakuwa hatarini."

Kisha akamfanya aketi kwenye kiti cha nyuma cha nyumbu wake na akaenda naye kwenye kambi ya jeshi la Uislamu. Wale watu wawili wengine (Budayl bin Warqa na Hakam bin Hizam), waliokuja na Abu Sufyani kufanya uchunguzi wakarudi Makka.

Sasa kama iwezavyo kuonekana, Abbas alifanya kazi kwa faida ya Uislamu na akamfanya Abu Sufyani kuwa na woga mno juu ya nguvu za jeshi la Waislamu kiasi kwamba hakuweza kulifikiria jambo lolote ila kusalimu amri. Na kitendo chake kilichokuwa muhimu sana kilikuwa kwamba hakumruhusu Abu Sufyani arudi Makka bali alimleta kambini kwa Waislamu wakati wa usiku wa manane na hivyo kamtenga na pande zote mbili. Angelirejea Makka, basi ingeliwezekana kwamba angeshawishiwa na watu wenye siasa kali na wangeweza kufanya upinzani wa masaa machache.

Abbas Amfanya Abu Sufyan Apite Kwenye Kambi Ya Waislamu

Yule ami yake Mtume (s.a.w.w.) alimpanda nyumbu maalum wa Mtume (s.a.w.w.) na Abu Sufyani alifuatana naye. Alimpitisha baina ya ule moto mkubwa na lile jeshi kubwa lenye askari waendao kwa miguu na wenye kuwapanda wanyama. Wale walinzi wa doria walimtambua Abbas pamoja na yule nyumbu maalum wa Mtume (s.a.w.w.), na hivyo basi wakampisha apite, macho ya Umar yalimwangukia Abu Sufyani akiwa ameketi kwenye kiti cha nyuma cha nyumbu wa Abbas, na hapo akataka kumuuwa

(Abu Sufyani) mara moja. Hata hivyo, kwa vile ami yake Mtume (s.a.w.w.) amempa hifadhi, yeye (Umar) akajizuia kufanya hivyo. Hatimaye Abbas na Abu Sufyani wakalifikia hema la Mtume (s.a.w.w.). Ami yake Mtume (s.a.w.w.) alipiga hodi na kisha akaingia. Hapo yalitokea mabishano makali baina ya Abbas na Umar mbele ya Mtume (s.a.w.w.). Umar alishikilia kwamba kwa vile Abu Sufyani alikuwa adui wa Allah hana budi kuuawa mara moja, ambapo Abbas alisema kwamba amempa hifadhi. Mtume (s.a.w.w.) aliwanyamazisha kwa kumwomba Abbas amweke Abu Sufyani kwenye hema wakati wa usiku ule na kumleta mbele ya Mtume (s.a.w.w.) asubuhi yake.

Abu Sufyan Afika Mbele Ya Mtume (S.A.W.W)

Kulipokucha Abbas alimleta Abu Sufyani mbele ya Mtume (s.a.w.w.) wakati ule Muhajiriin na Ansar walikuwa karibu na Mtume (s.a.w.w.). Macho ya Mtume (s.a.w.w.) yalipomwangukia Abu Sufyani, alisema: “Je, bado haujawadia wakati wa wewe kushuhudia ya kwamba hakuna mungu ila Allah?” Abu Sufyani akajibu akasema: “Wazazi wangu wawe fidia kwako! Wewe ni mvumilivu, mkarimu, na mpole kwa ndugu zako, kiasi gani! Sasa nimetambua kwamba kama angekuwako mungu ghairi ya Allah, hadi sasa angelifanya lolote lile kwa faida yetu.” Mtume (s.a.w.w.) alipoona kwamba ameushuhudia Upweke wa Allah, aliongeza kusema: “Je, wakati bado haujawadia wa wewe kutambua kwamba mimi ni Mtume wa Allah?” Kauli ya kwanza, akasema: “Wewe ni mvumilivu, mkarimu, na mpole kwa ndugu zako, kiasi gani! Hivi sasa bado ningali ninawaza juu ya Utume wako.”

Abbas alijihisi kuudhishwa na kule kuidhihirisha shaka yake (juu ya Utume wa Muhammad) na akasema: “Kama hutasilimu uhai wako utakuwa hatarini. Hivyo basi, huna budi kuushuhudia Upweke wa Allah na Utume wa Muhammad upesi sana kwa kadiri iwezekanavyo.” Abu Sufyani aliufuata ushauri ule na akajiunga na safu za Waislamu.

Abu Sufyani alisilimu kutokana na hofu, na imani ya aina hii haikuafikiana na malengo ya Uislamu hata kidogo, lakini katika hali hii ilifaa kwamba Abu Sufyani ajiunge na Waislamu kwa vyovyote vile iwavyo, ili kwamba kile kizuizi kikuu kilichoko kwenye njia ya watu wa Makka katika kusilimu kiondoke, kwa sababu yeye na wale walio mfano wake (yaani Abu Jahl, Ikrimah, Safwaan bin Umayah n.k) walikuwa ndio watu walioijenga hofu na woga tangu zamani na hakuna yeyote aliyeweza kuwa na moyo wa kuweza kuufikiria Uislamu au kuonyesha mwelekeo kwenye dini hii. Hata kama kusilimu kwa Abu Sufyani kusiwe na faida yoyote kwake, kulikuwa na faida mno kwa Mtume wa Uislamu (s.a.w.w.) pamoja na wale watu waliokuwa ndugu zake.

Hata hapo Mtume (s.a.w.w.) hakumwachilia Abu Sufyani, kwa kuwa hakuwa na uhakika juu ya matendo yake hadi Makka ilipotekwa. Hivyo basi, akamuelekeza kwamba kwa sababu zitakazotajwa baadae, hana budi kumzuia ndani ya njia nyembamba ya bonde. Abbas alimgeukia Mtume (s.a.w.w.) na kumwambia: “Abu Sufyani yu mtu mwenye tamaa ya cheo katika jamii na kwamba hivi sasa mambo yamegeuka kiasi hiki, ni bora umpe cheo fulani.”
Licha ya kweli kwamba katika kipindi cha miaka ishirini Abu Sufyani ameleta madhara makubwa sana

kwa Uislamu na Waislamu, Mtume (s.a.w.w.) akiyazingatia maslahi makubwa, alimpa Abu Sufyani cheo na akatamka kauli ifuatayo ionyeshayo ukuu wa roho yake (s.a.w.w.):

“Abu Sufyani anapewa mamlaka kuwathibitishia watu kwamba yeyote akimbiliaye kwenye maeneo ya Masjidul Haram au akaziweka chini silaha zake na akatangaza kusalimu amri au akajifungia nyumbani kwake au akakimbilia nyumbani kwa Abu Sufyani au nyumbani kwa Hakim bin Hiz?m, atasalimika kutokana na usumbufu wa jeshi la Uislamu.”13

Makka Yasalimu Amri Bila Ya Kumwaga Damu

Jeshi kuu la Uislamu lilikuwa limefika karibu na Makka. Hata hivyo Mtume (s.a.w.w.) alipenda kwamba auteke mji ule bila ya upinzani wowote au kumwaga damu na adui asalimu amri bila ya masharti yoyote. Miongoni mwa visababisho vya hali hiyo, ukiachilia mbali kujificha na mashambulizi ya kuotea yaliyosaidia sana katika kulifikia lengo hili, kingine kilikuwa kwamba, Abbas, ami yake Mtume (s.a.w.w.) alikwenda Makka akiwa ni ishara ya hisani kwa Waquraishi na kumleta Abu Sufyani kwenye kambi ya Kiislamu, kwani machifu wa Waquraishi hawakuweza kuchukua uamuzi wa mwisho akosekanapo Abu Sufyani.

Abu Sufyani alipojisalimisha mbele ya ukuu usio kifani wa Mtume wa Uislamu (s.a.w.w.), Mtume aliamua kupata faida kubwa katika kuwaogofya waabudu masanamu kwa kadiri iwezekanavyo kutokana na Abu Sufyan kuwako kwake pale. Hivyo basi alimtaka Abbas kumtia kizuizini kweye njia nyembamba ya bonde ili kwamba vikosi vya lile jeshi la Uislamu viweze kupita karibu yake na zana zao zote, naye aweze kuiona ile nguvu ya Uislamu na kisha atakaporejea Makka, aweze kueleza kuhusu jeshi la Uislamu na awazuie wasifanye upinzani. Baadhi ya vikosi vya Uislamu vilikuwa kama ifuatavyo hapa chini:

1. Kundi la askari elfu moja wenye nguvu, wa kabila la Bani Salim chini ya uongozi wa Khalid bin Walid, lililokuwa na bendera mbili. Moja ya bendera hizi ilishikwa na Abbas bin Mird?s na nyingine ilishikwa na Miqdadi.

2. Vikosi viwili vya mashujaa mia tano vilivyokuwa chini ya uamiri jeshi wa Zubayr Aww?m aliyekuwa na bendera nyeusi mkononi mwake. Wengi wa askari wa vikosi hivi viwili walikuwa ni Muhajiriin.

3. Kikosi chenye nguvu cha askari mia tatu wa kabila la Ghif?r chini ya uamiri jeshi wa Abu Dharr Ghif?ri aliyekuwa ameishika bendera.

4. Kikosi chenye nguvu cha askari mia nne cha kabila la Bani Salim kilichokuwa chini ya uamiri jeshi wa Yazid mwana wa Khusayb, aliyekuwa ameichukua bendera.

5. Vikosi viwili vyenye askari mia tano wa kabila la Bani Kaab vilivyokuwa chini ya uamiri jeshi wa Busr bin Sufyan, ambaye naye alikuwa kaishika bendera.

6. Kundi la askari elfu moja wenye nguvu wa Bani Muzaynah lililokuwa na bendera tatu. Bendera hizi zilikuwa mikononi mwa Nu'm?n bin Maqran, Bilal bin Harith na Abdullah Amr.

7. Kundi lenye askari mia nane la kabila la Bani Juhaynah, lilikuwa na bendera nne zilizoshikwa na Ma'bad bin Khalid, Suwayd bin Sakhra, Raafi bin Makith na Abdullah Badr.

8. Makundi mawili ya askari mia mbili wa makabila ya Bani Kananh, Bani Layth na Bani Hamzah, wakiwa chini ya uamiri jeshi wa Abu W?qid Laythi aliyekuwa akiishika bendera.

9. Kikosi chenye askari mia tatu wa kabila la Bani Ashja', kilichokuwa kikichukua bendera mbili. Moja ya bendera hizi ilishikwa na Maqal bin Sanan na nyingine ilishikwa na Na'im bin Mas'ud.

Vikosi hivi vilipokuwa vipikipita mbele ya Abu Sufyani, upesi sana akataka maelezo kutoka kwa Abbas kuhusu vikosi hivi, na Abbas akampa jibu. Kitu kilichoongeza utukufu wa jeshi hili lenye utaratibu mwema kilikuwa kwamba wale makamandda wa jeshi walipofika mbele ya Abbas na Abu Sufyaan waliitamka Takbir *"Allahu Akbar"* mara tatu kwa sauti kubwa na baada ya hapo askari nao waliitamka mara tatu kwa sauti kubwa kwa njia ya ibada za Kiislamu.

Hii Takbir ilipiga mwangwi kwenye mabonde ya Makka kwa jinsi ambayo marafiki walivutiwa mno na ile nidhamu ya Uislamu, na maadui walijawa na hofu na woga mwingi. Abu Sufyani alikuwa akingojea bila ya subira kukiona kikosi alichokuwamo Mtume (s.a.w.w.). Hivyo, kila kikosi kilipopita karibu naye alimwuliza Abbas kama Muhammad alikuwamo mle.

Abbas aliendelea kumwambia: "Humu hayumo" hadi pale walipovutika na jeshi kubwa lililokuwa na takriban askari elfu tano ambamo mashujaa elfu mbili walikuwa wamevaa deraya na maamiri jeshi walikuwa wamezishika bendera nyingi kwa umbali maalum. Jina la kikosi hiki lilikuwa ni *'Katiba– i Khazraa'* – yaani 'jeshi kijani'. Askari wale walikuwa na silaha nyingi mno.

Miili yao yote iligubikwa na silaha na hakuna kilichoweza kuonekana ila macho yao maangavu. Farasi wenye mbio na ngamia wenye manyoya mekundu waliweza kuonekana kwa wingi kwenye kikosi hiki.

Mtume (s.a.w.w.) aliweza kuonekana katikati ya kikosi hiki akiwa amempanda ngamia wake maalum. Watu mashuhuri walikuwa wamemzunguka naye alikuwa akizungumza nao.

Utukufu wa kikosi hiki ulimtishia Abu Sufyani. Bila ya kudhamiria akamwambia Abbas: "Hakuna jeshi liwezalo kulizuia jeshi hili. Ewe Abbas! Ufalme wa mwana wa nduguyo umestawi kwa kiasi kikubwa mno." Abbas alimjibu kwa kumkemea: "Asili ya nguvu ya huyu mwana wa ndugu yangu ni Utume aliopewa na Allah, na hauna chochote kile kihusianacho na nguvu ya nje ya hapo wala ya kidunia."

Abu Sufyan Aenda Makka

Hadi hapo Abbas alikuwa amekwishatekeleza jukumu lake vizuri mno na amemvutia Abu Sufyani kwa ile

nguvu ya kijeshi ya Mtume (s.a.w.w.). Kufikia hapo Mtume (s.a.w.w.) aliona kwamba inafaa kumwachilia Abu Sufyani ili aweze kwenda Makka kabla ya kuwasili kwa vile vikosi vya jeshi la Uislamu ili awaeleze watu kuhusu ile nguvu isiyo na kifani ya Waislamu na vile vile kuwaeleza watu wa Makka kuhusu njia ya usalama wao, kwa sababu kuwatishia tu watu bila ya kuwaonyesha njia ya usalama kusingalimwezesha Mtume (s.a.w.w.) kulifikia lengo lake.

Abu Sufyani alifika mjini mle. Watu waliokuwa na wasiwasi na woga usiku wote ule nao hawakuweza kufanya uamuzi wowote ule wakati Abu Sufyani akiwa hayupo, ndipo wakamzunguka. Akiwa na uso uliojaa huzuni na mwili unaotetemeka, na akiwa anasoza kidole chake kuelekea Madina, alisema: “Vikosi vya jeshi la Waislamu, ambalo haiwezekani kwa mtu yeyote kulizuia, vimeuzingira mji na vitaingia katika muda mfupi ujao.

Kiongozi wao Muhammad, ameniahidi kwamba uhai na mali ya kila akimbiliaye msikitini au kwenye sehemu ziizungukazo Ka’abah, au akaacha kupigana na akajifungia nyumbani mwake ikiwa ni dalili ya kutounga mkono upande wowote, au akaingia nyumba yangu, au nyumba ya Hakim bin Hiz?m, atasamehemwa na atabakia kuwa salama.”
Kwa ujumbe huu wa Abu Sufyani, alizidhoofisha mno nyoyo za watu kiasi kwamba hata wale waliokuwa wakifikiria kutoa upinzani waliliacha wazo lile. Hivyo, matayarisho yote yaliyofanywa usiku uliopita kutokana na zile hatua alizozichukua Abbas, yalithibitisha kuwa ni yenye kuzaa matunda ya kutekwa kwa Makkah, na kule kutokuwepo na upinzani kutoka kwa Waquraishi, kulionekana kuwa ni jambo kuu. Wale watu walioingiwa na woga walikimbilia kwenye sehemu mbalimbali, na matokeo ya huu mpango wa Mtume (s.a.w.w.) wenye hekima ni kwamba yule adui mkuu wa Uislamu alitoa huduma kuu kwa ajili ya jeshi la Waislamu.

Wakati huohuo mkewe Abu Sufyani Hind, aliwachochea watu wapinge na akamtusi mumewe. Hata hivyo hakuna kilichoweza kutendwa sasa na vilio na malalamiko yote hayakuwa na faida yoyote. Hata hivyo, baadhi ya wale watu wenye msimamo mkali kama vile Safw?n bin Umayyah, Ikrimah (mpiganaji na mwakilishi maalum wa Waquraishi kwenye yale mapatano ya amani ya Hudaybiyah) aliapa kwamba watalizuia jeshi la Uislamu lisiuingie mji ule. Baadhi ya watu walidanganywa na kauli zao na huku wakiwa na panga zao mikononi waliifunga njia ya kile kikosi cha kwanza cha jeshi la Uislamu.

Jeshi La Waislamu Laingia Mjini

Kabla ya lile jeshi la Uislamu kuifikia barabara kuu ya mji wa Makka, Mtume (s.a.w.w.) aliwaita makamanda wa jeshi wote na kuwaambia: “Ningelipendelea kwamba Makka itekwe bila ya kumwaga damu. Hivyo basi, kuwaua watu wasiopigana hakuna budi kuepukwe. Hata hivyo, watu kumi ambao ni Ikrimah bin Abu Jahl, Habbar bin Aswad, Abdullah bin Saad Abi Sarah, Miqyas Subabah Layth, Huwairath bin Nuqayd, Abdullah Hilal na wanawake wanne waliotenda mauaji au makosa mengineyo au wameichochea vita, hawa hawana budi kuuawa upesi sana kutokana na makosa yao, wakati wowote ule watakapokamatwa.”14

Amri hii ilifahamishwa askari wote kupitia kwa makamanda wao. Ingawa hali ya kiakili ya watu wa Makka juu ya Mtume (s.a.w.w.) ilikuwa dhahiri kabisa, hivyo yeye (Mtume s.a.w.w) hakuacha kuchukua hatua za tahadhari za kijeshi wakati wa kuingia Makka. Mpango wake ulikuwa hivi:

Vikosi vyote vikiwa vimefanya mstari mmoja uliofika Zi–Tuw?15 wakati Mtume (s.a.w.w.) akiwa kazungukwa na kundi lenye askari elfu tano. Macho ya Mtume (s.a.w.w.) yalipoziangukia nyumba za Makka, machozi ya furaha yalilijikusanya machoni mwake, na ikiwa ni ishara ya kutoa shukrani kwa ajili ya ushindi ule alioupata bila ya upinzani kutoka kwa Waquraishi, yeye akiwa amempanda yule ngamia aliinama sana kiasi kwamba ndevu zake ziligusa matakia yaliyotandikwa mgongoni mwa ngamia yule. Ikiwa ni hatua ya tahadhari, aliligawa lile jeshi na akaipeleka sehemu yake kutoka upande wa juu na sehemu nyingine kutoka upande wa chini ya Makka. Hakutosheka na hilo tu, bali vilevile alivipeleka vikosi kupitia njia zote ziingiazo mjini mle.

Vikosi vyote viliingia mjini mle bila ya mapigano na malango ya mji yalifunguliwa kwa ajili yao ila kikosi kilichoongozwa na Khalid bin Walid. Kwa uchochezi wa Ikrimah, Safw?n na Suhayl, kikundi cha watu kiliamua kupigana na kikaudhihirisha upinzani wao kwa kufuma mishale na kuzitumia panga.

Hata hivyo, watu ishirini na wanane miongoni mwao walipouawa, wale wachochezi walikwenda kujificha na wengine wakakimbia.16

Kwa mara nyingine Abu Sufyani alitoa msaada kwa Uislamu kwenye tukio hili bila ya kuelewa.

Alikuwa bado kashikwa na woga mno na alijua ya kwamba upinzani haukuwa na chochote ila madhara tu. Ili kuzuia umwagaji wa damu alisema kwa sauti kuu aliwaambia watu: “Enyi Waquraishi! Msiyahatarishe maisha yenu, kwa sababu kupigana dhidi ya jeshi la Muhammad lenye utaratibu mzuri hakuna faida. Ziwekeni chini silaha zenu na kaeni majumbani mwenu au kimbilieni msikitini na maeneo yaizungukayo Ka’abah kwa kuwa kufanya hivyo maisha yenu yatasalimika!” Maneno ya Abu Sufyani yalikuwa na athari zilizohitajiwa, na hatimaye baadhi ya watu walijifungia majumbani mwao ambapo wengine walikimbilia msikitini.

Mtume (s.a.w.w.) aliona mianga ya panga za kikosi cha Khalid kutoka mahali paitwapo Az?khir, na akiwa anaitambua sababu ya ugomvi ule, alisema: “Mapenzi ya Allah yamekizidi kila kitu.”

Ngamia wa Mtume (s.a.w.w.) aliingia mji ule kwa heshima kuu na utukufu kutokea kwenye sehemu iliyoinuka ya mji wa Makkah (Az?khir). Alishukia mahali paitwapo Jahuun kandoni mwa kaburi la ami yake mpenzi Abu Twalib, na likakitwa hema maalum kwa aji yake. Ingawa watu walisisitiza kwamba akae nyumbani mwa mtu fulani, lakini yeye alikataa.

Kuyavunja Masanamu Na Kutoharisha Ka’abah

Mji wa Makka uliokuwa kitovu cha ibada ya masanamu kwa muda mrefu, ulisalimu amri kwenye jeshi la Uislamu na sehemu zote za mji ule zikawa chini ya mamlaka ya jeshi la Waislamu. Mtume (s.a.w.w.)

alipumzika muda fulani hivi kwenye lile hema. Baada ya hapo alimpanda ngamia na kwenda kwenye Masjidul Haram kufanya *Tawaaf* (kuizunguka) ya Kaabah. Alikuwa kavaa kofia ya chuma kichwani mwake na Muhajiriin na Ansari wakiwa wamemzunguka, na hali hiyo ilionyesha ukuu wake.

Hatamu za ngamia wa Mtume (s.a.w.w.) zilikuwa zimeshikwa na Muhammad bin Maslamah, na Waislamu na baadhi ya waabudu masanamu walikuwa wamejipanga mstari kwenye njia atakayopitia. Baadhi yao walishangazwa na kutishwa ambapo wengine waliweza kuidhihirisha furaha yao. Kwa ajili ya malengo mema, Mtume (s.a.w.w.) hakushuka kwenye ngamia wake hadi akafika kwenye Masjidul Haram. Hapo alishuka na akasimama upande wa pili wa *Hajarul Aswad* (jiwe Jeusi). Badala ya kulibusu jiwe hili, alilisoza kwa fimbo yake maalum aliyokuwa kaishika mkononi mwake na akaitamka *Takbir.*

Wakimuiga Mtume (s.a.w.w.), Masahaba waliomzunguka kiongozi wao Mtukufu waliitamka *Takbir* kwa sauti kuu. Ile sauti ya *Takbir* ilifika masikioni mwa waabudu masanamu wa Makka waliokimbilia majumbani mwao au kwenye sehemu za miinuko. Ghasia zisizo za kawaida zilisikika mle msikitini na makelele ya watu waliokuwa wakimzuia Mtume (s.a.w.w.) asifanye *Tawaaf* kwa amani. Mtume (s.a.w.w.) aliwaashiria watu wanyamaze. Mara moja kimya kamili kilipatikana na wale wote waliokuwa ndani na walio nje ya msikiti ule walianza kumtazama Mtume (s.a.w.w.). Alianza kufanya *Tawaaf* na kwenye mzunguko wa kwanza wa *Tawaaf* aliyageukia masanamu matatu makubwa yalitoiwa Hubal, Isaaf na Naa'ilah yaliyowekwa juu ya lango la Kaabah. Aliyaangusha kwa fimbo au mkuki aliokuwa kaushika mkononi na akaisoma aya hii: **"Na sema: Kweli imefika na uwongo umetoweka. Hakika uwongo lazima utoweke." (Sura Isra, 17:81)**

Kama alivyoamrisha Mtume (s.a.w.w.) Hubal lilivunjwavunjwa vipande vipande mbele ya macho ya waabudu masanamu. Hili sanamu kubwa lililozitawala fikara za watu wa Rasi ya Uarabuni kwa kipindi kirefu mno lilipoangushwa, Zubayr alimwambia Abu Sufyani kwa kumdhihaki: "Hubayl, lile sanamu kubwa limevunjwa!" Abu Sufyani akamwambia Zubayr kwa huzuni kubwa: "Jiepushe na kusema hivyo. Kama Hubal angalikuwa na uwezo wa kufanya lolote lile tusingelipatwa na hali hii." Amekwisha kutambua kwamba mwishilizo wao haukuwa mikonini mwa sanamu hili.

Mtume (s.a.w.w.) akaimalizia *Tawaaf* yake na akakaa akijipumzisha kwa kiasi fulani hivi kwenye pembe ya msikiti. Kwenye siku hizo Uthman bin Talhah alikuwa mshika funguo za Ka'abah na nafasi yake hii ilikuwa ya kurithi. Mtume (s.a.w.w.) alimtuma Bilal kwenda nyumbani kwa Uthman kwenda kuileta funguo ya Ka'abah.
Bilal aliufikisha ujumbe wa Mtume (s.a.w.w.) kwa yule mtunzaji wa funguo. Hata hivyo mama yake alimkataza asiutoe ule ufunguo, akisema: "Ulinzi wa Ka'abah ni heshima yetu ya kurithiana na hivyo hatuwezi kuipoteza heshima hii." Uthman aliushika mkono wa mama yake na akampeleka kwenye chumba cha faragha na akamwambia: "Kama hatuitoi funguo hii kwa hiari, basi uwe na uhakika kwamba wataichukua kutoka kwetu kwa nguvu!"[17]

Yule mtunza Ka'abah akaifungua ile Ka'abah na Mtume akaiingia. Usamah bin Zayd na Bilal na yule mwangalizi mwenyewe wakamfuatia Mtume (s.a.w.w.). Kama alivyoamrisha Mtume (s.a.w.w.), lango la

Ka'abah lilifungwa, na Khalid bin Walid akasimama nje ya lango lile ili kuwazuia watu wasijazane karibu na lango lile. Kuta za ndani wa Ka'abah zilijaa picha na masanamu ya Mitume. Kama alivyoamrisha Mtume (s.a.w.w.), zile kuta zilisafishwa kwa maji ya kisima cha Zamzam na zile picha zikafutwa.

Mtume (s.a.w.w.) aliamrisha lile lango la Ka'bah lifunguliwe. Kisha akaiweka mikono yake miwili kwenye mhimili wa ubao wa lango lile na watu wakaweza kuuona uso wake mtukufu na wenye kung'aa, aliwaambia watu wale hivi: "Sifa zote zamstahiki Allah Aliyeitimiza ahadi Yake na Akamsaidia mja Wake na Akawashinda maadui."

Allah Mwenye nguvu zote alikuwa amemuahidi Mtume (s.a.w.w.) kwa njia ya wahyi kwamba atamfanya arejee kwenye sehemu aliyozaliwa: **"Hakika aliyekulazimisha kuifuata Qur'ani hapana shaka atakurudisha mahala pa marejeo (ulipozaliwa) … " (Surat al-Qasas, 28:85).** Kwa kusema: "Allah Ameitimiza ahadi Yake." Mtume (s.a.w.w.) aliutaja usahihi wa ile ahadi ya Allah na tena aliudhihirisha ukweli wake.

Kimya kilitawala kabisa kwenye maeneo yauzungukao msikiti na nje ya maeneo hayo. Watu wakizizuia pumzi zao, walikuwa wakiyafikiria mambo tofauti. Katika saa hii watu wa Makka walikumbushwa ule ukatili, uonevu na udhalimu waliowatendea Waislamu na mawazo mengine mbalimbali yalikuja akilini mwao. Watu walioamka mara kadhaa kupigana vita za kumwaga damu dhidi ya Mtume, wamewajeruhi na kuwauwa marafiki na masahaba, na wameamua kufanya mashambulizi ya usiku nyumbani kwake na kumkatakata vipande vipande, sasa wako chini ya mamlaka yake naye angaliweza kulipiza kisasi cha aina yoyote ile dhidi yao.

Watu hawa wakati yanatajwa makosa makubwa makubwa waliyoyatenda, walikuwa wakiambiana: "Bila shaka atatukata kwa upanga au atawauwa baadhi yetu na kuwafunga wengine na kuwafunga wanawake na watoto wetu."

Walikuwa wamezama kwenye fikara nyingi za kishetani, mara kwa ghafla Mtume (s.a.w.w.) alikivunja kimya kile na kusema: "Mnasema nini na mnanifikiriaje?" Wale watu wenye kuogopa wakiukumbuka wema aliowatendea Mtume (s.a.w.w.) hapo zamani, walisema kwa sauti ya unyonge: "Hatuna tunachokifikiria juu yako ila upole na wema. Sisi tunakufikiria kuwa u ndugu yetu mheshimiwa na mwana wa ndugu yetu mheshimiwa."

Wakati Mtume (s.a.w.w.) aliyekuwa na huruma mno na mwenye kusamehe akizisikia kauli hizi zenye kuzivutia hisia kutoka kwao, aliwajibu akisema: "Mimi nami ninakuambieni yaleyale ambayo ndugu yangu Yusufu aliwaambia wale nduguze wasio na huruma: "Leo hapana lawama juu yenu. Allah atakusameheni, Naye ni Mwingi wa kurehemu kuliko wote wanaorehemu."[18]

Kitu kilichowafanya watu wa Makka kuwa na matumanini, ukiyaachilia mbali maneno haya, kilikuwa ni kule kwenda kinyume kwa Mtume (s.a.w.w.) na maneno ya mmoja wa maafisa wake mwenyewe, ambaye wakati wa kuwasili Makka alikuwa akiyatamka maneno ya hamasa ya: "Leo ni siku ya vita. Leo uhai wenu na mali zenu vinachukuliwa kuwa halali (kwa Waislamu)."

Mtume (s.a.w) aliudhishwa na hizi hamasa zisizo za kawaida, na ili kumwadhibu afisa aliyehusika, alitoa maelezo ya kwamba anyang'anywe bendera aliyokuwa kaishika na atolewe kwenye ukamanda. Sayyidna Ali (a.s.) aliteuliwa kuichukua ile bendera kutoka kwa afisa yule, na kwa mujibu wa masimulizi mengine mwana wa afisa yule aliteuliwa kuwa kamanda badala ya baba yake na akaichukua ile bendera kutoka kwa baba yake. Afisa huyu alikuwa ni Saad bin Ubadah, chifu wa kabila la Khazraji. Alifanya hivyo ili kuidhihirisha huruma hii (kwa watu wa Makka) mbele ya macho ya watu wale walioshindwa kuwa na matumaini fulani kwamba watapata msamaha. Na kisha msamaha wa wale waliokimbilia kwenye Ka'abah au nyumbani kwa Abu Sufyani au waliojificha majumbani wamo na wakaifunga milango yao tayari umeshatolewa kupitia kwa Abu Sufyani.

Mtume (S.A.W.W) Atoa Msamaha Kwa Watu Wote

Alipokuwa akitoa msamaha kwa watu wote, Mtume (s.a.w.w.) aliwaambia watu wa Makka hivi: "Mmekuwa ndugu zangu wa kabila moja msiotumia akili. Mliukataa utume wangu na mkanitoa nyumbani mwangu. Na nilipokimbilia kwenye sehemu ya mbali, mliamka kupigana nami. Hata hivyo, ukiyaachilia mbali makosa yenu yote haya, ninakusameheni nyote na ninakufanyeni huru na ninatangaza kwamba mnaweza kwenda kutafuta maisha."

Bilal Atoa Adhana (Mwito Wa Swala)

Muda wa sala ya adhuhuri uliwadia, Bilal mwadhini rasmi wa Uislamu, alipanda kwenye paa la Ka'abah na kwa sauti kuu alitamka Upweke wa Allah na Utume wa Muhammad, huku akiifanya sauti hiyo kuyafikia masikio ya wale walioko kwenye mkutano mkuu. Waabudu masanamu walio wakaidi walikuwa wakisema kila aina ya mambo. Mmoja wao alisema: "Mtu fulani alikuwa na bahati njema, kwa kuwa alifariki dunia mapema na hivyo hakuisikia *Adhaana."* Wakati huo huo Abu Sufyani alisema: "Sitasema lolote lile juu ya jambo hili kwa sababu idara ya habari ya Muhammad ni yenye ustadi mkubwa sana kiasi kwamba ninachelea kamba hizi na chembe chembe za mchanga zilizomo humu msikitini zitamuarifu kuhusu mazungumzo yetu."

Mzee huyu mkaidi asiyeamini kwa uhakika juu ya Uislamu hadi mwishoni mwa maisha yake, aliichukulia elimu ya Wahyi na upatikanaji wa ukweli kutokana na wahyi wa Allah kuwa ni sawa na ujasusi na uchunguzi wa madhalimu wa ulimwengu na kuyachanganya mambo haya. Hata hivyo, ukweli ni kwamba taarifa azipatazo Mtume kupitia kwa Malaika ni tofauti kabisa na wazipatazo wanasiasa, Mtume (s.a.w.w.) alisali sala ya adhuhuri. Kisha akamwita Uthman bin Talhah na kumrudishia ile funguo ya Ka'abah, na kusema: "Cheo hiki ni chako na kitabakia katika hali ya usalama kwenye familia yako!" Na hakuna jingine liwezalo kutegemewa kutoka kwa Mtume (s.a.w.w.) ambaye hupata maamrisho kutoka kwa Allah na kuwaeleza watu: **"Hakina Allah anakuamrisheni mzirudishe amana kwa wenyewe, . . ."** (***Suratun-Nisa, 4:58***).

Bila shaka angeliwapendelea watu wengine kushika amana kubwa kiasi kile. Yeye haziharibu haki za

watu kwa nguvu za kijeshi. Hivyo alitangaza waziwazi akisema: “Utunzaji wa funguo za Ka’abah ni haki ikubalikayo ya mwana wa Talhah na hakuna yeyote anayeshirikiana naye kwenye haki hii.”

Hivyo basi, alizifuta kazi zote zihusianazo na Ka’abah, ila zile zilizokuwa na faida kwa watu, kwa mfano ule utunzaji wa funguo, kuifunika shuka Ka’abah na kuwapatia maji mahujaji wa Ka’abah.

Mtume (S.A.W.W) Awashauri Sana Ndugu Zake

Ili ndugu wa karibu wa Mtume (s.a.w.w.) waweze kujua kwamba uhusiano wao na yeye sio tu kwamba bado haujauondoa mzigo kutoka mabegani mwao bali umelifanya jukumu lao kuwa zito zaidi, alishauri kwamba wasiruhusiwe kuiruka mipaka ya sheria za Uislamu kwa sababu ya uhusiano wao na yeye au kujinufaisha kinyume na haki kutokana na uhusiano wao na kiongozi wa Dola.
Katika hotuba aliyoitoa kwenye mkutano waliohudhuria watu wa familia za Bani Hashim na Bani Abdul Muttalib, alishutumu kila aina ya ubaguzi na akatilia mkazo juu ya umuhimu wa uadilifu na usawa baina ya watu wa matabaka yote, na akasema: “Enyi wana wa Hashim na Muttalib! Allah amenituma kwenu ili niwe Mjumbe Wake na vifungo vya huba na huruma baina yenu na mimi vilevile si vyenye kuvunjika.

Hata hivyo, msidhanie ya kwamba uhusiano wenu na mimi tu utakuthibitishieni wokovu kwenye Siku ya Hukumu. Ninyi nyote hamna budi kutambua ya kwamba rafiki yangu kutoka miongini mwenu na wengineo ni yule aliye mchamungu na mwema, na uhusiano wangu na wale wajao mbele ya Allah na mzigo mzito wa dhambi umekatika. Sitaweza kukufanyieni lolote lile katika Siku ya Hukumu. (Katika siku hiyo) Mimi na ninyi tutawajibika kwa matendo yetu.”19

Hotuba Ya Kihistoria Ya Mtume (S.A.W.W.) Kwenye Msikiti Wa Masjidul Haram

Ulikuwako mkusanyiko mkubwa wa watu kwenye Masjidul Haram kuizunguka Ka’abah. Waislamu, waabudu masanamu, marafiki na maadui walikuwa wamekaa bega kwa bega pamoja, na hapo utukufu wa Uislamu na ukuu wa Mtume (s.a.w.w.) vilitoa tamasha kuu mle msikitini.

Utulivu ulitawala pote mjini Makka na sasa muda ukawadia kwa Mtume (s.a.w.w.) kuwaonyesha watu sifa halisi za mwito wake, na kuukamilisha ujumbe wake aliouanzisha miaka ishirini iliyopita, lakini alikuwa bado hajafaulu kuukamilisha kutokana na kuchelewa kwa waabudu masanamu.

Yeye Mtume (s.a.w.w.) mwenyewe alikuwa mkazi katika mazingira yaleyale, naye aliyatambua vizuri maradhi ya jamii ya Kiarabu na dawa yao. Aliijua sababu ya kuanguka kwa watu wa Makka. Hivyo akaamua kuyatazama maradhi ya kijamii ya jamii ya Kiarabu na kuwatibu kwa ukamilifu.

Hapa chini tunatoa baadhi ya maelekezo ya Mtume wa Uislamu (s.a.w.w.). Kila moja lilidhamiriwa kuponya maradhi maalum.

Suala la mtu kujitukuza kwa sababu ya familia yake binafsi, nyumba yake au kabila lake ilikuwa moja ya maradhi yenye mizizi iliyoshamiri mno ya jamii ya Kiarabu, na fahari kuu kwa mtu ilikuwa kwamba atokane na tawi la Kabila maarufu kama vile Waquraishi.

Mtume (s.a.w.w.) aliushutumu msingi huu wa ubora wa kimawazo tu, alisema: “Enyi watu! Allah chini ya mafundisho ya Uislamu amekomesha kutoka kwenu misingi ya fahari ya zama za ujinga, na kujitukuza kwa ajili ya nasaba.

Ninyi nyote ni dhuria wa Nabii Adamu, na Adamu aliumbwa kwa udongo. Aliye bora miongoni mwenu ni yule aziambaaye dhambi na uasi.”

Ili kuwafanya watu watambue kwamba kipambanuzi cha ubora ni uchamungu tu, yeye kwenye moja ya hotuba zake aliwagawa watu wote kwenye makundi mawili, na akatangaza kwamba wale walio wachamungu ndio wastahilio kuheshimiwa kwa ubora.

Kutokana na mgao na upangaji huu wa madaraja, alibatilisha vipimo vyote vya kimawazo vya madaraja na vyeo, na akasema: “Mbele ya Allah watu wana makundi mawili tu:

Moja kati ya makundi hayo ni lile la watu wachamungu, walio waheshimiwa mbele ya Allah, na kundi la pili ni lile la waasi na wenye dhambi, ambao ni duni na waliotwezwa mbele Yale (Allah)”.

Ubora Kutokana Na Kuwa Mwarabu

Mtume (s.a.w.w.) alitambua kwamba Waarabu walichukulia kuwa kizazi cha Kiarabu ni heshima kuu kwao; walijivunia kuwa na nasaba ya Kiarabu. Ari hii ilikuwa kama maradhi ya kuambukiza kwao. Kuyatibu maradhi haya na kuiondolea mbali ile dhana ya ubora huu aliwageukia watu na kusema: “Enyi watu! Kuwa Mwarabu si kigezo cha ubora wenu au sehemu ya utu wenu, ila ni aina tu ya usemaji. Fahari ya kinasaba haina faida yoyote kwa mtu asiyeyatekeleza majukumu yake barabara, na haifanyi masahihisho kwenye mapungufu ya utendaji wake.”

Je, inawezekana kupata kauli iliyo fasaha na yenye kuelezea waziwazi kuliko hii? Yule mtangazaji halisi wa uhuru hakutosheka na kauli tulizozinukuu hapo juu, bali ili kuuthibitisha usawa wa wanadamu na jamii, aliongeza kusema: “Watu wote wamekuwa sawa hapo kale na pia wako sawa hivi sasa kama yalivyo meno ya kitana, na Mwarabu hana ubora wowote kwa asiyekuwa Mwarabu, wala mtu mwekundu si bora kuliko mweusi. Kigezo cha ubora ni uchamungu.”

Kwa kauli hii aliondoa aina zote za ubaguzi usio sahihi na vizuizi visivyo na mipaka miongini mwa mataifa ya ulimwengu, ni katika nyakati hizi za awali tu bila kuchelewa akalitekeleza jukumu lake ambalo ‘Tangazo la Haki za Binadamu’ la siku hizi au ‘Haki ya Uhuru na Usawa wa Mwanadamu’ havikuweza kulitekeleza ingawa kuna makelele yote haya juu ya hayo.

Vita Vya Miaka Mia Moja Na Mifundo Ya Tangu Kale

Kutokana na vita vya ndani na umwagaji wa damu uliokuwa ukiendelea, watu wa Uarabuni wamekuwa taifa la wenye kulipiza kisasi na daima walikuwa kwenye vita wenyewe kwa wenyewe. Baada ya kutwaa udhibiti kamili kwenye Rasi ile ya Uarabuni, Mtume (s.a.w.w.) aliliondoa tatizo hili la kijamii na ilikuwa muhimu kwamba ayatibu maradhi haya ili kuthibitisha upatikanaji wa usalama wa Dola ya Kiislamu.

Aliipata tiba ya maradhi haya kwa kuwataka watu kuacha umwagaji damu wa aina zote uliokuwa ukitendeka kwenye zama za ujinga, na kuyachukulia mambo yote kama hayo kuwa yamefutwa kabisa. Kwa njia hii alizuia umwagaji wa damu uliovuruga amani na utaratibu mwema, na akawafanya watu wayasahau maasi, utekaji nyara na mauaji, vitu vilivyozaa madai ya dia au mapambano. Ili kuifikia hatima hii, alitangaza akisema: “Ninayatupilia mbali madai yote yahusianayo na uhai na mali na heshima zote za kimawazo tu, za siku za kale, na ninazihesabu kuwa ni zisizo na msingi.”

Udugu Wa Kiislamu

Sehemu ya yale aliyoyasema Mtume (s.a.w.w.) siku ile ni kuhusiana na umoja wa Waislamu na haki alizonazo Mwislamu juu ya nduguye Mwislamu. Lengo lake katika kuzitaja faida hizi lilikuwa kwamba, kwa kuvidumisha vifungo hivi vya urafiki na umoja, pamoja na kuziheshimu haki walizonazo Waislamu juu ya wao kwa wao, wale wasiokuwa Waislamu waweze kuuelekea Uislamu na kuweza kujiunga na safu za Waislamu. Yafuatayo ni maneno ya maelezo hayo: “Mwislamu yu ndugu wa Mwislamu mwenzie na Waislamu wote ni ndugu wao kwa wao, nao huwa mkono mmoja wawapo dhidi ya wasiokuwa Waislamu.

Damu ya kila mmoja wao ni sawa na ile ya wengine na hata yule aliye mdogo zaidi miongoni mwao anaweza kuweka ahadi kwa niaba ya wenzie.”20

Wahalifu Wakamatwa

Hakuna shaka juu ya ukweli uliopo kwamba Mtume (s.a.w.w.) alikuwa kigezo kikuu cha huruma na msamaha, na ingawa ulikuwepo mwelekeo wenye nguvu wa kundi lenye msimamo mkali, alitoa msamaha kwa watu wote. Hata hivyo, walikuwepo watu wachache waliokuwa na makosa na majinai makubwa mno, na isingelifaa kwamba pamoja na maovu yote haya wapewe uhuru wa kwenda huko na huko miongoni mwa Waislamu, kwa sababu iliwezekana kabisa kwamba wakijichukulia fursa zisizostahili za ule msamaha waliopewa wangeliweza kufanya makri dhidi ya waislamu.

Baadhi yao waliuawa na Waislamu mitaani au kwenye Masjdul Haram na wawili miongoni mwao walikimbilia nyumbani kwa Ummi H?ni, dada yake Sayyidna Ali (a.s.). Ali akiwa na silaha kikamilifu aliizingira nyumba ya Ummi H?ni. Alipokabiliana uso kwa uso na afisa asiyetambulika, alijitambulisha upesi sana na akasema: “Nikiwa ni mwanamke wa Kiislamu, nimewapa kimbilio watu wawili na kimbilio

alitoalo mwanamke wa kiislamu linaheshimiwa kama lile alitoalo mwanaume wa Kiislamu.” Wakati huo, ili kujitambulisha kwa Ummi Haani, Sayyidna Ali (a.s.) aliivua kofia yake. Yule bibi alimwona umbu lake ambaye mageuko ya nyakati yalimtenga kutoka kwake kwa miaka mingi. Mara macho yake yalijawa na machozi na akaikumbatia shingo ya Sayyidna Ali (a.s.). Baada ya hapo, wote wawili walikwenda mbele ya Mtume (s.a.w.w.) na yeye naye alilihesabu lile kimbilio alilolitoa Ummi Hani kuwa ni lenye kuheshimiwa.

Abdullah bin Saad bin Sarah aliyesilimu lakini baadae akaritadi, alikuwa mmoja wa wale watu kumi waliokuwa wanaume. Yeye naye alikiepuka kifo kwa uombezi wa Uthman.

Hadith Ya Ikrimah Na Safwan

Ikrimah bin Abu Jahl, aliyeviwasha vita vilivyoifuatia vile ya Badr, alikimbilia Yaman. Hata hivyo, yeye naye alisamehewa kwa mapendekezo ya mkewe. Safw?n alikuwa mwana wa Umayyah, aliyeuawa kwenye vita vya Badr. Pamoja na makosa na maovu mengine, Safw?n alimnyonga Mwislamu mjini Makka wakati wa mchana wa dhahiri ili kulipizia kisasi cha baba yake. Akiichelea adhabu, aliamua kuitoka Hijaz kwa njia ya bahari, hasa kwa sababu alitambua kwamba jina lake nalo lilikuwamo miongoni mwa wale watu kumi tuliowataja.

‘Umayr bin Wahab alimwomba Mtume (s.a.w.w.) kumsamehe Safw?n. Mtume (s.a.w.w.) aliyakubali mapendekezo yake, na ikiwa ni dalili ya hifadhi aliyopewa Safw?n alimpa ‘Umayr kilemba alichokuwa amekivaa wakati wa kuwasili kwake Makka. ‘Umayr alikwenda Jidah na kilemba kile na kumleta Safw?n mjini Makka. Macho ya Mtume (s.a.w.w.) yalipomwangukia mkosefu huyu mkuu wa zama zile, alimwambia kwa huruma nyingi: “Uhai wako na mali zako vimethibitishiwa usalama. Hata hivyo itakuwa bora kama ukisilimu.” Aliomba apewe muda wa kipindi cha miezi miwili ili kulifikiria jambo hili. Mtume (s.a.w.w.) akasema: “Mimi niko tayari kukupa muda wa miezi minne badala ya hiyo miezi miwili ili kwamba uweze kuichagua dini hii kwa ufahamu kamili.” Kipindi cha miezi minne kilikuwa bado hakijamalizika wakati Safw?n aliposilimu.21

Ukiutupia jicho ule wakati ambao Mtume (s.a.w.w.) alimpa Safw?n uhuru huudhirisha ukweli ulio kinyume kabisa na fikara za mustashirik wenye ubinafsi. Ukweli uliopo ni kwamba machifu wa ushirikina walifaidi uhuru kamili katika suala la kusilimu. Si hilo tu bali vilevile hakukuwa na shurutisho lolote lililofanywa kwenye jambo hili, lakini juhudi zilifanywa kwamba waifuate hii dini ya Allah baada ya kufikiria na kujifunza kwa makini wala si kutokana na hofu na kutishiwa.

Matukio Ya Baada Ya Kutekwa Kwa Mji Wa Makka

Matukio muhimu na yenye mafunzo yahusianayo na kutekwa kwa mji wa Makka yameshasimuliwa. Hata hivyo, yako matukio mengine mawili yaliyo muhimu, ambayo ni haya tutakayoyasimulia hapa chini:

Baada ya kiapo cha utii cha Aqabah,22 Mtume (s.a.w.w.) kwanza alichukua kiapo cha utii kutoka kwa

wanawake, ambacho ni kuyatekeleza majukumu haya: Kutomshirikisha Allah na yeyote yule, kutovunja ahadi, kutojishughulisha na matendo maovu, kutowauwa watoto wao, kutowahusisha na waume zao watoto ambao ukweli uliopo ni kwamba wao ni watoto wa watu wengine, kutompinga Mtume kwa jambo lolote lile.

Uendeshaji wa kiapo tulichokitaja hapo juu ulikuwa hivi: Kama alivyoamrisha Mtume (s.a.w.w.) aliletewa chombo kilichojazwa maji, naye akayachanganya maji yale na manukato. Kisha akaitumbukiza mikono yake humo na akaisoma Aya ya 12 ya *Surah al–Mumtahinah.* Baada ya hapo aliamka pale alipokuwa kaketi na kuwaambia wale wanawake: “Wale walio tayari kula kiapo hiki cha utii kwangu chini ya masharti niliyoyasema watumbukize mikono yao kwenye chombo hiki na watamke kwamba watayatekeleza masharti haya kwa uaminifu.”

Sababu ya kula kiapo hiki ilikuwa kwamba walikuwepo wengi miongoni mwa wanawake wa Makka waliokuwa wakiishi maisha ya upotofu, na kama haichukuliwi ahadi ya kuishi maisha ya heshima kutoka kwao, basi ulikuwapo uwezekano kwamba wangeliendelea kuyatenda matendo yao maovu kwa siri. Mmoja wa wanawake hao alikuwa ni ‘Hind’ mkewe Abu Sufyani na ambaye ni mama yake Muawiyah aliyekuwa na historia nyeusi. Akiwa fidhuli mno, Hind aliweka utashi wake juu ya mumewe Abu Sufyani; na hata katika ile siku ambayo alielekea kwenye amani, alikuwa akiwachochea watu wapigane na kumwaga damu.

Ilitokana na uchochezi wa Hind kwamba vita vilipiganwa kule Uhud na ikambidi Mtume (s.a.w.w.) kuyatoa mhanga maisha ya watu sabini akiwamo Hamza, ili kuzimisha vita ile. Na mwanamke huyu mshenzi alilipasua tumbo la mwili wa Hamza kwa ukatili usio kifani na kulitoa ini lake na kulikata mapande mawili kwa meno yake. Mtume (s.a.w.w.) hakuwa na njia nyingine ila kuchukua kiapo cha utii kutoka kwa mwanamke huyu na wengineo wa mfano wake mbele ya hadhara.

Wakati Mtume (s.a.w.w.) alipokuwa akiyasoma masharti ya mapatano yale, alikisoma kifungu ‘kutovunja ahadi’, Hind ambaye wakati ule alikuwa kakifunika gubigubi kichwa chake na uso wake, aliamka pale alipokuwa na kusema: “Ewe Mtume wa Allah! Unawaamrisha wanawake kutozivunja ahadi. Mimi nifanye nini? Mume wangu ni bahili mno na bwana mwonevu, na kwa sababu hii hapo awali nimekuwa nikiitumia bila ya haki mali yake iliyowekwa amana kwangu.” Abu Sufyani akaamka kwenye kiti chake na kusema: “Ninakihalalisha kila ulichokichukua hapo awali lakini huna budi kuahidi kwamba hutaiba tena katika siku zijazo.” Hapo Mtume (s.a.w.w.) alimtambua Hind kutokana na yale maneno ya Abu Sufyaan, na akamwambia: “Je, wewe ni binti wa Utbah?”Akajibu: “Ewe Mtume wa Allah! Ndio. Tusamehe dhambi zetu ili Allah Mwenye nguvu zote Akubariki.”

Mtume (s.a.w.w.) alipoitamka kauli isemayo: ‘Kutozini,’ Hind akaamka tena kutoka pale alipokaa na kuitamka kauli ya kujitoa katika lawama (kujibu rai), ambayo kwayo alimfunulia bila ya kupenda yale yaliyomo akilini mwake. Alisema: “Je, mwanamke muungwana anazini?” Kisaikolojia kujihami kwa aina hii kwenyewe tu kulikuwa aina fulani ya kuzifunua fikara za mtu. Kwa vile Hind alijitambua kuwa yu mwanamke wa aina ile, na alikuwa na uhakika kwamba katika kuisikia (kutoka kwa Mtume s.a.w.w) kauli

tuliyoitaja hapo juu, watu watamtazama, ndipo mara moja aliuliza kwa njia ya tahadhari, kama mwanamke asiyekuwa mjakazi anaweza kuzini.

Hata hivyo, baadhi ya watu waliokuwa na uhusiano haramu na Hind katika zama za Ujinga walishangaa na wakacheka kule kukataa kwake, na vicheko vyao na kule kujihami kwake vikawa fedheha yake zaidi.23

Ukiyachunguza zaidi maneno yaliyomo kwenye kiapo hiki utayakuta yakidhihirisha jukumu la mwanamke wa Kiislamu. Vilevile kutokana na sentensi hii inadhihirika kwamba, Mtume (s.a.w.w.) hakupata ahadi yoyote kutoka kwa wanawake kuhusiana na kujihami, ambapo kwenye kiapo alichoapiwa pale Aqabah na chini ya ule mti (pale Hudaybiyah) kifungu kilichokuwa muhimu sana alichokitoa kilikuwa ni kile kihusianacho na ulinzi wa Uislamu na kumhami Mtume (s.a.w.w.).

Mahekalu Ya Masanamu Mjini Makka Na Viungani Mwake Yavunjwa

Idadi kubwa ya mahekalu ya masanamu ilijengwa kandokando ya mji wa Makka, na yalikuwa vyanzo vya heshima kwa makabila mengi. Ili kuing'oa ibada ya masanamu kutoka kwenye eneo la Makka, Mtume (s.a.w.w.) alipeleka vikundi vya askari pande mbalimbali kwenda kuyavunja mahekalu ya masanamu yaliyokuwako huko. Vilevile ilitangazwa mle mjini Makka kwamba kila aliye na sanamu nyumbani mwake alivunjevunje mara moja.24

Khalid bin Walid alikwenda akiliongoza kundi la askari hadi kwenye nchi ya kabila liitwalo Jazimah bin Aamir kuwaita kwenye Uislamu. Mtume (s.a.w.w.) alimwamrisha asiimwage damu yoyote na kutopigana vita yoyote ile, vilevile alimtuma Abdur Rahman bin Awf pamoja naye akiwa chini yake.

Katika Zama za Ujinga, kabila la Bani Jazimah lilimwua ami yake Khalid na baba yake Abdur Rahman walipokuwa wakirejea kutoka Yemen na kuziteka nyara mali zao, na Khalid bado alikuwa ana mfundo dhidi yao juu ya kisa hiki. Alipokuja uso kwa uso na watu wa kabila la Bani Jazimah, aliwaona wote wakiwa wameshika silaha na wakiwa tayari kujihami.

Yule kamanda (yaani, Khalid) akasema kwa sauti kuu: "Ziwekeni chini silaha zenu, kwa sababu kipindi cha kuyaabudu masanamu kimekwisha na Makka imeshatekwa, na watu wote wameshasalimu amri mbele ya jeshi la Uislamu."

Machifu wa kabila waliwashauri watu wao kwamba wazitoe silaha zao na kujisalimisha mbele ya jeshi la Uislamu. Mtu mmoja miongoni mwao alikuwa na akili kiasi cha kuweza kutambua kwamba nia ya yule kamanda wa jeshi haikuwa nzuri.

Hivyo basi, akiwahutubia machifu wa kabila lile, alisema: "Matokeo ya kusalimu amri yatakuwa ni kuchukuliwa mateka na baada ya hapo ni kifo."

Hatimaye maoni ya wale machifu yalitekelezwa na zile silaha zilitolewa na kupewa askari wa Uislamu. Wakati huo huo yule kamanda wa kundi lile la askari akiwa katika hali ya woga na kinyume na maamrisho ya Uislamu, aliamrisha kwamba mikono ya watu wa kabila lile ifungwe kinyumenyume na watiwe kizuizi. Baada ya hapo, ilipofika asubuhi baadhi yao waliuwawa kwa amri ya Khalid na wengine wakaachiliwa.

Taarifa za kosa hili la kutisha alilolitenda Khalid zilimfikia Mtume (s.a.w.w.) na akachukia mno. Upesi sana akamteua Sayyidna Ali (a.s.) kwenda kwa watu wa kabila lile na kuwalipa gharama za uharibufu wa vita vile na dia baada ya Kasma ya makini kabisa. Sayyidna Ali (a.s.) aliifanya hesabu ya hasara yao kwa makini mno kiasi kwamba alilipa hata gharama ya chombo kilichotengenezwa kwa mti ambacho mbwa wa kabila lile walikuwa wakinywea maji na kilichovunjika wakati wa mapambano ya Khalid. Kisha akawaita machifu wote waliodhulumiwa na akawauliza kama fidia yote ya vita vile na dia ya watu waliouawa kwa kuonewa imelipwa kwa ukamilifu nao, wote wakajibu:

“Ndio.” Baada ya hapo, akiuzingatia ukweli uliopo kwamba iliwezekana kwamba wamepata hasara ambayo bado hawajaitambua, Saidian Ali (a.s.) aliwapa pesa fulani kwa njia ya zawadi na kisha akarejea Makka na kutoa taarifa yake kwa Mtume (s.a.w.w.).

Mtume (s.a.w.w.) alimsifu Sayyidna Ali (a.s.) kwa kitendo chake kile na huku akiwa ameelekea Qiblah aliinua mikono yake na kuomba akisema: “Ee Mola! Unatambua kwamba mimi nimechukizwa na kosa la Khalid nami katu sikumwamrisha kupigana vita.”25

Alipokuwa Amirul–Mu’minin (a.s.) akiwalipa fidia wale watu wa Bani Jazimah, vile vile aliyazingatia madhara ya kiroho na ya kitabia waliyoyapata na akawapa pesa wale watu waliokumbwa na hofu kutokana na mashambulizi ya Khalid na akawafariji.

Mtume (s.a.w.w.) alipoitambua tabia ya unyoofu ya Amirul–Mu’minin (a.s.), alisema: “Ewe Ali! Mimi sitakibadili kitendo chako hiki na idadi kubwa ya ngamia wenye manyoya mekundu.26

Ewe Ali! Umeipata radhi yangu. Allah akuridhie! Ewe Ali! Wewe ni kiongozi wa Waislamu. Amebahatika yule akupendaye na akaifuata njia yako, na yu mwenye bahati mbaya yule akupingaye na akaifuata njia iliyo potoka.27 Cheo chako kwangu ni kama kile alichokuwa nacho Harun kwa Musa ila tu kwamba hatakuja Mtume baada yangu.”28

Kosa Jingine La Khalid

Kosa tulilolitaja hapo juu halikuwa kosa pekee la Khalid alilolitenda katika kipindi cha uhai wake wa kujifanya kuwa yu Mwislamu, kwa kuwa hivyo, katika kipindi cha Ukhalifa wa Abu Bakr alitenda kosa lililokuwa kubwa kuliko hilo la awali.

Tukieleza kwa ufupi tu ni kwamba, baada ya kufariki dunia Mtume (s.a.w.w.) baadhi ya makabila yaliritadi, au ili kueleza kwa usahihi zaidi ni kwamba, hawakuutambua Ukhalifa wa Abu Bakr na

wakakataa kutoa Zaka. Khalifa alituma makundi mbalimbali ya watu kwenye sehemu mbalimbali kwenda kuwaadhibu wale walioritadi.

Khalid bin Walid alilishambulia kabila la Maalik bin Nuwayrah, kwa sababu watu hao wameritadi. Maalik na watu wote wa kabila lake walikuwa tayari kujihami, na walikuwa wakisema: “Sisi ni Waislamu na hivyo basi haistahili kwamba tushambuliwe na jeshi la Uislamu.”

Hata hivyo, Khalid aliwanyang’anya silaha kwa kufanya udanganyifu na akamwua yule chifu wa kabila lile Maalik bin Nuwayrah, aliyekuwa Mwislamu, na kisha akamnyanyasa mkewe.29

Je, hii historia nyeusi ya Khalid yathibitisha haki ya kwamba tumwite ‘***Saifullah***’ (Upanga wa Allah) na tumchukulie kuwa yu mmoja wa maafisa wakuu wa Uislamu?30

---

1. Budayl alikuwa mmoja wa watu watukufu na wazee wa kabila la Khuza’ah waliokuwa wakiishi mjini Makka. Wakati ule alikuwa na umri wa miaka 97. (Amaali Tusi, uk. 239).
2. Maghaazil–Waaqidi, Juz. 2, uk. 792.
3. Maghaazil–Waaqidi, Juz. 2, uk. 780–794; Siiratu Ibn Hishamu, Juz. 2, uk. 389– 387; Bihaarul Anwaar, Juz. 21, uk. 102.
4. Siiratu Ibn Hishamu, juz.2, uk.399; Majma’ul Bayaan, juz.9, uk. 269–270.
5. Ibn Hisham, Juz. 2, uk. 399 na Majma’ul Bayan, Jz. 9, uk. 269–270.
6. Heroes an Hero Worship cha Thomas Carlyle.
7. Maombi yote haya yamesimuliwa mwenye Surat al–Israa, 17:90–93.
8. Sura Yusuf, 12:91–92.
9. Siiratu Ibn Hisham, Juz. 2, uk. 402.
10. Bihaarul An’waar, Juz. 21, uk. 114.
11. Jina la uzazi (kun'ya) la Abu Sufyani.
12. Jina la uzazi (kun'ya) la Abbas
13. Siiratu Ibn Hisham, Juz. 2, uk. 400 – 404 Majmaul Bayan, Juz. 10, uk. 554– 556; Maghaazil–Waaqidi, Juz. 2, uk 816–818; Sharhu Abil Hadid, Juz. 17, uk. 268 kama alivyonuku kutoka Maghaazil–Waaqidi.
14. Siiratu Ibn Hisham, Juz. 2, uk. 409.
15. Hii ni sehemu ya mwinuko ambayo mtu awapo hapo aliweza kuziona nyum– ba za Makka pamoja na Kaabah na Masjidul Haraam.
16. Maghaazil–Waaqidi, Juz.2, uk. 825–826.
17. Maghaazil–Waaqidi, juz. 2, uk 833.
18. Maghaazil–Waaqidi, Juz. 2, uk. 835; Bihaarul Anwaar, juz. 21, uk. 107 na 133
19. Bihaarul Anwaar, Juz.1, uk. 111.
20. Nukuu hizi tumezitoa kwenye vitabu hivi; Rawzatul–Kafi, uk. 246; Siiratu Ibn Hisham, juz. 2, uk. 412; Maghaazil–Waaqidi, juz. 2, uk. 836; Bihaarul An’waar, juz. 21, uk. 5; Sharhu Abil Hadid, Juz. 17, uk. 281.
21. Siiratu Ibn Hisham, Juz. 2, uk. 417.
22. Katika kiapo cha utii kilichofanyika pale ‘Aqabah kabla ya kuhajiri kwa Mtume (s.a.w.w.) wanawake watatu walikuwa miongoni mwa watu waliokuwa zaidi ya sabini waliokula kiapo kile.
23. Majma’ul Bayaan, Juz. 5, uk. 276.
24. Bihaarul Anwaar, Juz. 21, uk. 140.
25. Siirah–i Hishamu, Juz. 2, uk. 430.
26. Khisaal, Juz. 2, uk. 125.

27. Majlis–i Ibn Shaykh, uk. 318.
28. Amaali Suduq, uk. 105.
29. Uhalisia wa kisa hiki ni kuwa Khalid aliyetumwa na Abu Bakr alimwingilia mke wa Malik katika usiku uleule aliomuuwa mumewe. Historia ya Uisilamu hai– jui ni Aya ipi iliyomruhusu Khalid kumwingilia mjane huyo siku ileile, na wala ni Uisilamu upi uliomruhusu kumuuwa Malik, lakini historia yajuwa kuwa Malik ni sahaba aliyeaminiwa na Mtukufu Mtume na hivyo akampa jukumu la kusimamia zaka za jamaa zake. Malik na watu wake walikataa kukabidhi zaka hizi kwa Abu Bakri kwa kuwa wao hawakumtambua kama Khalifa wa Mtume, kwani walichokijua wao kutoka kwa Mtume ni kuwa, Khalifa baada yake ni Ali (a.s.). – Mhariri.
30. Hapa ndipo inapokulazimu kuelewa ni upi ukweli wa nadharia yetu isemayo “Si kila Sahaba ni mwadilifu” Mhariri

Orodha Ya Vitabu Vilivyo Chapishwa Na Al-Itrah Foundation:

1. Qur'an Al-Kariim – Tafsir Al-Kashif Juzuu ya kwanza mpaka Thalathini
2. Uharamisho wa Riba
3. Uharamisho wa uwongo Juzuu ya kwanza
4. Uharamisho wa uwongo Juzuu ya pili
5. Hekaya za Bahlul
6. Muhanga wa Imamu Husein (A.S.)
7. Mikingamo iliyomzunguka Imamu Ali (A.S.)
8. Hijab vazi Bora
9. Ukweli wa Shia Ithnaashari
10. Madhambi Makuu
11. Mbingu imenikirimu
12. Abdallah Ibn Saba
13. Khadijatul Kubra
14. Utumwa
15. Umakini katika Swala
16. Misingi ya Maarifa
17. Kanuni za Ndoa na maadili ya Familia
18. Bilal wa Afrika
19. Abudharr
20. Usahihi wa Historia ya Uislamu na Waislamu
21. Salman Farsi
22. Ammar Yasir
23. Qur'an na Hadithi
24. Elimu ya Nafsi

25. Yajue Madhehebu ya Shia
26. Ukusanyaji na Uhifadhi wa Qur'an Tukufu
27. Al–Wahda
28. Ponyo kutoka katika Qur'an.
29. Uislamu mfumo kamili wa maisha ya kijamii
30. Mashukio ya Akhera
31. Al Amali
32. Dua Indal Ahlul Bayt
33. Udhuu kwa mujibu wa Kitabu na Sunna.
34. Haki za wanawake katika Uislamu
35. Mwenyeezi Mungu na sifa zake
36. Amateka Na Aba'Khalifa
37. Nafasi za Ahlul Bayt (a.s)
38. Adhana.
39 Upendo katika Ukristo na Uislamu
40. Nyuma yaho naje kuyoboka
41. Amavu n'amavuko by'ubushiya
42. Kupaka juu ya khofu
43. Kukusanya swala mbili
44. Bismillah ni sehemu ya Qur'ani na husomwa kwa Jahara
45. Kuwaongoza vijana wa kizazi kipya
46. Kusujudu juu ya udongo
47. Kusheherekea Maulidi Ya Mtume (s)
48. Tarawehe
49. Malumbano baina ya Sunni na Shia
50. Kupunguza Swala safarini
51. Kufungua safarini
52. Umaasumu wa Manabii
53. Qur'an inatoa changamoto
54. as–Salaatu Khayrun Mina –'n Nawm
55. Uadilifu wa Masahaba
56. Dua e Kumayl
57. Sauti Ya Uadilifu wa Binadamu
58. Umaasumu wa Mitume – Faida Zake Na Lengo Lake
59. Umaasumu wa Mitume – Majibu Ya Aya Zenye Utata
60. Umaasumu wa Mitume – Umaasumu wa Mitume Muhammad (s)
61. Nahju'l–Balaghah – Juzuu ya Kwanza
62. Nahju'l–Balaghah – Juzuu ya Pili
63. Kuzuru Makaburi

64. Maswali Na Mishkili Elfu – Sehemu ya Kwanza
65. Maswali Na Mishkili Elfu – Sehemu ya Pili
66. Maswali Na Mishkili Elfu – Sehemu ya Tatu
67. Maswali Na Mishkili Elfu – Sehemu ya Nne
68. Maswali Na Mishkili Elfu – Sehemu ya Tano
69. Maswali Na Mishkili Elfu – Sehemu ya Sita
70. Tujifunze Misingi Ya Dini
71. Sala ni Nguzo ya Dini
72. Mikesha Ya Peshawar
73. Malezi Ya Mtoto Katika Uislamu
74. Ubora wa Imam 'Ali Juu ya Maswahaba Na Ushia ndio njia iliy onyooka
75. Shia asema haya, Sunni asema haya, Wewe wasemaje?
76. Liqaa–u–llaah
77. Muhammad (s) Mtume wa Allah
78. Amani na Jihadi Katika Uislamu
79. Uislamu Ulienea Vipi?
80. Uadilifu, Amani na Mtume Muhammad (s)
81. Mitala na Ndoa za Mtume Muhammad (s)
82. Urejeo (al–Raja'a)
83. Mazingira
84. Utokezo (al – Badau)
85. Sadaka yenye kuendelea
86. Msahafu wa Imam Ali
87. Uislamu na dhana
88. Mtoto mwema
89. Adabu za Sokoni
90. Johari za hekima kwa vijana
91. Maalimul Madrasatain Sehemu ya Kwanza
92. Maalimul Madrasatain Sehemu ya Pili
93. Maalimul Madrasatain Sehemu ya Tatu
94. Tawasali
95. Imam Mahdi katika Usunni na Ushia
96. Maana ya laana na kutukana katika Qur'ani Tukufu
97. Hukumu ya kujenga juu ya makaburi
98. Swala ya maiti na kumlilia maiti
99. Shiya na Hadithi (kinyarwanda)
100. Mariamu, Yesu na Ukristo kwa mtazamo wa Kiislamu
101. Hadithi ya Thaqalain
102 Fatima al–Zahra

103. Tabaruku
104. Sunan an–Nabii
105. Historia na sera ya viongozi wema (Sehemu ya Kwanza)
106. Idil Ghadiri
107. Mahdi katika sunna
108. Kusalia Nabii (s.a.w)
109. Ujumbe –Sehemu ya Kwanza
110. Ujumbe – Sehemu ya Pili
111. Ujumbe – Sehemu ya Nne
112. Ngano ya kwamba Qur'ani imebadilishwa
113. Shiya N'abasahaba
114. Iduwa ya Kumayili
115. Maarifa ya Kiislamu.
116. Ukweli uliopotea sehemu ya Kwanza
117. Ukweli uliopotea sehemu ya Pili
118. Ukweli uliopotea sehemu ya Tatu
119. Ukweli uliopotea sehmu ya Nne
120. Ukweli uliopotea sehmu ya Tano
121. Johari zenye hekima kwa vijana
122. Safari ya kuifuata Nuru
123. Historia na sera ya vijana wema
124. Myahudi wa Kimataifa
125. Kuanzia ndoa hadi kuwa Wazazi
126. Visa vya kweli sehemu ya kwanza
127. Visa vya kweli sehemu ya Pili
128. Muhadhara wa Maulamaa
129. Mwanadamu na mustakabali wake
130. Imam Ali binamu ya Mtume Sehemu ya Kwanza
131. Imam Ali binamu ya Mtume Sehemu ya Pili
132. Khairul Bariyyah
133. Uislamu na mafunzo ya kimalezi
134. Vijana ni Hazina ya Uislamu.
135. Yafaa ya kijamii
136. Kusoma sura zenye Sijda ya wajibu
137. Taqiyya
138. Mas–ala ya Kifiqhi
139. Uislamu na Mazingatio Sehemu ya Kwanza
140. Uislamu na Mazingatio Sehemu ya Pili

Back Cover

Historia inatuambia kuhusu ustaarabu mkubwa uliopita hapo kale na mwishowe ukapotea. Hivi sasa tumebakiwa na masalio na magofu bubu yanayotukumbusha zama za kale za wanaadamu zilizochakaa. Imam Ali (a.s.) alimpa dokezo la fikra zake mwanawe ambalo ni lenye kuhusika na jambo hili.

Alisema: “Mwanangu mpenzi! Ingawa muda wa maisha yangu si mkubwa kama ule wa watu wengine waliofariki dunia kabla yangu, lakini nilijichukulia hadhari kubwa kujifunza maisha yao.

Kwa juhudi nyingi niliyapitia matendo yao na nilizifikiria fikra na matendo yao. Niliyachunguza masalio ya vitu vyao visivyo na uhai na magofu, na nikayafikiria maisha yao kwa makini mno kiasi kwamba nilijihisi kana kwamba niliishi na kufanya kazi pamoja nao tangu kwenye zama za awali za historia hadi kwenye hizi nyakati zetu, na ninayajua yaliyowatendea mema na yaliyowadhuru.”

Hakika sifa moja ya historia iangazayo mno ni kwamba, inazichukua taarifa za maisha ya watu wakuu wa kale. Hakika watu hawa waliiunda historia kwa kuwa walileta mapinduzi na mabadiliko kwenye mtindo wa maisha ya wanaadamu.

Miongoni mwa hawa watu wakuu, hakuna hata mmoja aliyeishi maisha yenye mambo mengi, ya kimapinduzi na yenye maana kama aliyoishi Mtukufu Mtume Muhammad (s.a.w.w.). Hakuna yeyote miongoni mwao aliyeziacha athari za kudumu kwenye jamii aliyojitokeza kama alivyofanya Mtume wa Uislamu (s.a.w.w.). Huu ni ukweli uliokubaliwa na karibuni wanahistoria wote – wawe ni wa Mashariki au wa Magharibi.

Kimetolewa na kuchapishwa na:
Alitrah Foundation
S.L.P. 19701 Dar es Salaam, Tanzania
Simu: 255 22 2110640 / 2127555
Barua Pepe: alitrah@raha.com [15]
Katika mtandao: www.ibn-tv.com [16]

Source URL: https://www.al-islam.org/node/25220

Links
[1] https://www.al-islam.org/user/login?destination=node/25220%23comment-form
[2] https://www.al-islam.org/user/register?destination=node/25220%23comment-form
[3] https://www.al-islam.org/person/sheikh-jafar-subhani
[4] https://www.al-islam.org/organization/al-itrah-foundation-0
[5] https://www.al-islam.org/person/maalim-dhikiri-um-kiondo
[6] https://www.al-islam.org/library/general-history-politics

[7] https://www.al-islam.org/tags/historia

[8] https://www.al-islam.org/tags/wayahudi

[9] https://www.al-islam.org/tags/vita

[10] https://www.al-islam.org/tags/waqurayshi

[11] https://www.al-islam.org/tags/jeshi

[12] https://www.al-islam.org/person/mtume-muhammad-saw

[13] https://www.al-islam.org/person/bibi-zainab

[14] https://www.al-islam.org/person/imam-ali-1

[15] mailto:alitrah@raha.com

[16] http://www.ibn-tv.com